

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 6 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. LUCY J. SABU – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI,
Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

Na. 139

Ujenzi wa Daraja la Mto Mzizima

MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. KENETH E. NOLLO
aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja la kudumu kwenye Mto Mzizima ili barabara ya Kigwe hadi Chipanga Wilayani Bahi iweze kuitika mwaka mzima?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia *TARURA* Wilaya ya Bahi, imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 620.23 kwa ajili ya ujenzi wa daraja (*box culvert*) lenye urefu wa mita 34. Ujenzi wa daraja hili umeanza tarehe 20 Februari, 2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 19 Agosti, 2022 na ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia 30. Kazi hiyo inafanywa na Mkandarasi *Ravji Construction Ltd.*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo utaifanya barabara ya Kigwe – Chipanga kupitika wakati wote na hivyo kuondoa kero ya wananchi kutumia muda mwingi wa kusubiria maji ya mto yapungue ili wavuke na kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shangazi kwa niaba.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali yenye matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Bahi, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kata ya Mwangoi na Kata ya Dule Mlalo ambako linaunganishwa na Mto Umba, mto ule umehama na kusababisha kina cha maji kushuka chini zaidi na hivyo daraja limezama katika eneo lile, lakini Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* wameshafanya tathmini.

Sasa nauliza ni lini ujenzi wa daraja jipya linalounganisha Kata ya Mwangoi na Kata ya Dule katika Kijiji cha Chamlesa litaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo ameianisha pamoja na hilo eneo ambalo daraja linahitajika, kati ya Mwongoi na Dule, daraja hilo lipo katika mpango na tutalitekeleza katika mwaka wa fedha 2022/2023 yaani mwaka unaofuatia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasunga.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, katika Kata ya Isalalo kwenda kwenye Kata ya Ikunga, kuna mto mkubwa wa Nkana.

Je, Serikali ina mpango gani ili kuwafanya wananchi wa Isalalo waweze kuvuka kwenda Kata ya Ipunga kwenye Kijiji cha Ipanzya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri eneo ambalo amelianisha Mheshimiwa Mbunge ninalifahamu na bahati nzuri niko huko huko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshawaagiza watu wa TARURA Mkoa wa Songwe waende wakafanye tathmini katika eneo hilo ili watupe tathmini ili tutafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani na barabara ya Kisukulu - Maji Chumvi ambayo imeharibika sana sasa hivi na wananchi hawawezi kupita?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo ameianisha Mheshimiwa Mbunge inafanyiwa tathmini kwa wakati wa sasa na watakapomaliza tathmini tutampatia taarifa Mheshimiwa Mbunge, ni lini sasa tunaanza rasmi ujenzi katika eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Joseph Kakunda.

Na. 140

Hitaji la Shule za Msingi kila Kitongoji

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isipitishe mkakati maalum kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 wa kujenga shule za msingi kwenye vitongoji vyote vyenye watoto zaidi ya 200?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Serikali ni kuwa na Shule ya Msingi kila Kijiji ikiwemo na vitongoji katika jimbo la Sikunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kuwa Jimbo la Sikunge kwa sasa halina shule za msingi za kutosha, Halmashauri ya Sikunge kuititia fedha toka Serikalini na kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri inaendelea kuhimiza wananchi, jamii na wadau wa maendeleo kujenga miundombinu ya shule za msingi ili kukidhi mahitaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya kujenga shule za msingi kila kitongoji kutategemeana na hali ya uchumi wa nchi na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, kwa jinsi sera ilivyo hatujafikia hatua ya kujenga shule kwa kila kitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shughuli ya ujenzi wa shule inawahusisha wananchi na jamii kwa ujumla, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuendelea kushirikiana na wananchi na Halmashauri kujenga shule katika kila kijiji ili kuwezesha wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule kuweza kupata nafasi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, nimepokea wito wa Serikali kwamba tuendelee kushirikiana na wananchi kujenga shule; na kwa kuwa mwaka jana tulileta maombi ya kujengewa/kumaliziwa shule 58 za shikizi tukapata shule kumi tu katika ya 58 bado shule 48 zimeongezeka sasa hivi ziko 55.

Je, Serikali itatupatia lini fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa shule hizo shikizi 55 ambazo zipo sasa hivi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, usajili wa shule za msingi na usajili wa shule za sekondari hufanywa kwa mikondo, mkondo mmoja wa shule za msingi una watoto 45 na mkondo mmoja wa shule za sekondari nadhani una watoto 40. Sasa maana yake ni kwamba shule yenye mikondo minne inatakiwa iwe na wanafunzi kwenye darasa moja wanafunzi 180 katika shule ambazo zimeshazidi idadi ya wanafunzi wanaohitajika kwenye mikondo. Kwa nini Serikali isiwe na mkakati maalum wa kitaifa wa kujenga shule mpya karibu na maeneo ambayo shule zimezidi idadi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mbunge kwamba moja ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunamalizia shule shikizi zote na kwa awamu ya kwanza katika mwaka wa fedha huu hapa ambao tupo, Mheshimiwa Rais alitoa fedha na tukajenga madarasa 3000 nchi nzima kwenye maeneo ya shule shikizi.

Kwa hiyo, hizo shule kumi ambazo tulileta katika maeneo yako, na sasa hivi tuna mlipango mingine ambayo tuna fedha, na baadhi ya fedha tutazielekeza katika maeneo ambayo bado yanaupungufu na yana mahitaji hususani katika shule shikizi, kwa hiyo, katika kipaumbele tutakachotoa ni pamoja na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatapisha shule zote ambazo zina wanafunzi wengi na ikiwemo kusajili katika maeneo ambayo sasa idadi ya wanafunzi ni kubwa hususani katika hizi shule shikizi ambazo zimezidi.

Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge haya yote yapo katika mpango wa Serikali na tunaendelea kuyatekeleza na mfano mzuri katika mwaka huu wa fedha na katika bajeti ambayo tumeipitisha hapa ya mwaka 2022/2023.

NAIBU SPIKA: Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, si ulisimama?

Waheshimiwa tunaendelea swali lingine Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

Na. 141

Hitaji la Watumishi wa Manispaa ya Mpanda

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi katika Manispaa ya Mpanda hasa katika maeneo ya afya, elimu na maendeleo ya jamii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ina jumla ya watumishi 1,226 kati ya watumishi 1,773 wanaohitajika sawa na asilimia 69.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi kwa awamu ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 watumishi 7,612 wa kada za afya na watumishi 9,800 wa kada za elimu wataajiriwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa bahati mbaye, Manispaa ya Mpanda ni kati ya Manispaa zilizopo pembezoni, mwaka jana tulipata walimu sita na watumishi wa afya saba. Serikali inasema nini katika kuinusuru Halmashauri hii na upungufu wa watumishi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wamekuwepo watu ambao wamekuwa wakijitolea kwa muda mrefu bila kuathiri taratibu za ajira, Serikali inasema nini katika kuajiri watu hawa ambao wamekuwa wakijitolea?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Kapufi kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya kwa kuwasemea Wananchi wa Mpanda Mjini na nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie kwamba tunajua mwaka uliopita walipata watumishi hawa sita wa elimu na saba wa afya lakini ukiangalia asilimia ya watumishi kwa Mpanda ni asilimia 69.1 angalia kidogo ukilinganisha na Halmashauri nyingine. Lakini hii haimaanishi kwamba hatutaleta watumishi na ndio maana kwenye ajira hizi za mwaka huu bado Mpanda itapata kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pili kwa watumishi wanaojitolea Serikali imeweka utaratibu wa kuwapa kipaumbele watumishi wale ambao wanajitolea kwenye vituo vyetu na shule zetu ili ajira zinapotoka waweze kupata ajira kuwa kipaumbele zaidi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri hiyo kipaumbele mnasema hapa, kwenye uhalisia huko hawapewi vipaumbele. (*Makofii*)

Wanajitolea kwa miaka minne, mitano inapofika kazi wanachaguliwa watu wengine hilo mlizingatie hilo. Mheshimiwa Minza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MINZA S. MJIKA: Mhesimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona, naomba niulize swali la nyongeza, je, ni lini Serikali itaongeza watumishi wa afya katika Wilaya ya Meatu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa Mkundi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Halmashauri ya Meatu ina upungufu wa watumishi na itapewa kipaumbele kwenye ajira hizi ambazo zimekwishatangazwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina upungufu wa watumishi kada ya ualimu zaidi ya 1,700 ambayo ni karibu asilimia 40 na watumishi karibu 170 ambao ni karibu asilimia 56 kwenye kada ya afya. Je, Serikali iko tayari sasa kwenye ajira zinazokuja hivi karibuni kutoa kipaumbele kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe? Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathimini kuona maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wa elimu, afya na watumishi wa kada nyingine ikiwemo Ukerewe na maeneo haya ndiyo yatakayopewa kipaumbele

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

cha juu zaidi kuliko yale maeneo ambayo yana watumishi wa kutosha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutatoa kipaumbele Ukerewe, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri ajira mlizotangaza, hakuna *option* inaonesha wale waliojitolea muda mrefu, mnaweza mkawatambua na kuweza kuwasaidia katika kuwachagua. Ni nini Serikali mtafanya kuhakikisha hao wanaojitolea wanapewa kipaumbele cha kwanza na wengine wanafuata? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweka utaratibu wa kutoa matangazo kwa ajili ya ajira za watumishi, lakini naomba Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako tukufu lifahamu kwamba pamoja na watumishi ambao wanajitolea, si watumishi wote waliomaliza vyuo wanaomba kujitolea wanapata nafasi ya kujitolea. Kwa hiyo, bado kuna changamoto ya wale wanaokubaliwa kupata nafasi ya kujitolea. Kwa hiyo, tukiweka kujitolea ya kwamba ni *absolute criteria* maana yake kuna wale ambao walikuwa na nia ya kujitolea, lakini walioomba hawakupata, watakosa nafasi ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio tunakwenda kwa utaratibu kwamba tunawapa kipaumbele kwa sababu wanajitolea na Wakurugenzi sasa wanatupa orodha ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watumishi waliokuwa wanajitolea kupitia Halmashauri zetu, lakini na sisi hata ambao hawajitolea tunawapa *criteria* ya priority kwa sababu wako walioomba na hawakufanikiwa kupata nafasi hiyo, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko.

Na. 142

Kuongeza Wataalamu wa Saikolojia kwenye jamii nchini

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza wataalam wa saikolojia kwenye jamii ili kutoa huduma za ushauri wa afya ya akili na namna ya kuondokana na msongo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu na inathamini huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii ambayo inatolewa na wataalam wa saikolojia kwa lengo la kukidhi mahitaji ya mtu kimwili, kihisia, kijamii, kiroho na kiakili katika mazingira anayoishi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malleko.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ashante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa Serikali kupitia vyuo vikuu hapa nchini inatoa mafunzo ya saikolojia. Kwa nini basi isiajiri wataalamu wa saikolojia ili kupunguza tatizo hili kwa sababu kumekuwa kukiongezeka kesi za mauaji na ukatili kila kukicha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa nini Serikali isiwe na mpango wa kusajili chama cha wataalamu wa saikolojia kama ilivyo kwa taaluma nydingine nchini kama udaktari? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza ni ajira; Serikali inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kupata kibali kwa kuajiri wataalamu hao kadri bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kuunda bodi ya wataalamu; Serikali ipo kwenye mchakato wa kukamilisha utungaji wa Sheria ya Wataalamu wa Ustawi wa Jamii ili kuona kwamba itakapomalizika basi bodi hiyo itaundwa ili kusajili wataalamu hao wa ustawi wa jamii ikiwemo wanasaikolojia. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Neema jiandae Mheshimiwa Taofiq

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa sera ya Wizara ya Elimu inatambua umuhimu wa kuwa na walimu wanaotoa ushauri wa nasaha kwenye shule zetu.

Je, Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ina mpango gani wa kuhakikisha ya kwamba jambo hili linatekelezeka na kwenye shule zetu kunakuwa na walimu wanaotoa ushauri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nasaha kwa watoto wetu hususan ukizingatia kwamba kuna wanafunzi wengi wanaohitimu masomo ya saikolojia na kwa kuanzia wanaweza kuanza kwa njia ya kujitolea? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wanaaskolojia hao. Kwa hiyo Serikali ipo katika kujipanga na kuhakikisha kwamba pale tunapopata nafasi za ajira basi wataalamu hao tutawaajiri na kushirkiana na Afisa wa Maendeleo ya Jamii kuwapa elimu wananchi wetu. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wataalamu wa saikolojia na unasihi bado ni tatizo; je, Serikali haioni imefikia wakati wakaanza kliniki tembezi ili kuweza kutembea katika maeneo mbalimbali na kutoa huduma hiyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum wapo wataalamu hao katika kila mikoa na wanafanya kazi katika Halmashauri hadi vijiji. Pale wananchi ambapo wanapata tatizo katika vijiji vyao basi wamfuate mkuu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kijiji. Mkuu wa Kijiji atatoa taarifa katika Halmashauri kuhakikisha wataalamu wale wanakuja kuwapa elimu ya saikolojia watoto hao. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, tazito hili ni kubwa kiasi ambacho sasa hivi watu wanaishia Mirembe badala ya kutibiwa wakiwemo wanaume wanaopigwa na wake zao, wakiwepo watoto wa shule ambao wanajeruhiwa na wenzao au na walimu.

Je, ni lini hasa Serikali itaona ni wakati muafaka wa kutoa hata mafunzo hadharani wakati wanaposhughulikia hizo ajira?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kama nilivyoeleza Wizara imejipanga kuhakikisha tunatoa elimu kwa wananchi wote hasa wale ambao wanakuja katika sehemu zetu husika wana matatizo ya saikolojia basi tunawapa elimu na tumejipanga kwamba tutakapopa wafanyakazi wengi basi elimu hiyo tutaitoa kwa kila mikoa na kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata elimu hii ili kuondokana na matatizo ya saikolojia na kuondokana na msongo wa mawazo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri. (*Makof*)

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Chumi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 143

Vikao vya Bodi ya *Parole* kwa Mwaka

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Je, Bodi za *Parole* za Mikoa na Kitaifa zinakaa vikao vingapi kwa mwaka na wafungwa wangapi wamepata msamaha kwa mwaka 2020/2021?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya *Parole* ya Taifa na Mikoa iliundwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 1994 na ikafanyiwa marekebisho na Sheria Na. 5 ya mwaka 2002 kwa lengo la kutaka wafungwa wengi wanufaike na mpango huu. Bodi za Mikoa na Taifa kisheria zinatakiwa kufanya vikao vyake angalau mara nne kwa mwaka.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 idadi ya wafungwa waliopata msamaha kuitia Bodi ya *Parole* nchini ni 70. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali yanasema kwamba katika mwaka 2020/2021 ni wafungwa 70 tu waliopata msamaha kuitia Bodi za *Parole*. Sheria ilikuja ili kupunguza mzigo na mrundikano wa wafungwa katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

magereza yetu ambapo mpaka sasa takribani wafungwa ni 15,000. Sasa ikiwa kwa mwaka tu bodi inatusaidia kusamehe wafungwa 70. Je, Serikali inaona kweli bodi ziko kazini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili matokeo haya ya kusamehe wafungwa 70 tu inawezekana kabisa ni kutokana na kwamba vikao hivi vyaa bodi vyaa kimikoa ambavyo vinakaa mara nne kwa mwaka yawezekana kabisa iko mikoa vikao hivi havikaliwi.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuwezesha vikao hivyo viwe vinakaa mara nne kwa mwaka kama sheria inavyoelekeza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Sheria ya Bodii za *Parole* iliwekwa ili kusaidia kupunguza msongamano wa wafungwa gerezani kwa kuwapa msamaha wale wanaokidhi vigezo. Nikiri kwamba kwa mwaka uliopita 2020/2021 vikao vingi havikukaa kwa sababu bodi ziliisha muda wake na bahati mbaya sana mapendekezo yale yalichelewa kumfikia Waziri wa Mambo ya Ndani. Lakini hivi tunavyozungumza bodi izote zimeshaundwa mikoa yote, kwa hivi maelekezo yaliyotoka ni kuhakikisha kwamba vikao vinakaa kwa mujibu wa mwongozo ili wafungwa wanaokidhi vigezo waweze kunufaika na uwepo wa bodi hizi.

NAIBU SPIKA: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Mbunge Dar es Salaam.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mahabusu kuna wanawake ambao wanakuwa wamewekwa mle wakiwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

matatizo mbalimbali na ni wajawazito, sasa wanajifungua wakiwa bado kesi zao hazijasilikizwa.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha wale watoto wanaozaliwa mama zao wakiwa mahabusu hawapati changamoto za kisaikolojia mama zao wanapokuwa pale ndani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wakati baadhi ya wafungwa wanakuwa na changamoto, wanakuwa na hali ya ujauzito na kujifungua watoto wakiwa magerezani. Upo utaratibu unaowawezesha wafungwa wa namna hii kupata huduma stahiki ikiwa ni pamoja na hao watoto wanatengwa na kupewa nafasi ya kunyonyeshwa na mama zao kama miongozo ya sekta ya afya inavyoelekeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi juu ya watu hawa kwa sababu taratibu za kuwalinda zipo. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

Na.144

Ujenzi wa Mradi wa Maji Wilaya ya Mkinga

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Maji Mkinga kutoka Mto Zigi au Kinyatu utaanza kutekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dunstani Luka Kitandula, Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Mkinga pamoja na maeneo ya pembezoni, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi wa maji wa Mkinga kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Zigi mwezi Machi, 2022. Aidha, taratibu za kupata mkandarasi zinaendelea na anatarajiwani kuanza kazi mwezi Juni, 2022 na utekelezaji utaendelea katika mwaka wa fedha 2022/2023.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Serikali kwa majibu hayo na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mradi huu ndio utakuwa mkombozi kwa ukanda wote wa Pwani wa Wilaya ya Mkinga. Je, Serikali inataka kutuambia ni lini hasa mradi huu utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kwa kuwa Waziri anaahidi hapa kwamba mradi huu sasa unaenda kuanza, yupo tayari kuandamana nami twende tukafanye mikutano ya kuwaaminisha wananchi hawa kwamba tatizo lao sasa linaenda kuondoka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri. Ninyi wote njia moja. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimponeze sana Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Dunstan Luka Kitandula, kwa kweli hali ya upatikanaji wa maji Mkinga yalikuwa ni changamoto kubwa sana na tumefanya jitihada kama Serikali ya kuchimba visima lakini kwa jiografia ile imekuwa ni changamoto.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, maelekezo ambayo tumepata na *support* ya Mheshimiwa Rais ni kuyatoa maji sasa ya Mto Zigi, Tanga na kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo la maji katika Jimbo la Mkinga. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji tumetoa maelekezo itakapofika Juni mkandarasi awepo *site* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu mkubwa na historia itakumbuka wananchi wa Mkinga kwa jitihada unazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juu ya kuambatana naye, mimi niko tayari kuongozana naye katika kuhakikisha tunaenda kufanya mikutano ili tuweze kuwahabarisha wananchi juu ya utekelezaji wa mradi huu mkubwa katika Jimbo la Mkinga. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, changamoto ya maji katika Jimbo la Ushetu ni kubwa sana, lakini pia hata miradi iliyoanzishwa toka mwaka 2019 hasa katika Kata za Saba Sabini, Mkunze na Chambo hajakamilika.

Je, ni lini Serikali itaweza kukamilisha miradi hii ili wananchi hawa wa Ushetu waweze kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimwombe Mheshimiwa Waziri...

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa umesauliza imetosha. Mheshimiwa majibu.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kaka yangu Cherehani kwa kweli ameingia muda mfupi, lakini amekuwa anawapigania watu wake na si mara moja ameshafika ofisini. Kubwa utekelezaji wa miradi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya maji inategemeana na fedha, tutatoa fedha kwa Jimbo la Ushetu kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati na wananchi wa Ushetu waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunatumia sasa maji ya Ziwa Victoria kuhakikisha wananchi wa Ushetu wanaenda kupata maji ya uhakika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Profesa.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, tunamshukuru sana Waziri kwamba tumepata mradi wa maji katika Kata ya Mabogini. Lakini baada ya manunuzi ya vifaa havijatosha kufikisha maji Umashaini eneo la Remiti. Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, lakini kikubwa nataka nimhakikishie maeneo yote ambayo panaishi watu na wanahitaji maji Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imetoa maelekezo kuhakikisha tunawafikishia maji na wananchi waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa miji 28 ulikuwa ni mradi mkombozi sana kwenye majimbo ambayo hatujawahi kuona maji ya bomba, kila nikiuliza mnaahidi mwezi mmoja unaniambia nini ili wananchi wangu wapate faraja ya maji ya miji 28?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, lakini nataka nimtie moyo ukiona giza linatanda ujue kumekucha. Taratibu zote zinazohusiana na manunuzi ya mradi wa miji 28 zimekwishakamilika na kabla ya Bunge la Bajeti ya Wizara yetu ya Maji tutakaa na Waheshimiwa Wabunge tukubaliane lini tunakwenda kusaini mradi ule taratibu zote tumeshakamilisha tunaenda kwenye *signing* ya mradi, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simon.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipata ahadi ya Serikali kupitia Waziri Aweso kuanza kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Lakini mpaka sasa haujaanza na tuliahidiwa kwamba ungeanza mwezi wa nane mwaka jana. Nini *commitment* ya Serikali juu ya mradi huu kuanza kwa ajili ya kunufaisha wananchi wote hao nilowataja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, nikiri maelekezo ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ni kutumia rasilimali toshelevu ikiwemo mito pamoja na maziwa kuhakikisha kuwa tunatatua matatizo ya maji. Tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 400 kwa ajili ya kutumia Ziwa Victoria na kutatua tatizo la maji katika Mkoa wa Simiyu ikiwemo Bariadi, Busega na Itilima.

Kwa hiyo, mkakati wa Serikali sasa hivi tupo hatua ya kumpata mkandarasi na tupo hatua za mwisho. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi atapatikana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa wakati na utekelezaji wake tunaenda kuanza mara moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Almas.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Je, lini Serikali itakamilisha miradi ya maji kutoka Ziwa Victoria katika vijiji vya Mogwe, Ikongolo, Majengo, Kiwembe, Mbiti na Muswa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, jilanda Mheshimiwa Midimu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimponeze Mheshimiwa Mbunge pamoja na Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati, Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuyatoa maji katika Ziwa Victoria na kuyaleta katika Mji wa Tabora, Igunga na Nzega. Kazi iliyobaki ni kufanya tu usambazaji.

Nataka nimhakikishie usambazi huo tutaufanya katika vijiji ambavyo amevitaja ili katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Midimu, jilanda Mheshimiwa Iddi.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Isanga na Guduwe Wilaya ya Bariadi wana shida sana ya maji, muda mwingi wakina mama wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. Ni lini Serikali itachimba visima virefu katika kata hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwanza kilio cha Wanabariadi kwa maana ya Mkoa wa Simiyu kimesikika na tumpata fedha kama nilivyoeleza zaidi ya shilingi bilioni 400 katika kuhakikisha tunaenda kutekeleza mradi mkubwa. Tumefanya jithada kubwa za kuchimba visima eneo la Mkoa wa Simiyu, lakini imekuwa ni changamoto. Kwa hiyo, *solution* pekee kwa ajili ya kutatua tatizo la maji Bariadi na Mkoa wa Simiyu ni kuhakikisha tunayatoa maji ya Ziwa Victoria katika kuhakikisha Wanasiyuu na Wanabariadi wanapata maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mradi wa Mhangu - llogi ni mradi uliochukua muda mrefu sana na mwaka jana niliuliza swali la msingi na Mheshimiwa Waziri alinipa majibu kwamba mwezi wa sita mwaka jana mradi ule ungezinduliwa. Sasa nataka kufahamu majibu ya ukweli ni lini sasa mradi huo wa Mhangu - llogi utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. (*Makofi/Kicheko*)

Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali baada ya saa saba tukutane ofisini ili kuhakikisha kwamba hili jambo tunalikamilisha na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy Sabu.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii lakini kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu Mheshimiwa Songe kashauliza swali, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri. Aah *okay* Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri umekuwa ukiulizwa maswali ya uhitaji wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maji na Wabunge, na umekuwa ukiwapa wote ahadi za matumaini, lakini tunajua bajeti yako ni ndogo.

Sasa hudhani ni wakati sahihi wa kuliambia Bunge hili tukufu kipi kipaumbele cha Serikali kwa mwaka huu wa fedha? Kwa sababu haiwezekani kila Mbunge amesimama unampa matumaini, lakini matumaini hayatekelezwi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima uliza swali lako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nini kipaumbele cha Serikali vijijini, mijini; maeneo gani na kwa mawanda yapi? Kuliko kupeana ahadi hapa unaanza kuulizwa tunataka utupe ahadi ya mwisho, siyo jambo jema.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe hofu, wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imejipanga juu ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe mfano, eneo la vijijini kuititia bajeti yetu tunakwenda kutekeleza miradi 1,176 vijijini, hajawahi kutokea. Lakini pia dhamira ya Mheshimiwa Rais sasa hivi katika dola milioni 500 ambazo tumezipata, katika miji 28 tunakwenda kutatua tatizo hili la maji. Kwa hiyo, kipaumbele cha Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha wananchi wa mijini na vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gulamali.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na miradi mingi sana ya maji ndani ya jimbo letu na tumekuwa tukikuomba uje uikague miradi hiyo kuona ubora wake na thamani ya fedha inayotumika.

Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri na timu yako utapata nafasi ya kuja kukagua miradi hiyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa Suma na Mheshimiwa Kilave.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhidi Mheshimiwa Gulamali baada ya Bunge letu la Bajeti nitafanya ziara katika jimbo lake katika kuhakikisha tunasimamia na kufuatilia miradi katika Jimbo lake la Manonga. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suma.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Tukuyu una changamoto kubwa sana ya maji ikiwa ni Kata za Bulyaga, Msasani, Bagamoyo, Makandana, Ibigi, Kawetele; na Serikali iliahidi kupeleka shilingi bilioni 4.5 lakini mpaka sasa wamepeleka shilingi milioni 700 tu. Wananchi wa kule hasa akina mama wanaacha kufanya kazi kubwa za kutafuta riziki kwa ajili ya watoto wanashinda kutafuta maji.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili kumalizia mradi huo wa maji? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua maji hayana mbadala, maji ni uhai na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan kila mwezi tunapokea zaidi ya shilingi bilioni 14, 15 katika Mfuko wetu wa Maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nataka nimhakikishie tutawapa kipaumbele Wanatukuyu ili kuhakikisha miradi yake nayo inapata fedha ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati wananchi wapate huduma ya maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kilave.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, mimi nina swali moja tu; kuna upotevu mkubwa sana wa maji Mkoa wa Dar es Salaam hasa kwenye Jimbo la Temeke, nadhani mabomba yale ni chakavu na ya siku nyingi.

Je, mna mkakati gani sasa wa kubadilisha yale mabomba kuweka mabomba mapya ili tusipate taabu ya maji tena?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Ni kweli moja ya changamoto kubwa juu ya miradi ni upotevu wa maji na tumetoa maelekezo mahususi juu ya kuhakikisha kwamba tunakarabati na kujenga miundombinu mipyä ili kuhakikisha upotevu huu unakuwa katika *standard*.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na *DAWASA* katika kuhakikisha tunakarabati na kujenga miundombinu mipyä ili upotevu huu usiendelee na wananchi wahakikishe wanapata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Ujenzi Upya Bwawa Lilipo Kata ya Kasamwa – Geita

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga upya Bwawa la Kasamwa na kutenganisha mwingiliano wa binadamu na mifugo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Kasamwa lilijengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kutoa huduma za maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, viwanda, kunyweshea mifugo pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itafanya usanifu kwa ajili ya kukarabati bwawa hilo ambapo pia itajumuisha miundombinu kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ahadi ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye mwaka huu wa fedha, lakini Bwawa la Kasamwa pamoja na kuhudumia wananchi limesababisha Kiwanda cha Pamba cha Kasamwa pamoja na Kiwanda cha Mafuta kutofanya kazi kwa sababu hakuna maji. Sasa ni lini baada ya upembuzi yakinifu ujenzi wa bwawa hilo utafanyaika?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nawapongeza *GEUWASA*, wanafanya kazi yao ya kusambaza maji vizuri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Lakini maji ya *GEUWASA* ni ya nyumbani (*domestic*) na maji ya bwawa yanategemewa kwa ajili ya mifugo na kuna mnada mkubwa pale wa mifugo. Sasa ni lini ujenzi wa bwawa hilo utapewa kipaumbele ili kuokoa mifugo inayokwenda Kasamwa pale? Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe hofu Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nataka nimhakikishie kuwa kupitia Wizara yetu ya Maji tumepata fedha kwa ajili ya kununua mitambo seti tano kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa. Kwa hiyo, moja ya maeneo ambayo tutaweza kuwapa kipaumbele ni eneo katika Jimbo lake la Geita Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kikubwa, nataka nimhakikishie kuwa mitambo itakapokuwa imefika mwezi huu wa Juni, moja ya maeneo ambayo tutayapa kipaumbele ni eneo la Geita kwa sababu kumekuwa na uhitaji mkubwa sana. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hokororo.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itasafisha ili kuongeza kina cha Bwawa la Lukuledi ikiwa ni ahadi yake Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2021, maji ambayo yanatumika katika Vijiji vya Lukuledi, Mwangawaleo, Ndomoni, Mraushi na Nambawala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa moja ya changamoto kubwa katika utekelezaji wa mabwawa ilikuwa suala zima la vifaa. Lakini tumekwishapata fedha juu ya ununuzi wa vifaa hivi vya kisasa na moja ya maeneo ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tutayapa nguvu na ya kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunajenga mabwawa. Kwa hiyo, tutawapa kipaumbele katika kuhakikisha mabwawa ambayo yatakayokuwa yamejengwa na yeze jimboni kwake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matondo.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mwanza tumekuwa na shida sana na kero ya maji, na hasa miradi ambayo haitekelezeki, na ukizingatia Mwanza tumezungukwa na ziwa.

Je, ni lini Serikali itatekeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Mwanza tukaondokana na kero ambayo inatukumba mpaka muda huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa Pallangyo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri katika Jiji la Mwanza pamoja na mradi tuliokuwa nao lakini ongezeko la watu limesababisha uhitaji mkubwa wa maji. Tuna mradi sasa hivi tunaongeza chanzo katika eneo la Butimba ili kuongeza uzalishaji na wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 65 katika kuhakikisha kazi ile inaanza na mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa sisi kama Wizara ya Maji tutausimamia na kuufuatilia mradi ule ukakamilike kwa wakati ili uweze kuongeza uzalishaji na wananchi wa Jiji la Mwanza kwa maana ya llemela pamoja na Nyamagana kuweza kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pallangyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi na kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri ambaye wakati alipokuwa jimboni kwangu mara ya mwisho alitoa maelekezo ya namna ya kutatua changamoto ya mafuriko yanayosababishwa na kufukiwa korongo la Mto Nduruma na kutesa wananchi wa Kata za Shambarai Burka, Mbuguni, Majengo na Makiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya ziara ya wale wataalam ambao walitumwa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pallangyo swali.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: ...kimya kimetanda. Swalii sasa, je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kutatua ile changamoto ya mafuriko?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimefanya ziara katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge la Arumeru Mashariki na moja ya ahadi ni kuwapatia fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshatoa fedha mwezi huu, shilingi milioni 100, kwa ajili ya uanzaji wa kazi ile. Mheshimiwa Mbunge unaweza ukafuatilia katika hilo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani.

Na. 146

Kufupisha Miaka ya Elimu ya Msingi na Sekondari

MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. NG'WASI D. KAMANI aliuliza: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, lini Serikali itafupisha muda wa miaka saba kwa elimu ya msingi na sita ya sekondari ili kupunguza muda kwa wanafunzi wenyewe uwezo mkubwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatayyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miaka inayotumika kumuandaa mhitimu wa elimu ya msingi na sekondari hutegemea kiasi cha maudhui yanayotakiwa kujengwa ili kumuwezesha mhitimu kupata stadi na ujuzi unaohitajika kulingana na mahitaji ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua uwepo wa wanafunzi wenyewe uwezo tofauti katika kujifunza mwaka 2019 ilioa mwongozo kuhusu utaratibu wa kurusha darasa wanafunzi wa elimu ya msingi. Mwongozo huo unatoa utaratibu unaopaswa kufuatwa na uongozi wa shule kwa kushirikiana na mzazi wa mtoto husika katika kumrusha darasa wanafunzi anayeonekana kuwa na uwezo mkubwa darasani. Aidha, baada ya kufanyika kwa tathmini ya utekelezaji wa mwongozo huo Serikali itaona namna ya kuendelea na utaratibu huo kwa ngazi nyingine za elimu. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwongozo huu ulitoka mwaka 2019 na sasa ni mwaka 2022; je, Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imefanya tathmini na kugundua changamoto zipi juu ya mwongozo huo, na nini majibu ya Serikali baada ya kugundua changamoto zilizopo katika mwongozo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ni lini Serikali itakamilisha uandaaji wa Sera mpya ya Elimu ya Sekondari ili kumpunguzia kijana wa Kitanzania mzigo wa kukaa muda mrefu shulen? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tunakumbuka Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 akihutubia Bunge hili tukufu alituagiza Wizara ya Elimu kuweza kufanya mapitio ya sera, sheria pamoja na mitaala yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hilo ndilo ambalo linaendelea hivi sasa na katika mapitio haya ya sera, sheria pamoja na mitaala, suala la miongozo hii kufanyiwa tathmini nalo limeingizwa ambapo tutafanya tathmini ya kina kuona namna gani miongozo hii tunaweza kuirekebisha kulingana na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, anauliza muda gani tutatumia; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa mpaka kufika mwaka wa fedha ujao tutakuwa tumekamilisha utaratibu wa mapitio ya sera, sheria pamoja na mitaala hii ili iweze kuanza kutumika. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua kubwa ya wahitimu nchini wa sekta ya elimu, zaidi ya asilimia 70 ya wahitimu wa vuyo nchini ni walimu.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka sasa wa kuhamasisha fani nyingine ili vijana wetu wanapomaliza kidato cha nne waweze kusoma fani nyingine kwa mazingira wezeshi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo anazungumza Mheshimiwa Mbunge ni kweli, na kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, kwa vile sasa tunafanya mapitio ya sera, sheria pamoja na mitaala yetu ambayo tunakwenda kuhakikisha kwamba maeneo mengi ambayo yanabeba fani za ufundi tunakwenda kuyafanya kazi. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi katika eneo hilo, kwa vile amesema wengi ni walimu hata huko huko kwenye ualimu nako tukiweka na stadi zlie za kazi tunaweza tukaondoa changamoto hiyo ya ajira.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Kandege.

Na. 147

Kuwezesha Mkoa wa Rukwa Kulima Zao la Maharage ya Soya

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mkoa wa Rukwa unalima zao la maharage ya soya lenye uhitaji mkubwa zaidi duniani?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa ni moja ya mikoa inayozalisha maharage ya soya kwa wingi nchini kwa ajili ya chakula na biashara. Katika mwaka 2020/2021 mkoa ulizalisha jumla ya tani 121,356 katika eneo la hekta 120,432. Mwaka 2021/2022 mkoa umelenga kuzalisha jumla ya tani 128,672 za maharage katika eneo la hekta 121,961.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza kilimo cha maharage ya soya Mkoani Rukwa, Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za maharage ya soya nchini kupitia sekta binafsi, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*TARI-Uyole*) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*) na kupitia vikundi vya wakulima wazalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa ubora (*QDS*) na kutoa mafunzo ya uzalishaji wa maharage ya soya kwa Maafisa Ugani 64 katika ngazi ya Halmashauri, kata na vijiji ili kuwezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ugani hao wanatumika katika kutoa ushauri na kuandaa mashamba ya mfano ya kilimo cha maharage ya soya katika maeneo yao, kupima afya ya udongo ili kuwezesha matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo, kuhamasisha kilimo cha mkataba kati ya wakulima na wanunuzi ili kuwa na uhakika wa soko la mazao ya wakulima wanaolima maharage ya soya nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kandege.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, maharage ya soya niliyokuwa namaanisha ni maharage ambayo yanatumika kukamua mafuta ya kula, lakini katika majibu ambayo yametolewa na Serikali naamini wanamaanisha maharage ya kula kama mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na majibu hayo, lipo tatizo kubwa sana la upatikanaji wa mbegu za maharage ya soya ambayo yanatumika kwa ajili ya kukamua mafuta. Utakubaliana na mimi kwamba sisi kama Taifa tumepata soko kupeleka maharage haya China.

Swali langu; je, Serikali inafanya mpango gani mahususi wa kuhakikisha kwamba mbegu hizi zinapatikana kwa ajili ya wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Ruvuma na mingine yote Tanzania ili tuweze kujitosheleza katika kilimo cha mafuta? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni ukweli usiopingika kwamba kuna *formulary synergy*, kwamba moja kujumlisha moja ni tatu na siyo mbili, kwa sababu *soya meal* inayopatikana ni chakula kizuri sana kwa ajili ya mifugo ikimaanisha ng'ombe, samaki na kuku.

Je, siyo wakati mwafaka kwa Serikali, kwa sababu Wizara ya Mifugo bado bajeti yake haijaja ikahakikisha kwamba ina-*inject* kiasi cha fedha ili mbegu bora zipatikane ili wakulima na wafugaji wetu wasihangaike ili wawe na uhakika wa chakula kwa ajili ya mifugo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kandege kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja kati ya changamoto kubwa tuliyonayo hivi sasa ni upatikanaji wa mbegu bora za soya na Serikali imeanza kuchukua hatua na hatua za kwanza ambazo tumezichukua ni kwa kushirikiana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Taasisi za *TOSCI* pamoja na ASA kuruhusu uingizaji wa mbegu kutoka nchi za karibu za Malawi na Zambia ili tuweze kufanya *seed multiplication* na lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunasambaza mbegu hizi kwa wakulima wengi zaidi na zipatikane kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kunayo changamoto hiyo kubwa, lakini *TOSC/na ASA* wameshakaa chini na kukubaliana na uingizaji wa mbegu hizi katika hatua ya awali na lengo letu kubwa ni kufanya wananchi wengi zaidi waweze kuzipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli liko soko kubwa sana la mahitaji ya *soya beans* duniani na hasa kule nchini China, mahitaji ni zaidi ya *metric tons* milioni 100, na kama nchi tumejandaa pia kuliflikia soko hilo. Na katika maeneo ambayo tutayapa kipaumbele ni maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja na hivi sasa Mkurugenzi Mkuu wa ASA yuko njiani anaelekea...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: ...anaelekea kwenda katika Mikoa ya Rukwa na Katavi kwa ajili ya kupata mashamba mengine makubwa kwa ajili ya uzalishaji mbegu ambayo yatakidhi mahitaji ya maeneo husika.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Zaytun.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha wanafanya vizuri sana kwenye zao la vitunguu hapa nchini na hata Afrika Mashariki; je, Wizara ina mkakati gani wa kuwasaidia wakulima hawa ili waweze kuongeza tija na pia kupata masoko ya uhakika? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati tulionayo hivi sasa ni kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanalima kwa tija na ili waweze kuyafikia masoko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi; na kwa kuanzia tumeanza kuwapa maelekezo Maafisa Ugani kwa mazao mahususi ikiwemo vitunguu ili kuwasaidia wakulima waweze kuzalisha kwa tija.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Njombe na Rukwa ilikuwa inajulikana kama *The Big Four* kwa kilimo cha mahindi, lakini wakulima wengi sasa hivi wametetereka sana kutokana na bei kubwa ya pembejeo.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba bei ya pembejeo inapungua ili mikoa hiyo iendelee kulima kilimo kikubwa kabisa cha mahindi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambayo Serikali tutaichukua kumpunguzia maumivu ya pembejeo mkulima katika bajeti inayokuja tutaaniszha Mfuko maalum, (*Price Stabilization Fund*) ambao ikitokea pembejeo zitakwenda juu Serikali itatoa ruzuku ili mkulima asiumie sana katika upatikanaji wa pembejeo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBI SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali sasa aulize swali lake.

Na. 148

Ujenzi wa Barabara ya Fulo – Nyambiti – Malya kwa Kiwango cha Lami

MHE. KASALALI E. MAGENI aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya kilometra 73 kutoka Fulo – Nyambiti – Malya itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaifanyia upembizi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Fulo – Nyambiti – Malya yenye urefu wa kilometra 73 wakati wowote pindi fedha itakapopatikana. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hii. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kasalali.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa barabara hii ni ya muhimu sana kwenye utalii wa Serengeti ya Kusini na vipande vya kuanzia Karatu, Mbulu, Haydom, Sibiti mpaka Maswa vimeshafanyiwa upembizi yakinifu na baadhi ya maeneo yameshaanza kujengwa. Lakini kipande cha kutokea Maswa – Malya – Nyambiti – Fulo havijawahi kufanyiwa upembizi yakinifu na imekuwa ni ahadi kila mara.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sasa kwamba kuna umuhimu wa kulichukulia jambo hili kwa ukubwa wake na kufanya upembuzi yakinifu na hatimaye kujenga kwa lami barabara hii ili watu wa Jimbo la Sumve na Mkoa wa Mwanza na wenyewe wafaidi matunda ya utalii ambayo Serikali imeshaanza kufanya juhudini kubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa barabara pacha ya barabara hii ni barabara inayotokea Magu kupitia Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa; na barabara hii yenye urefu wa kilometra 71 tumekuwa kila siku tukiizungumza na Serikali katika bajeti inayoisha Juni imepanga kujenga kilometra 10 lakini hakuna dalili zozote za kuanza kujenga.

Je, nini tamko la Serikali kuhusu barabara hii ya muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Kwimba?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo ameulizia ambayo ipo kwenye swali la msingi nimesema Serikali itahakikisha kwamba kwanza tunaifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kama ambavyo imeainishwa katika llani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tunaitakeleza. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba kazi hiyo tutaifanya kama ilivyoainishwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, barabara aliyoitaja ya Hungumalwa – Ngudu – Magu, barabara hii usanifu wa kina umeshapatikana na ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba mipango ipo na tuna hakika kwamba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo tumeainisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; barabara ya Singida – Iguguno – Mkarama – Sibiti – Meatu imejengwa kilometra 25 tu, na sote tunafahamu barabara hii ni *shortcut* kwa watumiaji au wasafirishaji wanaokwenda Mikoa ya Mara na Simiu.

Sasa ni kwa nini Serikali isitafute fedha kwa udharura wake kuhakikisha kwamba hii barabara inakamilika ile sehemu iliyobaki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu na ni njia fupi sana, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga na inaendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba barabara hii sasa tunaijenga na kuikamilisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kipande cha barabara ya kutoka Uvinza – Kasulu kuititia Basanza hakina lami, na mara nydingi matukio ya unyang’anyi na ujambazi hutokea katika barabara hiyo ya Uvinza – Kasulu.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja tayari imeshafanyiwa usanifu wa kina na ni barabara kuu ambayo inaunganisha barabara kutoka Mpanda – Uvinza kwenda Kasulu. Sehemu aliyokuwa anaisema ilikuwa inafanyika utekaji tuliamua kuipiga zege ili pawe rahisi kuitika, lakini mpango ni kuikamilisha barabara hii kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Sillo, jiandae Mheshimiwa George Mwenisongole.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza naipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Kondoaa hadi Babati. Lakini ni lini Serikali itajenga mizani katika barabara hii ili isiharibike ndani ya muda mfupi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, sijalisikia vizuri swali lake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sillo, rudia swali lako; barabara ya kutoka Kondoaa kwenda wapi?

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Kondoaa hadi Babati. Lakini ni lini sasa Serikali itajenga mizani katika barabara hii ili isiharibike ndani ya muda mfupi? Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ya Dodoma – Kondoa hadi Babati haina mizani, na ni kwa sababu wakati stadi inafanyika hapakuonekana kama kutakuwa na *traffic* kubwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunafanya mipango ya kutafuta eneo kujenga mizani ili kuilinda hii barabara ikiwa ni pamoja na barabara ya kutoka hapa kwenda Iringa ambapo napo hapakuwa na lami, tayari tumeshaanza kujenga mizani. Kwa hiyo, Serikali imeshaliona hilo na tuko mbioni kujenga mizani ili kuilinda hiyo barabara. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa George Mwenisongole.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Napenda kuuliza swali kuhusu barabara ya Mlowo – Kamsamba mpaka Utambalila; barabara hii upembuzi yakinifu na usanifu wa kina vimeshakamilika, na mwaka jana nilipouliza swali kuhusu hii barabara Mheshimiwa Naibu Waziri aliniambia kwamba Serikali inatafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu ni hili; je, Serikali bado inaendelea kutafuta fedha au mpango umeishia vipi? Kwa sababu wananchi wa Mbozi wanasubiri kwa hamu sana hii barabara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa ustawi wa Mkoa wa Songwe. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina Serikali inatafuta fedha ili ianze kujenga kwa kiwango cha lami barabara yote ya kutoka Mlowo hadi Kamsamba, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara ya kutoka Makete kwenda Mbeya ni barabara ya kiuchumi, na katika barabara 16 ambazo Mheshimiwa Rais alisaini zianze kujengwa moja ni barabara kutoka Makete kuelekea Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmekuwa mkituambia mko kwenye *tendering*, tunaomba majibu wananchi wa Makete; ni lini barabara hii itanza kujengwa ili ifanye ukombozi wa uchumi wa wananchi wa Makete?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makete – Kikondo kwenda Isyonje ni barabara ambayo ilipata kibali cha kutangazwa na ilitangazwa lakini ilikosa wakandarasi. Barabara hiyo imetangazwa tena na tarehe 22 mwezi uliopita ndio ilikuwa mwisho na sasa hivi barabara hii tuko kwenye *evaluation* ili tujue mkandarasi yupi atapata hiyo kazi.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tuko kwenye taratibu za manunuzi, tunafanya *evaluation* ya *tender*, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Justin Nyamoga.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya kutoka llula – Mlafu – Mkalanga – Kising'a hadi Kilolo kwa sasa haipitiki kutokana na uharibufu mkubwa wa mvua.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuiagiza *TANROADS* kufanya marekebisho ya haraka ili barabara hii muhimu iweze kuendelea kupitika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalil ya nyongeza la Mheshimiwa Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TANROADSM* kuo wa Iringa ahakikishe kwamba anakwenda kwenye hii barabara ndani ya siku mbili ili kwenda kufanya tathmini na kufanya marekebisho ya sehemu zote ambazo hazipitiki ili wananchi wa Kilolo waweze kuendelea kupata huduma ya barabara hii.

NAIBU SPIKA: Ahsante; Mheshimiwa Ally Kassinge.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Kiranjeranje – Nanjilinji mpaka Ruangwa ni barabara ambayo Serikali imeahidi kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 mpaka 2025 lakini pia upembuzi wa kina umeshafanyika. Lini Serikali inakwenda kujenga barabara hii kwa manufaa ya wakazi wa maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ni lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalil

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii tumeshakamilisha usanifu wa kina, na haya ni maandalizi kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hii hatua ya kukamilisha usanifu wa kina Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula sasa aulize swali lake.

Na 149

Ujenzi wa Madarasa Kampasi ya Kibirizi

MHE. SYLVIA F. SIGULA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa madarasa katika Kampasi ya Chuo cha Uvuvi Kibirizi utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (*FETA*) kuititia kampasi ya Kibirizi ulianza kutoa mafunzo ya muda mrefu ya tasnia ya uvuvi mwaka 2013/2014 kwa kutumia majengo ya kilichokuwa Kiwanda cha Mashua Kigoma ambacho kilikuwa katika eneo la Kibirizi. Hivyo, kwa sasa kampasi ya Kibirizi inatoa mafunzo ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

teknolojia ya ukuzaji viumbe maji (*aquaculture technology*) katika ngazi za Astashahada na Stashahada kwa kutumia madarasa yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha Kampasi ya Kibirizi kwa kujenga madarasa mapya na kuipatia vitendea kazi ili iweze kutoa mafunzo zaidi ikiwemo masomo ya sayansi na teknolojia ya uvuvi (*fisheries science and technology*) na usimamizi wa uvuvi (*fisheries management*) ngazi za Astashahada na Stashahada, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sylvia.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Wizara, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza; uchumi wa vijana wengi wa Mkoa wa Kigoma unategemea sana uvuvi, na sasa hivi tunashukuru kwa sababu tumeanza usafirishaji wa samaki kutoka ndani kwenda nje. Lakini kumekuwa na changamoto, pamoja na kuwa na hiki chuo bado kuna tatizo kubwa la ubora wa samaki wetu kukidhi kwenye masoko ya nje na ndani na chuo hiki kinatoa kozi moja.

Je, Serikali haioni sasa ni muda mwafaka wa kuongeza kozi ya *fish processing, quality assurance and marketing* ili tuweze kupata wataalam wengi wa kusimamia ubora wa samaki wetu ili kupunguza hasara kwa wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; je, Waziri yuko tayari kuongozana na mimi au Mbunge wa jimbo husika kwenda katika chuo hiki kuona hizi changamoto yeye mwenyewe? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Sylvia, wakati mwingine hata Kiti kinaweza kikaongozana na wewe ili kujiridhisha. Mheshimiwa Waziri. (*Makofii/Kicheko*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua umuhimu wa vijana kuingia katika tasnia hii ya uvuvi hasa vijana wa Mkao wa Kigoma kwa sababu ya mazingira waliyonayo ya Ziwa Tanganyika. Chuo chetu hiki cha Kibirizi kiko kwenye eneo dogo na sisi kama Wizara tunachukua hatua za makusudi kutafuta eneo lingine kwenye Manispaa hiyo hiyo ya Kigoma ili tuweze kukipanua chuo hiki kiweze kutoa mafunzo zaidi kwa vijana hawa ikiwa ni pamoja na kozi aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la kufika Kigoma ili kuweza kuona mazingira halisi, niko tayari kuambatana naye.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwenda. Sasa nitawatambua wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji - Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Profesa Godius Kahyarara - Katibu Mkuu; Dkt. Hashil Abdallah - Naibu Katibu Mkuu Viwanda na Biashara; Ndg. Ally Gugu - Naibu Katibu Mkuu Uwekezaji; Dkt. Khamis Mkanachi - Mkuu wa Wilaya ya Kondoa; Ndugu Angelina Ngalula - Mwenyekiti wa *TPSF* na Ndugu Paul Makanza - Mwenyekiti wa *CTI*, karibuni. (*Makofii*)

Yupo pia Ndugu Paul Koyi - Rais wa *TCCIA*; Ndugu Raphael Laizer - Mkurugenzi Mtendaji wa *TPSF* ambao wameambatana na Wenyeviti wa Bodi katika Taasisi za Wizara, Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara na Wakuu wa Idara na Vitengo. (*Makofii*)

Wapo pia wadau wa maendeleo, kampuni na taasisi ambaao ni Shirika la Maendeleo la Umoja wa Taifa (*UNDP*);

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Shirika la Maendeleo ya Viwanda Umoja wa Mataifa (*UNIDO*), *Trade Nari East Africa*; Shirika la Taifa la Utangazaji (*TBC*) na Kampuni ya Bakhresa, karibuni. (*Makof*)

Wapo pia Waheshimiwa Madiwani 15 kutoka Jimbo la Kondoa; wanachama wa CCM pamoja na wapiga kura kutoka Jimboni Kondoa. (*Makof*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ndugu Tousif Bhojan, karibu. (*Makof*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Wanakwaya wa Mtakatifu Anna kutoka Jimbo Katoliki Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Padri Canisius Milyango, karibuni. (*Makof*)

Wageni wengine 20 wa Mheshimiwa Dkt. Mabula ambao ni wanafamilia kutoka Mwanza na Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Emmiliana Lubala, karibuni. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Taifa la *ESEER* ambaye ni Gereza la Tarime, Mkoani Mara, Ndugu Chiwanga Chacha. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni viongozi kutoka Bulyanhulu, Mkoani Shinyanga, Ndugu Agapiki Kisoka na Ndugu Baraka Sheemahonge. (*Makof*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ni walimu wa sekondari iliyoongoza kwenye Halmashauri ya Manyoni kidato cha nne mwaka 2021 na viongozi wa Kata ya Nkonko na Watendaji wa Vijiji wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Ndugu Ezekiel Ezekiel. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbozi, Mkoa wa Songwe. (*Makofi*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanatoka Arumeru Magharibi, Mkoani Arusha. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Salim Shaibu Mbuma, mfanyabiashara ni daktari wa magari aina ya Toyota na Ndugu Raymos Alfred Ntubwa mfanyabiashara wa viwanja, nyumba na dalali. (*Makofi*)

Wageni 90 wa Mheshimiwa Condester Sichalwe ambao ni viongozi wa Kanisa la Moravian, Idara ya Umoja wa Wanawake, wakazi wa Mtaa wa Mabibo, Dar es Salaam kutoka Mkoa wa Songwe, karibuni. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni Katibu, Ofisi ya Mbunge Ndugu Charles Kato na mwanamaendeleo Ndugu George Kissinza kutoka Misenyi, Mkoa wa Kagera. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Venant Daud ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer Samweli Hhayuma* ambao ni Wachungaji kutoka Hanang, Mkoa wa Manyara. (*Makofi*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi Chief Dodo ya Mkoa wa Manyara, karibuni. (*Makofi*)

Wanafunzi 70 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari *Shephard Junioriliyopo* Jijini Arusha wakiongozwa na Ndugu Maiko Mvungi. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wote siku ya Jumamosi tarehe 7 Mei, 2022 kuanzia saa nne asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo itahusu Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa kuhuduria semina hiyo muhimu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kutakuwa na semina nyingine tarehe 9 Mei, 2022 saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo itahusu huduma za Bima ya Afya kwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa kuhuduria semina hiyo.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji,
Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 24, 25 na 28 Machi, 2022 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022. (*Makofii*)

Aidha, ninaliomba Bunge lako tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka 2022/2023. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge. Hii ni Wizara muhimu na ni sekta ambayo inahusiana na *private sector*, tusikilize kwa makini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia waja wake baraka na afya tele na hivyo kutuwezesha kuwa pamoja leo kutekeleza wajibu wetu kwa Taifa. Naomba tuungane sote kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutujaza yaliyo mema na kuyapa kibali chake masuala tuliyoyapanga ili yampendeze na yakafanikiwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya nafsi yangu naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Ameonesha utashi mkubwa katika kuvutia uwekezaji kutoka kona zote za dunia kuja kuwekeza ndani ya nchi yetu kwa manufaa ya pande zote mbili. Amekuwa ni zaidi ya mlezi kwa sekta binafsi akitambua mchango wa sekta hii kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Mwenyezi Mungu azidi, kumpa afya njema, hekima na busara ili aendelee kulitumikia Taifa letu kwa matokeo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii pia ikiwa nawasilisha hotuba yangu ya kwanza ya bajeti nikiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuongoza Wizara hii. Hakika ni dhamana kubwa kwangu na nimeipokea kwa moyo mkunjufu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, viongozi na watumishi wenzangu wa Wizara na Taasisi zake nitayatekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia kwa moyo, uwezo, juhudhi na ujuzi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wangu wote kwa kushirikiana na Baraza la Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuchochea maendeleo ya uwekezaji, viwanda na biashara. Pia namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake yenye kutia chachu na hamasa katika kuimarisha Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini. (*Makofii*)

idha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako tukufu tarehe 6 Aprili, 2022. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa mwaka 2022/2023 ambapo Wizara yangu itaizingatia katika utekelezaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu na kuwaleta Watanzania maendeleo. (*Makofii*)

idha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Mudrick Ramadhan Soraga, Waziri wa Uwekezaji, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi pamoa na Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kuliongoza Bunge la Kumi na mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hiyo inadhihirisha namna

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sisi Waheshimiwa Wabunge tulivyo na imani kubwa kwenu katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2022/2023. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa hotuba hii ninayoiwasilisha leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangal, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawaahidi kuwapa ushirikiano unaohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya ujenzi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Wenyevit wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mzuri ambao Wizara na wadau wetu wameendelea kuupata. Niwahakikishie kuwa tutaendelea na kuudumisha ushirikiano huo ili Watanzania wanufaikie na matokeo chanya ya utekelezaji wa majukumu ya kisekta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambazo limekuwa likifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Kupitia kwako naliomba Bunge liendelee kutupatia ushirikiano ili kuendeleza sekta hii ambayo ni msingi mkuu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ujenzi wa uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wote wa Jimbo la Kondo la imani yao kwangu, kwa kunipa moyo na ushirikiano mzuri ulioniwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha pili na pia katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili. (*Makofii*)

Naishukuru pia familia yangu, mume wangu na watoto wangu, ndugu na jamaa kwa dua zao na ushirikiano wao mzuri unaoniwezesha kuwatumikia Watanzania na hususan wawekezaji, wanaviwanda na wafanyabishara bila ya kuchoka. Nawaombeni tuendelee kushikamana ili tufikie malengo tuliyokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi. Kwa uchache, napenda kuwatambua; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania – *TPSF*, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania – *CTI*, Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania – *TCCIA*, Baraza la Kilimo Tanzania, Chama cha Wadau wa Ngozi, Chama cha Wafanyabiashara Wanawake, Vikundi vya Biashara Ndogo na Taasisi nyingine zote kwa michango yao katika kuendeleza uwekezaji, viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia wamiliki na waandishi wa vyombo vyahabari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara, Taasisi na uendelezaji wa sekta zake, kuvutia wawekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Nawaomba tuendeleze ari hiyo kwa lengo la kukuza uelewa kwa umma ili washiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe - Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Naibu Waziri, Profesa Godius Kahyarara - Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil T. Abdallah - Naibu Katibu Mkuu, Viwanda na Biashara, Bw. Ally S. Gugu - Naibu Katibu Mkuu, Uwekezaji, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara yetu. Napenda kuwapongeza sana na kuwasihii kuendeleza moyo huo wa kujituma katika kuwatumikia Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wote waliokumbwa na kadhia ya kuondokewa na wapendwa wao. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa familia na wapiga kura wa Jimbo la Ngorongoro kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa William Tate Olenasha na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Mawaziri wote walionitangulia kuwasilisha na kuitishiwa bajeti zao za mwaka 2022/2023 hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kuwa Mipango na Bajeti zilizowasilishwa zitaendelea kuwa chachu na kuleta ufungamanisho wenyewe tija na sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji ninayoiwasilisha inabainisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, hotuba hii imeainisha hali na mwenendo wa sekta, uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, viwanda na ufanyaji biashara nchini, mchango wa sekta katika ukuaji wa pato wa pato la Taifa, utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2021/2022, changamoto na jithhada za kutua changamoto hizo, malengo na vipaumbele vya sekta kwa mwaka 2022/2023, mwelekeo wa sekta na maombi ya bajeti ya mwaka 2022/2023. (Makofii)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 na malengo ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumbukumbu ya Bunge naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwekezaji Tanzania ina rasilimali nyangi na mfumo wa kitaasisi na kisheria wa kusimamia uwekezaji ambayo inatoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kupitia *T/C* na *EPZA* na Wizara za kisekta. Hivyo uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali hususan katika miundombinu ya umeme, mawasiliano, maji na usafirishaji kwa njia ya barabara, reli na anga ni kichocheo kikubwa kinachotoa fursa zaidi ya ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na uzalishaji nchini. Miradi mingi iliyoasajiliwa italeta fursa nyangi za ajira, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa Serikali kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na hivyo huchangia katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika sekta ya viwanda umeendelea kukua na kumilikiwa kwa sehemu kubwa na sekta binafsi na viwanda vingi vinajishughulisha na uongezaji thamani kwa kutumia malighafi za ndani. Aidha, sehemu kubwa ya viwanda hivyo ni vidogo sana ambavyo ni 62,400, viwanda vidogo ni 17,267, viwanda vya kati ni 684 na vikubwa ni 618. Kutokana na usajili wa viwanda chini ya *T/C* inategemewa kuwa viwanda vipyta vikubwa 500 vitajengwa kufikia mwaka 2025 na kufanya idadi ya sasa ya viwanda vikubwa vinavyoajiri wafanyakazi zaidi ya 500 kuongezeka kutoka 41 hadi 541.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeanza utekelezaji wa Kongani ya Viwanda ya Kwala ambayo uwekezaji wake ni takribani dola za Marekani bilioni tatu ambayo itakuwa na viwanda 200 vikubwa kwa ajili ya kutengeneza nguo, vifaa vya umeme, vifaa vya ujenzi, dawa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na aina nyingine. Awamu ya kwanza itakamilika mwaka 2024 na kutoa ajira za moja kwa moja 100,000 na zisizo za moja kwa moja 300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na sekta binafsi itajenga viwanda katika maeneo maalum ya Nala hapa Dodoma na kongani itakayojengwa katika Mkoa wa Mwanza. Uwekezaji huo utachochaea matumizi ya reli ya kisasa ya *SGR*, bandari za maziwa makuu, bahari pamoja na barabara. Uwekezaji huo utaifanya Tanzania kuwa nguzo ya uchumi ya Bara la na kiunganishi kupitia bahari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda vidogo na vya kati, jitihada zitakuwa katika ujenzi wa viwanda vidogo vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu ili kuzalisha bidhaa ambazo zinaagizwa kwa wingi kutoka nje ilhali zinaweza kutengenezwa hapa nchini. Viwanda vitaanzia katika Kongani ya Dumila, Morogoro na Kitaraka, Singida ikilenga kukuza teknolojia, kuwezesha nchi kujitosheleza kimahitaji kupitia viwanda vidogo ambavyo uwekezaji wake hautumii mitaji mikubwa, kuongeza fursa za masoko ya mazao na kuondoa utegemezi wa bidhaa za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa biashara mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenye soko la China yaliongezekwa kwa asilimia 14.31 na kufikia dola za Marekani milioni 273.1 mwaka 2021 kutokana na uzalishaji na uuza kwa wingi hususan tumbaku, pamba na mbegu za ufuta. Mauzo katika soko la India yaliongezekwa kwa asilimia 90.79 na kufikia dola za Marekani milioni 1,008.7 mwaka 2021 kulikotokana na ongezeko la mauzo ya madini, korosho, mbaazi na maharage ya soya. Mauzo katika soko la Japan yaliongezekwa kwa asilimia 20.97 na kufikia dola za Marekani milioni 67.5 mwaka 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yalipungua kwa asilimia 41.89. Aidha, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2021 yaliongezekwa kwa asilimia 43.73

na kufikia dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 kutokana na ongezeko la mauzo ya chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (*methyl bromide*), saruji na mafuta ya kupaka. Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yalipungua kwa asilimia 10.06 kufikia dola za Marekani milioni 1,311.5 mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini; kumekuwepo upandaji wa bei usioendana na uhalisia katika soko kwa baadhi ya bidhaa hasa zinazoagizwa kutoka nje katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba, 2021 hususan kwenye bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo. Kwa mfano, wastani wa bei ya mondo moja ya milimita 12 imepanda kwa asilimia 31.8 kutoka shilingi 20,393 kipindi cha mwezi Machi, 2021 na kufikia shilingi 26,875 mwezi Machi, 2022. Wastani wa bei ya bati la geji 30 imepanda kwa asilimia 33.3 na kufikia shilingi 27,714 mwezi Machi, 2022 kutoka shilingi 20,786 mwezi Machi, 2021. Wastani wa bei ya rejareja ya saruji kwa mfuko wa kilo 50 imepungua kwa asilimia 1.4 kutoka shilingi 17,662 mwezi Machi, 2021 hadi wastani wa shilingi 17,423 mwezi Machi, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa bei ya mafuta ya kula katika soko la dunia imeendelea kupanda na kufikia mwezi Machi, 2022 wastani wa bei ya mafuta ya alizeti kwa tani moja ilikuwa ni dola za Marekani 1,491.30 na mafuta asili ya mawese ilikuwa dola za Marekani 1,776.96 kutoka dola za Marekani 711.71 na 573.02 kwa tani moja mtawalia kipindi cha mwezi Machi, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za bidhaa mbalimbali za viwandani hususan zile zinazotegemea malighafi kutoka nje au kuagizwa kutoka nje zikiwemo mafuta ya kula, mafuta ya petroli na ngano zitaendelea kuyumba kutokana na athari za UVIKO-19 na vita inayoendelea Urusi na Ukraine na hivyo kuathiri urari wa biashara.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi na mafuta ya kula, kumekuwa pia na ongezeko la bei za mazao ya chakula nchini. Kwa mfano, wastani wa bei ya maharage imepanda kwa asilimia 6.2 kufikia shilingi 188,294 kwa gunia la kilo 100 mwezi Machi, 2022. Wastani wa bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 imeongezeka kwa asilimia 23 na kufikia shilingi 59,861 mwezi Machi, 2022. Wastani wa bei ya mchele kwa gunia la kilo 100 imeongezeka kwa asilimia 33.1 na kufikia shilingi 185,278 mwezi Machi, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uzito wa jambo hili, Serikali kuititia Wizara yangu iliratibu na kufanya tathmini ya kina kuhusu suala hili ili kulitafutua ufumbuzi. Tathmini imeonesha kuwepo kwa visababishi kadhaa vya upandaji wa bei ya bidhaa hizo ikiwa ni pamoja na:-

(i) Uwepo wa janga la UVIKO-19 liliilosababisha chumi nyingi kufungwa kama moja ya njia ya kukabiliana na ugonjwa huu na hivyo kuzuia bidhaa na rasilimali kuhama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine;

(ii) Vitendo vya baadhi ya wasambazaji wa bidhaa sokoni kupandisha bei, kinyume na makubaliano na wazalishaji;

(iii) Kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kunakotokana na ukosefu wa makasha ya kubebea bidhaa duniani;

(iv) Mgogoro kati ya Urusi na Ukraine pia umeonekana kuathiri mwenenedo wa bei ya baadhi ya bidhaa duniani ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi Serikali imeanza kuchukua hatua za muda mfupi na muda mrefu kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kwa kushirikiana na wadau na kutafuta

vyanzo mbadala vya upatikanaji wa bidhaa hizo ili kukidhi mahitaji ndani ya nchi;

(ii) Kuagiza wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha bei za bidhaa walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa bei ya soko;

(iii) Kuuza bidhaa husika kwa kuzingatia gharama halisi za uingizaji, uzalishaji na usambazaji;

(iv) Kuzalisha na kusambaza bidhaa husika kulingana na uwezo wa viwanda uliosimikwa ili kukidhi mahitaji ya soko na ndiyo maana sasa tunaona bei ya saruji ikiwa imeshuka kulingana na ilivyokuwa mwishoni mwa mwaka 2021;

(v) Serikali inawaelekeza wauzaji na wasambazaji wa mbolea zenyе bei elekezi wahakikishe wanazingatia bei zilizopangwa na Serikali na wale wote watakaokiuka watachukuliwa hatua kali za kisheria; na mwisho

(vi) Tume ya Ushindani kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara wa bidhaa muhimu ambazo zimeonesha kuathirika zaidi na upandaji wa bei na kuchukua hatua za kisheria kwa watakobainika kukiuka Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

(vii) Kuendelea kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwenye uzalishaji wa bidhaa ambazo tumekuwa tegemezi kwa kiwango kikubwa kutoka nje ya nchi ikiwa ni pamoja na mafuta ya kula, sukari na ngano. Lengo likiwa ni kuwa na uzalishaji unaotosheleza mahitaji ya soko la ndani na hatimaye kuuza nje kwa sababu fursa ya kuzalisha na kuuza nje tunayo kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo upandaji bei holela usio na msingi wa kufanya hivyo ni jinai na Serikali itachukua hatua. Sheria zipo za kusimamia biashara na kitendo cha kupandisha bei kiholela bila sababu za msingi ni kosa la jinai chini ya kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Ushindani Namba 8 ya mwaka 2003. Kwa mujibu wa kifungu hicho,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupanga bei au kufanya mgomo, kukubaliana katika manunuzi; na kuzuia uzalishaji ni makosa yanayostahili adhabu hiyo. Hivyo, yoyote atakayethibitika kufanya vitendo hivi atachukuliwa hatua kali za kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, viwanda na biashara nchini Wizara inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Viwanda ya mwaka 1996, Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 na Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ya mwaka 2003 ili ziendane na mazingira ya sasa ya uwekezaji na biashara na zipo kwenye hatua mbalimbali za kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sheria Wizara inafanya marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003; Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997; Sheria ya Viwango; Sheria ya Leseni za Biashara na Sheria ya Vipimo. Sambamba na hilo Wizara inaendelea na maandalizi ya kutunga Sheria ya Ahueni ya Athari za Biashara ya mwaka 2022 ili ziendane na hitaji la Serikali la kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imefanya marekebisho ya sheria ya kuratibu ajira za wageni ambapo imekuwa ni malalamiko makubwa kwa wawekezaji wetu na kwa sasa sheria hiyo inaruhusu mwekezaji kuingiza watalaam hadi kumi kwa masharti nafuu kutoka watano ilivyoukuwa kabla ya mwezi Oktoba, 2022 lakini pia na kuondoa sharti la kupata ithibati ya vyeti vya elimu kutoka *TCUna NACTE* kwa wanaoomba vibali vya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, Serikali imeunganisha Mifumo ya Kielektroniki ya Utoaji wa Vibali vya Kazi kwa Wageni na Wawekezaji (*Online Work Permit Application and Issuance System*). Mfumo huo umefungamanishwa na mfumo wa kielektroniki wa maombi

ya vibali vya ukazi ili kupunguza muda wa kusafiri kutoka ofisi moja kwenda ofisi nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na sasa tuone ni upi mchango wa sekta ya viwanda na biashara katika ukuaji wa pato la Taifa letu; mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 0.4. Vilevile kasi ya ukuaji wa sekta ya viwanda ilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2020 kulikotokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya biashara katika pato la Taifa letu kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 0.2.

Vilevile kasi ya ukuaji wa sekta ya biashara ilikuwa asilimia 4 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2020. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa baadhi ya bidhaa zilizouzwa zikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo na bidhaa zilizozalishwa viwandani. Sekta ya biashara imewezesha ongezeko la asilimia sita la mauzo nje ya bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 675.6 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani 6,371.1 kwa mwaka 2020 ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususan bidhaa za viwandani, mazao ya mbogamboga na bidhaa nyinginezo zikijumuisha mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/2022; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambayo kwa mwaka 2020/2021 imeendeshwa kwa Fungu 11, Fungu 44 na Fungu 60 ilikuwa na bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 112.69 hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 55.15 sawa na asilimia 48 ya jumla ya bajeti iliyotengwa. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 4.87 kutoka Fungu 11 sawa na asilimia 69; shilingi 31.82

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoka Fungu 44 sawa na asilimia 39 na shilingi 18.46 kutoka Fungu 60 sawa na asilimia 76 ya bajeti zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa bajeti ya utekelezaji wa mwaka 2021/2022 ni kama unavyoonekana kwenye ukurasa wa 30 hadi 32 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Mpango Wizara kwa kushirikiana na *Trademark East Africa* inatengeneza mfumo wa dirisha moja la kutoa huduma kwa wawekezaji kwa njia ya kielektroniki na kufikia mwezi Machi, 2022, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 90. Katika awamu ya kwanza, mfumo unaunganisha mifumo *NIDA*; Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; *BRELA*; *TRA* na *TIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa kanzidata ya benki ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu uwekezaji katika kongani maalum za viwanda zinazowezesha kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, kuzalisha ajira kwa wingi na kukuza uchumi wa Taifa letu. Uwekezaji huu ni pamoja na Kongani ya Viwanda Mafuta ya Kula ya Alizeti, Kitaraka iliyopo Wilaya Manyoni, Mkoa wa Singida ambapo ekari 45,000 zimepatikana. Katika sekta ndogo ya sukari kuna Kongani ya Sukari eneo la Dakawa Magole, Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro ambapo wawekezaji wadogo wanaotumia mashine zenye uwezo wa kuchakata tani 200 hadi 500 za miwa kwa siku wameanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika eneo la Kwala Mkoa wa Pwani, Kampuni ya *Sino Tan Kibaha Industrial Park Limited* inaendeleza uwekezaji katika kongani lenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo viwanda 400 vinatarajiwा kujengwa na kuwekeza kiasi cha dola za Marekani bilioni tatu, kuzalisha

ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizo za moja kwa moja 300,000 na kuzalisha bidhaa za takriban dola za Marekani bilioni sita kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa eneo maalum la kiuchumi la Mkulazi lenye ukubwa wa hekta 60,103 limepangwa kwa uwekezaji ambapo hekta 28,000 kwa ajili ya kilimo cha miwa na hekta 32,103 kwa ajili ya kilimo cha mazao mengine yakiwemo alizeti, mtama na mpunga. Mradi huo utajumuisha Kanda Maalum za Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Kilimo, Wizara imesaini hati ya makubaliano na Kampuni ya *Syphomy Investment Ltd.* iliyoonesha nia ya uendelezaji wa mradi huo wakati wa Maonesho ya Biashara ya *Expo 2020 Dubai* na tayari kampuni hiyo ipo nchini wameshamaliza upimaji wa ardhi na kuanza uwekezaji mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia inaratibu uendelezaji wa Mradi wa Bandari na Kanda Maalum ya Kiuchumi Bagamoyo (*Bagamoyo Special Economic Zone*). Katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea na majadiliano na wawekezaji wa Kampuni za *China Merchants Holdings International Limited* na *Oman Investment*. Majadiliano hayo yanahusu eneo dogo la mradi wa *Bagamoyo Special Economic Zone* kwa kuendeleza eneo la hekta 3,087 kati ya hekta 9,887 ambapo unahusisha ujenzi wa bandari yaani *sea port* na kituo cha usafirishaji yaani *logistics park* kwenye eneo la hekta 887 na uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (*Portside Industrial City*) kwenye eneo la hekta 2,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa marejeo ya majadiliano hayo ambayo yalisimama mwaka 2018 ni kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza maeneo ambayo ni wajibu wake kama vile ujenzi wa miundombinu wezeshi, barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano na lango la kuingilia bandarini yaani *dredging* kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Uwekezaji katika maeneo ya mradi yatafanywa kwa kuvutia wabia wa sekta ya umma na sekta binafsi au kufanywa ...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri muda wako unakwisha omba maombi yako ya fedha ya mwaka 2022/2023.

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba nimalizie kipande hiki halafu nielekee huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kuhamasisha na kuvutia wawekezaji nchini Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara katika nchi za Ufaransa, Ubelgiji, Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Marekani na hivyo kutoa mchango mkubwa katika kukuza uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo Mheshimiwa Rais aliweka kipaumbele katika kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kueleza jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Ziara hizo zilifanikisha kuandaliwa kwa mikutano baina ya uwekezaji na Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe, kufanyika kwa makongamano ya uwekezaji na kusainiwa kwa hati za makubaliano katika nyanja mbalimbali zilizohusu sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara ya Ufaransa nchi yetu ilifanikiwa kupatikana kwa fedha zitakazoelekeza katika sekta za uchukuzi, sekta ya kilimo, uchumi wa bluu na wafanyabiashara wadogo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 wawekezaji 11 kutoka Ufaransa na wawekezaji sita kutoka Ubelgiji tayari walishafika nchini na kuanza majadiliano ya uwekezaji huo.

Vilevile kuanzia tarehe 3 hadi 6 Mei, 2022 wawekezaji kutoka makapuni 35 kutoka nchini Norway na Uingereza wako nchini kwetu katika *mission* ya uwekezaji wakikutana na viongozi mbalimbali wa Serikali na sekta binafsi kwa ajili ya kutafuta fursa za uwekezaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika ziara ya Umoja wa Falme za Kiarabu jumla ya hati za makubaliano 37 zenye thamani ya dola za Marekani billioni nane sana na shilingi triliioni 18.5 zilisainiwa. Miradi hiyo itazalisha ajira 204,575 katika maeneo ya kilimo, mafuta na gesi, usafirishaji na miundombinu pamoja na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ziara ya Marekani ambayo ilijumuisha uzinduzi wa *Royal Tourism* wezesha kuna hadifursa za uwekezaji nchini na kufanikiwa kuvutia uwekezaji wa dola za Marekani triliioni 11.7 katika sekta za kilimo, utalii, biashara, nishati na uchukuzi zitakazozalisha ajira 301,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye anafanya jitihada kubwa za kuvutia uwekezaji kama sehemu moja ya kukuza uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika maombi ya fedha na malengo tuliyopanga kutekeleza kama Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 vipaumbele vikuu vya Wizara ni hivi vifuatavyo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kipaumbele iliyopo katika Mpango na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020/2025;

(ii) Uwekezaji katika Kongani na maendelezo kwenye *Special Economic Zone, Economic Processing Zone*, Kongani za Viwanda mfano Kongani ya Kwala na Kitaraka pamoja na ya Nala Dodoma;

(iii) Usimamizi na udhibiti wa masoko;

(iv) Ushiriki katika shughuli za Kikanda pamoja na za Kimataifa;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(v) Kuondoa urasimu katika kuhudumia wawekezaji na wafanyabiashara; na

(vi) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi moja kwa moja katika uchumi na uwezeshaji wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liridhie na kuitisha makadirio ya shilingi 99,105,506,000 katika Fungu 44 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa mchanganuo ufuatao: -

(i) Shilingi 68,308,687,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati ya fedha hizo zinajumuisha shilingi 8,728,788,000 ni za matumizi mengineyo na shilingi 59,579,899,000 ni kwa ajili ya mishahara.

(ii) Shilingi 30,796,819,000 ni za matumizi ya maendeleo kati ya fedha hizo shilingi 30,346,819,000 ni fedha za ndani na shilingi 450,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote na hasa wazalendo wa nchi hii kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara. Katika kipindi kilicho mbele yetu, tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ni jukumu kubwa ambalo linapaswa kuendelea kuungwa mkono na wapenda maendeleo wote na hasa Watanzania na wazalendo wote. Tunahitaji kila Mtanzania popote alipo kutimiza wajibu wake, kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na kuendeleza uwekezaji, viwanda na biashara kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge

kwa kunisikiliza. Hotuba hii pamoja na vielelezo vyote inapatika katika tovuti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ASHATU K. KIJAJI (MB.),
WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 24, 25 na 28 Machi, 2022, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2022/2023.

2. Mheshimiwa Spika, Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia waja wake baraka na afya tele na hivyo kutuwezesha kuwa pamoja leo kutekeleza wajibu wetu kwa Taifa. Naomba tuungane sote kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutujaza yaliyo mema na kuyapa kibali chake masuala tuliyoyapanga ili yampendeze na yafanikiwe.

3. Mheshimiwa Spika, Napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Mwenyezi Mungu azidi, kumpa afya njema, hekima na busara. Aidha, nitumie

fursa hii pia ikiwa nawasilisha Hotuba yangu ya kwanza ya Bajeti nikiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuongoza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Hakika ni dhamana kubwa kwangu na nimeipokea kwa moyo mkunjufu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, Viongozi na Watumishi wa Wizara na Taasisi zake nitayatekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia kwa moyo, uwezo, juhudni ujuzi wangu wote kwa kushirikiana na Baraza la Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote.

4. Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuchochlea maendeleo ya uwekezaji, viwanda na biashara. Pia, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake yenye kutia chachu na hamasa katika kuimarisha Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 6 Aprili, 2022. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Mwaka 2022/2023 ambapo Wizara yangu itaizingatia katika utekelezaji wake.

5. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuendelea kuelekeza na kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu na kuwaletaa Watanzania maendeleo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ) na

Mheshimiwa Mudrick Soraga, Waziri wa Uwekezaji (SMZ) kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

6. Mheshimiwa Spika, Ninapenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kuliongoza Bunge la Kumi na Mbili (12) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hiyo inadhihirisha namna Waheshimiwa Wabunge walivyo na imani kubwa kwenu katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

7. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nichukue fursa hii kumpongeza, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawaahidi kuwapa ushirikiano unaohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya ujenzi wa Taifa letu.

8. Mheshimiwa Spika, Niwapongeze pia Wenyevitii wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mzuri ambao Wizara na wadau wetu wameendelea kupata. Niwahakikishie kuwa tutaendeleza na kuendumisha ushirikiano huo ili Watanzania wanufaikie na matokeo chanya ya utekelezaji wa majukumu ya kisekta.

9. Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wote wa Jimbo la Kondoa kwa imani yao kwangu, kwa kunipa moyo na ushirikiano mzuri ulioniwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge wao na pia katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili. Naishukuru pia familia yangu, ndugu na jamaa kwa dua zao na ushirikiano wao mzuri unaoniwezesha kuwatumikia Watanzania na hususan wawekezaji, wanaviwanda na wafanyabishara bila ya kuchoka. Nawaombeni tuendelee kushikamana ili tufikie malengo tuliyokusudia.

10. Mheshimiwa Spika, Ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa Sekta Binafsi. Kwa uchache, napenda kuwatambua: Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania -TPSF; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - CTI; Chama cha Wafanyablashara, Viwanda na Kilimo Tanzania - TCCIA; Baraza la Kilimo Tanzania - ACT; Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania – L A T ; Chama cha Wafanyabiashara Wanawake – TWCC; na Vikundi vya Biashara Ndogo (VIBINDO) kwa michango yao katika kuendeleza uwekezaji, viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo.

11. Mheshimiwa Spika, Nawashukuru pia wamiliki na waandishi wa vyombo nya habari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara, taasisi na uendelezaji wa Sekta zake, kuvutia wawekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Nawaomba tuendeleze ari hiyo kwa lengo la kukuza uelewa kwa umma ili washiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata.

12. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Mheshimiwa Exaud S. Kigahe - Mbunge wa Mufindi Kaskazini Naibu Waziri; Prof. Godius W. Kahyarara, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Dkt. Islam S. Salum, Katibu Mkuu wa

Biahsara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ); Dkt. Habiba Hassan Omar, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji (SMZ); Dkt. Hashil T. Abdallah, Naibu Katibu Mkuu - Viwanda na Biashara; Bw. Ally S. Gugu, Naibu Katibu Mkuu - Uwekezaji, Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kuwapongeza sana na kuwasihii kuendeleza moyo huo wa kujituma katika kuwatumikia Watanzania. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

13. Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali katika kuendeleza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Hivyo, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote wakiwemo Washirika wetu wa Maendeleo (Development Partners) na pia wadau wa ndani.

14. Mheshimiwa Spika, Ninapenda kuungana na Viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wote waliokumbwa na kadhia ya kuondokewa na wependwa wao. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa familia na wapiga kura wa Jimbo la Ngorongoro kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa William Tate Olenasha na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum Rukwa. Aidha, nawapa pole wananchi mbalimbali waliokumbwa na kadhia ya mafuriko na ajali nichini katika Mwaka huu na kusababisha majeruhi, ulemavu na uharibifu mkubwa wa mali. Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa ahueni waathirika wote ili warejee katika hali njema na hivyo kuendelea kulijenga Taifa letu.

15. Mheshimiwa Spika, Ninawapongeza Mawaziri wote walionitangulia kuwasilisha na kupitishiwa Bajeti zao za Mwaka 2022/2023 hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kuwa mipango na bajeti zilizopitishwa zitaendelea kuwa chachu na kuleta ufungamanisho wenye tija na Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

16. Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji ninayoiwasilisha inabainisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, Hotuba hii imeainisha Hali na Mwenendo wa Sekta; Uboreshaji wa Mazingira ya uwekezaji, viwanda na ufanyaji biashara nchini; Mchango wa Sekta; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti 2021/2022; Changamoto na jitihada za kutatua changamoto hizo; Malengo na Vipaumbele vya Sekta kwa Mwaka 2022/2023; Mwelekeo wa Sekta; na Maombi ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

17. Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 na Malengo ya Mwaka 2022/2023.

2. HALI NA MWENENDO WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

2.1 Uwekezaji

18. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni eneo la kimkakati kijirografia na lenye rasilimali nyingi zenyet kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi zikiwemo viwanda, madini, utalii, kilimo na biashara. Uwekezaji huo ambao hufanywa kwa kiwango kikubwa na Sekta Binafsi umechochewa na uwepo wa mazingira rafiki ya uwekezaji na mfumo wa kitaasisi na kisheria wa kusimamia uwekezaji nchini. Mifumo hiyo, pamoja na mambo mengine, inatoa vivutio vya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuititia TIC, EPZA na Wizara za kisekta. Sheria ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ/EPZ) ya Mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017, Tanzania imeendelea kuvutia na kuchochea uwekezaji wa ndani na mitaji kutoka nje (Foreign Direct Investment - FDI).

19. Mheshimiwa Spika, Serikali imejielekeza katika uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya msingi na saidizi

ikiwemo ya umeme, mawasiliano, maji na usafirishaji kwa njia ya barabara, maji, reli na anga ambayo ni kichocheo kikubwa cha uwekezaji. Vilevile, maboresho ya mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kuititia utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini unatoa fursa zaidi kwa ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za uzalishaji nchini. Kutokana na jitihada mbalimbali, Tanzania imeweza kusajili na kuvutia uwekezaji mkubwa zaidi katika sekta mbalimbali za kiuchumi ambaou utaleta fursa nydingi za ajira, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa Serikali, kuongezeka kipato cha mtu mmoja mmoja na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini.

2.2 Uwekezaji katika Viwanda

20. *Mheshimiwa Spika*, Uwekezaji katika Sekta ya Viwanda umeendelea kukua na kumilikiwa kwa sehemu kubwa na Sekta Binafsi. Uwekezaji huo wa viwanda uko katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ na SEZ) na maeneo binafsi. Viwanda vimesambaa nchi nzima na sehemu kubwa ya viwanda hivyo ni vidogo sana ambavyo ni 62,400 sawa na asilimia 77.07, wakati vidogo ni 17,267 sawa na asilimia 21.33, vya kati ni 684 sawa na asilimia 0.84 na vikubwa ni 618 sawa na asilimia 0.76. Kati ya Viwanda Vikubwa 618 (Vinavyoajiri kuanzia watu 100), Viwanda 41 pekee vinaajiri zaidi ya watu 500. Viwanda vingi vinajishughulisha na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo na vinajielekeza katika kutumia malighafi za ndani kuzalisha bidhaa hizo.

21. *Mheshimiwa Spika*, Kutokana na usajili wa viwanda chini ya TIC na EPZA, inategemewa kuwa viwanda vipyta vikubwa 500 vitajengwa kufikia mwaka 2025 na kufanya idadi ya sasa ya viwanda vikubwa vinavyoajiri wafanyakazi zaidi ya 500 kuongezeka kutoka 41 hadi kufikia 541. Tayari Serikali ya Awamu ya Sita imekwishaanza utekelezaji wa Kongani kubwa ya Viwanda ya Kwala ambayo itakuwa na viwanda 200 vikubwa kwa ajili ya kutengeneza nguo, vifaa vya umeme, vifaa vya ujenzi, dawa na aina nydingine. Mradi huo umekwishaanza na awamu ya kwanza itakamilika ifikapo mwaka 2024 na viwanda vitatoa ajira

za moja kwa moja 100,000 na zisizo za moja kwa moja 300,000. Aidha, uwekezaji katika eneo hilo unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani Bilioni 3 na unalenga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha bidhaa za viwanda katika Soko la Pamoja la Afrika.

22. Mheshimiwa Spika, Viwanda vingine vitatokana na uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Nala - Dodoma ambapo tayari Serikali imeanzisha Eneo Maalum la Uwekezaji, pamoja na kongani nyingine kubwa itakayojengwa katika Mkoa wa Mwanza. Uwekezaji huo utafanywa na Serikali ikishirikiana na Sekta Binafsi. Ni matarajio yetu kuwa, uwekezaji huo utachochea matumizi ya kiuchumi ya miundombinu ya ndani ya nchi hasa Reli ya Kisasa ya SGR, Bandari za Maziwa Makuu, Bahari pamoja na barabara. Matokeo makubwa yanatarajiwa kupatikana katika kuongeza wigo wa kodi, kukuza teknolojia na kwa Taifa letu kujitosheleza kwa bidhaa ambazo zimekuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi.
Aidha, uwekezaji huo utaifanya Tanzania kuwa nguzo ya uchumi ya Bara la Afrika (Africa Economic Power House) ikitumia fursa yake iliyopewa na Mwenyezi Mungu ya kuwa kiunganishi kupitia Bahari - *GateWay*.

23. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Viwanda Vidogo na vya Kati, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau kuendeleza mkakati wake wa ujenzi wa viwanda vidogo vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu ili kuzalisha bidhaa ambazo zinaagizwa kwa wingi kutoka nje ilhali zinaweza kutengenezwa hapa nchini. Bidhaa hizo ni pamoja na *toothpicks*, *cotton-buds*, sukari, mafuta ya kula, *tomato source* na nyinginezo. Viwanda hivyo vitatengewa Kongani maalum na kwa kuanzia kuna Kongani ya Dumila - Morogoro na Kitaraka - Singida. Utekelezaji wa miradi hiyo unafanywa kwa pamoja baina ya Sekta Binafsi na Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) na Mpango wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo chini ya NSSF, Benki ya Azania na SIDO. Matokeo ya Mpango huo ni kukuza teknolojia, kuwezesha nchi kujitosheleza kimahitaji kupitia viwanda vidogo ambavyo

uwekezaji wake hautumii mitaji mikubwa, kuongeza fursa za masoko ya mazao na kuondoa utegemezi wa bidhaa za nje ambazo zinaweza kuzalishwa nchini.

2.3 Biashara

24. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina fursa mbalimbali za masoko ya kuuza mazao na bidhaa inayozalisha. Uwezo wa nchi kuuza nje mazao na bidhaa unaongezeka na hususan uuzaaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi umeongezeka na hivyo kuchochaea kupunguza uagizaji nje wa baadhi ya bidhaa na malighafi na hivyo kuiwezesha nchi kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Pamoja na kuwepo kwa uagizaji wa bidhaa za mwisho (final products), kumekuwa na ongezeko la uagizaji nje wa bidhaa za kati na za mitaji (intermediate input and capital goods) zinazotokana na mahitaji ya viwanda vinavyowekeza hapa nchini.

25. *Mheshimiwa Spika*, Kutokana na athari za UVIKO-19 na vita inayoendelea kati ya nchi ya Urusi na Ukraine, ugavi wa mazao na bidhaa unaendelea kuathiri bei za bidhaa mbalimbali za viwandani hususan zile zinazotegemea malighafi kutoka nje au kuagizwa kutoka nje zikiwemo mafuta ya kula, mafuta ya petroli na ngano. Hii inatokana na utegemezi wa biashara ya malighafi na bidhaa hizo ambazo uzalishaji na usambazaji wake unaguswa na uchumi wa Urusi na Ukraine. Hali hiyo itaathiri urari wa biashara kutokana na kuyumba kwa biashara katika masoko hayo ikiwianishwa na uwezo wa kulipia bidhaa kutoka nje.

26. *Mheshimiwa Spika*, Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imechukua hatua zenye matokeo ya muda mfupi na muda mrefu. Kwa upande wa masuala ya mafuta ya kula ya alizeti, katika Mkataba wa Makubaliano (MoU) ya uwekezaji yaliyofikiwa mwaka 2022 huko Marekani, kuna Mkataba wa Mradi wa kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula (Kitaraka – Manyoni) ambao utachochaea jitihada za

Serikali kuhakikisha kuwa inaimarisha uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo tunategemea soko la nje. Pia kuna Mkataba wa mradhi unaolenga kuongeza uzalishaji wa ngano. Aidha, Waziri Mkuu aliagiza TARI kugawa miche ya kisasa ya michikichi huko Kigoma ili kuongeza uzalishaji wake. Vilevile, mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu ni mikoa ya kimkakati ya kuzalisha alizeti ili kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula nchini. Jitihada hizo pia zinachochewa na Mradi wa Kuwajengea Uwezo Wazalishaji na Wachakataji Wadogo na wa Kati walio kwenye Mnyororo wa Thamani (Strengthening MSMES Capacity to Improve Competitiveness in Domestic, Regional and International Markets for Selected Value Chains Project - EIF Tier 2) wa zao la Chikichi ili waweze kuyafikia Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa. Pia, Wizara kuitia SIDO itajenga Viwanda Viwili (2) vidogo vya kuzalisha mafuta ya Mawese katika Kijiji cha Nyamuhoza kilichoko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma (DC) na Kijiji cha Sunura kilichoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Ujiji. Vilevile, Wizara kuitia SIDO ilitoa mafunzo ya Kilimo Biashara (Farming as a Business) kwa vikundi 50 vya wanawake na vijana wa vijiji vya Nyamuhoza na Sunura ambapo Viwanda viwili (2) Vidogo vitajengwa katika maeneo hayo.

27. Mheshimiwa Spika, Mauzo ya bidhaa kwenye soko la China yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 238.9 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani Milioni 273.1 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 14.31. Ongezeko hilo linatokana na uzalishaji na uuzaji kwa wingi mbegu za ufuta. Bidhaa zingine zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na tumbaku, pamba, jute, manila (coconut, abaca) na nguo na mavazi. Manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,940.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 2,696.2 mwaka 2021, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 38.94 (**Jedwali Na. 1**).

28. Mheshimiwa Spika, Mauzo katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 528.7 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani Milioni 1,008.7 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 90.79. Ongezeko hilo lilitokana

na mauzo ya bidhaa mbalimbali zikiwemo Madini, Korosho, MBAazi na Maharage ya Soya. Aidha, Manunuzi ya Tanzania kutoka India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 1,940.3 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani Milioni 2,696.2 mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 38.96 (**Jedwali Na. 2**).

29. Mheshimiwa Spika, Mauzo katika soko la Japan yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 55.8 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani Milioni 67.5 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 20.97. Manunuzi ya bidhaa kutoka Japan yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani Milioni 338.4 mwaka 2020 ikilinganiswa na Dola za Marekani Milioni 469 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 38.59. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni zile zinazotumika kwenye uzalishaji viwandani kama vile mashine, mitambo na kemikali (**Jedwali Na. 3**).

30. Mheshimiwa Spika, Bidhaa zilizonunuliwa na Tanzania kutoka Jumuiya ya Ulaya ziliikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 1,072 mwaka 2020 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,003.7 kwa mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 6.37. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na; vifaa vya mitambo, mashine mbalimbali, vipuri vya magari, magari, nguo, vyombo vya majini (marine vessels), gesi na mafuta, vifaa vya madawa (medical apparatus), paper board, fittings, gas tubes, mineral/chemical fertilizers, data processing machines, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya uchunguzi wa kimaabara. Pia, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 1,475. kwa mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 857.1 mwaka 2021, ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 41.89. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni bidhaa za tumbaku, madini, kahawa, maharage ya soya, alizeti, pamba na maua (**Jedwali Na. 4**).

31. Mheshimiwa Spika, Mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2021 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,161.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani

Milioni 807.9 mwaka 2020 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 43.73. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na mbogamboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Kwa upande mwingine, uagizaji wa Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo uliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 324.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 523.4 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 61.39. Kutokana na hali hiyo, urari wa biashara ni chanya kwa Dola za Marekani Milioni 637.8 (**Jedwali Na. 5**).

32. Mheshimiwa Spika, Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, mwaka 2020 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,458.3 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1,311.5 mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 10.06. Uagizaji wa Tanzania kutoka katika soko hilo ulipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 492.4 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani Milioni 232.5 mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 52.78 (**Jedwali Na. 6**).

2.4 Mwenendo wa Bei za Bidhaa Muhimu Nchini

33. Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa kupanda bei kusikoendana na uhalisia wa soko ni kati ya changamoto zinazokabili sekta yetu ya biashara. Licha ya kuwepo sababu za msingi za kupanda kwa bei kwa baadhi ya bidhaa hasa zinazoagizwa kutoka nje, katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba, 2021, kulikuwa na taarifa za uhaba na upandaji wa bei usioendana na uhalisia wa soko kwenye bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo. Kwa upande wa vifaa vya ujenzi, wastani wa bei ya Nondo moja ya mm 12 imepanda kutoka Shilingi 20,393 kipindi cha mwezi Machi, 2021 na kufikia

Shilingi 26,875 mwezi Machi, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 31.8; Nondo moja ya mm 16 imepanda kutoka Shilingi 36,036 na kufikia Shilingi 46,607 sawa na ongezeko la bei la asilimia 29.3; Nondo moja ya mm10 imepanda kutoka Shilingi 15,857 na kufikia Shilingi 19,157 sawa na ongezeko la asilimia 20.8. Vilevile, bei ya Nondo moja ya mm 8 imepanda kutoka Shilingi 12,161 na kufikia Shilingi 15,750 sawa na ongezeko la bei la asilimia 29.5 (**Jedwali Na. 7**).

34. Mheshimiwa Spika, Wastani wa bei ya Bati la geji 30 imepanda kufikia Shilingi 27,714 mwezi Machi 2022, kutoka Shilingi 20,786 mwezi Machi, 2021, sawa na ongezeko la asilimia 33.3; Bei ya Bati la geji 32 imepanda kwa asilimia 15.5 na kufikia Shilingi 18,679 kutoka bei ya Shilingi 16,179 mwezi Machi, 2021; na Bati la geji 28 imepanda kufikia wastani wa Shilingi 37,500, sawa na ongezeko la bei la asilimia 36.2 kutoka Shilingi 27,536. Aidha, Wastani wa bei ya rejareja ya Saruji kwa mfuko wa kilo 50 ni Shilingi 18,283, sawa na ongezeko la bei kwa asilimia 3.5 ukilinganisha na wastani wa bei ya Shilingi 17,662 ya mwezi Machi, 2021 (**Jedwali Na. 8-10**).

35. Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla wake bei za vifaa vya ujenzi ikiwemo mabati na nondo zimeendelea kuwa juu kutokana na kuongezeka kwa bei za malighafi za vifaa vya ujenzi katika soko la dunia. Tathmini iliyofanyika ilibaini kuwa upandaji wa bei ya saruji unatokana na uhaba unaosababishwa na mahitaji makubwa ya saruji katika miradi ya kitaifa; usambazaji hafifu wa bidhaa hiyo kuwafikia watumiaji wa mwisho na ucheleweshaji wa upatikanaji wa saruji kutoka kiwandani. Wizara imeendelea kukusanya taarifa za bidhaa sokoni ikiwa ni pamoja na bei za mazao makuu ya chakula na mafuta ya kula katika masoko mbalimbali hapa nchini ili kuwafahamisha wananchi na wadau wengine kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali.

36. Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa bei ya mafuta ya kula katika soko la dunia imeendelea kupanda kutokana

na Janga la UVIKO -19 na athari ya vita ya Urusi na Ukraine ambapo kufikia mwezi Machi, 2022 wastani wa bei ya mafuta ya alizeti kwa tani moja ilikuwa ni Dola za Marekani 1,491.30 na mafuta asili ya mawese ilikuwa Dola za Marekani 1,776.96 kutoka Dola za Marekani 711.71 na 573.02 kwa tani moja mtawalia kipindi cha mwezi Machi, 2019, sawa na ongezeko la asilimia 149.67 (**Jedwali Na. 11**).

37. Mheshimiwa Spika, Sambamba na kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi, kumekuwa pia na ongezeko la bei za mazao ya chakula Nchini. Wastani wa bei ya Maharage imepanda kutoka Shilingi 177,340 kwa gunia la kilo 100 kwa mwezi Machi, 2021 hadi Shilingi 188,294 Mwezi Machi, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Wastani wa bei ya Mahindi kwa gunia la kilo 100 imeongezeka kutoka Shilingi 48,341 Mwezi Machi, 2021 hadi 59,861 Mwezi Machi, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 23. Vilevile, wastani wa bei ya Mchele imeongezeka kutoka Shilingi 139,212 mwezi Machi, 2021 hadi Shilingi 185,278 mwezi Machi, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 33.1 (**Jedwali Na. 12**).

38. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia unyeti wa suala hilo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiagiza Wizara yangu kuratibu na kufanya tathmini ya kina ya suala hilo ili kulitafutia ufumbuzi. Kwa kuzingatia tathmini iliyofanywa, hatua zifuatazo zinachukuliwa katika kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa muhimu:-

i. Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu hususan zile zilizoonekana kuathiriwa na UVIKO-19 sambamba na vita kati ya Ukraine na Urusi. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutafuta vyanzo mbadala vya upatikanaji wa bidhaa hizo ili kukidhi mahitaji;

ii. Serikali imeendelea kuwaagiza wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha mara moja bei

za bidhaa walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa bei ya soko;

iii. Serikali inawaelekeza wazalishaji na wafanyabiashara wa bidhaa muhimu kuuza bidhaa husika kwa kuzingatia gharama halisi za uingizaji, uzalishaji na usambazaji;

iv. Serikali inawaelekeza wazalishaji wa bidhaa muhimu kuzalisha na kusambaza bidhaa husika kulingana na uwezo wa viwanda uliosimikwa ili kukidhi mahitaji ya soko;

v. Serikali inawaelekeza wauzaji na wasambazaji wa mbolea zenyе bei elekezi wahakikishe wanazingatia bei zilizopangwa na Serikali na wale wote watakaokiuka watachukuliwa hatua kali za kisheria, ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni za biashara; na

vi. Tume ya Ushindani (FCC) inaelekezwa ifuatilie kwa karibu mwenendo wa biashara wa bidhaa muhimu ambazo katika tathmini iliyofanyika zimeonesha kuathirika zaidi na upandaji wa bei na kuchukua hatua za kisheria kwa watakaobainika kukiuka Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003.

vii. Serikali imeendelea kushawishi na kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje kwenye uzalishaji wa mazao ambayo tumekuwa tegemezi kwa kiwango kikubwa kutoka nje ya nchi ikiwa ni pamoja na mafuta ya kula, sukari na ngano. Lengo likiwa ni kupata uzalishaji unaotosheleza mahitaji ya soko letu la ndani na hatimaye kuuza nje kwa sababu hiyo tunayo kama Taifa.

39. Mheshimiwa Spika, Upandaji bei holela ambao kamwe haukulaliki, ni jinai na Serikali itachukua hatua. Sheria zipo za kusimamia biashara na kitendo cha kupandisha bei kiholela bila sababu za msingi ni kosa la jinai chini ya Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Ushindani Na. 8 ya 2003 (Fair Competition Act, No.8 of 2003 Kwa mujibu wa Kifungu hicho, makubaliano ambayo malengo au matokeo tarajiwa ni washindani: kupanga bei; kufanya mgomo;

kukubaliana katika manunuzi; na kuzuia uzalishaji ni makosa yanayostahili adhabu hiyo. Hivyo, kwa maeneo ambayo wafanyabiashara hawana sababu ya kupandisha bei, tutatumia sheria na kanuni zilizopo kudhibiti mwenendo batili wa bei.

40. *Mheshimiwa Spika*, Ninapenda kusitiza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kote nchini kuwasimamia ipasavyo Maafisa Biashara kwenye maeneo yao ili watekeleze wajibu wao wa kufuatilia mwenendo wa bei za bidhaa muhimu na kuwasilisha taarifa hizo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa wakati.

3. UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

3.1 Sera

41. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini, Wizara inafanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali inayozisimamia na zipo kwenye hatua mbalimbali za kukamilishwa. Sera zinazofanyiwa mapitio ni Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Viwanda (1996-2020), Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003), Sera ya Taifa ya Biashara (2003) na Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (2003). Sera hizo zinafanyiwa mapitio ili ziendane na mazingira ya sasa ya uwekezaji na biashara ikiwa ni pamoja na kujumuisha vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Zoezi hilo la kuititia Sera litasaidia kukidhi mahitaji yanayotokana na mabadiliko mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi na kiteknolojia.

3.2 Sheria

42. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inafanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuweka mazingira rafiki katika uwekezaji, viwanda na biashara. Kwa sasa, Wizara

inaendelea kufanya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003; Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997; Sheria ya Viwango ya Mwaka 2009; Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208; na Sheria ya Vipimo Sura na 340 na mapitio yake ya mwaka 2002. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea na maandalizi ya Kutunga Sheria ya Ahueni ya Athari za Biashara ya Mwaka 2022 (Trade Remedies Act, 2022). Lengo la Marekebisho hayo ni kufanya kazi upungufu uliopo katika Sheria hizo ili ziendane na hitaji la Serikali la kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini.

43. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imekamilisha marekebisho ya Sheria tatu (3) zinazosimamiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Sheria hizo ni: Sheria ya Makampuni, Sura 212; Sheria ya Majina ya Biashara, Sura 213; na Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura 326. Marekebisho yake yamefanyika na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.3 ya Mwaka 2021 iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 11 Oktoba, 2021. Lengo la Marekebisho hayo ni kuweka mazingira mazuri na wezeshi ya ufanyaji wa biashara nchini.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imefanya marekebisho ya Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na.1 ya Mwaka 2015 ambapo kwa sasa Sheria hiyo inaruhusu Mwekezaji kuingiza Wataalam hadi 10 kwa masharti nafuu kutoka watano (5) ilivyokuwa kabla ya Mwezi Oktoba, 2021 na kuondoa sharti la kupata ithibati ya vyeti vya elimu kutoka TCU na NACTE kwa wanaoomba vibali vya kazi. Halikadhalika, Serikali imeunganisha Mifumo ya Kielektroniki ya Utoaji wa Vibali vya Kazi kwa Wageni na Wawekezaji (Online Work Permit Application and Issuance System-OWAIS). Mfumo huo umepunguza muda wa kushughulikia maombi ya Vibali vya Kazi kutoka siku za kazi 14 hadi saba (7) na kupunguza hatua za uchakataji wa

kibali kutoka hatua 33 hadi saba (7). Pia, Mfumo huo umefungamanishwa (integrated) na Mfumo wa Kielektroniki wa Maombi ya Vibali vya Ukaazi (Online System for Application of Residence Permit - e-Permit).

3.3 Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini

45. Mheshimiwa Spika; Katika jitihada za kuweka mazingira rafiki na wezeshi ya kufanya uwekezaji na biashara nchini. Maboresho ya mazingira ya uwekezaji na biashara yamejikita katika kupunguza gharama, muda na taratibu za kufanya biashara nchini. Utekelezaji wa maboresho hayo yanajumuisha: Kufanya marejeo ya Sheria, Kanuni na Taratibu, Leseni, Tozo na Faini; Kuimarissha utoaji wa huduma za leseni na vibali na malipo kwa njia ya mtandao; Kuondoa baadhi ya tozo, faini na gharama za leseni na vibali; Kuondoa muingiliano wa majukumu kwenye baadhi ya mamlaka za udhibiti; Kuimarissha mifumo ya ukaguzi; na Kuanzisha na kuimarissha Vituo vya Pamoja vya Kutoa Huduma (OSBC). Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini. Wizara imeandaa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara ambao unatekelezwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali nchini chini ya uratibu wa Wizara yangu. Kutokana na utekelezaji wa Mpango huo, Serikali imewezesha kufutwa kwa tozo kero na faini na kuunganisha majukumu yanayofanana katika mamlaka za udhibiti ili kupunguza gharama za kufanya biashara nchini.

46. Mheshimiwa Spika; Tayari maboresho hayo yameanza kuonesha matokeo chanya katika kuchochera uwekezaji na biashara katika Sekta Binafsi. Ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ambayo yatachochea na kuongeza kasi ya uwekezaji nchini.

4 MCHANGO WA SEKTA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

47. *Mheshimiwa Spika*, Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 0.4 (*Jedwali Na. 13*). Vilevile, Kasi ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda ilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2020 (*Jedwali Na. 14*). Ongezeko hilo la ukuaji lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani kama vile uzalishaji wa biskuti na tambi uliongezeka kwa asilimia 35.5 kila moja, rangi (asilimia 33.9), nguo (asilimia 23.2), chibuku (asilimia 7.2), dawa za pareto (asilimia 6.5), bati (asilimia 6.1), chuma (asilimia 4.9), kamba za katani (asilimia 4.8), nyavi za uvuvi (asilimia 4.6) na saruji (asilimia 0.5) Kwa upande mwingine, Sekta ya Viwanda imetoa ajira 345,615 mwaka 2021 ikilinganishwa na ajira 370,485 mwaka 2020 (*Jedwali Na. 15*).

48. *Mheshimiwa Spika*, Mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Vilevile, Kasi ya Ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa asilimia 4.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2020. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa zikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo na bidhaa zilizozalishwa viwandani. Sekta ya Biashara imewezesha uuzaji nje wa bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani 6,755.6 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na Dola za Marekani 6,371.7 kwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia sita (6) Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususan bidhaa za viwandani, mazao ya mbogamboga na bidhaa nyinginezo zikijumuisha mahindi na mpunga.

5 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA 2021/2022

5.1 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022

5.1.1 Bajeti iliyoidhinishwa na Fedha iliyopokelewa kwa Mwaka 2021/2022

49. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara mpya ambayo imeundwa kwa Tamko la Serikali Namba 384 la mwaka 2022. Kwa Mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara inaendeshwa kwa Bajeti za Fungu 11, 44 na 60 zilizopitishwa mwaka 2021/2022 chini ya iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji (Fungu 11); na iliyokuwa Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44 na 60). Jumla ya Shilingi 112,688,672,000.00 ziliidhinishwa kutumiwa katika mafungu hayo ambapo Fungu 11 ni Shilingi 7,018,213,000.00; Fungu 44 ni Shilingi 81,398,833,000.00; na Fungu 60 ni Shilingi 24,271,626,000.00.

50. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, Wizara ilikuwa haijakusanya maduhuli yoyote ikilinganishwa na lengo la kukusanya Shilingi 15,000,000. Pia, katika kipindi hicho, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 55,157,194,610.17 sawa na asilimia 48 ya jumla ya Bajeti iliyotengwa. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 4,872,606,782.92 kutoka Fungu 11 (sawa na asilimia 69); Shilingi 31,821,858,869.34 kutoka Fungu 44 (sawa na asilimia 39) na Shilingi 18,462,728,957.91 kutoka Fungu 60 (sawa na asilimia 76) ya Bajeti zilizotengwa.

5.1.2 Fedha za Matumizi ya Kawaida

51. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 11 ilitengewa jumla ya Shilingi 7,018,213,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, Shilingi 3,229,915,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 3,818,298,000.00 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022, Wizara ilikuwa

imepokea jumla ya Shilingi 2,310,164,437.38 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na asilimia 71 ya fedha zilizotengwa na Shilingi 2,562,442,345.54 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 67 ya fedha iliyotengwa. Katika Mwaka 2021/2022, Wizara katika Fungu 44 ilitengewa jumla ya Shilingi 28,310,947,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

52. Mheshimiwa Spika, Kati yahizo, Shilingi 5,119,373,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 23,191,574,000 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 4,308,198,554.12 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na asilimia 84 ya fedha zilizotengwa na Shilingi 17,028,147,001.51 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 73 ya fedha iliyotengwa. Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 60 ilitengewa jumla ya Shilingi 24,271,626,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 1,470,091,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 22,801,535,000.00 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 1,189,507,846.46 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na asilimia 80 ya fedha zilizotengwa na Shilingi 17,273,221,111.45 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 76 ya fedha iliyotengwa.

5.1.3 Fedha za Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

53. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 44 ilitengewa Shilingi 53,087,886,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 52,687,886,000 fedha za ndani na Shilingi 400,000,000 fedha za nje. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 15,870,545,473.13 ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 30 ya fedha zilizotengwa. Wizara haijapokea fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Aidha, Fungu 11 na 60 hazikutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

5.2 Utekelezaji wa Mipango

5.2.1 *Sekta ya Uwekezaji*

A. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji

54. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya *Trademark East Africa* (TMEA) inatengeneza Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa Njia ya Kielektroniki (*Tanzania Electronic Investment Single Window* - TelW) ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2022, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 90. Katika awamu ya kwanza, mfumo unaunganisha mifumo ya taasisi saba (7) ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wakala wa Usajili na Leseni (BRELA); Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Mfumo huo utasaidia kupunguza gharama za ufanyaji biashara pamoja na urasimu ikiwemo kuondoa taratibu za mwekezaji kujaza fomu mbalimbali zenye taarifa zinazojirudia na kuwasilisha viambatisho vinavyofanana kwenye taasisi mbalimbali.

55. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilihamasisha wawekezaji nchini kuwasilisha changamoto wanazokabiliana nazo ambapo hadi Mwezi Machi, 2022 jumla ya changamoto 112 zilipokelewa. Changamoto hizo zinahusu kunyanganywa au kucheleweshwa utoaji wa leseni za udhibiti, kuchelewa kwa umilikishwaji ardhi, kuchelewa kwa marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), makadirio makubwa ya kodi, kuchelewa kutolewa kwa zabuni za kuzalisha umeme na kutolipwa mauzo ya umeme kwenye mikataba ya maziano ya umeme (PPA). Nyingine ni kuchelewa kwa vibali vya NEMC, kuchelewa kwa vibali vya ujenzi, taratibu za malipo ya tozo za mazao, kuchelewa kwa vibali vya kazi, migogoro ya mikataba ya kuchimba madini, ukiukwaji wa kilimo cha mkataba na kuchelewa kulisipwa deni kwa vifaa vya mabomba vilivyouzwa kwa wakandarasi waliopewa kazi na Halmashauri mbalimbali.

Hata hivyo, Wizara imefanikiwa kuratibu utatuzi wa changamoto 75 na changamoto nyingine zinaendelea kufanyiwa kazi katika sekta husika chini ya uratibu wa Wizara yangu.

56. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa Kanzidata ya Benki ya Ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 Kanzidata hiyo ilikuwa na jumla ya maeneo yenye ukubwa wa hekta milioni 1.6 kwa ajili ya uwekezaji. Wizara inaendelea na jitihada za kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji kutoka katika Sekta ya Umma na Binafsi.

57. Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kuhamasisha wamiliki wa maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa aina mbalimbali kuwasilisha taarifa hizo kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) pamoja na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA) kwa ajili ya kutangazwa kwa wawekezaji wa ndani na nje wanaohitaji maeneo ya uwekezaji. Wizara kuitia TIC na EPZA zitahakikisha taratibu za makubaliano zinafikiwa kwa mujibu wa Sheria za nchi.

B. Kuratibu Uwekezaji wa Miradi ya Kimkakati yenye Manufaa Makubwa

58. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu uwekezaji katika Kongani Maalum za Viwanda katika sekta zenye manufaa makubwa kwa nchi zinazowezesha kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, kuzalisha ajira kwa wingi na kukuza uchumi. Katika Sekta Ndogo ya Mafuta ya Kula, Wizara inaratibu uwekezaji wa Kongani ya Viwanda vya Mafuta ya Kula yanayotokana na mbegu za Alizeti katika eneo la Kitaraka, Wilaya ya Manyoni, Mkao wa Singida. Tayari ardhi yenye ukubwa wa ekari 45,000 imepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo. Vilevile, katika Sekta Ndogo ya Sukari, Wizara inaratibu uwekezaji wa Kongani ya Sukari eneo la Dakawa Magole, Wilaya ya Kilosa, Mkao wa Morogoro. Mradi utahusisha wawekezaji wadogo wanaotumia mashine zenye uwezo wa

kuchakata tani 200 hadi 500 za miwa kwa siku. Mradi huo utawanufaisha wananchi katika mnyororo wa thamani wa Zao la Miwa na shughuli nyingine zinazoambatana na kilimo na usindikaji wa miwa.

59. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu uwekezaji wa kongani kubwa zitakazovutia uwekezaji wa viwanda katika eneo moja na hivyo kupunguza gharama za miundombinu na kuimarisha ushindani wa uzalishaji. Katika eneo la Kwala Mkoa wa Pwani, Kampuni ya *Sino Tan Kibaha Industrial Park Limited* inaendeleza uwekezaji katika kongani lenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo viwanda 400 vinatarajiwu kujengwa na kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani Bilioni 3, kuzalisha ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizo za moja kwa moja 300,000 na kuzalisha bidhaa za takriban Dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka.

60. Mheshimiwa Spika, Wizara inaratibu uendelezaji wa Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi la Mkulazi ambalo linajumuisha ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda. Eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 60,103 limepangwa kwa uwekezaji wa kilimo cha mazao mbalimbali ambapo hekta 28,000 kwa ajili ya kilimo cha miwa na hekta 32,103 kwa ajili ya kilimo cha mazao mengine yakiwemo alizeti, mtama na mpunga. Mradi huo utajumuisha Kanda Maalum za Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Kilimo ikiwa ni pamoja na yale yatakayozalishwa katika eneo hilo na mikoa ya jirani. Uendelezaji wa eneo hilo, unakwenda sambamba na ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya Jiji la Dar es Salaam na Mikoa ya Morogoro na Pwani. Aidha, Wizara imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Kampuni ya *Syphomy Investment Ltd* iliyoonesha nia ya uendelezaji wa Mradi huo wakati wa Maonesho ya Biashara ya *Expo 2020 Dubai*.

61. Mheshimiwa Spika, Wizara inaratibu uendelezaji wa Mradi wa Bandari na Kanda Maalum ya Kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone – BSEZ) unaolenga kuwezesha nchi kuendana na ushindani wa

biashara za usafiri wa majini (marine transport services) na muunganisho na shughuli nyingine za kiuchumi ikiwemo viwanda na utalii.

62. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2021/2022, Wizara imefufua majadiliano na wawekezaji wa Kampuni za *China Merchants Holdings (International) Co. Ltd* (CMHI) na *Oman Investment Authority* (OIA) ambayo awali ilikuwa inaitwa Mfuko wa Uwekezaji wa Serikali ya Oman (State General Reserve Fund – SGRF). Majadiliano hayo yanahusu eneo dogo la Mradi wa BSEZ kwa kuendeleza eneo la hekta 3,087 kati ya hekta 9,887 ambapo unahusisha ujenzi wa Bandari (Sea Port) na Kituo cha Usafirishaji (logistics Park) kwenye eneo la hekta 887 na uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial City) kwenye eneo la hekta 2,200. Msingi wa marejeo ya majadiliano hayo ambayo yalisimama mwaka 2018 ni kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza maeneo ambayo ni wajibu wake kama vile ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) na lango la kuingilia bandarini (dredging) kwa maslahi mapana ya Taifa. Uwekezaji katika maeneo ya Mradi yatafanywa kwa kuvutia wabia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) au kufanywa na mwekezaji binafsi.

c. Kuhamasisha na Kuvutia Uwekezaji

63. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu maandalizi ya Maonesho ya Wafanyabiashara na Kongamano la Uwekezaji liliofanyika Zanzibar ikiwa ni moja ya shughuli za kuelekea Kilele cha Maadhisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kongamano hilo ilikuwa na lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini katika Sekta ya Uchumi wa Buluu, Utalii, Uzalishaji, Usafirishaji, Madini na Sekta ya Huduma za Jamii (afya na elimu). Kupitia Kongamano hilo, Kampuni mbalimbali zilizoonesha nia ya kuwekeza nchini katika viwanda vya dawa, chakula, bidhaa za nyumbani, kilimo, vifaa vya nyumbani, hoteli za kitalii (Resorts), uwekezaji katika majengo (Real Estate) na uzalishaji wa nyaya za umeme (Power Cables).

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imeshiriki kwenye makongamano mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kongamano la Uwekezaji kati ya Tanzania na Burundi, Kongamano la Wadau wa Sekta ya Alizeti, Kongamano la Uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza na Makongamano ya Uwekezaji katika Maonesho ya Kibashara Dubai (Dubai EXPO 2020). Katika Maonesho hayo Mikataba ya Makubaliano (MoU) 37 yenye thamani ya Shilingi triliuni 18.5 ilisainiwa na ipo katika hatua mbalimbai za utekelezaji. Aidha, Wizara kupitia TIC ilishiriki katika makongamano na mikutano ya uwekezaji nje ya nchi ikiwemo Afrika Kusini, Algeria, Misri, Italia, Kenya, Uturuki, Oman, Qatar, Ufaransa na Ubelgiji ambapo ilikutana na wawekezaji mbalimbali. Kati ya wawekezaji hao, wawekezaji sita (6) waliotoka Ubelgiji na wawekezaji 11 waliotoka Ufaransa wameonesha nia ya kuwekeza nchini. Vilevile, Wizara kupitia TIC imeendelea kuwasiliana na wawekezaji hao ili kuwasaidia na kuhakikisha wanawekeza hapa nchini.

65. Mheshimiwa Spika, Katika jitihada za kuendelea kuvutia wawekezaji nchini, Serikali iliamua kuandaa Filamu Maalum ya Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo ya vivutio vya uwekezaji vikiwemo Utalii, Madini, Usafirishaji na Kilimo. Ziara hiyo ambayo inajulikana kama *Royal Tour* ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Marekani katika Jimbo la New York katika Jengo la Makumbusho la Guggerheim tarehe 18 Aprili 2022 na baadaye huko Los Angels, Jimbo la California tarehe 21 Aprili, 2022. Aidha, uzinduzi huo hapa nchini umefanyika Jijini Arusha tarehe 28 Aprili, 2022 na unategemewa pia kufanyika Zanzibar tarehe 7 Mei, 2022.

66. Mheshimiwa Spika, Kutohaka na ziara iliyofanyika Marekani, Mikataba yenye thamani ya Shilingi triliuni 11.7 ilisainiwa na inatarajiwaka kutengeneza jumla ya ajira 301,110. Mikataba hiyo inahusisha Sekta za Kilimo na Biashara za Sekta nyingine za uchumi Miradi mingine iliyosainiwa inalenga kuwekeza kwenye mnyororo wa thamani katika

Kanda ya Kaskazini ya Sekta ya Utalii wa Tanzania, ikiwemo kwenye maeneo ya kutangaza utalii na kuongeza idadi na ubora wa huduma zinazotolewa.

67. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na kusimamia uhamasishaji wa matumizi ya Mwongozo wa Uwekezaji (Investment Guide) ambao umeainisha miradi mbalimbali katika Sekta ya Madini, Afya, Usafirishaji (Anga na Reli ya Kisasa - SGR), Mafuta na Gesi Asilia, Nguo na Mavazi, Uchumi wa Buluu, Utalii, Uvuvi, Kongani za Viwanda pamoja na fursa za uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Mwongozo huo unapatikana katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, tovuti ya Kituo cha Uwekezaji nchini na Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi.

68. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, miradi 221 ilisajiliwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA). Miradi hiyo inatarajiwa kuwekeza mitaji yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,922.2 na kuzalisha ajira 45,369. Pia, miradi 77 sawa na asilimia 34.8 inamilikiwa na wawekezaji kutoka nje, miradi 75 sawa na asilimia 33.9 ni ya Watanzania na miradi 69 sawa na asilimia 31.2 ni ya ubia. Aidha, kati ya miradi 221, TIC ilisajili miradi 206 yenye thamani ya Dola za Marekani 1,859.4 ambayo inatarajiwa kutoa ajira 37,451. Kati ya hiyo Miradi 72 sawa na asilimia 35 ni ya wawekezaji kutoka nje, miradi 70 sawa na asilimia 34 ni ya Watanzania na miradi 64 sawa na asilimia 31 ni ya ubia. Vilevile, EPZA ilisajili miradi 15 yenye thamani ya Dola za Marekani Millioni 62.8 na inayotarajiwa kutoa ajira 7,918 (**Jedwali Na. 16**).

69. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIC imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kupitia Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Centre) Kituo hicho kwa sasa kinaweza kuchakata maombi ya vibali na leseni mbalimbali kwa wawekezaji wakiwa TIC. Hadi Mwezi Machi, 2022 jumla ya vibali, vyeti na hati mbadala za ardhi 7,734 zilitolewa kwa wawekezaji

mbalimbali kupitia Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja. Wizara kupitia TIC imeanzisha Kituo cha Mawasiliano kwa Wawekezaji (Tanzania Investment Call Centre) ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 mpaka Machi, 2022, jumla ya wateja 916 walifanya mawasiliano kupitia kituo hicho, ili kupata huduma mbalimbali zikiwemo taarifa kuhusu taratibu na upatikanaji wa vibali, usajili, yeti, taratibu na fursa mbalimbali za uwekezaji.

70. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIC ilitembelea jumla ya miradi 1,672 kati ya miradi 1,500 iliyokuwa imepangwa na kupatiwa huduma (After-Care Services and Project Verification Visit - PVV). pia Wizara iliweza kuwafikia na kuwahudumia wawekezaji 1,402 kwa njia ya simu. Miradi hiyo iliweza kufikiwa na kupita lengo kutokana na zoezi rasmi liliofanyika TIC katika kipindi husika kwa kushirikiana na Maafisa Biashara kutoka katika Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam.

71. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIC kwa kutumia wataalam wa ndani ilifanya utafiti wa kuibua na kuchambua fursa za uwekezaji zinazotokana na Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) katika eneo la Dar es Salaam hadi Morogoro. Jumla ya miradi ya uwekezaji 30 imeibuliwa, kati ya hiyo, miradi tisa (9) imefanyiwa upembuzi yakinifu.

5.2.2 Sekta ya Uvezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi

A. Kukuza Maendeleo ya Sekta Binafsi

72. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha nia ya dhati ya kukuza na kuimarisha majadiliano na ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa kutambua hilo, Serikali imejenga uwezo wa uendeshaji wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya mikoa na wilaya ambapo mafunzo ya uendeshaji majadiliano yamefanyika katika Mikoa saba (7) ya Dodoma, Iringa, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma na

Singida. Jumla ya washiriki 217 walipatiwa mafunzo ambapo kati yao, 129 walitoka Sekta ya Umma na 88 walitoka Sekta Binafsi. Lengo la mafunzo hayo ilikuwa ni kuongeza tija na ufanisi wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuwa endelevu kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Mafunzo hayo yamewezesha Mikoa ya Rukwa, Singida na Ruvuma ambayo ilikuwa haifanyi Mikutano ya Mabaraza ya Biashara na Sekta Binafsi kuanza kufanya mikutano hiyo.

73. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imeratibu ushiriki wa Sekta Binafsi katika ziara za Serikali (Kenya, Burundi na Marekani)na ziara za kikazi(Malawi, Msumbiji na Uganda). Katika ziara hizo, Sekta Binafsi ilishiriki majadiliano ya kutatua changamoto zinazoikabili Sekta hiyo katika kufanya biashara katika masoko ya nchi mbalimbali. Aidha, kupitia ushirikishwaji huo, Vikwazo Visivyo vya Kikodi (NTBs) 42 kati ya 64 vilijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi na hivyo kuwezesha ustawi wa biashara baina ya Tanzania na Kenya.

74. *Mheshimiwa Spika*, Vilevile, Sekta Binafsi ilishiriki katika Maonesho ya *Dubai Expo 2020* yaliyofanyika Jijini Dubai. Kutokana na Maonesho hayo, Sekta Binafsi iliweza kutangaza bidhaa zao na kupata fursa za masoko na kuingia mikataba 23 ya ushirikiano baina ya Sekta Binafsi ya Tanzania na kampuni kubwa za nchi za nje.

75. *Mheshimiwa Spika*, Matokeo ya ziara hiyo ni kuimarishwa kwa ushirikiano wa taasisi za Sekta Binafsi na Vyama vya Biashara baina ya Tanzania na Malawi na Tanzania na Burundi. Pia, kuongezeka kwa fursa za biashara na uwekezaji katika nchi za Burundi, Dubai, Kenya, Malawi na Uganda kwa wafanyabiashara wa Tanzania. Mfano Kampuni ya Taifa Gas kutoka Tanzania kupata soko la Kenya.

76. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imefanya tathmini ya matumizi ya Ushoroba wa Dar es Salaam na miundombinu mingine inayotumika na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo

ya Kusini Mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Lengo la tathmini ilikuwa ni kuangalia kinachosababisha kudorora kwa matumizi ya Ushoroba wa Dar es Salaam na miundombinu mingine ya Tanzania inayotumiwa na nchi za SADC na EAC. Tathmini hiyo inaonesha kuwa, Ushoroba wa Dar es Salaam una ufanisi mdogo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu na za uendeshaji. Tathmini hiyo imeweza Serikali kuandaa Mpango na Mkakati wa Pamoja wa Kukuza Biashara na Uwekezaji kwa ajili ya masoko ya nchi jirani.

b. Kukuza Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji

77. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuititia NEEC imeendelea kuratibu ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji unaofanyika hapa nchini (Local Content). Katika suala hilo, tunasitiza maslahi ya Watanzania kwenye maeneo ya ajira, matumizi ya bidhaa za Tanzania, ushiriki wa kampuni za Kitanzania, uhaulishaji wa teknolojia, mafunzo na ushiriki wa jamii kiuchumi. Kwa msingi huo umefanyika ufuatiliaji katika miradi yote ya kimkakati ikiwemo Reli ya Kisasa (SGR), Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda kwenda Chongoleani Tanga nchini Tanzania, uchimbaji wa madini kwenye migodi yote, miradi ya umeme na maji vijijini, ujenzi wa barabara na madaraja na viwanda vyote vyenye uwekezaji wa kutoka nje.

78. *Mheshimiwa Spika*, Matokeo ya ufuatiliaji huo unaonesha kuwa, Mwaka 2021, jumla ya ajira 72,395 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zilizalishwa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini. Kati ya ajira hizo, ajira 68,305 sawa na asilimia 94.35 zilitolewa kwa wazawa na ajira 4,090 zilitolewa kwa wageni sawa na asilimia 5.65. Aidha, Miradi ya Kimkakati ilitoa kandarasi ndogo ndogo kwa kuingia mikataba na Kampuni 2,019 za Watanzania kwa huduma za chakula, ulinzi, biashara, bidhaa za ujenzi kama vile saruji, nondo, kokoto, mchanga, kampuni za usafiri, kampuni za bima na kampuni za mafuta.

c. Mifuko na Programu za Uwezeshaji

79. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia NEEC imeendelea kuimarisha uratibu wa mifuko na programu za uwezeshaji 62 ili iweze kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo huduma za mikopo, dhamana na ruzuku. Kati ya mifuko na programu hizo, mifuko na programu 52 zinamilikiwa na Serikali na mifuko na programu 10 zinamilikiwa na taasisi binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 903 ilitolewa kwa wanufaika 5,932,668 kutoka katika mikoa 26 wakiwemo wanawake 3,737,581 na wanaume 2,195,087.

80. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia NEEC imeendelea na mkakati wa kuanzisha Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Vituo tisa (9) vimeanzishwa katika Mikoa ya Dodoma, Geita na Rukwa na hivyo kufikia jumla Vituo 17 vilivyoanzishwa katika mikoa sita (6) ya Shinyanga (Kahama), Geita, Singida, Rukwa (Sumbawanga), Kigoma (Vituo 6) na Dodoma (Vituo 7). Nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma za kuwawezesha wananchi kiuchumi zikiwemo za mikopo, mafunzo, urasimishaji wa biashara, ujuzi wa wafanyabiashara, uongezaji thamani ya mazao, elimu ya kodi na upatikanaji wa masoko, zinapelekwa karibu na walengwa.

81. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia NEEC inasimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo ya Ujasiriamali (National Entrepreneurship Training Framework, 2015) ili kuendeleza ujasiriamali hapa nchini. Katika Mwaka 2021/2022, jumla ya Watanzania 78,908 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali kwa kushirikiana na Shule, Vyuo vya Ualimu, Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu, Wizara na Taasisi za Serikali na Binafsi. Aidha, Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Biashara (Geita Entrepreneurship Development Program - GEDP) katika Mkoa wa Geita, ambapo jumla ya wafanyabiashara 365 kutoka Mkoa wa Geita wamenufaika na mafunzo ya kukuza biashara zao. Utekelezaji wa Mpango huo umeleta

matokeo chanya ya uanzishaji wa Kituo cha Uwezeshaji katika Mji wa Geita ambapo taasisi za Mfuko wa *SELF MicroFinance*, *Tanzania Women Chamber of Commerce*, *Tanzania Bureau of Standards* na *GSI Tanzania* zinatoa huduma kwenye kituo hicho.

82. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetekeleza Programu ya Vijana 2JIAJIRI (2JIAJIRI Youth Entrepreneurship Training Program) kwa ushirikiano na Benki ya KCB. Programu hiyo inawawezesha vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundu kupata mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kuijendeleza kwenye biashara zao. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya vijana 303 wakiwemo wanawake 172 na wanaume 131 wamenufaika na programu hiyo Zanzibar na katika mikoa mitano (5) ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Morogoro na Mwanza.

83. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NEEC ilihamasisha uanzishwaji wa vikundi vya kijamii vya kiuchumi kama inavyoelekezwa na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya vikundi 13,711 vilisajiliwa katika ngazi ya Halmashauri. Wizara imeendelea na jukumu lake la msingi la kuhamasisha vikundi hivyo kuanzishwa na kuendelezwa kwa kuvunganisha na fursa mbalimbali za kiuchumi.

84. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NEEC inaratibu Programu ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Mikoa, Wilaya, Kata, Vijiji na Mitaa. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 kuna jumla ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi 991 yakiwemo majukwaa 23 katika ngazi ya Mkoa, 144 katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, 302 katika ngazi ya Kata, na majukwaa 522 katika ngazi ya Kijiji. Majukwaa hayo yanahusika katika kujadili kwa pamoma changamoto zinazowakwamisha wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuweka mipango ya utatuzi. Katika kuimarisha Majukwaa hayo, Mwaka 2021, Serikali imefufua Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (Presidential Trust Fund) ili utumike katika kuimarisha

majukwaa kwa kuwawezesha wanawake kupata mafunzo ya ujasiriamali na mikopo.

85. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia NEEC inatekeleza Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme) ambao ulizinduliwa tarehe 10 Julai, 2020 kwa lengo la kutoa fursa kwa Watanzania kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati hususan vinavyochakata mazao ya kilimo na mifugo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Mpango huo umewezesha kutolewa mikopo yenye jumla ya thamani ya Shilingi 1,746,557,651.29 kwa miradi 32 katika mikoa nane (8). Mikoa hiyo ni pamoja na: Mwanza iliyowezeshwa kupata miradi sita (6) yenye thamani ya Shilingi 296,000,000; Arusha miradi 10 yenye thamani ya Shilingi 465,460,000; Dar es Salaam miradi mitatu (3) yenye thamani ya Shilingi 274,250,000; Kilimanjaro miradi mitatu (3) yenye thamani ya Shilingi 482,847,651.29; Mbeya miradi sita (6) yenye thamani ya Shilingi 108,000,000; Geita miradi miwili (2) yenye thamani ya Shilingi 35,000,000; Dodoma mradi mmoja (1) wenyе thamani ya Shilingi 15,000,000; na Shinyanga mradi mmoja (1) wenyе thamani ya Shilingi 70,000,000. Kipekee napenda kutoa wito kwa wananchi wenyе viwanda vidogo na vya kati na wanaotaka kuanzisha viwanda kutumia fursa ya uwepo wa Mpango huo kupata mitaji yenye masharti nafuu.

5.2.3 Sekta ya Viwanda

A. Kuendeleza Miradi ya Kimkakati

86. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia NDC imepanga kurudia zoezi la uthamini wa fidia katika mradi wa Mchuchuma na Liganga katika Mwaka 2022/2023 kutokana na uthamini uliofanyika mwaka 2015 kuwa wa muda mrefu kulingana na Sheria ya Uthaminishaji ya Mwaka 2016 Kipengele cha 52:2. Kwa mujibu wa Kipengele hicho, mara baada ya uthamini kufanyika, malipo ya fidia yanapaswa kufanywa ndani ya kipindi cha miezi sita (6),

na isipolipwa katika kipindi hicho, riba ya kibishara itatozwa katika kipindi kisichozidi miaka miwili, na baada ya kipindi hicho uthamini huo unakosa uhalali wa kisheria na unapaswa kufanywa upya. Hivyo, katika hali hiyo, ulipaji wa fidia utafanyika baada ya kukamilika kwa tathmini mpya. Aidha, Majadiliano na Mwekezaji anayetarajiwu kutekeleza Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu ulio karibu na eneo la Mchuchuma na Liganga yamekamilika. Maandalizi ya Mkataba wa Ubia yako kwenye hatua za mwisho ambapo yakikamilika ulipaji wa fidia utafanyika na utekelezaji wa Mradi utaanza mara moja. Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu utakuwa ni awamu ya kwanza ya Mradi wa uzalishaji wa chuma nchini ukifatiwi na utekelezaji wa Mradi wa Chuma wa Liganga.

87. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NDC imefanya utafiti wa Mradi wa Magadi Soda-Engaruka ambapo Upembuzi Yakinifu (Techno-Economic Study) umekamilika kwa asilimia 100. Kazi nyininge zilizokamilika ni pamoja na kufanya tathmini ya Athari za Kimazingira (Environmental Impact Assessment - EIA) iliyochangia upatikanaji wa Cheti cha Mazingira na utafiti wa masoko ya Magadi Soda; Uthamini na uhakiki wa ardhi na mali za wananchi watakaopisha Mradi; Maombi ya leseni 29 kwa ajili ya uchimbaji (Mining Licence) yenye gharama ya Dola za Marekani 58,000; na maandalizi ya kutafuta mwekezaji wa kujenga kiwanda yameanza kwa kuandaa na kukamilisha nyaraka muhimu za kutangaza zabuni.

88. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NDC, inaendelea na ufuatiliaji wa madeni ya wakopaji wa Matrekta ya URSSUS na kuendelea kutoa huduma za kiufundi kwa wateja wa matrekta hayo. Aidha, Timu za Majadiliano za Serikali ya Tanzania na Serikali ya Poland pamoja na Kampuni ya URSSUS zinaendelea kufanya majadiliano ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto na kupata hatma ya Mradi huo. Changamoto zinazotafutiwa ufumbuzi ni pamoja na changamoto za kiteknolojia, kisheria na kibashara.

89. Mheshimiwa Spika, Kutohana na kukua kwa Jiji la Arusha, sehemu ya eneo linalozunguka Kiwanda cha Matairi Arusha kwa sasa linatumika kwa shughuli za maendeleo ya kijamii ambazo zimeashiria haja ya kutafakari upya juu ya matumizi yanayozingatia mazingira ya sasa. Kimsingi, Wizara kupitia NDC inakusudia kubadili matumizi ya eneo hilo kuwa Kongani la Viwanda vya Kati (light industries). Hivyo, Upembuzi Yakinifu utafanywa ili kubaini aina ya viwanda vinavyofaa kusimikwa kwenye eneo hilo.

90. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NDC imeanza maandalizi ya awali kwa ajili ya kuzalisha mbolea zisizo na kemikali (Bio-fertilizer) kwenye Kiwanda cha *Tanzania Bio-tech Product* kilichopo Kibaha, Mkoa wa Pwani. Hii ni pamoja na kufanya stadi ya kiufundi ili kujua mahitaji halisi ya mashine zilizopo na gharama za kuzalisha mbolea hiyo. Aidha, Kiwanda cha *Tanzania Bio-tech Product* kinakamilisha taratibu za kufanya majaribio ya pili ya viuatilifu (Bio pesticides), usajili pamoja na kupata vibali vya uzalishaji wa kibiashara. Majaribio hayo ya pili ni katika kuendana na taratibu za Afrika Mashariki zinazotaka majaribio hayo yafanyake mara mbili. Majaribio ya awali yalifanyika kwenye pamba, mahindi na mbogamboga ambapo viuatilifu hivyo vilionesha ufanisi mkubwa. Uzalishaji wa Viuatilifu utatumia mashine zilizopo kiwandani za kuzalisha viuadudu na kuongeza ufanisi na tija kwenye Kiwanda cha TBPL.

91. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO, imeendelea kufanya kazi ya kupima ubora wa makaa ya mawe kutoka kwenye Shirika la STAMICO na kutoka kwa Kampuni mbalimbali zinazochimba makaa ya mawe yakiwemo *Magamba Coal, TANCOAL, Amil Coal Company, Kamba s Group of Companies, Kiasi Ltd na Edenville International*. Upimaji huo ulionesha kuwa makaa ya mawe yanayochimbwa hapa nchini yana ubora wa hali ya juu na yanaweza kutumika katika miradi ya chuma, viwanda vya saruji na kufua umeme. Hii imeondoa uhitaji wa kuagiza makaa ya mawe kutoka nje ya nchi. Matokeo ya utafiti pia yamesaidia kuongeza usafirishaji wa makaa ya mawe

kutoka Tanzania na kuuzwa nje ya nchi kama Rwanda na kuongeza kuchangia katika Pato la Taifa.

b. Mwongozo wa Mitaa ya Viwanda na Kanzidata ya Viwanda

92. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeandaa rasimu ya Andiko la Mwongozo wa Mitaa ya Viwanda na Mgawanyo wa Viwanda nchini (Guideline for Industrial Parks Development and Management in Tanzania and Classification of Industries). Andiko hilo litaweka utaratibu maalum wa kuwasaidia wawekezaji katika sekta mbalimbali. Wizara pia imeandaa Kanzidata ya Viwanda ambapo mapitio ya awali yamefanyika. Aidha, Wizara imeandaa miongozo mbalimbali ya Sekta ya Viwanda kama Mwongozo wa Viwanda ikiwemo pamoja na Mgawanyo wa Viwanda. Vilevile, Wizaraimeendelea kuhamasisha utengaji na uendelezaji wa maeneo ya uwekezaji viwanda kwenye kila Mkoa na Halmashauri.

c. Tathmini ya Uzalishaji na Mahitaji ya Bidhaa Viwandani

93. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango na Bodi ya Sukari Tanzania ilifanya tathmini ya uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani zikiwemo mafuta ya kula, sukari, vifaa vya ujenzi, vinywaji na taulo za kike. Lengo ni kujua hali halisi ya uzalishaji wa bidhaa hizo ili kufanya maamuzi sahihi yatakayowezesha upatikanaji wake katika soko na kwa bei stahiki. Kwa upande wa mafuta ya kula, tathmini imeonesha kuwa Tanzania ina changamoto ya kujitosheleza kutokana na uhaba wa malighafi kwa ajili ya kuzalisha mafuta hapa nchini. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa alizeti na michikichi kwa kutumia teknolojia za kisasa. Aidha, tathmini ya uzalishaji wa dawa za binadamu ilifanyika sambamba na uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba Nchini. Tathmini hiyo ilibainisha kuwa Tanzania inatumia fedha nydingi kuagiza dawa kwa kuwa viwanda vya ndani vinatosheleza kwa

asilimia 11 tu ya mahitaji ya nchi. Hivyo, Mkakati huo wa kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba Nchini umeainisha njia na mazingira bora ambayo Serikali na Sekta Binafsi inatakiwa kuchukua ili kuwekeza kwenye sekta hiyo muhimu.

D. Kuhamasisha Uongezaji wa Thamani Mazao ya Kilimo

94. Mheshimiwa Spika, Wizara imeshiriki katika maandalizi ya Mradi wa kuanzisha Maeneo Maalum ya Viwanda vya Kusindika Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi yaani 'Special Agro-Processing Zone (SAPZ)'. Aidha, tarehe 4 hadi 10 Agosti 2021, Timu ya Wataalam kutoka Wizara za: Kilimo; Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Mifugo; Uvuvi na Ofisi ya Waziri Mkuu; UNIDO na AfDB ilitembelea maeneo yenye ngombe wengi katika Mikoa ya Mwanza - Misungwi na Igunga - Tabora (Ibologero) ambako Vituo vya Uchakataji wa Awali - *Agricultural Transformation Centre (ATCs)* vitaanzishwa. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na uwepo wa maeneo yaliyopendekezwa kwa ajili ya ATCs pamoja na kukusanya taarifa za awali za maeneo hayo zitakazojumuishwa katika Andiko la Mradi. Ziara kama hiyo ilifanyika tarehe 26 Septemba hadi 4 Oktoba 2021, katika Mikoa ya Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu, Singida, Shinyanga na Tabora ambako Vituo vya Ukusanyaji wa Mazao (Aggregation Centres - ACs) vitaanzishwa.

95. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 umefanyika uhakiki wa taarifa za maeneo ya utekelezaji wa mradi zilizowasilishwa katika kipindi cha maandalizi ya mradi ikiwemo taarifa ya upembuzi yakinifu, kufanya majadiliano na wadau, kutathmini mahitaji muhimu ya utekelezaji wa mradi na kujadili mfumo wa utekelezaji pamoja na kutoa maoni na mapendekezo kabla ya kuidhinishwa kwa mradi. Vilevile, Wizara imeendelea na utengaji wa maeneo ya kongani yakiwemo Eneo la Kongani ya Korosho -Mtwara, Pamba - Kishapu na Kahama pamoja na Mchikichi - Kigoma.

96. Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo (Bagamoyo Sugar Limited) kilichopo katika Wilaya ya Bagamoyo, kinamilikiwa na Bakhresa Group of Companies kina eneo kwa ajili ya Kiwanda na mashamba lenye ukubwa wa takriban ekari 10,000. Kiwanda hicho ambacho ujenzi wake umeanza kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 35,000 za sukari kwa mwaka. Aidha, Kiwanda kinatarajia kuanza uzalishaji wa sukari mwezi Julai 2022, ambapo uzalishaji unatarajia kuanza kwa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka na kuajiri wafanyakazi 600 inayojumuisha wafanyakazi 250 wa kudumu na vibarua 350. Aidha, Kiwanda kitakapokamilika msimu wa mwaka 2024/2025 kinatarajia kuzalisha sukari tani 70,000 kwa mwaka na kutoa jumla ya ajira 1,000.

97. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia CAMARTEC imebuni na kuunda Mashine za kupura mtama, maharage na alizeti; Mashine za kubangua Korosho; Mtambo wa kuzalisha mvuke wa kuchemshia Korosho; Jiko sanifu la kuni la kuchemshia Korosho; na Mashine za kukaushia mbogamboga, matunda na mazao mengine. Teknolojia hizo zinalenga kuongeza tija katika shughuli za kilimo nchini. Aidha, teknolojia hizo zinaundwa kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wa uhitaji wa zana za kilimo na teknolojia za vijivji uliofanywa na CAMARTEC katika maeneo mbalimbali nchini.

98. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TEMDO imekamilisha usanifu wa mtambo wa kukausha muhogo na utengenezaji wa Parts za mtambo huo zinaendelea. Ili kukamilisha chasili cha mtambo huo TEMDO imenunua mashine mbili (2) muambato (Grating and hydraulic pressing machines) kutoka Kampuni ya Kitanzania ya *Intermech Engineering Company Ltd*, sambamba na utengenezaji wa mtambo huo. Utengenezaji wa sehemu ya kuzalisha joto la kukaushia uko katika hatua ya mwisho kukamilishwa. Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kukausha tani 12 za muhogo mbichi kwa saa 10 na kutoa tatu (3) za unga wa muhogo. Usanifu wa mtambo huo umekamilika kwa asilimia 100 na utengenezaji wa mtambo huo upo asilimia 85, na

unategemea kukamilika kwa kwa asilimia 100 ifikapo mwezi Juni, 2022 ili uweze kupelekwa kwenye kikundi cha wakulima Handeni. Vilevile, TEMDO imekamilisha usanifu na michoro ya mtambo wa kukausha korosho.

99. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TEMDO pia imekamilisha usanifu na michoro ya mtambo mdogo wa kutengeneza sukari kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na utengenezaji (fabrications and manufacture) umeanza. Baadhi ya mashine zinazotengenezwa ni *cane crusher, sugar cane juice heaters, sugar cane juice clarifier, vacuum pan evaporator, sugar crystallizer, rotary dryer, na mini boiler*. Pia, usanifu wa mashine ya kuandaa mbegu za miwa ili zisishambuliwe na magonjwa (Hot water seed treatment plant) umekamilika na utengenezaji wake unaendelea. Mtambo huo mdogo wa sukari utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 10 ya miwa (10 TCH), na kutoa tani moja (1) ya sukari kwa saa moja.

100. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TEMDO limekamilisha pia usanifu wa teknolojia ya kuhifadhi mazao ya matunda na mbogamboga (Cold rooms), na uundaji wa mtambo unaendelea. TEMDO tayari ina makubaliano (MoU) na TAHA kwa ajili ya kuwatengenezea mitambo yenye teknolojia bora ya kuhifadhia mazao ya mbogamboga. Aidha, usanifu wa chasili cha mtambo wa kusindika mafuta ya kula yatokanayo na Zao la Chikichi umekamilika na utengenezaji unaendelea.

101. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TEMDO imekamilisha utengenezji wa mashine ndogo ya kuchakata mkonge (Raspador) ili kutoa nyuzi zake. Mashine hiyo imefanyiwa majaribio ya awali katika karakana ya taasisi na imeonesha matokeo mazuri ya kutoa nyuzi. Mashine hiyo inategemewa kupelekwa kwa wadau wachakataji wa mkonge ili kuweza kubaini kama kuna maboresho yatakayohitajika kufanyika. Pia, mtambo wa ukubwa wa kati (Corona) umesanifiwa baada ya TEMDO na Bodi ya Mkonge Tanzania kushirikiana na kuonekana uhitaji huo

upo na utawawezesha wachakataji wa viwanda vyat kati kupata teknolojia hiyo.

102. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imesimamia ufufuaji wa Kiwanda cha Chai Mponde kilichopo chini ya umiliki wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSSSF na WCF). Tayari baadhi ya vifaa vinavyohitajika ikiwemo vyat umeme na *mechanical* kwa ajili ya maboresho vimenunuliwa na ufungaji wa vifaa hivyo umefanyika.

103. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imekuwa msimamizi mkuu katika uanzishwaji na usimamizi wa ujenzi wa viwanda nchini kama vile Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha Mkuyuni Mwanza chenye uwezo wa kukoboa tani 96 kwa siku ambacho kinamilikiwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB). Hadi Mwezi Machi, 2022 Kiwanda kimekamilika na kimeanza uzalishaji na msimamizi (TIRDO) ipo katika hatua ya kipindi cha uangalizi. Shirika pia linasimamia uanzishwaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Viatu cha *Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited* kinachomilikiwa kwa ubia kati ya PSSSF na Jeshi la Magereza. Kiwanda hicho kimekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na uzalishaji wa viatu na bidhaa nyingine za ngozi umeanza.

E. Utekelezaji wa Mikakati ya Pamba, Nguo na Mavazi, Ngozi na Bidhaa za Ngozi na Mafuta ya Alizeti

104. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitekeleza Mikakati ya Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi; Ngozi na Bidhaa za Ngozi na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Alizeti. Mikakati hiyo ambayo imefikia ukomo mwaka 2020 na sasa Wizara inaendelea na mapitio ya Mikakati hiyo.

i. Mkakati wa Ngozi na Bidhaa za Ngozi

105. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO inaendelea kusimamia ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza V i a t u vyat Ngozi cha *Kilimanjaro International Leather Industries*

Company Limited kinachomilikiwa kwa ubia kati ya PSSSF na Jeshi la Magereza. Sehemu ya kwanza ambayo ni Kiwanda cha Kuzalisha Viatu kimekamilika kwa asilimia 100. Sehemu ya pili ambayo ni ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Ngozi umekamilika kwa asilimia 90 na Uzalishaji wa Viatu na Bidhaa nyingine za ngozi umeanza. Kwa sasa Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha jazi 500 za viatu kwa siku.

106. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa ushirikiano na REPOA imetoa mafunzo ya kitaalam kwa wadau wa ngozi 407 wa mnyororo wa thamani ikijumuisha wafugaji 270, wachunaji ngozi 75, wafanyabiashara wa ngozi 25 na wasindikaji ngozi 10 na watengeneza bidhaa za ngozi 27. Mafunzo hayo yamefanyika katika Mikoa 11 nchini kwa kuzingatia ile yenye mifugo mingi, machinjio ya kimkakati na viwanda vingi vya ngozi ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Pwani, Shinyanga na Tabora. Aidha, TIRDO kwa kushirikiana na REPOA imefanya tathmini ya hali ya sasa ya Sekta ya Ngozi ya Tanzania na kuandaa taarifa na andiko la kitaalam ambalo litasaidia kuandaa mkakati na utafutaji ufadhili.

107. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa kushirikiana na REPOA imeandaa miongozo minne (4) ya mafunzo kwa kila sehemu ya mnyororo wa thamani wa Zao la Ngozi na kuisambaza kwa wahusika kwa ajili ya mafunzo zaidi na rejea. Pia, *policy brief* mbili (2) z a uboreshaji wa Sekta ya Ngozi zimeandaliwa na zinapatikana kupitia <https://www.repoa.or.tz/wp-content/uploads/2021/06/Leather-PB.pdf> na pia udhibiti wa matumizi ya madawa ya kusindika ngozi yenye kemikali sumu ipo katika hatua ya ukamilishwaji.

ii . Mkakati wa Mafuta ya Alizeti

108. Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba, 2021 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, pamoja na Sekta Binafsi ilifanya tathmini ndogo ya Sekta ya Mafuta ya Alizeti katika mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Morogoro na Singida.

Tathmini hiyo ilifanywa chini ya Mradi wa TRF unaofadhiliwa na EU kupitia SADC ili kuangalia kipengele cha ushindani katika sekta hiyo. Utafiti huo umebaini kwamba bado kuna changamoto ya uzalishaji mbegu za kutosha za Alizeti kwa ajili ya viwanda. Aidha, Viwanda vingi vidogo na vya kati vina changamoto ya kiteknolojia ya kuchakata mafuta ya kula hadi hatua ya mwisho. Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imeanza taratibu za kuandaa Mkakati mpya wa kukuza tasnia ya alizeti.

109. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO pia imekamilisha utafiti wa soko, taarifa za uzalishaji wa Zao la Chikichi na kupata taarifa za awali za teknolojia. Pia, ukamilishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa Kiwanda cha Mafuta ya Mawese unaendelea ili kuweza kutoa ushauri wenye tija juu ya uanzishwaji wa Kiwanda hicho katika Mkoa wa Kigoma. Kiwanda hicho kitakuwa soko kwa wakulima wa Zao la Chikichi, kitatoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 300 (100 wakiwa ni waajiriwa wa kudumu, 200 wakiwa waajiriwa wa mkataba) na ajira zisizo za moja kwa moja zaidi ya 50,000.

110. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TEMDO imekamilisha usanifu na michoro ya mtambo wa kusindika Mafuta ya Kula ya Alizeti na utengenezaji wa mtambo huo unaendelea kufanyika (Fabrication and manufacture). Mitambo ina uwezo wa kukamua, kusafisha na kuweka virutubisho (seed cleaning, pressing, filtration, refining and fortification). Mitambo itakuwa na uwezo wa kusafisha tani moja (1) ya mafuta kwa siku (Lita 1,000) na kutoa ajira 15 za moja kwa moja na ajira zaidi ya 100 zisizo za moja kwa moja.

F. Kueneza Dhana ya KAIZEN Nchini

111. Mheshimiwa Spika, KAIZEN ni falsafa inayoweka kanuni na taratibu ambazo zinahitaji mwendelezo katika uboreshaji wa mfumo wa uzalishaji unaozingatia ubora wa bidhaa, uwezo wa uzalishaji, mawasiliano, matumizi ya nafasi na kuwa na uwezo wa kuwatunza wateja na

wafanyakazi. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) inatekeleza Mradi wa KAIZEN ambao hapa nchini ulanza kutekelezwa mwaka 2013. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mradi wa KAIZEN umefanya uhamasishaji wa dhana ya KAIZEN upande wa Pemba ambapo wanufaika 80 walishiriki na upande wa Unguja ambapo wanufaika 20 walipata mafunzo hayo. Aidha, Wizara imefanya tathmini katika Mikoa sita (6) ambayo inatekeleza KAIZEN. Vilevile, Wizara ilishiriki kwenye Maonesho ya Viwanda Kitaifa yaliyofanyika Zanzibar na Maonesho ya Tamasha la JUAKALI la Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Mwanza. Kushiriki kwenye maonesho hayo kuliwezesha kutangaza falsafa KAIZEN na kuhamasisha kuhusu umuhimu wa kutumia falsafa na hivyo kufanya watu wengi kuhitaji huduma hiyo.

112. Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa mafunzo ya KAIZEN kwa nadharia na vitendo katika Mikoa ya Kagera, Mtwara, Pwani na Tanga ambapo takriban viwanda 20 vimenufaika na mafunzo hayo na wakufunzi 36 wamepatiwa mafunzo hayo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na CTI iliandaa semina ya wadau iliyofanyika Dar es Salaam iliyowalenga wenyewe viwanda. Washiriki 18 walinufaika ambapo asilimia 50 kati yao walionesha nia ya kutaka kupatiwa mafunzo kwa kina. Vilevile, Wizara ilifanya mafunzo kazini (Intensive on the Job Training – OJT Program for Advanced KAIZEN Trainers) yaliyofanyika Dar es Salaam kwa muda wa wiki nane (8) na kuhusisha wabobezi wa Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya na Morogoro. Jumla ya Washiriki 14 wamenufaika na mafunzo hayo ambayo yalivifikia jumla ya viwanda vinne (4).

G. Uendelezaji na Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi

113. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia EPZA kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi - SEZ. Kutokana na uhamasishaji huo, Makampuni mapya 15

yamesajiliwa kufikia Mwezi Machi, 2022. Kampuni hizo ni *Kriishi Green Limited, Green Bridge Commodities Limited, Diamond Foods Limited, NB Industries Limited, Coastal nuts Tanzania Limited, Tanzania Huafeng Agriculture Development Limited, East Africa zhenyuan Group Company Ltd, Apeck Export Group Limited, Unicarb Minerals Limited, Tanite Minerals Limited, Octavian Mshiu Trust Company Limited, Future Agro Pro Limited, Akofa East Africa Limited, Tanso Investment Limited na Polytex Africa Limited*. Uwekezaji wa Kampuni hizo kwa ujumla utaleta jumla ya ajira za moja kwa moja 7,918, Mtaji unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 62.8 na mauzo nje yanayokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 94.85 (**Jedwali Na. 17**).

114. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia EPZA imeendelea kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 EPZA kwa kushirikiana na taasisi ya Trade Mark East Africa (TMEA) imefikia hatua ya Tathmini (Evaluation) ya nyaraka za zabuni ili kumpata mkandarasi atakayetengeneza mfumo unaolenga kuboresha huduma za uwekezaji zinazotolewa na Mamlaka kwa kutumia TEHAMA. Mradi huo unahusisha utengenezaji na utekelezaji wa Mfumo wa kielektroniki wa huduma za pamoja (One Stop Service Centre) ambao utaunganishwa na mifumo mingine ya wadau muhimu katika kuboresha huduma za Uwekezaji. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) imetengeneza tovuti mpya ya Taasisi na tayari imekwishesimikwa kwa ajili ya matumizi.

H. Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

115. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa kushirikiana na Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) wanazalisha teknolojia ya utengenezaji wa mkaa mbadala (Briketi) wenye nguvu, usiovunjika, usiota majivu mengi na kutokuwa na moshi mwangi ambao ni rafiki kwa mazingira kwa kutumia makaa ya mawe. Aidha, Shirika limefanikiwa kuandaa programu za mafunzo ya namna ya kutengeneza mkaa mbadala ulio katika ubora

unaotakiwa kwa matumizi ya majumbani kwa wajasiriamali mbalimbali. Vilevile, TIRDO imenunua mtambo wa kati wa kuzalisha tofali ndogo, wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili (2) kwa saa na umesimikwa kwa majoribio katika jengo lillipo TIRDO.

116. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imefanya kaguzi katika viwanda mbalimbali ili kuona uwezekano wa kuvirudisha katika hali ya uzalishaji au kushauri matumizi mbadala yenye tija kwa uchumi wa Taifa. Viwanda hivyo ni *Mwanza Tannery Ltd, Buhongwa Industrial Area na Nyanza Glass Work Ltd*. Pia, Shirika limefanya ukaguzi wa matumizi bora ya nishati katika viwanda vidogo vilivyopo Mkao wa Dodoma, Singida na Shinyanga ambavyo ni *Kibaigwa Flour Supplies Ltd* (Dodoma), *Musoma Food Co. Ltd* (Shinyanga) na *Mwenge Sunflower Oil Mills Company Ltd* (Singida). Taarifa ya ukaguzi huo itawasilishwa kwenye taasisi zinazohusika.

117. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imefunga mtambo mdogo wa kupima ubora wa majiko yanayotumika kupikia majumbani, ikiwa ni sambamba na upimaji wa hewa/gesi zilizopo katika nishati mbalimbali (kuni, mkaa, mkaa mbadala) za kupikia majumbani ambapo zaidi ya sampuli 15 zimefanyiwa vipimo katika mtambo huo. Mtambo huo umefungwa katika ofisi za TIRDO Dar es Salaam ambapo watengenezaji mbalimbali wa majiko hayo kama vile TATEDO na watu binafsi wanashauriwa kurekebisha majiko yao endapo hayakidhi ubora unaotakiwa.

118. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imeendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani na kwa taasisi mbalimbali. Huduma zilizotolewa ni za upimaji wa kiwango cha uchafuzi wa mazingira kutohana na shughuli za uzalishaji viwandani. Viwanda na taasisi zilizopata huduma hizo ni pamoja na *Kilimanjaro Biochem Ltd, Tanzania Cigarette Public Ltd Company, Serengeti Breweries Ltd* Dar es Salaam, *TANESCO - Nyumba ya Mungu Power Plant* na Kiwanda cha Mabati cha ALAF. Katika kulinda mazingira, Shirika limetoa huduma za namna hiyo kwa miradi ya kimkakati kama

Mradi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway) katika kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupora.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa kushirikiana na COSTECH imefanya utafiti wa matumizi ya pumba na mapapai katika uchakataji ngozi zikiwa kemikali mbadala na mwongozo umeandaliwa tayari kwa matumizi katika Kongani la Ngozi la Kiwango liliopo SIDO Usangi lenye wanakongani 15. Pia, TIRDO kwa kushirikiana na COSTECH na SIDO imewajengea miundombinu ya kusindika ngozi ya Kongani ya Ngozi ya Kiwango. Miundombinu hiyo itatumiwa na vikundi vingine vitano (5) vya vijana vya usindikaji na kutengeneza bidhaa za ngozi vilivyoanzishwa.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa kushirikiana na COSTECH imebuni na kutengeneza chujio maalum la kuchuja tanini kutoka kwenye magome ya miti kwa ajili ya kusindika ngozi ikiwa ni mbadala wa kemikali sumu ya *kromiam*. Chujio hilo limekabidhiwa kwa Kongani la Kiwango kwa matumizi ya uchujaji dawa kwa ajili ya kusindika ngozi. Aidha, TIRDO imefanikiwa kupata ruzuku ya kukamilisha mtambo wa kuongeza thamani ya taka ngumu za ngozi kwa kutengeneza *leather board* na kwamba mchakato wa kufunga mtambo unaendelea. Shirika limefanya manunuzi ya vifaa kama vile *Photometer* itakayowezesha kitengo kuendelea na mchakato wa kuhakiki maabara ya mazingira. Vilevile, maabara imeshiriki katika upimaji wa sampuli za uthibitisho wa njia za upimaji wa *BOD*, *COD*, *Turbidity* na *TSS* ikiwa ni kigezo kimojawapo katika uhakiki wa maabara. Maabara pia imefanya ukarabati wa baadhi ya vifaa kama vile vya kupimia vumbi.

121. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imeweza kufanya upimaji wa sampuli za chakula na maji katika harakati za kuijandaa na mahitaji ya kupata ithibati (Accreditation) ya maabara hiyo. Maabara ya Chakula imeweza kuhakiki jumla ya sampuli 98 kwa ajili ya bidhaa za viwandani na hotelini kwa ajili ya kukidhi ubora unaohitajika.

Wateja wakubwa wa maabara hiyo ni viwanda, hoteli na Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

122. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO imefanya mashindano ya kimaabara kwa sampuli za unga lishe, karanga, chai, chumvi na pilipili. Maabara hiyo imeweza kuhakiki sampuli tisa (9) kwa wateja wanne (4). Katika jitihada za kuhakiki maabara hizo (Accreditation), wafanyakazi wapatao 27 wa maabara wamepatiwa mafunzo ya mfumo wa uhakiki wa maabara ISO17025/IEC 2017.

123. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TIRDO kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imeendeleza Mradi wa Teknolojia ya Kuzalisha Mwani na mazao yake yenye ubora kupitia ufadhili kutoka TEA. Aidha Mradi huo unaendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Kaskazini Pemba, Zanzibar ambapo TIRDO imefunga mtambo wenye teknolojia ya kukausha Mwani kwa kutumia nishati ya jua na *biomass* katika kijiji cha Makangalae. Kupitia Mradi huo wajasiriamali wamenunuliwa mashine ya kusagia Mwani baada ya kuukausha. Pia, TIRDO imetoa elimu ya uzalishaji na usindikaji wa Mwani kwa wajasiriamali 300 katika Kisiwa cha Pemba. Lengo ni kuwafundisha wajasiriamali 400, ambapo wajasiriamali 100 watatoka Kisiwani Unguja.

124. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia CAMARTEC imebuni na kuanza kutengeneza tela la kupakia mashine ambayo ilinunuliwa kwa lengo la kurahisisha kazi ya kuvuna Chikichi kwa kumpandisha mvunaji juu na kumshusha akiwa na matunda yaliyovunwa. Pia, Kituo kimehuisha mashine ilioingizwa kutoka nje ya nchi mahsus kwa ajili ya kutenganisha makademia nuts na maganda yake ili kuihuisha ifae kutenganisha viini vya chikichi na maganda yake baada ya kubanguliwa. Mashine imefanyiwa majaribio ya awali (on-station testing) CAMARTEC, kisha kupelekwa mkoani Kigoma ambako imefanyiwa majaribio ya kina ya utendaji wake (performance testing). Pia, CAMARTEC imebuni na kuunda kipandio cha kupanda

mbegu za mafuta (ufuta, alizeti, pamba na karanga) ili kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao yenyе kutoa mafuta ya kula nchini.

125. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia CAMARTEC inaendelea na matengenezo ya teknolojia za kulima, kupanda na kuchakata mazao mbalimbali. Teknolojia hizo ni trekta dogo aina ya 'CAMARTECFastTrucktor - CFT , vipandio vya mbegu; mashine za kubangua Korosho; jiko sanifu la kuni la kuchemshia Korosho; mashine za kupura mazao; na mashine za kuchakata na kufunga malisho ya mifugo.

126. Mheshimiwa Spika, Ili kusogeza huduma kwa wadau na kuongeza matumizi ya teknolojia katika uzalishaji vijiji, Wizara kupitia CAMARTEC inaanzisha Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (Engineering Technology Hub-ETH) katika Kijiji cha Mwandete kilichoko Wilaya ya Maswa katika Mkoa wa Simiyu. Teknolojia zinazohitajika kwa matumizi ya 'Hub hiyo zinaendelea kuandaliwa.

127. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia CAMARTEC ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali na kuwawezesha kutengeneza teknolojia zilizothibitishwa na zinazohitajika na wadau. Wajasiriamali waliofundishwa na kuwezeshwa ni pamoja na *Sumary Engineering Works – Kutengeneza mashine za kukatakata malisho ya mifugo (Forage chopper) na mashine ya kufunga majani kwa ajili ya mifugo (Baler); na Jowog Enterprise – Kutengeneza mashine ya kupura mtama na uwele inayokokotwa na Wanyamakazi*. CAMARTEC pia iliwaytembelea wadau wa korosho katika Wilaya ya Manyoni katika Mkoa wa Singida ili kuona uwezekano wa kusambaza mashine za kubangua korosho baada ya kutoa mafunzo, ambapo ilibainika kuwa uhitaji wa mashine hizo ni mkubwa sana. Vilevile, Kituo kilitembelea vikundi vya wadau wanaofuga ngombe wa maziwa na kuyasindika katika Wilaya ya Hai katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kuhawilisha teknolojia za

kukatakata na kufunga malisho ya mifugo ili kupunguza upotevu wa majani na hatimaye kuongeza uzalishaji wa maziwa.

128. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Bodi ya Dawa (MSD) asilimia 90 ya vifaa tiba vinaingizwa na Serikali kutoka nje ya nchi (MSD, 2022). Ili kuweza kutoa suluhisho la changamoto hiyo, TEMDO imekamilisha ujenzi wa eneo maalum la karakana litakalokidhi ubora wa viwango vya kutengeneza na kuhifadhi vifaa tiba. Ununuzi wa mashine mbalimbali za aina tano (5) kwa ajili ya mradi upo kwenye hatua za mwisho. TEMDO imetengeneza vifaa vya Hospitali ambavyo ni vitanda vya kujifungulia (*delivery beds*), vitanda vya kawaida (*normal hospital beds*), *drip stand*, vitanda vya uchunguzi (*examination tables*) na kabati ndogo za wodini zenyе gurudumu na zisizo na gurudumu. Vifaa hivyo vimekaguliwa na vimepitishwa na Mamlaka husika ya TMDA na MSD na TEMDO imepewa Ithibati inayoruhusu kuendelea kutengeneza vifaa tiba na kuvisambaza kwenye Hospitali mbalimbali hapa nchini. TEMDO tayari imepokea maombi ya kutengeneza vifaa tiba 150 vinavyojumuisha vitanda vya kawaida, vitanda vya kujifungulia na vitanda vya uchunguzi. TEMDO ina lengo la kujiimarisha zaidi kwenye uzalishaji wa aina mbalimbali za vifaa tiba vinavyohitajika nchini ili kuisaidia Serikali kupunguza gharama na matumizi ya fedha za kigeni. TEMDO inaendelea na usanifu wa vifaa vingine vya hospitali ambavyo ni *gynecologic examination bed, cardiac table, office table for food serving*, vitanda machela (*stretchers*), skirini za kukunja (*folding screen*) na majokofu ya kuhifadhia miili (*mortuary cabinets*) ya ngazi 3, 6 na 12.

Aidha, kutokana na mahitaji ya soko la teknolojia ya vichomea taka (incinerators), TEMDO inaendelea na usanifu wa kutengeneza mtambo (incinrators) wenye uwezo wa kuteketeza dawa za hospitali zilizoharibika (one tonne per batch), nyama za mifugo zisizofaa kwa matumizi ya binadamu na uteketezaji wa damu isiyo salama.

5.2.4 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

A. Ujenzi wa Miundombinu ya Mitaa ya Viwanda ya SIDO

129. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SIDO katika mwaka 2021/2022 ilipanga kujenga majengo ya viwanda (Industrial sheds) kwa ajili ya viwanda kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya pamba, korosho na mbegu za mafuta ya kula katika Mikoa ya Shinyanga (Kahama), Mtwara, Singida (Manyoni) na Tanga (Lushoto). Hadi Mwezi Machi, 2022 upembuzi yakinifu umefanyika, michoro ya kihandisi (architectural drawings) imeandaliwa na gharama zimeainishwa. Aidha, ujenzi wa majengo matano (5) yanayojumuisha Mikoa ya Mwanza (1), Katavi (2) na Morogoro (2) pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda katika Mikoa ya Kagera (uzio na mtaro), Kigoma (barabara na mitaro) na Chato - Geita (uzio, barabara na mitaro) umekamilika.

B. Uzalishaji Teknolojia kwa Matumizi ya Viwanda Vidogo na vya Kati

130. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SIDO inaendelea kuboresha Vituo vya Kuendeleza Teknolojia (TDC), ambapo katika kipindi cha Mwaka 2021/2022, Vituo viwili (2) vilivyopo katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya vinaendelea kufanyiwa maboresho. Kwa sasa gharama za mahitaji ya mashine na vipimo (specifications) zimeainishwa, taratibu za manunuzi zimefanyika na mzabuni amepatikana. Aidha, pamoja na maboresho yanayoendelea, Vituo saba (7) vya SIDO vya kuendeleza teknolojia (TDCs) vilivyopo katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Lindi na Shinyanga kwa mwaka 2021/2022, vimeweza kuzalisha mashine 313 na vipuri 1,014 ambavyo vilizwa kwa wajasiriamali. Vituo hivyo pia vinajihuisha na uendelezaji wa teknolojia na kutoa huduma za kiufundi kwa viwanda vidogo na vya kati mjini na vijiji katika mikoa husika kwa kuzingatia Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (ODOP) na fursa za kimasoko zinazojitokeza.

131. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kupitia SIDO imeweza kutoa mafunzo na ushauri mbalimbali kwa wajasiriamali wahitaji 26,800 katika maeneo ya uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji viwandani ambapo wajasiriamali 15,176 walipata mafunzo na wajasiriamali 11,624 walipata huduma ya ushauri. Aidha, mafunzo na huduma za ushauri wa kibashara na ufundi kwa wajasiriamali hutolewa katika nyanja za ufundi, uchumi, uongozi, masoko, ubora wa bidhaa, teknolojia, ubunifu, usanifu na uandaaji wa chambuzi yakinifu za miradi ya viwanda na biashara na kwa vikundi/vyama vya wajasiriamali kwa lengo la kuviimarissha na kuviwezesha kujenga msingi wa kujitegemea katika Sekta ya Viwanda na Biashara Ndogo na za Kati.

c. Kuongeza Fursa za Upatikanaji wa Masoko kwa Wajasirimali

132. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2021/2022, Wizara kupitia SIDO iliandaa Maonesho ya SIDO Kitaifa Wilayani Kasulu, Mkoani Kigoma na kushiriki Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF). Jumla ya Wajasirimali 935 na Taasisi 38 zilishiriki katika Maonesho ya SIDO Kitaifa yaliyofanyika Mkoani Kigoma. Aidha, Mauzo yenye thamani ya Shilingi milioni 796.9 yakiwemo ya fedha taslimu na miadi yalifanyika katika maonesho hayo.

133. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SIDO imeendelea kuhamasisha utumiaji wa bidhaa za wajasiriamali kupitia mitandao ya kijamii, radio, Iuninga, machapisho na mitandao ya kidijitali ya *SIDO Apps na web portal*. Aidha, matukio 128 na bidhaa 109 yalirushwa na kuwafikia watu 11,700. Pia, Shirika liliweza kusambaza majarida 1,500 kwa wadau na kupitia vituo vilivyopo ofisi za Mikoa. Vilevile, imeweza kutangaza bidhaa za wajasiriamali na kurusha makala kupitia TBC1 kwa muda wa miezi miwili (2) mfululizo kwenye kipindi cha 'SIDO Fahari Yetu.

134. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SIDO ilipanga kuunganisha Ofisi za Mikoa za Shirika katika Mkongo wa Taifa pamoja na mtandao wa makao makuu ya Shirika, kukamilisha kazi ya kusimika mfumo wa huduma za Masijara na kusanifu pamoja na kuunda mitandao ya ndani ya ofisi za Shirika hilo. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 Mikoa 13 ilikuwa tayari imeunganishwa katika Mkongo wa Taifa. Kukamilika kwa kazi hiyo kunafanya jumla ya ofisi za Mikoa za SIDO zilizounganishwa kwenye Mkongo wa Taifa kufikia 21. Pia, Mikoa 13 tayari imeunganishwa kwenye Mtandao wa Shirika, na kufanya jumla ya Mikoa iliyounganishwa kwenye mtandao wa Shirika kufikia 21.

135. Mheshimiwa Spika, Katika kutatua changamoto ya vifungashio kwa wajasiriamali, Wizara kupitia SIDO imeendelea kununua vifungashio kwa wingi kupitia kituo chake kilichopo katika Mtaa wa Viwanda wa Vingunguti, Jijini Dar es Salaam na kuvisambaza kwa wajasiriamali waliopo mikoani kupitia Ofisi za SIDO mikoani. Katika kipindi cha Mwaka 2021/2022, watengenezaji na wasambazaji wa vifungashio 20 walitambuliwa na kuunganishwa na wajasiriamali kupitia ofisi za SIDO Mikoani.

136. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mikopo kwa wajasiriamali, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kupitia Shirika la SIDO ilikuwa imepokea maombi ya mikopo 3,832 yenye thamani ya Shilingi bilioni 8.327, ambapo jumla ya mikopo 2,166 yenye thamani Shilingi bilioni 4.651 ilitolewa. Kati ya mikopo hiyo asilimia 47 ilitolewa kwa wanawake na kutengeneza ajira 5,321 kati ya ajira hizo 2,714 zilienda kwa wanawake. Aidha, Wizara kupitia SIDO imekuwa ikiwaunganisha wajasiriamali na taasisi za fedha kupata mitaji mikubwa kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi. Vilevile, kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali (SIDO SME - CGS), mikopo yenye jumla ya thamani ya Shilingi milioni 110 ilitolewa katika Mikoa ya Singida na Kigoma (**Jedwali Na. 18**).

5.2.5 Sekta ya Mtangamano wa Biashara

A. Majadiliano ya Biashara Kati ya Nchi na Nchi

137. Mheshimiwa Spika, Katika kukuza na kuimarisha biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Kenya, Wizara iliandaa na kushiriki kwenye Mkutano wa Saba (7) wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (Joint Trade Committee - JTC) kati ya Tanzania na Kenya uliofanyika tarehe 9 – 12 Machi, 2022 Zanzibar ulijadili masuala mbalimbali ya Sekta za Biashara, Kilimo, Forodha, Uhamiaji na Usafirishaji. Jumla ya vikwazo 30 vilijadiliwa ambapo kati ya hivyo vikwazo 10 vilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa, vikwazo vitano (5) vilifutwa kwa sababu ya kukosa taarifa za kutosha kuweza kujadiliwa, vikwazo 14 viliwekewa ukomo wa kuvitatua hadi tarehe 30 Juni, 2022 na Kikwazo kimoja kililibuliwa. Vilevile, Vikwazo sita (6) vilivyowasilishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vilisuluhishwa na kuondolewa katika orodha. Vikwazo hivyo ni: Ucheleweshaji wakati wa kupitisha mizigo mpakani kwa sababu ya taratibu za kiforodha; Ucheleweshaji wa utoaji wa vibali vyta kuagiza bidhaa za maziwa nje ya nchi; Ugumu wa taratibu za Mamlaka ya Mapato Kenya; Ugumu unaoipata Kampuni ya Taifa Gas katika kuwekeza nchini Kenya; Changamoto za kupata vibali vyta kufanyakazi kwa wataalam wa Tanzania; na kuhitajika kwa cheti cha UVIKO -19 kwa raia wa Tanzania wanaosafiri kwenda Kenya.

138. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Jamhuri ya Kenya masuala manne (4) yaliyowasilishwa na kupatiwa ufumbuzi ni: kuondolewa kwa ucheleweshaji wa vibali vyta huduma za ndege kwenye Mamlaka za Anga za Tanzania; kuzuiwa kwa kampuni ya ndege ya Jambojet ya Kenya kuendesha huduma za ndege za abiria Tanzania; Kuzuiwa kwa wahandisi wa Kenya kuingia Tanzania; na kuwepo kwa tozo ya Shilingi 5,000 kwa magari ya watalii yanayosafirisha watalii kutoka Kenya kuingia Tanzania katika mpaka wa Namanga.

139. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE kwa kushirikiana na TPSF Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na Ubalozi wa Uingereza nchini, iliratibu maandalizi ya Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza (Tanzania - UK Business and Investment Forum). Kaulimbiu ya Kongamano hilo ilikuwa ni ‘Kuimarisha Ustawi Endelevu wa Kiuchumi wa Pamoja . Kutokana na Kongamano hilo ushirikiano wa biashara kati ya Tanzania na Uingereza umeimarishwa ambapo pande zote mbili (2) zilisaini makubaliano ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

b. Majadiliano ya Kikanda

140. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika tarehe 17 - 18 Agosti, 2021 chini ya Kaulimbiu inayosema: “*Bolstering Productive Capacities in the Face of COVID - 19 Pandemic for Inclusive, Sustainable Economic and Industrial Transformation*”. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa viwanda wa SADC kwa mwaka 2020/21 ambapo ilitolewa taarifa kuwa kati ya Nchi Wanachama 16, ni nchi tatu (3) ambazo zimeridhia Itifaki ya Viwanda. Tanzania ikiwa ni nchi mojawapo ambayo hajjaridhia, inaendelea na taratibu za kuridhiwa Itifaki hiyo. Aidha, Nchi Wanachama ambazo bado hazijasaini Itifaki hiyo zilihimizwa kufanya hivyo. Kupitia Mkutano huo, Tanzania imenufaika kwa kuidhinishiwa ombi lake la kuwa Mwenyeji wa Kituo cha Kudhibiti Ugaidi katika Kanda, Aidha, Kituo husika tayari kimeshazinduliwa ambapo Tanzania itakuwa mwenyeji wa Kituo hicho kwa muda wa miaka mitatu; na kuidhinishiwa kwa Dola za Marekani 73,518.20 kwa ajili ya kuanza kutafsiri nyarakaa za msingi za Jumuiya katika Lugha ya Kiswahili. Hatua hiyo ni muhimu na inatoa fursa kwa Tanzania kuendelea kukuza na kuimarisha Lugha ya Kiswahili.

141. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Biashara, na Kikosi Kazi cha Mawaziri

wanaohusika na Mtangamano wa Kiuchumi wa Kikanda, uliofanyika tarehe 26 – 30 Julai, 2021 kwa njia ya Mtandao. Mkutano ulikuwa chini ya Uenyelekti wa Serikali ya Jamhuri ya Msumbiji na kuongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Carlos Alberto Fortes Mesquita, Waziri wa Viwanda na Biashara kutoka nchini humo. Pamoja na masuala mengine muhimu, Tanzania ilifanikiwa katika maeneo yafuatayo: Kuongezewa muda wa kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha katika bidhaa ya Sukari kutoka nchi za SADC kwa kipindi kingine cha miaka mitatu (3) kuanzia Septemba, 2020 hadi Septemba, 2023. Katika Mkutano huo, Tanzania iliahidi kuendelea kutimiza masharti yanayoendana na utekelezaji wa Upendeleo Maalum wa Kiushuru (Tariff Dispensation) na iliomba kuruhusiwa kutoa taarifa pale ambapo patakuwa na changamoto ya utekelezaji wake.

142. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilishiriki katika Kikao Kazi cha waratibu wa masuala ya Jumuiya ya Nchi zilizopo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Ream Association-IORA) tarehe 13-16 Septemba 2021, Zanzibar. Lengo kuu la kikao hicho lilikuwa ni kujipanga na kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika majadiliano mbalimbali katika Jumuiya ya IORA. Hivyo, katika kikao hicho ilisisitizwa kuwa ni wakati muafaka sasa wa Tanzania kuona umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika Jumuiya ili kuchangamkia fursa mbalimbali zitokanazo na Uchumi wa Buluu na pia kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika jumuiya hiyo.

143. *Mheshimiwa Spika*, Kikao kazi kilipanga vikundi kazi nane (8) vya ndani kulingana na uendeshaji wa Jumuiya. Vikundi kazi hivyo ni:- Masuala ya Ulinzi na Usalama wa Bahari; Masuala ya Sayansi; Teknolojia na Ubunifu; Biashara na Uwekezaji; Masuala ya Utalii na Utamaduni; Masuala ya Kupambana na Maafa, Uvezeshaji Wanawake Kiuchumi; Masuala ya Uvvi; na Uchumi wa Bluu. Aidha, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Mratibu na Kiongozi wa kikundi kazi cha Biashara na Uwekezaji na mratibu msaidizi ni Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda – Zanzibar. Vilevile, vikundi kazi

vyote vya kitaifa vilivyooundwa viliombwa kufanya kazi sambamba na vikundi kazi vya IORA ili kuboresha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya hiyo.

144. Mheshimiwa Spika, Wizara ilianda kikao cha wataalam wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Biashara ya Huduma kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya Biashara ya Huduma ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) kuanzia tarehe 13 – 17Desemba, 2021 mjini Moshi, Kilimanjaro. Mkutano huo ulipitia masuala mbalimbali yanayoendelea katika majadiliano ya Biashara ya Huduma ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA). Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na *GATS PLUS* na *GATS Minus in respect to Trade in services Offers*, Kanuni ya *Reciprocity* dhidi ya kanuni ya *Most Favored Nation*, uthibitishaji wa *offer za biashara ya Huduma, njia ya kuthibitisha offer* (Comments on the Verification methodology), na kupitia *offerya Jumuuya ya Afrika Mashariki* dhidi ya maombi mbalimbali. Masuala hayo yaliyojadiliwa katika hatua hizo za majadiliano ya utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji kwa Eneo Huru la Biashara ni muhimu kwa kuwa yanatoa picha namna nchi itavyonufaika na AfCFTA.

145. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki katika Kikao cha Kamati ya Biashara ya Huduma ya Eneo Huru la Biashara la Afrika kilichofanyika mjini Accra- Ghana kuanzia tarehe 01 – 05 Novemba 2021. Masuala yaliyojitokeza na kujadiliwa ni pamoja na kupitia mwongozo wa kupitisha *offer za nchi wanachama*, kuangalia namna ya kuanza kwa Biashara ya Huduma kwa nchi wanachama na taarifa za *offer zilizofanyiwa maboresho na nchi wanachama*. Vilevile, Wizara inashiriki katika maandalizi ya *Itifaki ya Uwekezaji* ya Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA Investment Protocol) na rasimu ya itifaki hiyo imeendelea kujadiliwa katika ngazi ya Watalam wa Nchi Wanachama kwa lengo la kuhakikisha Nchi Wanachama wanavutia na kukuza uwekezaji wenye tija na endelevu.

146. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Mkutano wa kupitia Kanuni na Sheria ya Sokola Pamoja la Biashara ya Huduma ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 23 – 25 Oktoba, 2021

Jijini Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine, kikao kilijadili kwa kina kuhusu uhuru wa watu kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine kwa mujibu wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya na kuona kuwa kuna umuhimu wa kuboresha eneo hilo kwa kuwa litarahisisha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja.

c. Majadiliano ya Kimataifa

147. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa Mawaziri wa G33 ndani ya WTO tarehe 16 Septemba, 2021 kwa njia ya mtandao. Kundi hilo linajumuisha nchi zenyе maslahi yanayofanana katika eneo la Kilimo. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujadili namna ya kuboresha Sekta ya Kilimo kwa kuzingatia madhara ya mlipuko wa UVIKO-19 duniani pamoja na kuwa na azimio la pamoja katika suala hilo katika Mkutano wa 12 wa Mawaziri wa WTO. Baadhi ya masuala ya msingi yaliyotetewa na Tanzania na baadaye kupitishwa katika azimio la pamoja ni: Nchi kuendelea kupata ridhaa ya kuwa na mpango wa kuhifadhi chakula kwa ajili ya usalama wa watu wake (food stockpiling program); na ruzuku kwa Sekta ya Kilimo ili kuendelea kuhamasisha uzalishaji.

148. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 15 wa Mawaziri uliozikutanisha nchi wanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) uliofanyika tarehe 3 hadi 7 Oktoba, 2021 kwa njia ya mtandao. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulifanya maamuzi muhimu yatakayoongoza uendeshaji wa Shirika hilo kwa kipindi cha miaka minne ijayo kuanzia mwaka 2022 ambapo kwa kushirikiana na mashirika mengine litaweza kuzisaidia nchi zinazoendelea kurejea katika hali zao za kawaida kiuchumi kufuatia janga la UVIKO-19. Katika Mkutano huo, Tanzania ilizitaka Jumuiya za Kimataifa kuruhusu uzalishaji wa dawa pamoja na chanjo dhidi ya UVIKO-19 kwa nchi zinazoendelea katika masharti nafuu. Aidha, Tanzania ilipendekeza Shirika la UNCTAD kwa kushirikiana na mashirika mengine kuendelea kutoa

misaada ya kiufundi na kifedha katika Sekta ya Uzalishaji hususan kilimo ambayo imeathirika zaidi kutokana na UVIKO-19. Masuala hayo pamoja na mengine yalipitishwa katika azimio la pamoja la Mawaziri ambalo lilipangwa kuwasilishwa katika Mkutano wa Mawaziri wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) uliopangwa kufanyika Disemba, 2021 lakini ukaahirishwa kutokana na mlipuko wa virusi vipya vya UVIKO-19.

D. Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani

149. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Committee on Trade Facilitation – NCTF) inaendelea na hatua za utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani kwa kuendelea kuandaa miradi ya kutekeleza maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda na msaada wa kifedha na kiufundi katika kuyatekeleza. Aidha, kupitia Kamati hiyo, Wizara inaendelea na utaratibu wa kupunguza taratibu zinazotakiwa katika kuingiza na kuuza bidhaa ndani na nje ya nchi kupitia mfumo wake wa utoaji taarifa za biashara kwa njia ya mtandao (Tanzania Trade Portal). Mfumo huo unawasaidia wafanyabiashara kufanya maamuzi yenye tija baada ya kupata taarifa sahihi.

5.2.6 Sekta ya Maendeleo ya Biashara

A. Kuwezesha Upatikanaji wa Fursa za Masoko

150. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) yaliyofanyika tarehe 28 Juni hadi 13 Julai, 2021, Jijini Dar es Salaam na Maonesho ya Sita (6) ya Bidhaa za Viwanda yaliyofanyika tarehe 3 hadi 9 Desemba, 2021 katika Viwanja vya Maisara Zanzibar. Lengo la Maonesho hayo ni kutoa fursa kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Biashara kujitangaza na kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali zikiwemo kilimo, elimu, fedha, nishati, maji, bidhaa za viwandani, usafirishaji, afya, ujenzi, mawasiliano,

madini, ardhi na makazi, burudani na michezo. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na maonesho hayo ni: Jumla ya Kampuni 3,002 zilishiriki katika Maonesho ya 45 ya DITF ambapo, kati ya hizo kampuni 2,926 ni za nchini na 76 kutoka nchi 16 na watembeleaji 177,390; Kampuni na Taasisi 113 zilishiriki Maonesho ya Sita (6) ya Bidhaa za viwanda Zanzibar. Hati za makubaliano kwa ajili ya mauzo ya bidhaa na mazao mbalimbali yenye thamani ya Shilingi bilioni 13.3 zilisainiwa kupitia mikutano ya Kibiashara (B2B) iliyyoratibiwa kwa njia ya Mtandao na kuwashirikisha jumla ya wafanyabiashara 167 kutoka ndani na nje ya nchi; na Shughuli mbalimbali wakati wa maonesho zilitoa fursa za ajira za muda zipatazo 1,200.

151. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TANTRADE iliratibu ushiriki katika maonesho na misafara ya kibiashara ambapo jumla ya Kampuni 382 zimefanikiwa kushiriki katika Misafara, Makongamano na Maonesho yaliyyoratibiwa katika nchi za Afrika Kusini, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uturuki na Uingereza. Kupitia ushiriki huo, Kampuni hizo zimefanikiwa kujitangaza, kujifunza na kutafuta masoko ya bidhaa zao. Makubaliano yafuatayo yalifikiwa:-

i. Kuingia Mkataba wa Makubaliano kati ya Sekta Binafsi ya Tanzania na Chemba ya Burundi ya kuendesha masoko ya pamoja mipakani (Kigoma Business Hub). Utekelezaji wa mkataba huo utawezesha kuimarisha biashara katika nchi hizi mbili (2);

ii. Kampuni ya *Wadi Degla Holding* iliyopo nchini Misri inayojishughulisha na ujenzi wa viwanja vya michezo, hoteli, migahawa na maeneo maalum ya viwanda imeingia makubaliano na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya kuwekeza nchini;

iii. Kampuni tano (5) za Kitanzania zinazojihusisha na kilimo, viwanda na huduma zilisaini Mkataba wa Ushirikiano na wafanyabiashara wa Burundi na kubaini fursa za uwekezaji katika Ziwa Tanganyika;

iv. Kujenga uhusiano na wamiliki wa viwanda utakaowawezesha kununua teknolojia ya uzalishaji bidhaa mbalimbali kwa bei nafuu zaidi hivyo kuepukana na udalali ya biashara ya teknolojia ya kilimo, madini, vipuri vya mashine na magari;

v. Majadiliano na Wamiliki wa Viwanda vinavyozalisha Mashine za Vipuri vya aina mbalimbali katika Sekta ya Kilimo yanaendelea ili kuwezesha kampuni za nchini Uturuki kufungua matawi ya viwanda vyao nchini Tanzania; na

vi. Kampuni ya *UK DIT Agri Techimeonesha* nia ya kuwekeza katika Sekta ya Kilimo. Vilevile, Kampuni ya *Perry Engineering* imetaka kuwekeza katika mashine za kilimo. Jumla ya wafanyabiashara saba (7) wa Alizeti walishiriki katika msafara wa biashara kwenye nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambao walipata fursa ya kutafuta masoko ya bidhaa katika nchi hiyo.

152. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE imeratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Maonesho ya *Expo 2020 Dubai* yaliyoanza tarehe 1 Oktoba, 2021 na kumalizika rasmi tarehe 31 Machi, 2022, ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi 192 zilizoshiriki. Kupitia Maonesho hayo, Tanzania imetangaza Miradi ya Kimkakati ya ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA, Nishati, Reli, Barabara, Bandari, Madaraja, Viwanja vya Ndege, Kilimo, Uvuvi, Mifugo na vivutio vya Utalii. Lengo ni kuvutia na kuhamasisha Wawekezaji kuwekeza na kutangaza fursa za kibashara, kuvutia watalii na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

153. Mheshimiwa Spika, Mafanikio yaliyopatikana kutokana na Maonesho hayo ni pamoja na:-

i. Kusainiwa kwa Hati za Makubaliano 37 zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 8.5 sawa na Shilingi trilioni 18.5 ambapo Hati 12 ni baina ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara na Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, Hati 23 ni baina ya kampuni binafsi kutoka Tanzania na kampuni nyingine

zenye nia ya kushirikiana katika sekta za kiuchumi, Hati moja (1) ni baina ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar na Wawekezaji kwenye Sekta ya Utalii. Aidha, sekta zinazotarajiwa kunufaika na makubaliano hayo ni pamoja na nishati, kilimo, utalii, miundombinu, usafiri na teknolojia. Idadi ya ajira zaidi ya 200,000 zinatarajiwa kupatikana kutokana na makubaliano yaliyofikiwa;

ii. Kampuni na Taasisi za Sekta Binafsi 640 kutoka Tanzania na Jumuiya ya Watanzania waishio nje ya nchi zilishiriki kwa nyakati tofauti katika kipindi cha miezi sita (6) kwa lengo la kujitangaza na kukutana na Wabia wa kibiareshara katika Sekta mbalimbali. Aidha, mikutano 101 ilifanyika ndani ya banda la Tanzania kati ya Taasisi hizo na wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali; na Programu 11 za kutangaza sekta za kilimo, madini, utalii, afya, ujenzi, miundombinu, usafirishaji, mifugo, uvuvi, nishati, maji, sanaa na utamaduni ziliratibiwa kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo katika sekta hizo. Kadhalika, makongamano matatu (3) ya utalii, uwekezaji na kilimo yaliratibiwa;

iii. Bidhaa za Kahawa, Chai, Korosho, Vito vya *Tanzanite, Essential oils* za Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC), vipodozi vya asili (nazi, mwani na viungo), ngozi, mkonge, sanaa za mikono na ubunifu zilifanikiwa kuuzwa katika mfumo wa soko la kmtandao la *Expo 2020 Dubai uiitwao World Souq*; na

iv. Jumla ya watembeleaji 928,469 kutoka mataifa mbalimbali wametembelea Banda la Tanzania kwalengo la kuona fursa za utalii, uwekezaji na biashara zilizotangazwa. Aidha, watembeleaji hao pia walipata fursa ya kujifunza mila, desturi na tamaduni za Watanzania; na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

154. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu Kongamano la Wadau wa Alizeti, Maonesho pamoja na Mikutano ya kibiareshara (B2B) kuanzia tarehe 10 – 15 Agosti, 2021 Mkoani Singida ambapo jumla ya wadau 364 wa Alizeti walishiriki. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na uratibu wa matukio

hayo ni pamoja na: Jumla ya wasindikaji wa Alizeti 16 kutoka mikoa mbalimbali waliingia mikataba ya Kilimo cha Mkataba na wakulima zaidi ya 32,000 ndani ya nchi chini ya Wizara ya Kilimo. Aidha, Kampuni saba (7) ambazo ni wajumbe wa Umoja wa Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti Nchini (TASUPA) waliratibiwa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa ajili ya mikutano ya kibashara na makampuni yanayosambaza mafuta ya kula na bidhaa za walaji nchini humo, pamoja na kuangalia fursa za kibashara kwa bidhaa zitokanazo na mbegu za alizeti, kama vile mafuta, mashudu, vipodozi, sabuni, na nta ya alizeti. Lengo ni kuwezesha Sekta Binafsi kuwa na fursa pana ya masoko ya bidhaa wanazozalisha kwa nchi za EAC na SADC.

155. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia TANTRADE imefanya majadiliano na wanunuzi mbalimbali kwa kushirikiana na Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nje ya nchi, ambapo fursa za masoko ya bidhaa zifuatazo zilipatikana: Kampuni ya *DLYLK For Food Trade* ya Qatar imeingia mkataba na Kampuni ya *Borema Affairs* ya nchini Tanzania wa kupeleka nyama ya mbuzi na kondoo tani 120 kwa mwezi. Aidha, machinjio matatu (3) yanayomilikiwa na Kampuni za: *TanChoice - Kibaha*, *Eliya Food Industries-Arusha* na *Alpha Choice* yamekidhi vigezo na Kampuni hizo zipo tayari kuanza mazungumzo ya uuzaji wa tani 100 za nyama ya ngombe kila mwezi kwa Kampuni ya Panda kutoka Saudi Arabia.

156. Mheshimiwa Spika, Pia, Wizara imefanikisha Kampuni tisa (9) kutoka Tanzania kupata nafasi ya kushiriki Maonesho ya Saba ya Kahawa na Chokoleti yaliyofanyika nchini Saudi Arabia kuanzia tarehe 8 hadi 12 Desemba, 2021. Kampuni hizo ziliweza kutangaza bidhaa wanazozalisha kama vile kahawa, chai, korosho, kashata na viungo na kuingia makubaliano na wanunuzi; na Kuratibu zoezi la ukaguzi wa ubora na usalama wa asali kwa Kampuni 22 kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa ya nchini Saudi Arabia. Kampuni zitakazokidhi viwango vya ubora unaohitajika zitaunganishwa na wanunuzi wa Saudi Arabia ambao wapo tayari kununua asali kutoka Tanzania. Vilevile, Wizara

imefanikisha upatikanaji wa Soko la Asali nchini Saudi Arabia ambapo kampuni 22 zinakamilisha taratibu za ukaguzi wa ubora unafanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya nchini Saudi Arabia. Mara baada ya kukamilika zoezi hilo, Kampuni hizo zitaunganishwa na wanunuzi wa asali waliopo nchini Saudi Arabia.

157. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE kwa kushirikiana na Kituo cha Biashara ya Kimataifa (ITC) pamoja na Umoja wa Wadau wa Viungo nchini (TASPA) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) imefanikisha uzinduzi wa Nembo ya Viungo vya Tanzania (Tanzania Spice Label) katika Maonesho ya 45 ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) tarehe 9 Julai, 2021. Nembo hiyo itawasaidia wazalishaji wa viungo wa Tanzania kuweza kupata masoko na kuongeza ushindani wa bidhaa hizo katika soko la ndani na la kimataifa ambapo jumla ya Kampuni 10 zimekidhi vigezo vya kutumia Nembo hiyo.

158. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Posta ilizindua uendeshaji wa Duka Mtandao lijulikanalo kama *Posta e-Shop* kwa lengo la kupanua fursa za masoko kwa wazalishaji wa bidhaa nchini. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Februari, 2022 duka mtandao lila wafanyabiashara 800. Elimu zaidi inatolewa ili kuwafahamisha wafanyabiashara nchini kutumia fursa hiyo ya duka mtandao. Sambamba na hilo, Mamlaka inakamilisha taratibu za kutoa huduma saidizi za kibiashara kupitia Mfumo wa *eTradeDesks* ambao utarahisisha kutoa huduma kwa kampuni zinazofanya biashara kwa njia ya mtandao. Mamlaka pia imefanikiwa kuratibu kampuni za Kitanzania 58 na Mtandao wa *JD World Wide* wa nchini China kwa lengo la kupanua wigo wa masoko wa bidhaa za Tanzania.

159. Mheshimiwa Spika, Vilevile, Wizara kupitia TANTRADE imepata fursa ya kutangaza bidhaa za Tanzania katika mtandao maarufu unaojulikana kama *JD.com* kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini China. Ili kuhakikisha kampuni za Kitanzania zinatumia fursa hiyo ipasavyo, TANTRADE

imefanya uchambuzi wa Kampuni za Kitanzania ili kutambua bidhaa zilizokidhi vigezo vya kuunganishwa na mtandao huo. Hadi kufikia, Mwezi Machi, 2022 jumla ya Kampuni 58 za Kitanzania zilipatikana na kuunganishwa na mtandao huo.

160. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) na Taasisi inayosimamia Kongani ya Mwani Zanzibar Seaweed Cluster Initiative (ZASCI) ilifanya tathmini mbili (2) za biashara ikihusisha wafanyabiashara wa mchele kutoka Tanzania Bara na vikundi 28 vya wakulima, wasindikaji na wafanyabiashara wa zao la Mwani Unguja na Pemba ili kutambua changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

- i. Wafanyabiashara wa mchele kuunganishwa na masoko ya uhakika kwa upande wa Zanzibar;
- ii. Kuwezesha maandalizi ya ujenzi wa mtambo wa kukaushia Mwani kwa kutumia jua; na
- iii. Kuwezesha fursa za ununuzi wa mashine ya kusaga Mwani kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) ili kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko.

161. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE iliratibu majadiliano ya Kibashara ya wanunuzi kutoka nchi mbalimbali kama vile China, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa lengo la kufungua fursa ya kuuza mazao mbalimbali ikiwemo nafaka, karafuu, mchele, muhogo, soya na bidhaa nyingine. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Soko la karafuu tani 2,000 kwa mwezi kutoka Zanzibar (ZSTC) kuuzwa katika Falme

za Kiarabu (Dubai); Soko la mchele tani 60 kwa wiki kwenda nchini Kenya unauzwa na kampuni nne (4) za *G2L Limited*, Katani Rice, *Tarmo Rice na Ruaha Milling*; Bodi ya Nafaka kufungua ofisi ya bidhaa za Nafaka nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (Lubumbashi) na Kenya; Kampuni ya *Quality Pulse Exporters (QPE)* iliingia makubaliano ya kuuza soya tani 2,000 kwa Kampuni ya China ambapo biashara inatarajiwa kufanyika kuanzia msimu wa Mwezi Mei hadi Septemba, 2022. Pia, Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi cha Kilimanjaro kilifanikiwa kuuza jumla ya jozi 450 za viatu kupitia Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF); Soko la muhogo tani 600 ambapo wakulima kutoka Mkuranga walifanikisha kuiuzia Kampuni ya *Dar-Canton na Dalyon*. Aidha, Bodi ya Nafaka ilinunua tani 100,000 kutoka kwa Wakulima wa Mikoa ya Dodoma na Singida.

162. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia TANTRADE ilifanya tafiti kuhusu biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za ukanda wa Afrika Mashariki zikiwemo Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya na Uganda kwa lengo la kubaini fursa, vikwazo na changamoto za kibiashara zilizopo. TANTRADE imefanikiwa kutambua mazao na bidhaa mbalimbali zinazohitajika kwa wingi katika nchi hizo ambazo ni pamoja na nafaka, madini (chuma na dhahabu), mazao ya mbogamboga na matunda. Taarifa za fursa zimesambazwa kwa Wizara na Sekta za uzalishaji za Kilimo, Uvubi, na Mifugo.

163. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia TANTRADE inasimamia uanzishwaji wa Mradi wa Uongezaji Thamani wa Zao la Dagaa wenye thamani ya Dola za Marekani 1,855,925 utakaotekelezwa kwa muda wa miaka mitano (5) chini ya ufadhili wa Benki ya Afrika. Matokeo tarajiwaji ya Mradi huo ni pamoja na kuongeza mauzo ya dagaa katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na kutoa fursa ya ajira na kipato kwa wananchi wapatao 4,550 wanaojishughulisha na mnyororo wa thamani wa zao la dagaa.

b. Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Taarifa za Biashara na Masoko

164. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE imesambaza taarifa za fursa za masoko ya mazao ya Korosho, Viungo, Viazi, Nyama, Vitunguu, Asali, Nafaka na Bidhaa za Ngozi kwa wadau kutoka Umoja wa Ulaya, Falme za Kiarabu, Uganda, Misri, Malawi, Ghana na Kenya. TANTRADE pia imepokea na kujibu maulizo 251 yaliyowasilishwa na wafanyabiashara kuhusu taratibu za kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Vilevile, takwimu za biashara kati ya Tanzania na soko la Afrika Kusini, China, Indonesia, Rwanda, Singapore, Tunisia, Ubelgiji, Uingereza, Ujeruman, Urusi, Uturuki na Visiwa vya Komoro zimeandaliwa ili kutambua fursa zilizopo kibiashara katika masoko hayo. Vilevile, TANTRADE imesambaza bei za wastani za wiki za mazao ya kilimo na mifugo katika masoko ya Dar es Salaam na Dodoma na kuhuisha taarifa za Kampuni 1,315 kwenye Kanzidata ya Wafanyabiashara.

165. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) imefanya zoezi la ufuatilaji na tathmini ya mwenendo wa usambazaji wa bei ya vifaa vya ujenzi Tanzania Bara katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma, Kilimanjaro, Ruvuma, Pwani, Singida Shinyanga na Mwanza. Zoezi hilo lilitokana na changamoto ya uhaba na upandaji wa bei holela kwa vifaa vya ujenzi uliojitokeza kwa kipindi cha Mwezi Septemba, 2021 hadi Novemba 2021. Tathmini iliyofanyika ilibaini kuwa upandaji wa bei unatokana na uhaba wa saruji; mifumo duni ya usambazaji bidhaa hii kuwafikia watumiaji wa mwisho na ucheleweshaji wa upatikanaji wa saruji kutoka kiwandani. Aidha, Wizara imeendelea kukusanya taarifa za bidhaa sokoni ikiwa ni pamoja na bei za mazao makuu ya chakula, mafuta ya kula, vifaa vya ujenzi (saruji, nondo na Bati) katika masoko mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kuwafahamisha wananchi na wadau wengine kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali.

166. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE imezindua Mfumo wa Kuwezesha Upatikanaji wa Taarifa za Taratibu za Kufuata Kupata Leseni na Vibali mbalimbali vyta Biashara za Kimataifa. Mfumo huo ulizinduliwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Biashara Duniani (UNCTAD), Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Taasisi ya *TradeMark East Africa*. Aidha, Mfumo huo una watumiaji 30,203 na watembeleaji 88,890 kutoka ndani ya nchi na kwenye nchi za Afrika Kusini, Marekani, Zimbabwe, Uganda, India, Kenya, China, Malawi, Zambia na Uingereza. Bidhaa zilizopata maulizo kwa wingi ni pamoja na korosho, pamba, Sanaa za mikono na magari.

167. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANTRADE imeweka mfumo wa kuhakikisha mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini zinapata masoko endelevu ambapo inashirikiana na wazalishaji katika kuunda na kuimarisha vikundi vyta wazalishaji ili kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika kuyafikia masoko yenye tija. Vikundi vilivyoimariswa na idadi ya wananchama wake ni umoja wa wadau wa Muhogo (318), Umoja wa Wadau wa Viungo (150), Wazalishaji wa bidhaa za ngozi (160) na Umoja wa Wazalishaji wa embe (150).

c. Kuendelea Kuboresha Mazingira ya Biashara

168. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia BRELA imeendelea kuimarisha na kuboresha Mifumo yake ya *Online Registration System* (ORS) na *Tanzania National Business Portal* (TNBP) ambayo hutumika kutoa huduma za kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza na Leseni za Viwanda na Biashara. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 BRELA imesajili jumla ya kampuni 7,842 katи ya 11,100 yaliyokusudiwa sawa na asilimia 71. Pia, imesajili Majina ya Biashara 15,034 katи ya 19,500 yaliyopangwa, sawa na asilimia 77 na Alama za Biashara na Huduma 2,872 katи ya 4,500 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 64 . Vilevile, BRELA imefanikiwa kutoa Hataza 23 katи ya 35 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 66, leseni za Viwanda 96 katи ya 244 zilizokuwa zimepangwa, sawa na

asilimia 39 na leseni za Biashara 8,901 kati ya 13,200 zilizokuwa zimepangwa sawa na asilimia 67.

169. Mheshimiwa Spika, Pamoja na kukamilika kwa mifumo hiyo, BRELA inaendelea kufanya maboresho zaidi katika mifumo ili kuwa rafiki zaidi kwa watumiaji ambapo hadi kufikia Machi, 2022 kazi ya kufanya maboresho kwenye mfumo imekamilika na mifumo ipo kwenye hatua ya majaribio kwa Watumiaji wa ndani (User Acceptance Test - UAT).

170. Mheshimiwa Spika, Mafanikio hayo yametokana na juhudzi za Serikali katika kuendelea kuboresha mazingira kwa kuweka mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa leseni na usajili kwa njia ya mtandao na utoaji wa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali. Ongezeko hilo pia linatokana na uimara wa Serikali katika kusimamia na kudhibiti taratibu za ufanyaji wa biashara unaozingatia sheria na kanuni zilizopo. Maboresho yanaendelea kufanyika katika mifumo ili kuwa rafiki kwa watumiaji. Mifumo ili yokamilika kufanyiwa maboresho ipo kwenye hatua ya majaribio kwa Watumiaji wa ndani (User Acceptance Test - UAT).

171. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha biashara nchini, jumla ya wadau wa biashara 257 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Geita na Kigoma walipatiwa huduma ya utatuzi wa changamoto katika Kliniki ya Biashara inayoratibiwa na TANTRADE kwa kushirikiana na Taasisi Wezeshi za Biashara zipatazo 28. Lengo la Kliniki hiyo ni kusogeza huduma karibu na maeneo ya wananchi. Aidha, jumla ya changamoto 479 zinazowakabili wafanyabiashara zilitatuliwa.

172. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia TANTRADE ilishirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Biashara na Huduma Ndogo Zisizo Rasmi (Wamachinga) katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo la Mwongozo huo ni kuwa na usimamizi na uratibu wa uendeshaji wa biashara ndogo na zisizo rasmi nchini unaotambulika kitaifa ili kukabiliana na changamoto za

ufanyaji biashara katika maeneo hatarishi katika maeneo mbalimbali mijini. Vilevile, Wizara kupitia TEMDO imekamilisha usanifu wa vibanda bora vya biashara vitakavyowezesha wajasiriamali wadogo kufanya biashara kwenye maeneo maalum yaliyotengwa kwa mpangilio. Vilevile, TEMDO ilifanya mukutano na wadau wa biashara ndogo ndogo Jijini Dodoma na Dar es Salaam Mwezi Novemba, 2021 na Januari, 2022 na kupokea maoni yao kwa ajili ya uboreshaji wa usanifu na michoro ya vibanda hivyo na utengenezaji wa chasili kwa vibanda hivyo unafanyika. Utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa kushirikiana na wataalam wa dhana ya biashara ndogo kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

173. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TANTRADE imetembelea Taasisi zinazotoa Huduma ya Uwezeshaji Biashara (Cross Border Trade Facilitation) na Kamati za Pamoja Mipakani Kukuza Biashara za Mpakani katika Vituo vya Forodha vya Rusumo kwenye mpaka wa Tanzania na Rwanda; na Mtukula kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda. Lengo kuu la ziara hiyo ilikuwa kujadili fursa na changamoto za biashara kupitia vituo hivyo ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wafanyabiashara 215 kuhusu fursa zinazotokana na matumizi ya Utaratibu wa Kiforodha Uliorahisishwa ndani ya Jumuiya Kadhalika, ziara hiyo ililenga kuwedesha wafanyabiashara nchini kuchangamkia fursa za biashara katika nchi jirani na hivyo kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini.

D. Kutoa Elimu kwa Wafanyabiashara

174. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TANTRADE imetoa mafunzo kwa wadau 134 ili kuwajengea uwezo wa taratibu za kuuza bidhaa nje ya nchi hususan katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) na kufahamu fursa za kibbiashara zilizopo katika nchi hizo. Kupitia mafunzo hayo wafanyabiashara walifundishwa mbinu za kiushindani za kutafuta masoko na kufahamu mifumo saidizi ya biashara ya kielektroniki ya kuwawezesha kupata taarifa mbalimbali

za masoko na taratibu za kufanya biashara. Mifumo hiyo ni *e-Malalamiko*, *e-Shop*, *Market Access* na *Trade Information Portal*. Vilevile, Wizara kuititia TANTRADE ilishirikiana na UNCTAD kuratibu mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo wanawake 65 katika mipaka ya Mikoa ya Kilimanjaro (Holili/Taveta), Mbeya (Kasumulu) na Songwe (Tunduma/Nakonde). Kuititia mafunzo hayo, vikundi hivyo vilipata taarifa kuhusu taratibu za kufanya biashara kuititia mipaka halali.

175. Mheshimiwa Spika, Ili kuimarisha mahusiano na Halmashauri kwa lengo la kufikisha huduma kwa umma, BRELA imeanzisha Mkakati wa kutoa elimu kwa Maafisa Biashara na Maafisa TEHAMA wa Halmashauri na Mikoa nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kuwasaidia wafanyabiashara wa maeneo yao kupata huduma za Wakala. Mpaka kufikia Mwezi Machi, 2022, Mafunzo kwa Maafisa Biashara yamefanyika katika Mikoa 14 ambayo ni: Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Mara, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Singida, Simiyu na Songwe. Jumla ya Maafisa Biashara na Maafisa Sheria 172 walipatiwa mafunzo juu ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208 na utekelezaji wake. Lengo ni kuweza kuwajengea uwezo Maafisa Biashara kuwahudumia wafanyabiashara kwa weledi na kwa haraka ili kuboresha na kurahisisha uanzishwaji na ufanyaji wa biashara nchini. Aidha, mafunzo hayo yanaendelea kufanyika katika Mikoa mingine na uhusiano kati ya BRELA na Mamlaka za Serikali za Mitaa umeendelea kuimarika.

176. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia FCC ilitoa elimu ya uelewa kuhusu masuala ya ushindani wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ushindani Duniani yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 3 hadi 06 Desemba, 2021. Kuititia Kliniki ya Ushindani pamoja na kongamano lililofanyika Siku ya Kilele cha Ushindani Duniani, watu 187 walihudhuria na kupatiwa elimu kuhusu Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003 na kutolewa ufanuzi wa masuala mbalimbali hivyo kuongeza uelewa dhidi ya bidhaa bandia

na kuwashauri kutoa taarifa FCC mara wanapobaini viashiria vya vitendo vinavyoikiuka Sheria.

177. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TBS imetoa mafunzo na semina 54 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora ikiwa ni sawa na asilimia 36 ya lengo la kufanya semina 150 kwa mwaka. Aidha, jumla ya wadau 2,433 wa sekta mbalimbali ikiwemo sekta za korosho na bidhaa za korosho, mafuta ya kupikia, maziwa na bidhaa za maziwa, zabibu, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali walipewa mafunzo juu ya masuala ya viwango.

178. Mheshimiwa Spika, FCT imeendelea kujitangaza kwa njia mbalimbali ili kuongeza uelewa katika masuala yanayohusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa Soko. Hii ikiwa ni pamoja na kupitia Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dares Salaam (SabaSaba) ambapo zaidi ya washiriki 800 walitembelea banda la Baraza. Pia, elimu ya huduma za Baraza ilitolewa kwa zaidi ya washiriki 400 walitembelea banda la Baraza wakati wa Maadhishimo ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma kuanzia tarehe 23-29 Januari, 2022. Katika Maonesho hayo taarifa fupi mbalimbali zilitolewa kwa ajili ya wadau na wananchi, elimu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu shughuli za Baraza, elimu kuhusu umuhimu wa ushindani katika maendeleo ya uchumi wa viwanda Tanzania na ushiriki wa wadau katika kuimarisha ushindani katika maeneo wanayoyasimamia ilitolewa, maswali yaliulizwa na ushauri pia ultolewa na Wadau na Wananchi Aidha, vyombo vya habari mbalimbali vilishiriki katika kutangaza shughuli za Baraza wakati wa Maonesho hayo.

179. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia BRELA imeendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, maonesho na mikutano. Msisitizo ukiwekwa katika usajili, urasimishaji wa biashara, pamoja na mabadiliko ya sheria zinazosimamiwa na BRELA kama vile kuanzishwa kwa Daftari la kuwatambua Wamiliki Manufaa wa Makampuni (Beneficial Ownership Register). Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, vipindi 45 vilirushwa kupitia vyombo vya habari

mbalimbali ikiwemo runinga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii. Kupitia vyombo hivyo uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya BRELA umeongezeka. Villevile, hadi kufikia Februari 2022 BRELA imeshiriki katika maonesho 10 yakiwemo:-

Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), Maonesho ya Madini- Geita, Maonesho ya Jumuiya ya Afrika Mashariki- Mwanza, Maonesho ya Utalii-Geita, Maonesho ya SIDO- Kigoma, Maonesho ya siku ya Posta Duniani-Dodoma na Maonesho ya *Karibu Dodoma Festival*—Dodoma na Maonesho ya Bidhaa za Viwanda Tanzania-Zanzibar. Lengo la kushiriki maonesho hayo ni kufikisha huduma za usajili, utoaji wa leseni na kutoa elimu ya biashara kwa wananchi.

180. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WRRB ilitoa mafunzo na kufanya uhamasishaji kuhusu manufaa ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Geita, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida na Songwe kwenye mazao ya Korosho, Ufuta, Kahawa, Dengi, Choroko, Soya, Kokoa na Mpunga.

181. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WMA imetoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa kushiriki kwenye Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), Tamasha la Biashara Chato, Teknolojia ya Madini Geita, SIDO Kitaifa Kigoma, Maonesho ya Uhuru Singida, Tabora na Mapinduzi Zanzibar, Maonesho ya Wajasiriamali Iringa na Maonesho ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania. Wakala iliandaa na kurusha vipindi 13 vya TV na vipindi saba (7) vya redio pamoja na kutoa taarifa 50 kwenye magazeti mbalimbali. Pia, Wakala ilitoa elimu kwa Wafanyabiashara na Wakulima wa Viazi Mviringo na Parachichi Wilaya za Njombe Mjini, Makete, Wangingombe na kwenye Baraza la Madiwani Mpwapwa, Dodoma kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi.

E. Kuimarisha Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

182. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/2022, Wizara kuititia WRRB imewezesha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika katika Mkoa wa Morogoro kwenye zao la kakao. Wakulima wa kakao katika Mkoa wa Morogoro kwa mara ya kwanza waliuza zao hilo kwa bei ya wastani ya Shilingi 4,892.50 kwa kilo kutoka kipindi cha nyuma walichokuwa wakiuza kwa bei ya wastani ya Shilingi 2,000 kwa kilo, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya bei ya awali. Aidha, Bodi imewezesha wakulima wa zao la ufuta Mkoa wa Songwe kuuza tani 348.850 zilizokuwa na thamani ya Shilingi milioni 772.8. Mfumo wa Stakabadhi uliwawezesha wakulima wa ufuta Mkoa wa Songwe kuuza zao hilo kwa wastani wa bei ya Shilingi 2,221.53 ukilinganisha na wastani wa Shilingi 1,200 hadi Shilingi 1,700 kwa wakulima waliokuwa wameuza nje ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

F. Kushughulikia Mashauri ya Uvunjifu wa Sheria ya Ushindani

183. Mheshimiwa Spika, Wizara pamoja na mambo mengine ina jukumu la kulinda ushindani wa haki na kumlinda mlaji dhidi ya tabia hadaifu katika soko ili kuepusha athari za kiuchumi. Katika kusimamia hilo, Wizara kuititia FCT imepokea mashauri mapya 22 na kufanya kuwa na jumla ya mashauri 68 kwa kujumlisha mashauri 46 yaliyokuwa hayajaamuliwa katika kipindi cha 2020/2021. Aidha, mashauri 28 yameshughulikiwa kwa kusikilizwa na kutolewa maamuzi. Mashauri 40 yanaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali.

184. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia FCC imeendelea kufanya kazi jumla ya mashauri 15 yanayohusu ukiukaji wa Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003 ambayo ni: Mashauri matano (5) ya Ukiukwaji wa Sheria ya miungano ya Kampuni bila kuiarifu FCC; Mashauri Matano (5) ya kupanga bei kiholela; na Mashauri matano (5) ya matumizi mabaya ya nguvu za soko (5). Katika mashauri matano (5) yanayohusu miungano ya Kampuni yaliyofanyika bila

kuitaarifu FCC, wadaiwa katika mashauri manne (4) waliomba kuyamaliza kwa njia ya suluhu na shauri moja (1) liliobaki lipo katika hatua za awali za uchunguzi. Katika mashauri yanayohusu kupanga bei, wadaiwa katika shauri moja (1) waliomba FCC kufanya majadiliano kwa lengo la kumaliza shauri hilo kwa njia ya suluhu na mashauri mengine manne (4) yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Aidha, katika mashauri yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko, FCC imekamilisha uchunguzi kwenye shauri moja (1) na inaendelea na uchunguzi katika mashauri mengine manne (4).

185. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia FCC ilifanya chunguzi katika masoko mbalimbali ili kubaini mienendo kandamizi na hadaifu. Hivyo, mikataba 264 iliyoandalishiwa na upande mmoja (Standard Form Consumer Contracts) ilipitiwa. Kati ya hiyo, mikataba 134 ilipokelewa katika kipindi kilichopita. Mikataba hiyo ilitoka katika Sekta Ndogo za Benki na Fedha. Mapitio ya mikataba hiyo yaliwezesha usajili wa jumla ya mikataba ya watumiaji 35. Jumla ya maombi 229 yanaendelea kushughulikiwa na yapo katika hatua mbalimbali za kupata maamuzi.

186. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia FCC, ilichambua na kuitisha maombi 37 ya miungano ya Kampuni sawa na asilimia 64 ya maombi yaliyoshughulikiwa. Katika maombi yaliyoidhinishwa, maombi 36 yaliidhinishwa bila masharti na ombi moja (1) liliidhinishwa kwa masharti yenye lengo la kulinda ushindani, kukuza uchumi pamoja na kulinda maslahi ya umma katika soko husika. Maombi yaliyoidhinishwa yalilenga kuwezesha kampuni husika kuongeza mitaji kama ilivyofanyika katika Sekta Ndogo ya Benki iliyowezesha benki zilizoungana kukidhi matakwa ya kiasi cha mtaji kinachoelekezwa na Mdhibiti ambaye ni Benki Kuu ya Tanzania; Kuongezeka uzalishaji katika Sekta ya Madini na kuwezesha kampuni husika kuongeza kiasi cha uchimbaji na kuanza kuchimba madini ya aina nyingine tofauti na ya awali mfano machimbo ya Nickel, Mkoani Kagera; Kukuza uchumi wa ndani katika Sekta ya Bima iliyowezesha Watanzania kuwa na hisa katika kampuni

husika (local content); na Kuongezeka kwa ufanisi katika uzalishaji katika Sekta ya Kilimo iliyowezesha kampuni husika kupata zana za kisasa katika kilimo.

187. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia FCC ilikamilisha utafiti wa ushindani katika soko la dawa za saratani nchini. Utafiti ulibainisha changamoto mbalimbali za kiushindani katika soko la dawa za saratani ikiwemo uwepo wa miungano ya Kampuni iliyofanyika pasipo kuwa na baraka za Tume, uwepo wa mikataba baina ya viwanda vya uzalishaji dawa za saratani na waingizaji wa dawa hizo nchini kinyume cha Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003 na uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya nguvu za soko. Pia, utafiti ulibainisha uwepo wa mikataba inayofifisha ushindani baina ya viwanda vya utengenezaji wa mashine za utambuzi na hospitali nchini kwa kupewa mashine bure kwa sharti la kununua *reagents* zinazozalishwa na watengenezaji wa mashine hizo. Hali hiyo inazuia hospitali kununua *reagents* kutoka kwa wasambazaji wengine wenye bei nafuu. Kutokana na matokeo ya utafiti huo, FCC imeanza utekelezaji wa mapendeleko ya utafiti huo kwa masuala yanayoangukia katika mamlaka yake hususan suala la miungano ya kampuni isiyotolewa taarifa kwa FCC. Aidha, FCC inatarajia kuwasilisha masuala yaliyo nje ya mamlaka yake kwa wadau wengine ikiwemo Wizara ya Afya kwa ajili ya hatua stahiki.

188. Mheshimiwa Spika, Wizara kuptitia FCC ilipokea na kushughulikia malalamiko 17 kutoka kwa watumiaji wa bidhaa au huduma zisizokidhi matarajio yao. Malalamiko 11 sawa na asilimia 65 yalitokana na bidhaa na malalamiko sita (6) sawa na asilimia 35 yalitokana na kuwepo kwa vipengele kandamizi katika mikataba iliyoandaliwa upande mmoja ambayo hajjasajiliwa na FCC. Vilevile, FCC ilipitia mikataba iliyoandaliwa upande mmoja (Standard Form Consumer Contracts) 264. Kati ya hiyo, mikataba 134 ilipokelewa katika kipindi kilichopita. Mikataba iliyopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 ilitoka katika Sekta Ndogo za Benki na Fedha.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ushughulikiwaji wa mikataba hiyo ulisababisha usajili wa mikataba 46. Mikataba iliyosalia ipo katika hatua mbalimbali za ushughulikiwaji ikiwemo ufuatilaji wa taarifa zaidi kutoka kwa waombaji pamoja na kusubiri malipo ya ada ya usajili.

189. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TBS imekamilisha maandalizi ya viwango katika bidhaa za kilimo, chakula, uhandisi na vifungashio mbalimbali. Hadi mwezi Machi, 2022 jumla ya viwango 160 sawa na asilimia 27.6 ya lengo la kutayarisha viwango 580 kwa mwaka vilikamilika. Aidha, kati ya viwango 160 vilivyokamilika, viwango 43 ni katika bidhaa za kemikali, 32 ni za uhandisi umeme, 28 ni za mazingira, 16 ni za ujenzi na 41 ni za kilimo na chakula.

190. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TBS imetoa leseni 512 za nembo ya ubora ya TBS ambayo ni sawa na asilimia 85.3 ya lengo la kutoa leseni 600 kwa mwaka 2021/2022. Miiongoni mwa leseni hizo, leseni 250 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha mafuta ya kupaka, chaki, mchele, korosho, unga wa mahindi, sabuni za aina mbalimbali, viungo, mafuta ya nazi, keki, pombe za nafaka, mkate, pombe isiyotokana na nafaka, pombe kali, mvinyo, nyama za kuku, na nyama za kusindika. TBS imetoa mafunzo kwa wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora. Vileville, TBS imesajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 6,372 ambavyo ni sawa na asilimia 32.6 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 19,530 kwa mwaka. Pia, Shirika liliisajili bidhaa za chakula na vipodozi 1,290 ambavyo ni sawa na asilimia 21.4 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 6,040 kwa mwaka.

191. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TBS limetoa vyeti vyaa ubora 60,412 kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; sawa na asilimia 88.8 ya matarajio ya kutoa vyeti vyaa ubora wa bidhaa 68,000 kwa mwaka 2021/2022. Aidha, TBS kupitia Programu ya Ukaguzi wa Magari hapa Nchini (Destination Inspection) imekagua magari 31,231 yaliyotumika nje ya

nchi sawa na asilimia 69.4 ya lengo la kukagua magari 45,000 kwa mwaka. Vilevile, TBS imetoe taarifa 157 za kitaalam kwa wasafirishaji wa bidhaa nje ya nchi zilitolewa sawa na asilimia 130.6 ya lengo la kutoa ripoti za kitaalam 170 kwa mwaka.

192. Mheshimiwa Spika, Sampuli 24,087 zilipimwa katika maabara mbalimbali za TBS kwa lengo la kuhakiki ubora wake, sawa na asilimia 46.3 ya lengo la kupima sampuli 52,000 kwa Mwaka 2021/2022. Jumla ya vifaa 7,880 vilifanyiwa Ugezi sawa na asilimia 78.8 ya lengo la kufanya ugezi vifaa 10,000 kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. TBS imepata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la TBS Jijini Dodoma (Viwango House). Kwa sasa TBS lipo katika hatua ya kusaini mkataba pamoja na kukabidhi eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

193. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia TBS ina wajibu wa kuthibitisha mifumo ya ubora wa usimamizi (Management Systems Certification) katika taasisi na makampuni nchini. Hadi sasa, TBS imethibitisha na kutoa vyeti 13 vya usimamizi wa ubora wa mifumo kwa viwango vya kimataifa yaani *ISO 9001 Quality Management Systems, ISO 22000 Food Safety Management Systems* pamoja na *Hazard Analysis and Critical Control Point (HACCP)*. Kati ya hivyo, vyeti nane (8) vinahusu mifumo ya usalama wa chakula. Kampuni zilizothibitishwa na TBS zimevezeshwa kuuza bidhaa zao za vyakula nje ya nchi. Aidha, TBS imefanikiwa kupata cheti cha ithibati kutoka Taasisi ya Utoaji wa Ithibati ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa yaani *Southern Africa Development Community Accreditation Systems (SADCAS)*. Huu ni uthibitisho wa umahiri wa Shirika letu la TBS katika kutekeleza jukumu la kuthibitisha mifumo ya ubora kimataifa.

194. Mheshimiwa Spika, Mazao yanayohifadhiwa katika ghala chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yanakuwa na ubora ambapo wanunuzi wa mazao/ bidhaa wanatakiwa kununua kutoka kwenye ghala zilizosajiliwa. Aidha, WRRB imeendelea kuhamasisha wanunuzi wa

mazao kununua bidhaa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuwa uhakika wa upatikanaji wa mazao yenye ubora. Kwa Mwaka 2021/2022 katika Sekta Ndogo ya Korosho kilogramu 2,116,600 zilinunuliwa na wanunuzi wa ndani kupitia Mfumo huo.

195. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2021/2022, WRRB kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) imeandaa miongozo ifuatayo: -

- i. Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi wa Mwaka 2021/2022 Toleo la Kwanza; na
- ii. Mwongozo wa Biashara kwa Kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala uliotolewa chini ya TCDC, WRRB na TMX wa Mwaka 2021 kwa mazao ya Choroko, Ufuta, Soya na MBAazi.

196. Mheshimiwa Spika, Matumizi ya miongozo ya pamoja yamepunguza migongano baina ya Taasisi za Umma katika utekelezaji wa majukumu wakati wa misimu ya mazao. Aidha, ufumbuzi wa changamoto wakati wa utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo umerahisishwa kupitia kuunda timu ya pamoja. Aidha, Bodi imeandaa rasimu za Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Wanyama Hai (Mbuzi, Kondoo na Ngombe) na Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya viazi mviringo, pilipili manga na vitunguu maji ili kuongeza wigo wa matumizi ya mfumo.

197. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WRRRB ina jukumu la kufanya uhamasishaji wa ujenzi wa miundombinu bora ya uhifadhi wa bidhaa kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi. Katika kuendeleza jitihada hizo Bodi imejenga ghala mpya zifuatazo: Ghala la MAMCU – Nanyamba; Ghala Mohamed Kossa – Mangaka; Ghala la Liwale 'B – Liwale; na Ghala la RUNALI-Ruangwa. Pia, Bodi

imefanya marekebisho ya Ghala la Mhonda – Mvomero na Ghala la Ikungi – Singida.

198. *Mheshimiwa Spika*, Ili kuwezesha utoaji wa elimu ya Biashara, Wizara kuitia CBE iliwezesha Uwekaji wa jiwe la msingi kwenye ujenzi wa Kampasi ya Mbeya uliofanywa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Novemba, 2021. Kazi zilizofanyika ni pamoja na upauaji wa majengo yote 11 ikiwemo kumbi mbili (2) za mihadhara, madarasa manne (4), jengo moja (1) la maktaba, ofisi tatu (3) na maabara moja (1) ya kompyuta. Aidha, kazi zinazoendelea ni za umaliziaji wa majengo hayo ikiwemo; kuweka vigae kwenye sakafu pamoja na kutandaza mifumo ya umeme, maji na ya mawasiliano (ICT).

199. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuitia Chuo kimepata ithibati ya mitaala ya programu mpya saba (7) za masomo kwa ngazi ya cheti hadi shahada ya awali kwenye; Uendeshaji wa Biashara katika Utunzaji wa Kumbukumbu (Business Administration in Records and Archives Management), Uendeshaji wa Biashara katika Usimamizi wa Rasilimali Watu (Business Administration in Human Resources Management) Masoko na Utalii (Marketing and Tourism), Masoko ya Kimtandao (Digital Marketing), Uhasibu na Fedha (Accounting and Finance), Uhasibu na Kodi (Accounting and Taxation) pamoja na Huduma za Kibenki na Fedha (Banking and Finance). Aidha, Chuo kimekamilisha mtaala mpya wa masuala ya Ubunifu na Ujasiriamali (Innovation and Entrepreneurship). Mtaala huo utafundishwa kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili (Masters' Degree) baada ya kuitishwa na NACTVET. Pia, Chuo kinaendelea na uandaaji wa mitaala mingine minne (4) na kimeshawasilisha mitaala mingine minne (4) NACTVET kwa ajili ya kuomba ithibati.

G. Kufanya Kaguzi za Biashara

200. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuitia TBS imezuia bidhaa zisizokidhi viwango kutoka nje ya nchi kuingia sokoni

shehena 1,517 na limeteketeza bidhaa zisizo kidhi ubora zenye thamani ya Shilingi 6,737,453,243.31. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizozuiwa na zilizoondolewa kutoka sokoni ziliikuwa ni bidhaa za chakula na vipodozi. Hatua stahiki zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria ikiwemo kuelimisha Umma na bidhaa husika kuharibiwa.

201. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia BRELA imefanya ukaguzi elimishi katika viwanda mbalimbali nchini katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Jumla ya viwanda 97 vilikaguliwa na kupewa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA na namna ya kupata leseni za viwanda. Pamoja na ukaguzi wa Leseni za Biashara ulifanyika katika Mikoa ya Lindi na Mtwara tarehe 28 Juni, hadi 11 Julai, 2021, Shinyanga tarehe 22 Agosti hadi 05 Septemba, 2021 na Tanga tarehe 27 Septemba hadi 11 Oktoba, 2021. Pia, ukaguzi wa Makampuni 16 ulifanyika katika Jiji la Dar es Salaam mwezi Novemba na Desemba, 2021.

202. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Februari, 2022 WMA imekagua na kuhakiki vipimo 619,731 sawa na asilimia 74.98 ya lengo la kukagua vipimo 826,541 vilivyokadiriwa. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa Vipimo 18,648 vilirekebishwa na 489 vilikataliwa. Pia, Wakala ilifanya zoezi la ukaguzi wa kawaida na wa kushtukiza wa vipimo mbalimbali vitumikavyo kwenye biashara, afya, usalama na mazingira. Vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni mizani, pampu za kuuzia mafuta, dira za maji, malori ya kubebea mchanga/kokoto na magari ya kubebea mafuta.

203. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WMA iliendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa (prepacked goods) toka nje ya nchi na zile zinazozalishwa hapa nchini. Mipaka iliyokaguliwa kupitia vituo vya ukaguzi ilikuwa ni Sirari (Mara), Mtukula (Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Killimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga), Kasumulu (Mbeya), Kasesya (Rukwa). Aidha, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Vituo vipyta viwili (2) vilifunguliwa Manyovu (Kigoma) na Mbweni (Dar es Salaam) na asilimia 80 ya bidhaa zilizopita mipakani zimekaguliwa. Pia, WMA

ilipima vipimo 204 vilivyoingizwa nchini na kutoa idhini kwa vipimo 150 ili viweze kutumika hapa nchini na vilivyokataliwa ni vipimo 54.

204. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WRRB imeratibu kaguzi kwene ghalia 43, zilizopo katika Wilaya 21 za Mikoa saba (7) ya Lindi, Manyara, Mtwara, Pwani, Morogoro, Ruvuma na Mbeya Kaguzi hizo zililhusu ukaguzi kabla ya utoaji Leseni na ukaguzi wakati Mfumo ukiendelea. Pia, leseni 38 zimetolewa kwene mazao manne (4) ambayo ni korosho (33), kahawa (2), Dengu (2) na Kakao (1). Aidha, Kampuni 30 za waendesha ghalia na moja (1) ya Mameneja Dhamana (Collateral Managers) walipewa leseni za kuendesha ghalia. Tani 236,793.361 za mazao yakiwemo korosho tani 225,314.368, MBAazi tani 6,944.897, Soya tani 1,002.916 na kokoa tani 3,531.180 zimekusanya na kuhifadhiwa katika ghalia kuu.

205. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia WRRB ilifanya kaguzi za aina tatu katika msimu wa bidhaa husika, zikiwemo kaguzi kabla ya leseni kutolewa, kaguzi za kushtukiza na kaguzi baada ya msimu wa bidhaa kuisha. Hadi kufikia Mwezi Desemba 2021/2022, zaidi ya ghalia 50 zilikaguliwa na kusajili kampuni 32 za waendesha ghalia na kutoa leseni 41 katika mazao ya Korosho, Kahawa, Dengu na Kakao. Aidha, jumla ya kilo 242,914,484.50 zinazojumuisha mazao ya Korosho, Kokoa, Kahawa na Dengu zilihifadhiwa kwene ghalia katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mwaka 2021/2022.

206. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia FCC ilifanya ukaguzi wa mikataba katika Kanda ya Kusini (Lindi na Mtwara), Kanda ya Ziwa (Mara na Mwanza), Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam na Morogoro) na Kanda ya Kati (Tabora na Dodoma) ili kubaini taasisi zinazotumia mikataba isiyosajiliwa na FCC. Katika zoezi hilo, asilimia 40 ya taasisi katika Sekta Ndogo ya Huduma Ndogo za Kifedha (Microfinance) zinatumia mikataba iliyoandaliwa na upande mmoja ambayo hajasajiliwa na FCC. Pia, ilibainika kuwa baadhi ya taasisi hutumia mikataba tofauti na

iliyosajiliwa na FCC nyingine zikitumia mikataba iliyorejeshwa na FCC ili ifanyiwe marekebisho kabla ya kusajiliwa na FCC. Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa asilimia 90 ya benki zinatumia mikataba iliyosajiliwa na FCC.

207. Mheshimiwa Spika, Wizara kupyitia FCC ilifanya ukaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu (ICDs) ambapo jumla ya makasha (containers) 2,831 yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha 58 yalikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa (MMA) ya Mwaka 2003 Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na bidhaa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya pipipiki na magari, shajala pamoja na vifaa vya kielektroniki. Pia, kaguzi za kushtukiza 20 zilifanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Morogoro. Katika kaguzi hizo, bidhaa bandia zikiwemo simu za mikononi, betri za simu, vifaa vya umeme, dawa za kuua wadudu, kahawa, wino wa *printer*, udi, viatu na *charger* za simu zilikamatwa kwa MMA.

5.2.7 Masuala Mtambuka

A. Kuwezesha Utoaji wa Huduma

208. Mheshimiwa Spika, Ili kuwezesha utoaji wa huduma, Wizara imepokea watumishi 14 katika kada mbalimbali ambao wamehamia na kupunguza uhitaji katika idara na vitengo. Mchanganuo wa watumishi hao na kada zao ni kama ifuatavyo: Afisa Usafirishaji (1), Afisa Tawala (2), Afisa Utumishi (1), Dereva (3), Mchumi (1) Afisa Biashara (3), Afisa Sheria (2) na Afisa Ugavi (1). Wizara iliandaa Mpango wa Mafunzo wa mwaka mmoja ambao ndiyo dira ya kuongoza mafunzo kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Wizara imewawezesha watumishi tisa (9) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 11 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika kozi mbalimbali. Aidha, Wizara imewawezesha Watumishi saba (7) wanaostaafu katika mwaka huo wa fedha kuhudhuria mafunzo ya ujasiriamali mahsus katika kuwaandaa na maisha baada ya kustaafu.

B Kupambana na Rushwa

209. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kutoa elimu kuititia vikao vya watumishi, Baraza la Wafanyakazi, na Menejimenti na kusisitizwa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu. Wizara ilifanya semina kwa wajumbe wa Kamati ya Wizara ya Uadilifu mwezi Agosti, 2021. Wizara imeendeleza jitihada za kuboresha utendaji katika Dawati la Malalamiko kwa kupokea na kufanya kazi malalamiko kwa wakati. Aidha, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili uweze kujumuisha majukumu yote ambayo imekabidhiwa baada ya kuundwa kwa Wizara mpya

c. Janga la UKIMWI na UVIKO - 19

210. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuwashudumia watumishi wanne (4) walioathirika kwa kuwapa posho ya lishe na nauli. Wizara inaendelea na utoaji wa vifaa kinga (kondomu) kwa watumishi wa Wizara ili kuendelea kuwasisitiza umuhimu wa kutunza afya zao kwa kuepuka ngono zembe. Aidha, Wizara imewezesha maafisa wanaosimamia masuala ya mapambano dhidi ya UKIMWI/VVU kuhudhuria semina elekezi kuhusu upangaji wa mikakati ya kuhudumia watumishi waathirika pamoja na kuhudhuria maadhisho ya kitaifa ya siku ya UKIMWI duniani.

211. Mheshimiwa Spika, Wizara na taasisi zake imeendelea kupambana na maambukizi ya UVIKO-19 kwa kutoa elimu ya kujinga na virusi vya korona na kuweka vipukusi maeneo ya ofisi. Aidha, katika mapambano hayo, Wizara imeunda kikosi kazi ambacho kinaratibu masuala ya UVIKO-19 ambapo taarifa za Wizara na Taasisi huwasilishwa Wizara ya Afya.

5.2.8 Mawasiliano Serikalini

212. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara imeendelea kutoa elimu na kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na programu mbalimbali za

kuendeleza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia vyombo vya habari ikiwemo radio, runinga, magazeti, majarida, mitandao ya kijamii na maonesho ya biashara yanayofanyika nchini.

213. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Mawasiliano (MIIT Communication Strategy) unaotumika kama mwongozo wa uandaaji na usambazaji taarifa za Wizara kwa Umma na kuendelea na maboresho ya Tovuti ya Wizara www.mit.go.tz ili iendane na mahitaji halisi ya habari na teknolojia ya kisasa. Vilevile, Wizara imeanzisha kurasa maalum za mitandao ya kijamii, *Youtube, Twitter, Instagram na Facebook* inayopatikana kwa jina la **uwekezaji viwanda biashara**.

214. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utangazajil la Taifa (TBC) inaandaa na kutangaza kipindi cha Wekeza kinachorushwa mara moja kwa wiki katika chaneli ya TBC1. Vilevile, Wizara inaandaa programu za runinga, na video fupi zinazohusu matukio mbalimbali yanayorushwa moja kwa moja kupitia ukurasa wa Wizara wa *Youtube* unaopatikana kwa jina la **uwekezajiviwandabiashara**. Wizara imeanzisha jarida la mtandao linalotoa taarifa za kazi zilizotekelizwa na Wizara kila mwezi. Pia, Wizara huandaa mabango ya mtandaoni yanayolenga kuhabarisha na kuelimisha Umma kuhusu shughuli zote za maendeleo ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na matukio mbalimbali ya kitaifa.

5.2.9 Usimamizi wa Fedha na Ununuzi

215. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kuboresha usimamizi wa rasillimali fedha ikiwemo uzingatiaji wa sheria na kanuni za fedha na manunuvi ya umma. Aidha, katika kutekeleza masuala ya uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, Wizara imekuwa ikiandaa taarifa za fedha zinazokidhi viwango vya kimataifa katika uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi za umma (International Public Sector Accounting Standards - IPSAs)

na miongozo mbalimbali iinayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kutokana na taarifa zinazokidhi viwango vya kimataifa na miongozo mbalimbali ya Serikali, Wizara kwa miaka mingi imekuwa ikipata Hati Safi za Ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ikiwemo ya Mwaka 2020/2021.

216. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali mara k w a mara. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na matumizi sahihi ya rasilimali za Serikali, Wizara imefanya ukaguzi wa fedha, rasilimali watu na ununuzi na kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu zinafaatwa.

217. *Mheshimiwa Spika*, Wizara illandaa Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2021/2022, taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo mwaka pamoja na taarifa ya mwaka mzima na kuziwasilisha Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Wizara ilitumia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS), kuratibu vikao vya Bodi ya Zabuni kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi Na.7 na Kanuni zake za mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016. Pia, Wizara imeboresha Daftari la Mali la Wizara (Non-Current Fixed Asset Register) kwa kuzingatia Mwongozo wa Mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 na Kanuni zake GN 132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

5.2.10 TEHAMA na Takwimu

218. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2021/2022, Wizara imetengeneza Mfumo wa Ghala la Kuhifadhia Taarifa za Wizara na Taasisi zake ambao umekamilika kwa asilimia 50 na Kutengeneza Kanzidata ya Taifa ya Viwanda ambayo kazi hii imekamilika kwa zaidi ya asilimia 70. Mfumo wa Ghala la Kuhifadhia Taarifa kwa sehemu iliyobaki ni kuunganisha mifumo ya Taasisi katika Ghala hilo ili mifumo hiyo iweze kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

6 MWELEKEO WA SEKTA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

219. Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita unalenga kuongeza uwekezaji, kukuza Sekta Binafsi na kujenga uchumi shindani wa viwanda utakaowawezesha Watanzania kufikia na kunufaika na uchumi wa kati ifikapo 2025. Kufanya hivyo kutawezesha Watanzania kutumia fursa za kiuchumi na kijamii katika mifumo iliyoboreshw na inayozingatia haki na utawala bora. Ni nia thabiti ya nchi yetu kumfanya kila Mtanzania kuwa na maisha bora na kunufaika na rasilimali na fursa zilizopo na zinazojitokeza. Hivyo, ni jukumu letu sote kuwaandaa na kuwawezesha Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo ipasavyo.

A. Kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia na Uwekezaji

220. Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza uchumi wa viwanda, Serikali inaimarisha taasisi zake ili kukidhi mahitaji ya maendeleo na ujenzi wa viwanda nchini. Wizara inaziimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia yaani TIRDO, TEMDO na CAMARTEC, kwa kupitia upya na kwa kina majukumu na miundo ya kisheria ya taasisi hizo. Lengo ni kuzifanyia maboresho mahsusili ili ziweze kuwa na tija na ufanisi katika kuleta mwendelezo wa mafanikio ya taasisi hizo na pia kuongeza nguvu katika kuendeleza viwanda nchini.

221. Mheshimiwa Spika, Serikali itajielekeza katika kuimarisha taasisi za uwekezaji nchini hususan TIC, EPZA na NDC ili ziwe mihimili na nguzo za uwekezaji katika viwanda ambavyo ni muhimu katika kujenga uchumi wa Taifa. Msukumo ukiwa ni kujenga viwanda mama, viwanda vya kimkakati na viwanda ambavyo kutokana na umuhimu wake ni vyema Serikali ikashiriki.

B. Kuimarisha taasisi za uvezeshaji Kiuchumi

222. Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua umuhimu na mchango wa uvezeshaji wananchi katika uchumi na hususan ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati, Serikali

itachukua hatua za makusudi kuimarisha Mifuko na Programu za Uwezesaji ili kukuza ujasiriamali nchini. Kipaumbele kitakuwa katika kuimarisha taasisi ya NEEC na SIDO ili ziweze kutoa mikopo kwa wanaviwanda na wafanyabiashara hasa wadogo ili kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

223. *Mheshimiwa Spika*, Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaongeza unafuu wa mikopo inayotolewa na Mfuko wa NEDF. Hivyo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 riba za mikopo zitahuishwa ili ziwe chini ya riba za mabenki ya biashara. Viwango vya riba ya mikopo ya uzalishaji itapungua kutoka asilimia 18 hadi asilimia 9. Aidha, riba ya mikopo ya biashara na huduma itapungua kutoka asilimia 22 hadi asilimia 12.

c. *Utoaji Huduma kwa Kulenga Wateja*

224. *Mheshimiwa Spika*, Utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kiwango kinachoridhisha ni lengo kuu la mabadiliko ya kiutendaji ambayo Serikali ya Awamu ya Sita inayapa kipaumbele. Hivyo, mwelekeo wetu ni kuhakikisha kuwa taasisi za kisekta tukianzia na TIC, TBS, WMA na BRELA zinajielekeza katika kutoa huduma kwa kiwango kinachokidhi matarajio ya wananchi. Wizara yangu na taasisi zake itaongeza ubunifu katika utendaji kazi kwa tija na kutoa huduma kwa weledi ili kuchochea ufanisi katika Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.

D. *Kukuza Maendeleo ya Sekta Binafsi*

225. *Mheshimiwa Spika*, Mtazamo wa Sera za Taifa zinatambua nafasi ya Sekta Binafsi kama injini ya kukuza uchumi. Katika kukuza Sekta Binafsi hasa wajasiriamali wadogo na wa katii, Serikali itaweka mazingira wezeshi na rafiki kupitia upatikanaji wa mitaji, teknolojia rahisi na rafiki, masoko ya uhakika na huduma muhimu zinazolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ni suala lisilohitaji mjadala. Hivyo, katika kukuza Sekta Binafsi nchini, Serikali

itaimarisha majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji.

226. *Mheshimiwa Spika*, Kupitia Bunge lako Tukufu, natoa rai kwa Sekta Binafsi kutumia fursa ya uwepo wa mahitaji makubwa ya ngano, mafuta ya kula na sukari kushiriki katika uzalishaji na uchakataji wa mazao hayo nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

E: Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini

227. *Mheshimiwa Spika*, Ujenzi wa mazingira bora na endelevu ya biashara ni kichocheo kikubwa na muhimu katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Hivyo, Serikali kupitia Wizara yangu itahakikisha kuwa inaendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini. Maboresho hayo yatavutia wawekezaji wa ndani na nje katika viwanda na biashara na hivyo kuwezesha kutumia fursa mbalimbali za ndani na nje ya nchi kadri zinavyoitokeza. Misingi ya maboresho ya mazingira ya kibashara itawekewa nguvu ya kisheria na utaratibu wenye ushirikishaji mpana zaidi wa wadau. Aidha, katika kuhakikisha uendelevu na uhakika wa kuvutia wawekezaji na upatikanaji wa soko kwa bidhaa zetu nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutumia Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi kutangaza bidhaa zetu ikiwa ni pamoja na kuzishirikisha katika maonesho ya Kimataifa ambayo nchi inashiriki.

E. Ujenzi wa Miundombinu kwa ajili ya Uwekezaji wa Viwanda

228. *Mheshimiwa Spika*, Kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya msingi na wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara ni suala la msingi. Uendelezaji wa miundombinu hiyo kwa kushirikiana na sekta binafsi utapewa msukumo zaidi ili kuleta tija na mvuto kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Jithhada za kushirikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kumiliki, kuendeleza na kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji nazo

zitapewa kipaumbele kabla ya kukimbilia kutafuta wawekezaji wa nje.

229. *Mheshimiwa Spika*, Katika kujengea uwezo na kuendeleza uwekezaji wa wajasiriamali wadogo na wa katni nchini, mwelekeo wa Wizara ni kuhakikisha kuwa ujenzi wa *Industrial Shades* unafanywa katika mikoa yote nchini. Pia, msukumo ukitakiwa katika kukamilisha miradi iliyoanza kwa kufungamanisha maboresho ya vituo vyta biashara za mipakani na viwanda katika maeneo hayo.

230. *Mheshimiwa Spika*, Maendeleo ya Sekta za Uwekezaji, Viwanda na Biashara Nchini hutegemea uwepo wa maeneo yaliyo na miundombinu stahiki kwa ajili ya uwekezaji ikiwemo nishati ya umeme na gesi asilia, maji, usafiri wa reli pamoja na barabara. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine kuhakikisha kunakuwa na maeneo ya uwekezaji yenye miundombinu stahiki. Vilevile, Wizara yangu itahakikisha tunapunguza gharama za kuendesha biashara hasa katika utaratibu wa upatikanaji wa leseni na vibali mbalimbali vyta biashara, ili kwa pamoja tuweze kuvutia wawekezaji na kukuza Sekta ya Viwanda kwa kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vyta kuongeza thamani mazao ya kilimo pamoja na malighafi nyingine ikiwemo madini na mazao ya misitu hivyo kupunguza uuzaaji wa mazao na bidhaa ghafi nje ya nchi. Kwa kufanya hivi, Sekta ya Viwanda itaweza kuongeza ajira zitokanazo na uzalishaji viwandani.

F. Kukuza Masoko ya Bidhaa na Huduma zinazozalishwa Nchini

231. *Mheshimiwa Spika*, Kuthamini rasilimali na bidhaa za ndani ni ukombozi muhimu wa kiuchumi kwa Taifa lolote kwa kuwa, nchi ni soko la kwanza kabla ya kutafuta soko lingine. Suala la msingi ni wananchi kujenga imani na kupata thamani na ubora wanaouhitaji katika bidhaa na huduma za ndani ya nchi. Kwa msingi huo, Wizara itaendelea kuhamasisha uimarishaji wa ubora na matumizi ya bidhaa za ndani, nguvukazi na malighafi za ndani ili

kuleta ufungamanisho wa sekta katika kujenga uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Aidha, Wizara kupitia TANTRADE inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia kaulimbiu ya 'Nunua Bidhaa za Tanzania', Jenga Tanzania Kaulimbiu hiyo ni muhimu sana katika kipindi hiki cha ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuimarisha viwanda vya ndani kwa kutegemea soko la uhakika la ndani ya nchi. Hii itajumuisha kusimamia matumizi ya bidhaa, mazao na nguvukazi ya ndani katika miradi ya kimkakati na uwekezaji unaofanyika nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dhana ya ushiriki wa Watanzania.

232. Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaendelea kuhimiza na kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Jitihada zitaelekezwa katika kuhakikisha kuwa mipango na shauku ya wawekezaji kuwekeza Tanzania zinatimia kwa kushughulikia vikwazo, kuondoa usumbufu na urasimu na kuongeza bidii ya kuwashawishi wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza hapa nchini. Vilevile, Wizara itaweka msukumo mkubwa katika kuendeleza kwanza: Viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake itatoka ndani, hususan kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, madini na maliasili zilizopo nchini. Viwanda vya aina hiyo vitatupa fursa ya kujenga mfumo wa uzalishaji ndani ya nchi uliofungamana na kushikamana. Pili: Viwanda vya kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi humu nchini yaani bidhaa kama vile nguo, viatu, mafuta ya kupikia, n.k. Kwa hiyo, viwanda hivyo vitakuwa na uhakika wa soko la ndani kabla ya kufikiria soko la nje. Viwanda hivyo vitatarajiwa kuzalisha ziada kwa ajili ya masoko ya nje na hivyo kutuungezea akiba ya fedha za kigeni.

g. Kujenga Sekta Binafsi

233. Mheshimiwa Spika, Katika kufanikisha na kuimarisha soko la ndani, tunahitaji kuwa na Sekta Binafsi imara ambayo inaanaki utashi wa kisera na malengo ya kitaifa. Hivyo, pamoja na haki ambayo Sekta Binafsi inastahili, ina

wajibu wa kutekeleza majukumu ambayo yana tija na kuweza kuendeshwa kibashara ikiwemo kulipa kodi na ada stahiki za Serikali. Kwa upande wa wawekezaji kutoka nje, ni jukumu na wajibu wao kuhakikisha kuwa wanazingatia mikataba na masharti ya uwekezaji ikiwemo kuwajibika kulipa kodi na ada zinazostahiki kwa Serikali, kulipia michango ya wajibu kwa nchi, kujenga mahusiano mema katika maeneo ya uwekezaji na kuzingatia ushiriki wa Watanzania (matumizi ya bidhaa, wafanyakazi, malighafi, huduma za ndani, nk).

234. *Mheshimiwa Spika*, Kwa upande mwingine, wawekezaji wa ndani wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa mitaji, matumizi ya teknolojia duni, upatikanaji wa ardhi, upatikanaji wa masoko na ujuzi stahiki katika shughuli za uzalishaji viwandani na kuendesha biashara. Kimsingi, Sekta hiyo inahitaji kulindwa kwani viwanda vingi ni vidogo na vichanga kukabiliana na ushindani wa nguvu za soko na viwanda ambavyo tayari vimelindwa vya kutosha na kuijjengea uwezo mkubwa wa ushindani. Ulinzi huo tunaozungumzia kwa viwanda vyetu pia ulikuwa ukifanywa na nchi zilizoendelea kiuchumi zikiwemo China na India kwani biashara na uwekezaji katika eneo hilo la wazalishaji, wafanyabiashara na wawekezaji kwa sehemu kubwa ni wadogowadogo. Azma ya Serikali sio kuliinda shughuli za uzalishaji zisizo za tija bali ni kuhakikisha shughuli zenye tija zinaimarika na kuweza kushindana kimataifa.

7 VIPAUMBELE KWA BAJETI YA MWAKA 2022/2023

235. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka 2022/2023, Vipaumbele vikuu vya Wizara ni: -

i. Miradi ya kipaumbele iliyopo katika Mipango na llani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaanza utekelezaji;

ii. Uwekezaji katika Kongani na maendelezo kwenye SEZ, EPZA, Kongani za viwanda Mfano - Kongani ya Kigamboni, Kwala na Kitaraka;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- iii. Usimamizi na udhibiti wa masoko;
- iv. Ushiriki katika shughuli za Kikanda EAC, SADC, AfCFTA na Kimataifa;
- v. Kuondoa urasimu katika kuhudumia wawekezaji na wafanyabiashara; na
- vi. Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi moja kwa moja katika uchumi na uwezeshaji wa wananchi.

236. Mheshimiwa Spika, Vipaumbele mahsusni vifuatavyo: -

- i. Kuendelea kuratibu programu za uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje ya nchi;
- ii. Kuratibu masuala ya uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi;
- iii. Kuratibu ufanikishaji wa uwekezaji ikiwemo kuongeza ufanisi wa miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC);
- iv. Kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;
- v. Kuimarisha mifumo ya kushughulikia changamoto za uwekezaji;
- vi. Kuboresha mazingira wezeshi ya kuendeleza viwanda na biashara kwa kupitia na kutunga sheria, sera na mikakati ya kuvutia uwekezaji;
- vii. Kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) na Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zitakazouzwa nje (EPZ);
- viii. Kuimarisha taasisi za utafiti na kufanya tafiti kwa ajili ya maendeleo ya viwanda;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- ix. Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini na bidhaa zinazotumiwa kwa wingi nchini kama vile nguo, mafuta na sukari;
- x. Kuendeleza viwanda vyta usindikaji vinavyozalisha bidhaa za petroli (Petro-gas), kemikali, uzalishaji wa dawa za binadamu na vifaa vyta ujenzi;
- xi. Kuratibu programu za kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara inayolenga katika kupunguza gharama za uwekezaji na kufanya biashara;
- xii. Kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa;
- xiii. Kushughulikia masuala ya ubora na viwango nchini;
- xiv. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi; na
- xv. Kutafuta fursa za masoko na kuwaunganisha na wajasiriamali wa ndani.

8 MALENGO YA MWAKA 2022/2023

8.1 IDARA NA VITENGO VYA WIZARA

8.1.1 Maendeleo ya Uwekezaji

237. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka 2022/2023, Sekta ya Maendeleo ya Uwekezaji imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kukamilisha maandalizi ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji na kuanza utekelezaji wake;
- ii. Kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;
- iii. Kuendelea kuratibu programu za uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje ya nchi;

- iv. Kuimarisha mifumo ya kushughulikia changamoto za uwekezaji;
- v. Kuratibu programu za kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara inayolenga katika kupunguza gharama za uwekezaji na kufanya biashara;
- vi. Kuimarisha ushiriki na maslahi ya nchi katika masuala ya uwekezaji kwenye ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
- vii. Kuimarisha uhamasishaji wa fursa za uwekezaji na kuboresha Mfumo wa Kanzidata ya Takwimu za Uwekezaji na Kanzidata ya Benki ya Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji; na
- viii. Kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa.

8.1.2 Uvezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi

238. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Sekta ya Uvezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kufanya tathmini ya utendaji wa Sekta Binafsi katika uchumi wa nchi;
- ii. Kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Mkakati wake;
- iii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Mikutano ya Taifa ya Baraza la Biashara Tanzania (TNBC);
- iv. Kuandaa Kanzidata ya Sekta Binafsi Nchini;
- v. Kuandaa Dirisha kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya Sekta Binafsi;
- vi. Kufanya mapitio ya Mwongozo ya Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi za mikoa na wilaya;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- vii. Kutoa mafunzo katika Mikoa mitano (5) kuhusu majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya mikoa na wilaya;
- viii. Kuandaa Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji nchini;
- ix. Kufanya Mapitio ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004; na
- x. Kujenga Vituo vipyta vya Uwezeshaji Wananchi katika baadhi ya mikoa na wilaya ambayo hajajenga.

8.1.3 Maendeleo ya Viwanda

239. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Sekta ya Viwanda imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuhamasisha uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ili kuongeza ushindani;
- ii. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati;
- iii. Kufanya tathmini katika sekta za kipaumbele (Nguo na mavazi, Ngozi na bidhaa za Ngozi, Korosho na Mafuta ya kula);
- iv. Kuendelea kueneza dhana ya KAIZEN nchini;
- v. Kuwezesha utekelezaji wa Programu ya PCP;
- vi. Kuainisha mahitaji ya ujuzi viwandani;
- vii. Kukamilisha marejeo ya Sera ya Viwanda (SIDP) na Mkakati wake (IIDS);
- viii. Kuandaa mikakati ya Pamba, Nguo na Mavazi, Ngozi na Bidhaa za Ngozi na Mafuta ya Alizeti; na
- ix. Kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya sabuni, mboga na matunda na dawa za binadamu.

8.1.4 Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

240. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa utengaji na uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ii. Kukamilisha marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003) pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake; na
- iii. Kuhamasisha urasimishaji wa shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati lkiwa ni pamoja na kuelimisha faida za urasimishaji.

8.1.5 Mtangamano wa Biashara

241. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Sekta ya Mtangamano wa Biashara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini;
- ii. Kuendelea na majadiliano ya utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Continental Free Trade Area – CFTA);
- iii. Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu (Tripartite) linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;
- iv. Kukamilisha majadiliano ya Biashara ya Huduma kwa sekta sita (6) za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;

- v. Kutekeleza Itifaki ya Sokola Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya Biashara ya Bidhaa na Huduma;
- vi. Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa na utekelezaji wake katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo WTO, UNCTAD, CFC na ITC;
- vii. Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Ahueni ya Kibashara (Anti-dumping and Countervailing Measures);
- viii. Kukamilisha mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera mpya ya Taifa ya Biashara; na
- ix. Kuimarisha Kamati za Kitaifa za Kusimamia Urahisishaji wa Biashara Nchini.

8.1.6 Maendeleo ya Biashara

242. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Biashara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;
- ii. Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyakishara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatakonayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;
- iii. Uratibu wa kazi za Mafisa Biashara Nchini;
- iv. Uratibu na uendelezaji wa miundombinu ya masoko;
- v. Kuratibu majukwaa ya masoko nchini;
- vi. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;
- vii. Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;

viii. Kuhamasisha na kuwezesha utangazaji wa bidhaa na huduma za Tanzania; na

ix. Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali.

8.1.7 Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji wa Huduma

243. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara itatekeleza malengo yafuatayo kwenye eneo la Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu:-

i. Kuajiri watumishi 38 wa kada mbalimbali kwa lengo la kuwezesha Idara na Vitengo kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

ii. Kupandisha vyeo watumishi 57 wa kada mbalimbali;

iii. Kutoa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya 38, kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu watumishi 26, kuwawezesha watumishi 41 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbalimbali nichini ili kuboresha utendaji kazi, kukidhi mahitaji ya Muundo na kutoa mafunzo ya kuijandaa kustaafu kwa watumishi sita (6); na

iv. Kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*OPRAS*) kwa Watumishi 231.

8.2 TAASISI ZILIZOPO CHINI YA WIZARA

8.2.1 Kituo cha Uwekezaji Tanzania

244. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuboresha mifumo ya kusajili ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo;

ii. Kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo katika Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja (One Stop Facilitation Centre) ili kufanikisha uwekezaji;

- iii. Kuendelea na mkakati wa kufuatilia na kutathmini miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa (Project Monitoring & Evaluation);
- iv. Kuendelea na kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji;
- v. Kuendelea kuhamasisha uwekezaji ndani na nje ya nchi kupitia makongamano na semina;
- vi. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali ya uwekezaji nchini kupitia vyombo vya habari na mitandao;
- vii. Kuendelea kutatua migogoro na changamoto za uwekezaji;
- viii. Kufanya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na tafiti za kubua fursa za uwekezaji nchini, tafiti za kuboresha mazingira ya uwekezaji, tafiti za kuibua maeneo yenye fursa za uwekezaji kwa ajili ya wajasiramali wa kati na wadogo;
- ix. Kuendelea kushirikiana na Balozi za Tanzania katika kuitangaza Tanzania ili kuvutia uwekezaji kutoka nchi zilipo balozi hizo; na
- x. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

8.2.2 Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi

245. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN viwanda scheme);
- ii. Kuratibu masuala yanayolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi ili wanufaikie na fursa zilizopo na kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi;

- iii. Kuhamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na vikundi vyta uzalishaji mali, vyama vyta kuweka akiba na kukopa (SACCOS), benki za jamii vijijiini (VICOBA) na vikundi vingine vyta kiuchumi;
- iv. Kuimarisha uratibu wa utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
- v. Kuratibu upatikanaji wa elimu ya biashara, fedha, masoko, ithibati na ujasiriamali kwa vijana, vyama vyta ushirika na vikundi vyta kiuchumi; na
- vi. Kuratibu ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na uwekezaji hasa katika Sekta za vipaumbele kama vile mafuta na gesi asilia; kilimo, mifugo na uvuvi; ujenzi; viwanda; utalii na Sekta mtambuka.

8.2.3 Shirika la Taifa la Maendeleo

246. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati, na kukamilisha taratibu za ulipaji wa fidia na majadiliano katika miradi ya Mchuchuma na Liganga na Makaa ya Mawe Katewaka;
- ii. Kukamilisha majadiliano ya Mradi wa Matrekta ya URSUS;
- iii. Kuendelea na ukarabati wa Kiwanda cha KMTC katika Mkoa wa Kilimanjaro ;
- iv. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO na kufanya usanifu wa miundombinu ya msingi katika Kongani za Nyanza, KMTC na Kange;
- v. Kufanya tafiti ya matumizi sahihi ya eneo la Kiwanda cha Matairi Arusha;

vi. Kufanya maandalizi ya uchimbaji wa chuma ghafi (iron ore) Maganga Matitu na utafiti wa Makaa ya Mawe Mhukuru;

vii. Kuboresha Maktaba kwenda kwenye mfumo wa kidigitali; na viii. Kuendelea na uzalishaji wa viuadudu wa mbu waenezao malaria na kufanya majaribio ya pili ya viuatilifi pamoja na kukamilisha usajili na kupata vibali vya uzalishaji katika Kiwanda cha Viuadudu (TBPL).

8.2.4 Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje ya Nchi

247. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo SEZ);

ii. Kukamilisha malipo ya fidia pamoja na kuendeleza miundombinu ya msingi katika Eneo Maalum la Kiuchumi Nala (Nala SEZ) Dodoma;

iii. Kuhamasisha Sekta Binafsi pamoja na Serikali za Mikoa kuwekeza katika kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi – SEZ;

iv. Kufanya uratibu, tafiti, ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelawa na Mamlaka ya EPZ;

v. Kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA; na

vi. Kuimarisha Rasilimaliwatu katika Mamlaka ya EPZ.

8.2.5 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

248. Mheshimiwa Spika, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) limepanga kutekeleza malengo yafuatayo kwa Mwaka 2022/2023;

- i. Kuendelea kuimarisha Idara ya Uhandisi kwa kuongeza wataalam na vifaa hasa katika shughuli za upimaji ubora (Non Destructive Testing) wa mabomba ya mafuta na gesi ili kuendelea kukidhi viwango vya Kimataifa;
- ii. Kuendelea na kukamilisha mchakato wa ithibati (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira, kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi na vifaa ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
- iii. Kuendelea kufanya utafiti katika kanda saba (7) nchini ili kubaini fursa za uwekezaji na maeneo yenye viwanda na rasilimali zilizopo (Industrial Mapping) ili kutumia kikamilifu rasilimali zilizopo na kuongeza uwekezaji Nchini;
- iv. Kuendelea na ukamillishaji wa Jengo la Utawala ili kuongeza nafasi za maabara, viatamizi na Kituo cha Ubashiri wa Teknolojia na taarifa za maendeleo ya viwanda;
- v. Kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari ikiwa ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Shirika;
- vi. Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani zenyenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;
- vii. Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau 400 wa Sekta ya Ngozi kuhusu namna bora ya kuongeza thamani ya ngozi zinazozalishwa Nchini na Kuimarisha Maabara ya Ngozi ili kutoa huduma kwa wadau wa viwanda vidogo na vikubwa vya kuchakata ngozi;
- viii. Kuandaa kanzidata ya viwanda vya nguo na ngozi nchini na kufanya tathmini ya viwanda vya nguo na ngozi ili kubaini changamoto na kuainisha mapendekezo ya utatuzi wa changamoto; na

ix. Kuendelea kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sheria ya Bunge Na. 5 ya Mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO.

8.2.6 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijiini

249. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijiini (CAMARTEC) kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendeleza utafiti na uendelezaji wa teknolojia kwa kuanzisha Kiwanda Darasa cha Kubangua Korosho katika Wilaya ya Manyoni katika mkoa wa Singida; na Kufanya kazi za utafiti kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za utafiti ikiwa ni pamoja na kubaini mahitaji ya zana za kilimo, mifugo, uvuvi na teknolojia za vijiini kwa wakulima katika Wilaya za Momba Mkoa wa Songwe, na Chemba katika Mkoa wa Dodoma;

ii. Kuendeleza mafunzo na kuhawilisha zana za kilimo kwa kuanzisha Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (Engineering Technology Hub - ETH) katika Wilaya ya Karatu katika mkoa wa Arusha, Kujenga ufahamu wa zana za kilimo na teknolojia za vijiini kwa wadau, kuanzisha maktaba ya kisasa kwa ajili ya utafiti na uendelezaji wa teknolojia;

iii. Kufanya ukaguzi wa zana za kilimo na teknolojia za vijiini kwenye maeneo ya mipakani; na

iv. Kufanya ufuatiliaji, tathmini na ukaguzi wa miradi.

8.3 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania

250. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) limepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa chasili cha mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (sugar mini-processing plant) kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ili kutoa ujuzi na ajira na kupunguza upungufu wa sukari nchini;

- ii. Kusanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba vyat hospitali kwa awamu ya II (Wheel chairs, 6-body Mortuary cabinets, stretchers, theatre trolleys, Autoclave, and Laundry machines) ili kuisaidia Serikali kutoagiza vifaa tiba kutoka nje ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni;
- iii. Kubuni na kuendeleza mtambo wa kuchakata mkonge ili kupata nyuzi bora (export quality sisal fibres) na kuwezesha ukuaji wa viwanda na ongezeko la ajira;
- iv. Kubuni na kuendeleza teknolojia ya kutengeneza matofali yanayostahimili joto kali (Refractory bricks) hapa nchini;
- v. Kubuni na kuendeleza mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali mahsus kwa kuchomea damu isiyofaa, mabaki ya wanyama na dawa zillizoharibika na kuitwa na muda (incinerating carcass from livestock/cattle abattoir, biomedical waste blood and expired drugs) katika Sekta ya Afya;
- vi. Kusanifu na kuendeleza teknolojia ya kuhifadhi maziwa wakati wa kukusanya na kusafirisha ili yasiharibike mapema;
- vii. Kuendeleza na kuunda kibiashara teknolojia ya kuhifadhi mazao ya mbogamboga kwenye ubaridi (Coldrooms for smallholder horticulture farmers) ili kupusha mazao kuharibika haraka;
- viii. Kuboresha Karakana kwa kusimika mashine na vifaa vyat kisasa (Heavy duty 6-axes CNC Machines) na miundombinu, pamoja na kuanzisha ujenzi wa Karakana ya Useremala kwa ajili ya kuwezesha utengenezaji wa vifaa tiba nchini ili kuzalisha bidhaa kwa wingi;
- ix. Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo (Korosho) ili kuongeza thamani, na kubuni, kusanifu na kuendeleza teknolojia ya mtambo wa kuchakata chikichi ili kuongeza thamani;

x. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

xi. Kutangaza huduma za Shirika ili kujenga uelewa kwa umma kwa kushiriki kwenye maonesho ya teknolojia/ biashara, pamoja na kufanya ziara za kitaalam kwenye viwanda mbalimbali na kutatua changamoto za kihandisi;

xii. Kujenga uwezo wa Taasisi kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi katika nyanja za usanifu, uendelezaji wa teknolojia mpya na kujua matumizi ya teknolojia mpya; na

xiii. Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya karakananaofisiyausanicupamojanamiundombinu ya Taasisi kwa ujumla.

8.3.1 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

251. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO kwa kuweka miundombinu wezeshi na kukamilisha kutengeneza Mfumo Uganishi wa TEHAMA wa Shirika;

ii. Kuhawilisha teknolojia kwa kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) na Vituo vya Mafunzo na Uzalishaji (TPC) vya SIDO;

iii. Kuimarisha Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF);

iv. Kutangaza Shirika na bidhaa za viwanda vidogo;

v. Kuongeza wigo wa huduma za SIDO kwa wajasiriamali; na

vi. Kuimarisha utendaji kazi wa Shirika.

8.3.2 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

252. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) litatekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kutayarisha viwango 630 vya kitaifa katika sekta/ nyanja mbalimbali ikiwemo nyanja za uhandisi mitambo, kemikali, uhandisi umeme, nguo na ngozi, madini, kilimo na chakula, mazingira pamoja na Sekta mtambuka;
- ii. Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 650 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);
- iii. Kusajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 10,000;
- iv. Kusajili bidhaa za chakula na vipodozi 2,700;
- v. Kukagua na kutoa vibali 100,000 kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi;
- vi. Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa vyeti vya ukaguzi 50,000 wa magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini kwa utaratibu wa kukagua magari kabla ya kusafirishwa kuja nchini yaani *Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards (PVOC) Programme* na kwa utaratibu wa kukagua magari baada ya kufika nchini ikiwa waagizaji watakuwa hawajakagua nje ya nchi;
- vii. Kutoa mafunzo na kuendesha semina kuhusu viwango na udhibiti ubora kwa wadau 1,200 wa Sekta ndogo tatu (3) ambazo ni mchele, muhogo na viungo;
- viii. Kuthibitisha kampuni 12 chini ya mifumo ya ubora (management systems);
- ix. Kupima sampuli 40,000 za bidhaa mbalimbali;
- x. Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 12,000;

- xii. Kuendelea na ujenzi wa *Viwango House* Dodoma; na
- xiii. Ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Ziwa (Mwanza).

8.3.3 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

253. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuendelea kuelimisha umma juu ya utekelezaji wa sheria na umuhimu na faida za kufanya sajili mbalimbali za kibashara zinazofanywa na BRELA;
- ii. Kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za usajili na utoaji Leseni;
- iii. Kuendelea kusimamia hitaji la taarifa za Wamiliki Manufaa na zoezi la uhuishaji wa taarifa za Makampuni na Majina ya Biashara;
- iv. Kuendelea kuboresha mifumo-mtandao ya usajili na utoaji leseni na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;
- v. Kuendelea kuimarisha mahusiano kati ya BRELA na uongozi wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Biashara kwa lengo la kufikisha karibu huduma kwa umma katika maeneo yao;
- vi. Kukamilisha maandalizi ya nyaraka zote muhimu zinazohusiana na maslahi ya Watumishi pia miongozo ya kiutendaji na utoaji maamuzi; na
- vii. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi ikiwemo vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa Watumishi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma.

8.3.4 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

254. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kutoa leseni kwa waendesha ghala, kuanisha ghala na kufanya ukaguzi wa ghala, kusimamia upokeaji na utoaji wa bidhaa ghala kuu pamoja na uandaaji wa miongozo ya bidhaa zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala nchini;
- ii. Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- iii. Kuanisha viwanda vnavyoongeza thamani mazao yaliyo katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuwaunganisha na fursa mbalimbali;
- iv. Kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa wadau mbalimbali katika maeneo yanayotekeliza Mfumo, na maeneo mapya;
- v. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa lengo la kuboresha utendaji na ufanisi;
- vi. Kuendelea kupanua wigo na kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo mapya na yale yanayotumia Mfumo kwa sasa;
- vii. Kutengeneza Mkakati mahsusini kwa ajili ya kutangaza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- viii. Kuweka Mifumo mipya na kuimarisha Mifumo ya TEHAMA iliyopo ikiwemo ile ya maombi ya Leseni, upokeaji na utoaji wa bidhaa ghala kuu, mfumo wa utendaji kazi za kila za siku (e-office), mfumo wa ukaguzi wa ghala, mfumo wa usajili wa ghala nchini, mfumo wa ukusanyaji

wa takwimu na taarifa mbalimbali pamoja na kuhuisha nyaraka mbalimbali za WRRB ili ziendane na Mifumo ya ICT iliyopo;

ix. Kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Vyama vya Ushirika na Taasisi nyingine kuzitambua ghala zote nchini kwa lengo la kufanikisha ukarabati na ujenzi wa ghala za kuhifadhi mazao ya wakulima katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na udarajishaji wa ghala zote; na

x. Kukagua na kuangalia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo mbalimbali na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo.

8.3.5 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania

255. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuimarisha ushindani wa kibiasara nchini;
- ii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya ufanyaji Biashara;
- iii. Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania;
- iv. Kuboresha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara nchini; na
- v. Kuimarisha uwezo wa Taasisi.

8.3.6 Wakala wa Vipimo

256. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Wakala wa Vipimo (WMA) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;

- ii. Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (decrealed quantity);
- iii. Kununua vitendea kazi ikiwemo vitendea kazi vya kitaalam na magari manne (4);
- iv. Kuongeza idadi ya watumishi ikiwemo Maafisa Vipimo 150, Maafisa Vipimo Wasaidizi 50 na Madereva 50;
- v. Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo; na
- vi. Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo Mkao wa Dodoma.

8.3.7 Tume ya Ushindani

257. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuboresha hali ya ushindani katika soko;
- ii. Kumlinda mtumiaji kutokana na vitendo hadaifu na kandamizi katika soko;
- iii. Kuongeza mapambano dhidi ya bidhaa bandia na pia kuhakikisha kiwango cha bidhaa hizo kinapungua katika soko; na
- iv. Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa kuboresha afya za watumishi, kuongeza idadi ya wafanyakazi pamoja na kuwezesha mifumo ya kielekroniki ya utoaji huduma.

8.3.8 Baraza la Ushindani

258. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Baraza la Ushindani (FCT) litatekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kushughulikia mashauri ya rufaa yanayowasilishwa katika Baraza ili kutoa maamuzi ya mashauri 70;
- ii. Kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu ya Baraza ili kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri yanayowasilishwa katika Baraza ikiwa ni pamoja na: kuboresha mifumo ya Baraza; kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi na kuboresha vitendea kazi;
- iii. Kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi kuhusu ushindani kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri ya Baraza;
- iv. Kuongeza uelewa kwa wadau wengi zaidi na jamii kwa ujumla kuhusu shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa soko; na
- v. Kushughulikia masuala mtambuka.

8.3.9 Chuo Cha Elimu ya Biashara

259. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2022/2023, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

- i. Kuimarisha na kuendeleza rasilimaliwatu katika hatua za Shahada ya Uzamivu (PhD) na Shahada ya Uzamili (Masters' Degree);
- ii. Kujenga jengo jipya la Vipimo na Viwango katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam;
- iii. Kujenga jengo jipya katika Kampasi ya Dodoma ili kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;
- iv. Kuandaa Mpango Kabambe katika eneo la Nzuguni Kampasi ya Dodoma;
- v. Kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara katika Kampasi ya Mwanza ili kupunguza uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

vi. Kujenga mabweni ya wanafunzi eneo la Iganzo Kampasi ya Mbeya; na

vii. Kuanza ujenzi wa Kampasi mpya ya Zanzibar.

9 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

9.1 Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023

260. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,000,000** kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine.

9.2 Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023

261. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka 2022/2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya **Shilingi 99,105,506,000** katika Fungu 44. Kati ya fedha hizo, Wizara inaomba kutengewa **Shilingi 68,308,687,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 30,796,819,000** za Matumizi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 8,728,788,000** za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 59,579,899,000** za Mishahara. Aidha, Fedha za Matumizi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 30,346,819,000** fedha za ndani na **Shilingi 450,000,000** fedha za nje.

9.3 HITIMISHO

262. *Mheshimiwa Spika*, Naomba nichukua fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote na hasa Wazalendo wa Nchi hii kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Katika kipindi kilicho mbele yetu, tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ni jukumu kubwa ambalo linapaswa kuendelea kuungwa mkono na wapenda maendeleo wote na hasa Watanzania na wazalendo wote. Tunahitaji kila Mtanzania popote alipo kutimiza wajibu wake, kujituma, kubadilisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na kuendeleza uwekezaji, viwanda na biashara kwa maslahi ya nchi yetu. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

263. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara www.mit.go.tz.

264. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO

Jedwali Na. 1: Biashara kati ya Tanzania na China kwa Mwaka 2013 – 2021 (Dola za Marekani „000,000)

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	307.8	683.9	645.9	355.9	142.3	143.0	233.7	238.9	273.1
Bidhaa zilizoagizwa	1,444.2	1,571.1	2,147.6	1,630.2	1,408.1	1,762.0	1,987.7	1,940.3	2,696.2
Jumla	1,752	2,255	2,793.5	1,986.1	1,550.4	1,905.00	2,221.40	2,179.20	2,969.30

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Jedwali Na. 2: Biashara kati ya Tanzania na India kwa mwaka 2013-2021 (Dola za Marekani „000,000)

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	748.2	1,254.5	1,320.3	706.4	977.6	727.1	867.8	528.7	1,008.7
Bidhaa zilizoagizwa	2,088.2	1,848.6	1,458.3	1,421.6	1,077.6	1,762.0	1,987.7	1,940.3	2,696.2
Jumla	2836.4	3103.1	2778.6	2,128	2,055.2	3,704.90	3,704.90	3,704.90	3,704.90

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Jedwali Na. 3: Biashara kati ya Tanzania na Japani kwa mwaka 2013-2021 (Dola za Marekani „000,000)

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	220	247.8	263.4	139.2	75.7	66.0	64.2	55.8	67.5
Bidhaa zilizoagizwa	466.7	559.3	458.6	369.2	365.2	398.0	485.2	338.4	469
Jumla	686.7	807.1	722	508.4	440.9	464	549.4	394.2	536.5

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 4: Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya kwa

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	898.4	791.7	708.7	236.5	441.4	657.3	725.9	1,475.9	857.1
Bidhaa zilizoagizwa	2,759.4	2,895	1,159.8	557.7	936.1	982.4	1,069.9	1,072.0	1,003.7
Jumla	3,657.8	3,686.7	1,868.5	794.2	1,377.5	1,639.70	1,795.80	2,547.90	1,860.80

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Jedwali Na. 5: Biashara ya Bidhaa kati ya Tanzania na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2013 - 2021 (Dola za Marekani „000,000”)

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	419.1	598.1	1,062.4	437.7	349.6	444.3	674.4	807.9	1,161.2
Bidhaa zilizoagizwa	394.7	706.4	322.8	298.9	220.4	302.8	329.2	324.3	523.4
Jumla	813.8	1,304.5	1,385.2	736.6	570	747.1	1,003.6	11322	1684.6

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Jedwali Na. 6: Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa mwaka 2013 - 2021 (Dola za Marekani „000,000”)

Mwaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Bidhaa zilizouzwa	1,243.55	1,235.9	1,357.7	1,017.9	877.8	993.6	1,350.9	1,458.3	1,311.5
Bidhaa zilizoagizwa	835.9	773	771.2	612.4	1,7781.4	604.2	594.0	492.4	232.5
Jumla	2079.45	2008.9	2128.9	1630.3	18659.2	1,597.8	1,944.9	1,950.7	1,544

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 7: Mwenendo wa Bei ya Nondo

JIJI / MJI	NONDO 8mm(TZS/PC)			NONDO 10mm(TZS/ PC)			NONDO 12mm(TZS/PC)			NONDO 16mm(TZS/PC)		
	Machi , 2021	Machi , 2022	Badi- liko %	Machi , 2021	Machi , 2022	Badi- liko	Machi , 2021	Machi , 2022	Badi- liko %	Machi , 2021	Machi , 2022	Badi- liko %
Mtwara	11,750	15,500	31.9	17,000	19,000	11.8	21,500	27,250	26.7	42,500	47,500	11.8
Dar es Salaam	11,500	15,000	30.4	16,000	18,000	12.5	20,500	26,000	26.8	34,000	45,000	32.4
Musoma	11,000	16,000	45.5	15,500	19,000	22.6	21,000	27,000	28.6	34,000	44,000	29.4
Mwanza	15,000	16,500	10.0	16,000	19,000	18.8	19,500	26,500	35.9	35,000	48,000	37.1
Tanga	12,000	15,500	29.2	15,000	18,000	20.0	17,000	26,000	52.9	32,000	45,000	40.6
Arusha	13,500	15,000	11.1	16,000	18,500	15.6	20,000	26,500	32.5	32,000	46,000	43.8
Rukwa	14,000	16,000	14.3	17,000	20,000	17.6	22,000	26,500	20.5	36,000	45,000	25.0
Morogoro	12,000	15,500	29.2	15,500	19,200	23.9	20,000	26,500	32.5	35,000	46,000	31.4
Lindi	10,500	15,500	47.6	14,000	20,000	42.9	22,000	27,500	25.0	39,500	48,000	21.5
Kigoma	12,000	17,000	41.7	15,000	20,000	33.3	19,000	28,000	47.4	37,500	52,000	38.7
Moshi	11,000	15,000	36.4	15,000	18,500	23.3	19,000	27,000	42.1	37,500	46,000	22.7
Bukoba	12,000	17,000	41.7	17,000	20,000	17.6	21,000	27,500	31.0	37,000	48,000	29.7
Songea	13,000	15,500	19.2	16,000	19,000	18.8	21,500	27,000	25.6	36,500	46,000	26.0
Dodoma	11,000	15,500	40.9	17,000	20,000	17.6	21,500	27,000	25.6	36,000	46,000	27.8
Iringa	12,000	15,550	-87.1	15,500	20,000	29.0	20,000	27,000	35.0	35,000	45,000	28.6
Wastani	12,161	15,750	29.5	15,857	19,157	20.8	20,393	26,875	31.8	36,036	46,607	29.3

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Jedwali Na. 8: Mwenendo wa Bei ya Bati

JIJI MJI	BATI 32G (TZS/PC)			BATI 30G (TZS/PC)			BATI 28G (TZS/PC)		
	Machi , 2021	Machi , 2022	Badiliko %	Machi , 2021	Machi , 2022	Badiliko %	Machi , 2021	Machi , 2022	Badiliko %
Mtwara	16,000	16,000	0.0	20,000	28,000	40.0	28,000	37,000	32.1
Dar es Salaam	17,000	17,000	0.0	22,000	27,000	22.7	27,500	35,000	27.3
Musoma	16,000	16,000	0.0	22,000	28,000	27.3	26,000	40,000	53.8
Mwanza	15,000	22,000	46.7	20,000	27,000	35.0	28,000	37,000	32.1
Tanga	16,000	16,000	0.0	20,000	28,000	40.0	26,000	35,000	34.6
Arusha	16,000	22,000	37.5	20,500	28,000	36.6	26,500	37,000	39.6
Rukwa	15,500	15,500	0.0	21,000	28,000	33.3	26,500	40,000	50.9
Morogoro	16,000	21,500	34.4	22,000	28,000	27.3	27,000	37,000	37.0
Lindi	16,000	16,000	0.0	20,000	27,000	35.0	29,500	37,000	25.4
Kigoma	16,000	23,000	43.8	19,000	28,500	50.0	27,500	40,000	45.5
Moshi	16,000	16,000	0.0	20,000	27,000	35.0	27,000	37,000	37.0
Bukoba	17,000	17,000	0.0	21,000	28,000	33.3	28,000	38,000	35.7
Songea	17,000	21,500	26.5	21,500	28,500	32.6	30,000	40,000	33.3
Dodoma	17,000	22,000	29.4	22,000	27,000	22.7	28,000	35,000	25.0
Iringa	16,000	16,000	0.0	22,000	27,500	25.0	27,000	37,000	37.0
Wastani	16,179	18,679	15.5	20,786	27,714	33.3	27,536	37,500	36.2

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 9: Mwenendo wa Bei ya Saruji

JUJI/MJI	BEI YA MFUKOMOJA WA SARUJI WA KILO 50 (SH.)		
	Machi, 2021	Machi, 2022	Badiiko %
Mtwara	15,400	15,500	0.6
Dar es Salaam	15,550	16,000	2.9
Musoma	21,900	22,500	2.7
Mwanza	19,250	19,500	1.3
Tanga	14,000	15,000	7.1
Arusha	17,594	18,000	2.3
Rukwa	20,000	22,000	10.0
Mbogoro	15,750	16,750	6.3
Lindi	16,000	16,500	3.1
Kigoma	21,375	22,000	2.9
Moshi	15,333	16,000	4.4
Bukoba	21,375	22,000	2.9
Songea	16,222	17,000	4.8
Dodoma	17,800	18,000	1.1
Iringa	17,375	17,500	0.7
Wasani	17,662	18,283	3.5

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Jedwali Na. 10: Uwezo wa Uzalishaji wa Viwanda vya Saruji

Na.	Jina la Kiwanda	Kiwanda Klipo	Jina la Bidhaa inayozalishwa	Uwezo Ulosinrikwa (Tari) Tones	Uwezo wa Uzalishaji Uhudurika (Tari)
1	Tanzania Portland Cement Co Ltd	Tegeta- Wazohill	<i>Twiga Cement</i> (<i>Twiga</i> <i>Ordinary, Twiga Plus+,</i> <i>and Twiga Extra</i>)	2,000,000	1,400,000
2	Tanga Cement Co Ltd	Pongwe-Tanga	<i>Simba</i> <i>Cement</i>	1,250,000	1,000,000
3	Mbeya Cement Co Ltd	Mbeya Vijiri	<i>Tenbo</i> <i>Cement</i>	400,000	350,000
4	Lake Cement	Kigamboni (Kimbi) - DSM	<i>Nyati</i> <i>Cement</i>	500,000 M/ramum	83% (415,000)
5	Lee Building Materials Company Limited	Kilwa Masoko - Lindi	<i>Kilwa</i> <i>Cement</i>	300,000	240,000
6	ARM Cement Co Ltd/ Maveni Limestone Company	Muranga- Coast Region	<i>Rhino</i> <i>Cement</i>	750,000	Around 50% (375,000)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na.	Jina la Kiwanda	Kiwanda Kilipo	Jina la Bidhaa inayozalishwa	Uwezo Uliosimikwa (Tani) Tones	Uwezo wa Uzalishaji Unaotumika (Tani)
7	Camel Cement Ltd	Mbagala - DSM	Camel Cement	150,000	150,000
8	Dangote Cement Industry	Mikindani, Mtwara	Dangote Cement	3,000,000	2,250,000
9	Moshi Cement	Holii, Kilimanjaro	Moshi Cement	2,100,000	900,000
10	Kisarawe Cement Company	Coast	Lucky Cement	400 MT/DAY (120,000)	150 MT/DAY (45,000)
11	Fortune Cement Co Ltd	Mkuranga-Coast Region	Diamond Cement		300 tonnes/Day (90,000)
12	Chang Jiang	Mikindani, Mtwara	Mtwara Cement	150,000	100,000
13	Arusha Cement Co Ltd	Arusha-Ngorongoro	Zaidi Cement	500 MT/Day (150,000)	250 tonnes/day (75,000)
14	Kilimanjaro Cement Co	Tanga	Kilimanjaro Cement	108,000	43,200
JUMLA				10,978,000	7,433,200

^a *Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara*

Jedwali Na. 11: Mwenendo wa Bei za Mafuta ya Kula (2019 - 2022)

Bidhaa	Machi, 2019		Machi, 2020		Machi, 2021		Machi, 2022	
	Bei ya Dunia (\$/mt)	Nchini (Sh./Ltr)						
Mafuta ya Alizeti	711.71	4,176.92	730.00	5,216.46	1,611.11	5,512.50	1,491.30	7,625.00
Mafuta asili ya Mawese	573.02	3,359.09	636.25	3,475.00	1,030.48	4,987.50	1,776.96	5,685.71

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Jedwali Na. 12: Mwenendo wa Wastani wa Bei za Mazao Makuu ya Chakula Tanzania Bara (Gunia La Kilo 100)

Bidhaa	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022*
Maharage	159,452	159,306	175,103	165,589	172,170	198,231	176,202	185,786
Uwele	76,609	91,014	107,781	79,056	90,524	109,704	109,598	114,093
Ulez	111,786	112,546	150,316	140,728	133,203	128,488	151,480	168,354
Viasi Mviringo	76,031	83,174	76,786	77,235	72,647	77,778	68,838	79,742
Mahindi	50,844	63,190	78,059	43,862	65,481	62,849	47,713	62,684
Mccheli	161,609	158,059	177,463	169,128	170,049	159,198	141,251	184,348
Mtama	71,635	93,590	100,422	78,632	85,740	103,589	99,304	116,839
Ngano	117,413	124,096	124,736	116,242	124,598	122,293	122,098	149,940

Angalizo: Mwaka 2022* ni kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2022

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 13: Mwenendo wa Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa

Mwaka	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Asilimia	7.86	7.81	7.67	8.05	8.5	8.4	8.0

Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)

Jedwali 14: Ukuaji wa Sekta ya Viwanda

Mwaka	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Asilimia	7.1	10.8	8.2	8.3	5.8	4.5	5.1

Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)

Jedwali Na. 15: Idadi ya Ajira katika Sekta ya Viwanda 2013 – 2021

Miaka	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Ajira	231,098	242,654	254,786	267,524	280,899	306,180	336,797	370,485	345,615

Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)

Jedwali Na. 16: Usajili wa Miradi ya Uwekezaji Katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022

Sekta	Idadi ya Miradi	Miradi ya Watanzania	Miradi ya Wageni	Miradi ya Ubia	Ajira	Maji (USDMI)	% sekta katika Miradi	% sekta katika Maji
Klimo	20	7	7	6	2,751	244.0	9.7	13.1
Majengoya Biashara	17	9	4	4	2,647	302.0	8.3	16.2
Miundombinu	1	0	1	0	10,000	50.5	0.5	2.7
Nishati	1	0	1	0	3	100.0	0.5	5.4
Taasisi za Fedha	2	0	0	0	2,744	72.7	1.0	3.9
Raslimali watu	9	3	0	6	804	15.9	4.4	0.9
Uzalishaji Mwandari	99	28	43	29	12,135	498.0	48.1	268
Huduma	15	4	5	6	1,133	65.6	7.3	3.5
Mawasiliano	2	0	2	0	85	177.0	1.0	9.5
Utalii	17	6	6	6	866	55.7	8.3	3.0
Usafirishaji	23	13	3	7	4,283	278.0	11.2	15.0
	206	70	72	64	37,451	1,859.4	100.0	100.0

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 17: Usajili wa Miradi ya Uwekezaji EPZA Julai 2021 hadi Machi, 2022

Na.	Jina la Kumpuni	Mtaji utakao wekezwa (USD Milioni)	Makadriyo ya Mauzo Nje kwa mwaka (USD Milioni) 2021 /2022	Ajira	Sekta	Hilua iliydikwa	Nchi walikida Wawezaji
1.	Kishi Green limited	4.56	1.2	120	KILIMO - Kuchakata mazao ya jamii ya kunde.	Uendelezaji unaendelea	Indiana China (Hongkong)
2.	Green Bridge Commodities Limited	3.4	2.5	90	KILIMO - Kuchakata mazao ya jamii ya Kunde na Karanga.	Uendelezaji unaendelea	Tanzania na India
3.	Coastal Nuts Tanzania Limited	2.5	4.5	900	KILIMO Kuchakata Korosho	Uendelezaji (Development)	Tanzania
4.	NBIndustries Limited	5.3	16.5	30	KILIMO Kutengeneza vifungashio	Uendelezaji unaendelea	India
5.	Diamond Foods Limited	0.8	1.46	40	KILIMO Kutengeneza vyakula	Kimeanza Kazi	India
6.	Tanzania Huafeng Agriculture Development limited	4.56	1.2	120	K I L I M O - Kuchakata mihogo (chips) kwa ajili ya chakula na unga wa stachi kwa matumizi ya vivandari	Uendelezaji unaendelea	China
7.	East Africa zhenyuan Group Company Ltd	10	5.5	1000	KILIMO - Kuchakata mazao ya misitu (mbao)	Uendelezaji unaendelea	China

Chanzo: Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na 18: Mchanganuo wa Mikopo Iliyotolewa kupitia Mfuko wa NEDF Kimkoa kwa Kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022

Na	MKOA	MKOPO YOTE (SH)	WANIFAKA		
			JUMA	WANAWAKE	WANALUME
1	Dar es Salaam	65,345,138,917.60	429,311	287,590	141,721
2	Mbeya	52,680,428,537.23	346,107	237,666	108,441
3	Iringa	50,493,487,438.39	331,739	229,042	102,697
4	Njombe	49,849,605,700.78	327,511	226,508	101,008
5	Ruvuma	46,763,667,282.63	307,237	214,341	92,896
6	Klimnajaro	46,196,715,386.49	303,510	182,105	121,405
7	Arusha	45,592,245,167.28	299,541	179,726	119,815
8	Lindi	39,129,853,001.90	257,084	154,249	102,835
9	Tanga	38,931,818,761.55	255,782	158,469	97,313
10	Mwanza	37,715,726,251.92	247,788	158,675	89,113
11	Manyara	37,309,019,816.59	245,121	147,070	98,051
12	MtWARA	37,132,787,373.11	243,963	146,375	97,588
13	Mbagao	35,943,319,800.80	236,147	146,690	89,457
14	Rukwa	34,943,577,444.96	229,575	137,745	91,830
15	Mara	32,121,604,545.35	211,039	126,622	84,417
16	Pwani	29,951,597,026.84	196,781	118,067	78,714
17	Songwe	29,585,278,758.28	194,372	116,626	77,746
18	Shinyanga	27,973,763,858.42	183,785	110,272	73,513
19	Tabora	25,059,415,047.61	164,637	98,785	65,852
20	Dodoma	22,849,364,945.60	150,121	98,048	52,073
21	Singida	22,540,894,311.74	148,093	88,854	59,239
22	Kigoma	20,807,403,542.14	136,701	82,022	54,679
23	Kagera	20,333,473,647.67	133,592	80,155	53,437
24	Katavi	18,706,783,134.56	122,901	73,741	49,160
25	Simiyu	18,300,076,699.22	120,232	72,137	48,095
26	Geita	16,742,953,601.34	109,998	66,001	43,997
	Jumla	903,000,000,000.00	5,932,668	3,737,581	2,195,087

Chanzo: Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa lamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati, kwa niaba. *(Makof)*

MHE. MARTHA N. GWAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira na Wajumbe wenzangu wa Kamati, nashukuru kupata fursa hii kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uzima na kutuwezesha kukutana siku ya leo, kwa mara nyingine tena nitoe pole kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge, familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa Rukwa Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, kilichotokea tarehe 24 Aprili, 2022. Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati yetu na hadi wakati tunaandaa rasimu ya taarifa hii tulishirikiana naye. Mchango wake kwa Kamati ulikuwa wa umuhimu sana na tutamkumbuka daima. Kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati tunaendelea kumuombea apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Naomba taarifa yote hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa uwasilishaji wangu, naomba kulijulisha Bunge kwamba taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi; sehemu ya pili inayoripoti matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa kuchanganua kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; utekelezaji wa maendeleo na mpango wa Wizara, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati; sehemu ya tatu inayoripoti maoni na ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi na sehemu ya nne ni mwisho na hitimisho na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023 ni kama ifuatavyo; matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; maelezo kuhusu matokeo ukaguzi wa miradi ya maendeleo na maoni ya Kamati ni kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa tatu hadi 13 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022; maelezo ya Kamati kuhusu malengo ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 13 hadi wa 14 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara mpya ambayo imeundwa kwa Tamko la Serikali Namba 384 la mwaka 2022. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imeendeshwa kwa Bajeti za Fungu 11, 44 na Fungu 60 zilizopitishwa mwaka 2021/2022 chini ya iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji Fungu 11 na iliyokuwa Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 na Fungu 60. Jumla ya shilingi 112,688,672,000 ziliidhinishwa kutumiwa kwa mafungu hayo ambapo Fungu 11 ni shilingi 7,018,213,000.00 na Fungu 44 ni shilingi 81,398,833,000.00 na Fungu 60 ni shilingi 24,271,626,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Wizara ilikuwa haijakusanya maduhuli yoyote ikilinganishwa na lengo la ukusanyaji shilingi 15,000,000. Pia katika kipindi hicho Wizara imepokea jumla ya shilingi 50,154,649,590.78 sawa na asilimia 44 ya jumla ya bajeti iliyoitengwa. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi 4,358,755,320.93 kutoka Fungu 11 sawa na asilimia 62; shilingi 29,293,865,140.71 kutoka Fungu 44 sawa na asilimia 13; na shilingi 16,502,029,129.14 kutoka Fungu 60 sawa na asilimia 68 ya bajeti zilizotengwa. Mchanganuo kuhusu mafungu haya ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu 44 Viwanda lilitengewa shilingi 53,087,886,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha shillingi 52,687,886,000 fedha za ndani na shilingi 400,000,000 fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 10,220,313,313.71 ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 19 ya fedha zilizotengwa. Wizara haijapokea fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Fungu 11 na Fungu 60 hazikutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Fungu 11 na 60 ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka fedha 2021/2022, ni kama ifuatavyo; Fungu 44 Viwanda hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa bajeti ulipaswa kuwa asilimia 66.6 lakini Wizara imepokea asilimia 36 tu kwa maana kuwa utekelezaji umepungua kwa asilimia 46 na upande wa miradi ya maendeleo kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa ni asilimia 19 tu ya bajeti yote iliyoitengwa.

Kwa Fungu 60 – Biashara; mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina unaridhisha kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa bajeti ulipaswa kuwa asilimia 66.6. Aidha, kiasi kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2022 ilikuwa ni asilimia 68 ya bajeti yote, hata hivyo Fungu hili halikutengewa fedha za miradi ya maendeleo.

Kuhusu Fungu 11 – Uwekezaji; mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa wastani, kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa bajeti ulipaswa kuwa asilimia 66.6 hata hivyo, kiasi kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2022 ilikuwa ni asilimia 62 ya bajeti yote, hata hivyo Fungu hili halikutengewa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake Fungu 44 kwa sasa hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa bajeti ulipaswa kuwa asilimia 66.6 lakini Wizara ilikuwa imepokea asilimia 44 kwa maana kuwa utekelezaji umepungua kwa asilimia 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha umeathiri zaidi utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo mpaka kufikia Februari, 2022 kiasi kilichopokelewa kilikuwa shilingi 10,155,756,640.60 ambapo ni sawa na asilimia 19 tu kwa maana kuwa asilimia 81 ya miradi ya maendeleo haikutekelezwa. Aidha, fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo shilingi 400,000,000 ilikuwa hajapokelewa hadi wakati Wizara inawasilisha taarifa katika Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mtazamo wa Kamati kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara unaashiria kukwamisha utekelezaji kwa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara kwa mwaka huu wa fedha. Wizara hii inapaswa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa biashara inayolenga katika kupunguza ghamama za uwekezaji na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara. Aidha, Wizara ndio mtafuta

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

masoko wa mazao yatokanayo na kilimo, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha bajeti inayopangwa inaenda kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2021/2022; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendeleko kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi ya maeneo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Aidha, taarifa zaidi kuhusu utekelezaji wa mapato haya ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 21 na 22 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; uchambuzi wa malengo na mpango; Kamati ilibaini kuwa malengo yanayoonekana ni ya uwekezaji wananchi kiuchumi na maendeleo ya sekta binafsi. Hivyo kwa mwaka 2022/2023 malengo makuu ya sekta yatahusisha pia kuhamasisha na kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa makadirio ya matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi 99,105,506,000 katika Fungu 44; kati ya fedha hizo, Wizara inaomba kutengewa shilingi 68,308,687,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 30,796,819,000 kwa matumizi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 8,728,788,000 kwa matumizi mengineyo (*OC*) na shilingi 59,579,899,000 za mishahara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nenda kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

MHE. MARTHA N. GWAU K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa

Kamati; baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara - Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo; mpango wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 pamoja na kuunganishwa kwa mafungu matatu (Uwekezaji, Viwanda na Biashara) sasa bajeti ya Fungu 44 imepungua kwa asilimia 12 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022. Ni mtazamo wa Kamati kuwa upungufu huu hautaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara ilihali ikizingatia majukumu ya Wizara yameongezeka. Aidha, kwa kiasi kilichotengwa, Kamati inaishauri Serikali kuwa bajeti ipelekwe kwa wakati kama iliviotengwa ili isiathiri majukumu na utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya kimkakati hususan Mradi wa Liganga na Mchuchuma; Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inatarajiwa kutimiliwa mwaka 2025 na moja ya vipaumbele vikubwa ni kuhakikisha miradi ya kipaumbele inayotokana na llani ya Chama cha Mapinduzi inaanza utekelezaji; lakini hadi sasa miradi ya kimkakati hususan sekta ya viwanda iliyotajwa katika llani haijaanza kutekelezwa kama Liganga na Mchuchuma. Miradi hii inachochea kwa baadhi ya viwanda nchini hususani viwanda vyta chuma kwa kuwa inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo zingetumika katika viwanda hivyo na pia miradi hii ni muhimu katika uzalishaji wa nishati ya umeme kutokana na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo; kuhakikisha majadiliano yanakamilika katika mradi wa Liganga na Mchuchuma. Aidha, kipaumbele kwa mradi huu wa kimkakati ili itekelezwe mara moja; kulipa fidia wananchi wote ambao ardhi zao zilitwaliwa bila kusubiri hatma ya mazungumzo katika uuwekezaji wa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa umeme viwandani; Kamati ilitembelea viwanda viwili na changamoto

kubwa iliyoripotiwa ilikuwa ni ukatikaji wa umeme; katika masaa manne umeme ulikatika zaidi ya mara mbili; Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza kasi katika miradi ya uzalishaji wa umeme ili sasa umeme uweze kuwa wa kutosha kuhudumia maeneo mengi. Aidha, kwa maeneo ya viwanda, Serikali itoe msukumo katika kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika, vilevile, kuwepo kwa laini ya umeme ya viwanda ambayo ina tofautiana na laini ya majumbani ili kuepuka kukatika kwa umeme na hitilafu ndogo ndogo zinazoathiri upatikanaji wa umeme wa viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (*TANTRADE*); tumeshuhudia Serikali ikiongeza nguvu kubwa katika kutekeleza bajeti ya Wizara ya Kilimo, lakini Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ambayo ndio inatafuta masoko imetengewa bajeti ya shilingi bilioni moja tu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha kwa taasisi ya *TANTRADE* ili kupata nguvu ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kuratibu shughuli za utafutaji wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji wa kanzidata za viwandani; Kamati inasilitiza kanzidata inayoandaliwa iwe na hifadhi ya ukusanyaji wa taarifa na takwimu zilizo chakatwa na kupangwa kwa namna inayoridhisha upatikanaji wa taarifa hizo yaani *access, preserve, manage* na *updating*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji; pamoja na mafanikio na jitihada za Serikali kutafuta na kupunguza jumla ya tozo 60 ambazo zilikuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Kamati inazidi kuweka msisitizo kwa Serikali kuendelea kuwezesha kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na mfumo funganishi ili kuondoa kabisa adha kwa wawekezaji kupata huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utengaji wa maeneo ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogo yaani machinga; Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha

machinga nchi nzima wanapatiwa maeneo ya kufanya biashara. Aidha, maeneo hayo yawe wezeshi na rafiki kwa watu kufika ili wamachinga hawa waweze kupata soko na kuza bidhaa zao.

Vilevile viongozi wa mikoa na Halmashauri wanapaswa kuwaongoza machinga vizuri katika kuwapanga na kuhakikisha mazingira yao yanakua salama muda wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Kujunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika yaani *African Continental Free Area*; Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuridhia Mkataba wa Kujunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika. Kwa Tanzania kujunga na mkataba huu inakuwa sehemu ya soko kubwa barani Afrika lenye takribani watu bilioni 1.3 na pato ghafi la jumla ya kiasi cha triliioni 3.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mkataba huu Tanzania itanufaika kwa kuza bidhaa na huduma. Katika eneo hili Kamati inaishauri Serikali yafuatayo; kujipanga vyema katika eneo la uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa, aidha, kuweka usimamizi mzuri katika kuratibu masoko yetu kimataifa. Kwa kuwa Tanzania ilishawahi kujunga na mikataba wa aina hii na ilikwama katika utekelezaji wake, basi ipo haja ya Serikali kuangalia upya changamoto ambazo zinasababisha mkwamo huu ili zisiweze kujirudia tena katika awamu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuongoza Bunge letu tukufu kwa weledi mkubwa. Vilevile naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kushiriki kikamilifu katika kupertia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka katika taarifa hii na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Ashatu Kijaji - Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Naibu Waziri Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Katibu Mkuu Profesa Godius Kahyarara, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kujibu hoja za Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na kufafanua kwa kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndugu Dickson Bisile, kwa kusimamia vizuri na kuratibu shughuli zote za Idara ya Kamati. (*Makofii*)

Aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati Ndugu Felister Mgonja na Ndugu Nyamwanja Chipanda Chilemeji pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inapatikana na kuwasilishwa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba kulishauri Bunge lako tukufu kukubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA
MAJUKUMU YA WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA (FUNGU 44) KWA MWAKA 2021/2022
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA FUNGU 44 MWAKA WA FEDHA
2022/2023 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalla afya njema na uzima na kutuwezesha kukutana siku hii ya leo. Kwa mara nyingine tena, nitoe pole kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge, Familia, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mhe. Irene Alex Ndyamkama (Mb) kilichotokea tarehe 24 Aprili 2022. Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati yetu na hadi wakati tunaandaa rasimu ya Taarifa hii tulishirikiana nae. Mchango wake kwa Kamati ulikuwa na umuhimu sana na tutamkumbuka daima. Kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati tunaendelea kumuombea apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Naomba Taarifa yote hii iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa uwasilishaji wangu, naomba kulijulisha Bunge kwamba, Taarifa hii imegawanya katika sehemu kuu zifuatazo:-

- a) Sehemu ya **Kwanza** inayotoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa Taarifa pamoja na namna kamati ilivyofanya kazi;
- b) Sehemu ya **Pili** inayoripoti matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa kuchanganua kuhusu; utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utekelezaji wa malengo ya mpango wa Wizara hii, Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;
- c) Sehemu ya **Tatu** inayoripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na Uchambuzi;
- d) Sehemu ya **Nne** na ya mwisho inayohitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023

2.1 Matokeo ya Ulaguzi wa Miradi ya Maendeleo

- a) Miradi ya *Institutional Support - TAMCO Industrial Park, Mradi Namba 6260 Fungu 44, KIBAHA, PWANI*

Mheshimiwa Spika, Eneo la Viwanda la TAMCO limetengwa ili kujengwa viwanda vya sekta kuu tatu, pamoja na eneo la huduma kama ifuatavyo;

- i. Viwanda vya Sekta ya Madawa na Vifaa Tiba (*Pharmaceutical and Medical Facilities Industries*) lenye ukubwa wa **ekari 43.04 (21%)**;

- ii. Viwanda vya Kuunganisha Magari na Mitambo (*Motor Vehicles and Equipment Assembly*) lenye ukubwa wa **ekari 60 (30%)**;
- iii. Viwanda vya Nguo na Mavazi (*Textiles and Apparel Industries*) lenye ukubwa wa **ekari 77.41 (38%)**; na
- iv. Eneo la huduma kwa viwanda lenye ukubwa wa **ekari 26.37 (11%)** litatumika kutoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bwawa la maji taka, kituo cha kupozea umeme, tanki la maji safi, barabara za ndani na hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 jumla ya shilingi **765,000,000** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya TAMCO. Kwa mchanganuo, kiasi cha shilingi **640,000,000** zilitengwa kwaajili ya kukamilisha ujenzi wa mita 563 za barabara kwa kiwango cha lami kwenda kwenye Kiwanda cha Viuadudu (TBPL). Pia kiasi cha shilingi **25,000,000** zilitengwa kwa ajili ya Kufanya tathmini na ufuatilaji na kiasi cha shilingi **100,000,000** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ndani (Majengo na Barabara) katika eneo la Nyanza Industrial Park. Hadi kufikia Februari 2022, Fedha zilizokua zimepokelewa ni kiasi cha shilingi **1,200,000,000** sawa na asilimia **157** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwaajili ya kuendeleza Kiwanda cha Viuadudu (TBPL). Aidha, Fedha hizo zimetumika katika uendeshaji wa kiwanda na uzalishaji na zinapaswa kutumika kwa kipindi cha miezi sita. **Hatahivyo, hadi wakati Kamati inatembelea eneo hili, Fedha za Miradi mingine ya maendeleo zilizokua zimepangwa katika bajeti ya Mwaka 2021/2022 zilikuwa hazijapokelewa.**

Mheshimiwa Spika, kwakuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ndio yenyeye dhamana ya kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Na kwakuwa eneo hili la TAMCO *Industrial park* lilitengwa madhubuti kwaajili ya uwekezaji katika viwanda, hivyobasi, Kamati ilitembelea viwanda viwili vya binafsi katika eneo hili linaloendelezwa na Serikali kupitia NDC. Viwanda hivyo ni kiwanda cha kutengeneza chanjo cha **Hester Bioscience**

na kiwanda cha kuunganisha magari cha **GFA Vehicle Assemblers**.

Mheshimiwa Spika, *Hester Bioscience* ni kiwanda cha kuzalisha chanjo nchini. Kiwanda hiki kimegharimu kiasi cha shilingi **bilioni 44** kutoka kuanza ujenzi hadi sasa katika uzalishaji, ikiwa ni mkopo kutoka benki za nje. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuajiri wataalam wenye uwezo wa kuzalisha dawa wapataao 200 na kina uwezo wa kuzalisha dozi bilioni 1.5 kwa Mwaka na kuzalisha mapato (revenue) zaidi ya **Dola za Marekani milioni 30** kwa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha chanjo **aina 37** na mpaka sasa kimeshazalisha aina 2 za chanjo ambazo hazijaanza kuuzwa. Chanjo zinazozalishwa ni za kukinga **magonjwa 26** ya wanyama ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, farasi na nguruwe hivyo kitasaidia nchi kupunguza gharama ya uagizaji wa chanjo kutoka nje na kupunguza gharama ya Fedha za kigeni. **Serikali kuititia kiwanda hiki itapata mapato kuititia kodi za aina mbalimbali**.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa Ziara katika kiwanda hiki Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;

- i. Kukatika kwa umeme mara kwa mara;
- ii. Kutokuwepo na vifunganisho na malighafi kama vile *stickers* hapa nchini, hali inayopelekea kuagizwa kwa vitu hivi kutoka nje ya nchi na kuchelewa kuvipata kutokana na utaratibu mrefu wa kufanya *clearance* bandarini;
- iii. Riba kubwa kwenye mabenki nchini hali ianyopelekea kukopa mabenki ya nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea Kiwanda cha kuunganisha magari cha **GFA Vehicle Assemblers**. Kiwanda hiki kimegharimu kiasi cha shilingi **bilioni 12** katika uwekezaji wake. Kiwanda kimeshazalisha ajira za moja kwa moja 105 ambapo watanzania ni 101 na wageni ni wanne (4). Inatarajiwa kuwa ajira hizi zitaongezeka mpaka kufikia 700

pindi mitambo ya awamu ya pili (second production line) ikikamilika. Serikali pia itapata mapato kupitia kodi mbalimbali. Mpaka sasa kiwanda kimeunganisha **magari 375** aina ya FAW Trucks. Aidha, Kampuni imeongeza eneo kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda ambacho kitazalisha mabasi na gari *ndogo* (*pick up*).

Mheshimiwa Spika, wakati wa Ziara katika kiwanda hiki changamoto zifuatazo zilibainika;

- i. *Exercise duty* – Magari yanayoagizwa nje yana ushuru sawa na magari yanayozalishwa hapa nchini hivyo kuwa kikwazo kwa wazalishaji wa hapa nchini kwa kuwa bei zao zinakuwa sawa au juu ukilinganisha na magari yanayoagizwa nje ya nchi;
- ii. *Insufficient order* – uhaba wa maombi ya bidhaa zinazotengenezwa na kiwanda;
- iii. Sheria ambazo ni kero kwa wawekezaji hazitoi fursa kwa wawekezaji wa ndani na kulinda viwanda vya ndani;
- iv. Umeme usio wa uhakika.

Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Viwanda hivi;

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutembelea Viwanda vya **Hester Biosciences** na **GFA Vehicle Assemblers** inatoa ushauri ufuatao;

- i. Serikali ihakikishe kuwa kunakuwepo na umeme wa uhakika katika viwanda hivyo;
- ii. Serikali iangalie namna ya kutumia fursa kwa kuwaelimisha wawekezaji ili kuweza kuzalisha vifungashio na malighafi zingine kwa kutumia viwanda vya ndani;
- iii. Serikali kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi yanalindwa na kuzingatiwa;

- iv. Kiwanda GFA Vehicle Assemblers wanaagiza kila kitu kutoka nje ya nchi; Kamati inashauri vipuli, *Spring* na vitu vingine vinavyoweza kutengenezwa hapa visiagizwe nje na badala yake vichukuliwe vya hapa nchini ili kulinda viwanda vya ndani;
- v. Kutokana na umuhimu wa malighafi ya chuma katika kiwanda cha GFA, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudzi za kumaliza majadiliano ya Mchuchuma ili sasa malighafi hii iweze kutumika katika uzalishaji wa viwandani.

b) Institutional Support - TANTRADE;

Mradi Namba 6260 Fungu 44 - DAR ES SALAAM.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imepewa dhamana ya kuishauri Serikali kwenye masuala ya kuunda, kuendeleza, kusimamia na kutekeleza sera na mikakati ya biashara nchini. Aidha, TANTRADE inajukumu la kudhibiti na kuendeleza biashara nchini kwa kuunganisha bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa nchini na masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 TANTRADE ilitengewa kiasi cha shilingi 500,000,000 kwajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, hadi kufikia Februari 2022 TANTRADE ilikua imepokea jumla ya shilingi **1,960,881,386** sawa na asilimia **392**.

Mheshimiwa Spika, Fedha hizi zimeongezeka kwasababu TANTRADE ilifanya Uratibu na Ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Dunia ya Expo 2020 Dubai. Fedha hizi zote zilitumika kuratibu maonesho hayo. Hata hivyo, miradi mingine yote ya maendeleo haikupatiwa Fedha. Kamati ilitembelea eneo la TANTRADE, Dar Es Salaam na ilioneshwa Jengo la maonyesho linalohitaji kuboreshwa pamoja na kumbi mbalimbali ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Hata hivyo ufinyu wa Bajeti umekwamisha utekelezaji wa majukumu yao.

Maoni na Ushauri kuhusu ziara hii ya TANTRADE;

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutembelea eneo hili la TANTRADE inashauri yafuatayo;

i. Kwa kuzingatia kuwa maonesho ya sabasaba ni ya Kimataifa, Kamati inashauri TANTRADE wapate eneo kubwa litakalopangwa vizuri na ambalo litakua pembezoni mwa mji ili shughuli zote ziweze kufanyika kwa nafasi na kuongeza wigo wa kutoa huduma katika maonesho haya.

ii. Muda wa maonesho uongezwe walau hata kwa mwaka iwe mara tatu ili kukidhi haja ya wanaohitaji bidhaa kutoka kwa waoneshaji mbalimbali; Aidha, iangalie namna ya kuwa na maonesho mengine mfano ngoma za asili, waganga wa jadi ili kuibua fikra chanya kwenye utamaduni na mambo mengine ya asili;

iii. Zao la mwani liendelee kutangazwa katika maenesho ya kibiashara kwakuwa litaliingizia Taifa Fedha nyangi;

iv. Pawepo na mahusiano ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara nyingine ambazo zina uhusiano na biashara mfano Wizara ya Kilimo ili kuhakikisha uratibu mzuri wa bidhaa sokoni;

v. TANTRADE wawe na utaratibu wa kupata kumbukumbu za wadau wote wanaoshiriki maonesho yao (uwepo wa kanzidata) ili waweze kuwatambua na kuweza kufanya tathimini ya idadi ya washiriki katika maenesho.

c) Institutional Support – TIRDO;

Mradi Namba 6260 Fungu 44 - DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuanzisha Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), ili lifanye utafiti na kutoa huduma za kitaalam kwa viwanda vyote, badala ya kila kimoja kuwa na kitengo chake cha utafiti. Azma hiyo ya kujenga uchumi wa viwanda shindani na endelevu

inaendelea chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 TIRDO ilitengewa jumla ya kiasi cha Shilingi **1,850,000,000** kwa ajili ya

- i. Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Utawala ili kutoa nafasi ya kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashiri wa Teknolojia na Viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia **Shilingi 800,000,000**;
- ii. Ununuzi magari matatu (3) ili kufanikisha shughuli za utafiti na utekelezaji wa majukumu ya Shirika **Shilingi 600,000,000**; na
- iii. Kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji (Industrial Mapping) **Shilingi 450,000,000**.

Mheshimiwa Spika; Kamati ilitembelea eneo la TIRDO Msasani Dar es

Salaam na kuona utekelezaji wa mradi kama ilivyopangwa, na hadi Kamati inatembelea jumla ya kiasi cha shilingi **1,400,000,000** sawa na **asilimia 76** kilikuwa kimeshapokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo;

i. **Jengo la Utawala;** Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 zilitengwa Shilingi za Tanzania **800,000,000** kwa ajili ya kumalizia jengo la Utawala-TIRDO. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2021 TIRDO ilikuwa imeshapokea kiasi tangulizi (Advance payment) cha Shilingi **690,261,559.11** sawa na **asilimia 86.3** kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa ujenzi na Mkandarasi (SUMA JKT) ameshaanza maandalizi ya awali (Kusanifu jengo) ili kuanza utekelezaji wa umalizaji wa jengo la Utawala. **Kamati ilielezwa kuwa Ujenzi unatarajia kuanza mwezi Aprili, 2022.**

ii. **Mtambo wa kuzalisha mkaa mbadala (Briketi);** Shirika kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Uhandisi, imeshirikiana na Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) limeweza kuzalisha

teknolojia ya utengenezaji wa mkaa mbadala (Briketi) wenye nguvu, usiovunjika vunjika, usiota majivu mengi na kutokuwa na moshi mwingi ambao ni rafiki kwa mazingira kwa kutumia makaa ya mawe. Pia mtambo wa kati wa kuzalisha vitofali, (wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili kwa saa) tayari umekwisha nunuliwa na kusimikwa kwa majaribio katika jengo lilipo TIRDO. Aidha, katika eneo hili la TIRDO kamati pia ilitembelea eneo la maabara na kuoneshwa wabunifu mbalimbali wa mitambo ikiwemo fundi wa taa za kisasa (kidijitali). Kijana huyu wa Kitanzania anauwezo wa kutengeneza taa zinazofanya kazi kwa kupewa amri (*command light*). Wabunifu wengine walionesha namna walivyochukua majani ya asili na kuzalisha bidhaa mbalimbali kama vile mafuta na dawa za maji. Kamati inapongeza juhudhi binafsi za vijana hawa wa kitanzania ambao wanajitolea kutumia ubunifu wao kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuangalia vijana hawa wa kitanzania wanaojitolea kufanya kazi na kuonesha ubunifu wao katika kutengeneza bidhaa. Aidha, vipaji hivi vinapaswa kukuzwa kwa kupewa mitaji na kutafutiwa masoko ili waweze kunufaika na utaalamu na ubunifu wao.

Maoni na Ushauri kuhusu Ziara hii ya TIRDO;

- i. Kwakuwa Fedha za mradi wa Jengo la Utawala zimeshatoka kwa asilimia 86.3 ujenzi unapaswa kuanza kama ambavyo kamati ilielezwa;
- ii. Elimu inahitajika juu ya matumizi ya mkaa mbadala ili wananchi wengi waweze kuutumia;

Mheshimiwa Spika, Katika kuangalia azma ya Serikali katika kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi, kamati ilitembelea katika Viwanda vya Tanzania Distillers Ltd (TDL) na NIDA Textile Co. Ltd. Lengo la kutembelea viwanda hivi ni kuangalia mazingira yauwekezaji nchini na namna ambavyo sekta binafsi zinachangia katika ukuaji wa uchumi. Kwa maelezo zaidi kuhusu viwanda hivi ni kama ifuatavyo;

d) Kiwanda cha Tanzania Distillers Ltd (TDL), Temeke - Dar Es Salaam

Mheshimiwa Spika, Tanzania Distilleries Limited (TDL) ni kampuni tanzu ya Tanzania Breweries Limited (TBL), mwanachama wa *Anheuser-Busch InBev*. Kamati ilitembelea kiwanda hiki kilichopo jijini Dar Es Salaam na kuona shughuli mbalimbali za uzalishaji zinavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, TDL ni wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa divai na spiriti. Konyagi ni chapa ya bendera ya kampuni, lakini pia inajivunia kuhudumia watumiaji wengi. Aidha, bidhaa zingine zinazozalishwa katika kiwanda hiki ni pamoja na *Valuer Superior Brandy*, *Vladimir Vodka*, *Zanzi Cream Liqueur*, *Imagi Wine* na *Dodoma Wine*. TDL ina wigo tofauti wa kitaifa ndani ya Tanzania kuhakikisha kuwa bidhaa za kampuni zinapatikana nchini katika maeneo yote. Konyagi pia inasafirishwa kwenda kwenye masoko mengine kama vile Kenya, Rwanda, Zambia na Burundi.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii yafuatayo yalibainika;

i. Mfumo wa ulipaji kodi kielektroniki (Electronic Tax Stamp – ETS);

Toka kuanzishwa kwa mfumo huu ni mshauri elekezi mmoja tu ndio anashinda zabuni na anatoza gharama kubwa kupitia ukusanyaji wa kodi hali ambayo inapelekea kupunguza mitaji lakini pia inapunguza Akiba ya Fedha za Kigeni (National Forex Reserves). Aidha, gharama inayotozwa ni kubwa kuliko hata kodi inayokusanywa na Serikali. Mtazamo katika hili ni kuwa; Serikali kuangalia namna ya kupunguza gharama inayotozwa na mshauri elekezi au iangalie namna ya kumpata mshauri elekezi mwingine atakaetoza gharama nafuu na ambae atatokea nchini au ikiwa amepatikana kutoka nje ya nchi basi ashirikiane na kampuni ya ndani kutoa huduma hiyo.

ii. Uwepo wa bidhaa bandia (feki) sokoni

Iliripotiwa kuwa bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda hiki, wapo watu wanaozalisha kwa kuiga aina na ladha (kuzalisha

bidhaa feki). Hali inayopelekea Serikali kupoteza mapato kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa Mwaka. Hivyo ipo haja ya Serikali kuangalia namna ya kuongeza usimamizi na udhibiti wa bidhaa hizi bandia.

Kamati ilitoa Ushauri kwa Serikali kuchukua hoja zote zilizojitokeza na kuangalia namna ya kuzifanya kazi.

e) **Kiwanda cha NIDA TEXTILE CO. LTD – DAR ES SALAAM**

Mheshimiwa Spika, Nida Textile Mills ni kiwanda cha nguo kinachotengeneza khanga, vitenge, nyuzi za kushonea nguo na vitambaa. Kiwanda hiki kiko katika barabara ya Nelson Mandela Tabata, katika jiji la Dar es Salaam. Kiwanda kimetoa ajira kwa watu 3,000 katika maeneo yote ya uzalishaji na ajira zaidi ya elfu 7000 kwa wakulima. Kiwanda hiki ndio wanunuzi wakubwa wa pamba ya ndani kwa matumizi ya ndani, katika mwaka 2019, walinunua pamba ya ndani kwa \$0.72 kwa LBS wakati kiwango cha kimataifa kilikuwa \$0.57 tu kusaidia wakulima. Aidha, kwa sasa mashine na vifaa vya uzalishaji vina thamani ya zaidi ya Bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara katika kiwanda hichi, changamoto zifuatazo zilibainika;

i. Kuwepo kwa bidhaa zinazoingia nchini bila kulipa kodi na zinashindanishwa na bidhaa za NIDA ambazo zinalipiwa kodi;

ii. Riba kubwa kwenye mabenki nchini ukilinganisha na nchi nyingine. Mfano China riba ni asilimia 1-2 wakati nchini riba ni asilimia 16 -18;

iii. Upungufu wa pamba ambapo pamba inayozalishwa nchini inadumu sokoni kwa mwezi mmoja na nusu tu na baada ya hapo pamba haipatikani. Ikilinganishwa na nchi nyingine kama India na China ambapo pamba inanunuliwa kulingana na mahitaji. Hali hii inamlazimu mfanyakia shara awe na mtaji mkubwa.

Katika ziara ya kiwanda hichi, Kamati ilitoa Ushauri kwa Serikali kuchukua hoja zote zilizojitokeza na kuangalia namna ya kuzifanya kazi.

2.2 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya kisekta, Wizara na Taasisi zake katika Mipango Mikakati (Strategic Plan) yake imezingatia Dira ya Taifa ya 2025, llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Tatoo wa Maendeleo na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Taifa. Kamati iliangalia na kujiridhisha kuwa Malengo ya llani ya CCM mahsus yanoyohusu sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara kama yanaendana na kutekelezwa na Wizara, na Kamati ilibaini kuwa yanatekelezwa, mfano Ibara ya 22 (a) ya llani ya Chama cha Mapinduzi inaeleza kuhusu uimarishaji na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara nchini (blueprint) lengo hili limetekelizwa na Wizara pamoja na kuwepo kwa baadhi ya changamoto katika utekelezaji wake. Aidha, ibara zingine kuhusu sekta hii zinapatikana katika Ibara ya 18, 26, 27, 32, 46, 49, 122 ya llani ya CCM na Wizara inazingatia na kutekeleza malengo haya.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilijiridhisha kwa kuangalia utekelezaji wa Mpango wa Tatoo wa Miaka Mitano yanayohusu Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara mfano ukurasa **namba 31** wa Kitabu cha Mpango wa Tatoo wa maendeleo ya Taifa umeeleza kuhusu hatua za kukuza uwekezaji nchini. Lengo hili linatekelezwa na Wizara na tunashuhudia juhudhi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuvutia uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua malengo mazuri yaliyowekwa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, hata hivyo Kamati inaona ipo haja ya kuongeza nguvu katika Vipaumbele vya Sekta katika maeneo yafuatayo;

a) Kuendeleza miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa ambayo hadi sasa utekelezaji wake

haujaanzaa kama vile miradi ya Liganga na Mchuchuma,
Magadi Soda n.k

b) Kuimarisha mifumo ya uratibu na Uhamasishaji wa usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa yaani ndani na nje ya nchi;

c) Kuboresha mazingira wezeshi ya kuendeleza Viwanda na Biashara kwa kuititia na kutunga sheria, sera na mikakati ya kuvutia uwekezaji;

d) Kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) na Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zitakazouzwa nje (EPZ).

2.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara mpya ambayo imeundwa kwa Tamko la Serikali Namba 384 la Mwaka 2022. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara inaendeshwa kwa Bajeti za **Fungu 11, 44 na 60** zilizopitishwa Mwaka 2021/2022 chini ya iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji (**Fungu 11**); na iliyokuwa Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44 na 60**). Jumla ya Shilingi **112,688,672,000.00** ziliidhinishwa kutumiwa na mafungu hayo ambapo **Fungu 11** ni Shilingi **7,018,213,000.00**; Fungu 44 ni Shilingi **81,398,833,000.00**; na **Fungu 60** ni Shilingi **24,271,626,000.00**.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Wizara ilikuwa hajjakusanya maduhuli yoyote ikilinganishwa na lengo la kukusanya Shilingi 15,000,000. Pia, katika kipindi hicho, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 50,154,649,590.78 sawa na **asilimia 44** ya jumla ya Bajeti iliyotengwa. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 4,358,755,320.93 kutoka **Fungu 11** (sawa na asilimia 62); Shilingi 29,293,865,140.71 kutoka **Fungu 44** (sawa na asilimia 13) na Shilingi 16,502,029,129.14 kutoka **Fungu 60** (sawa na **asilimia 68**) ya Bajeti zilizotengwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mchanganuo kuhusu mafungu haya ni kama inavyoonekana katika **kielelezo namba 1**.


Kielelezo Na. 1 Muhtasari wa Mchanganuo wa Bajeti iliyodhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Majukumu chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa fungu 44, 11 na 60

Chanzo: *Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara*

Fungu 44

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara katika Fungu 44 ilitengewa jumla ya Shilingi 28,310,947,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 5,119,373,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 23,191,574,000 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 4,003,270,564.83 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na **asilimia 78** ya Fedha zilizotengwa na Shilingi 15,070,281,263.02 kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 65** ya Fedha iliyoitengwa.

Kielelezo Na 2 Ufafanuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 44 - Viwanda



Chanzo; Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Fungu 11

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara kuititia Fungu 11 ilitengewa jumla ya Shilingi 7,018,213,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 3,229,915,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 3,818,298,000.00 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 2,081,028,791.56 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na **asilimia 64** ya Fedha zilizotengwa na Shilingi 2,277,726,529.37 kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 60** ya Fedha iliyotengwa.

Fungu 60

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara kuititia Fungu 60 ilitengewa jumla ya Shilingi 24,271,626,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 1,470,091,000 kwa ajili ya Matumizi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mengineyo (OC) na Shilingi 22,801,535,000.00 kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 1,151,649,949.48 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na **asilimia 78** ya Fedha zilizotengwa na Shilingi 15,350,379,179.66 kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 67** ya Fedha iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 44 (V i w a n d a) lilitengewa Shilingi 53,087,886,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 52,687,886,000 Fedha za ndani na Shilingi 400,000,000 Fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 10,220,313,313.71 ya Fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 19 ya Fedha zilizotengwa. Wizara haijapokea Fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Fungu 11 na 60 hazikutengewa Fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Kielelezo Na. 3 Ufanuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 11 na 60

Chanzo; Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

2.3.1 Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44 & 60**) ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **15,000,000** (Fungu 44 – Viwanda Shilingi **9,000,000.00** na Fungu 60 – Biashara Shilingi **6,000,000.00**) kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote.

2.3.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa Fedha ikilinganisha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka Fedha **2021/2022**, ni kama ifuatavyo:-

a) Fungu 44 – Viwanda

Hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina, kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa Bajeti ulipaswa kuwa **asilimia 66.6** lakini wizara ilikuwa imepokea **asilimia 36** tu kwa maana kuwa utekelezaji umepungua kwa **asilimia 46** na Upande wa miradi ya maendeleo Kiasi cha Fedha kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 19** tu ya Bajeti yote.

b) Fungu 60 – Biashara

Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina unaridhisha kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa Bajeti ulipaswa kuwa **asilimia 66.6. Aidha**, kiasi kilichopokelewa hadi kufikia Februari 2022 ilikua ni **asilimia**

68 ya Bajeti yote, hatahivyo Fungu hili halikutengewa Fedha za Miradi ya maendeleo.

c) **Fungu 11 - Uwekezaji**

Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina ni wa wastani, kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa Bajeti ulipaswa kuwa **asilimia 66.6** hatahivyo, kiasi kilichopokelewa hadi kufikia Februari 2022 ilikua ni **asilimia 62** ya Bajeti yote, hatahivyo Fungu hili halikutengewa Fedha za Miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake **Fungu 44** (kwa sasa) hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina, kwani kiuhalisia mpaka kufikia Februari, 2022 utekelezaji wa Bajeti ulipaswa kuwa **asilimia 66.6** lakini wizara ilikuwa imepokea **asilimia 44** kwa maana kuwa utekelezaji umepungua kwa **asilimia 34**; **na Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha umeathiri zaidi utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo mpaka kufikia Februari, 2022 kiasi kilichopokelewa kilikuwa shilingi **10,155,756,640.60** ambacho ni sawa na **asilimia 19** tu kwa maana kuwa **asilimia 81** ya miradi ya Maendeleo haikutekelezwa. Aidha, Fedha za nje kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo **shilingi 400,000,000** ilikua haijapokelewa hadi wakati Wizara inawasilisha taarifa yake katika Kamati.

Mheshimiwa Spika, ni mtazamo wa Kamati kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara unaashiria kukwamisha utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara kwa Mwaka huu wa Fedha. Wizara hii inapaswa kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara inayolenga katika kupunguza gharama za uwekezaji na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara; Aidha, Wizara hii ndio mtafuta masoko wa mazao yatokanayo na kilimo, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha bajeti inayopangwa inaenda kwa wakati.

2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa ushauri wa kamati kuhusu Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi ya maeneo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali.

Maoni ambayo Kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni: -

a) Utekelezaji wa miradi ya Kimkakati kama vile Liganga na Mchuchuma na Magadi Soda;

Mheshimiwa Spika, miradi hii haijaanza kutekelezwa na Serikali hadi sasa. Kwa upande wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma bado Timu ya Majadiliano iliyoundwa toka tarehe 23 Julai 2019 haijamaliza majadiliano. Na Vilevile kwa mradi wa Magadi Soda bado Serikali iko katika hatua za kufanya maandalizi ya Zabuni ili kumpata mbia wa kuwekeza katika mradi huo.

Kamati inasisitiza umuhimu wa kuanza kutekeleza miradi hii hususani katika mwaka wa Fedha 2022/2023 kwani ina manufaa na tija kwa Taifa.

b) Pamoja na hatua nzuri zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kwa wawekezaji, bado kuna malalamiko kwa wawekezaji kuhusu mazingira rafiki ya kufanya biashara na uwekezaji nchini; mfano; hadi sasa hakuna mfumo unganishi wa wawekezaji kupata huduma zote kwa pamoja;

c) Bado Wazalishaji wa ndani wanakabiliwa na changamoto za kuuza bidhaa zinazozalishwa ndani. Masoko ya kufanya biashara bado ni changamoto na Serikali bado hajaweka nguvu ya kutosha kuvilinda viwanda vya ndani.

d) Mradi wa Kurasini Logistic Centre bado haujaanza utekelezaji kama ilivyoshauriwa na Kamati. Ukweli ni kuwa

tumekwisha lipa fidia ambayo ni Fedha nyindi (Bilioni 101) na hakuna kinachofanyika hivyo hatunufaiki na Fedha hizo kwa kuwa hakuna tija inayopatikana hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, ni mtazamo wa Kamati kwa Serikali kuendelea kufanya kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.

2.5 Uchambuzi wa Mpango wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

2.5.1 Uchambuzi wa Malengo/Mpango

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu malengo waliyojipangia kuyatekeleza kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa lengo la kujiridhisha na tija inayoweza kupatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 katika **Fungu 44**. Hata hivyo, malengo yote ya Mwaka 2021/22 yanaendelea kutekelezwa kwa Mwaka 2022/23.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Malengo hayo ni kuwa yameendana na majukumu ya msingi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini pia yamezingatia Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa na ilani ya uchaguzi ya chama (CCM) kinacholongoza Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa malengo yaliyoongezeka ni ya Uwekezaji na Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi. Hivyo, kwa Mwaka 2022/2023, malengo makuu ya Sekta yatahusisha pia Kuhamasisha na kuvutia **uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi**.

2.5.2 Makisio ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya Shilingi 6,000,000.00 ikiwa ni upungufu wa asilimia 60 ikilinganishwa na Makusanyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa Mwaka 2022/2023. Makusanyo haya ni kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine. Kiasi hicho cha maduhuli hutegemea mauzo ya nyaraka za tenda. Kamati ilielezwa kuwa Miaka ya nyuma Wizara ilikuwa na makusanyo makubwa kutokana na shughuli za utoaji wa Leseni za Biashara ambazo sasa zimehamishiwa BRELA.

Kielelezo Na. 4 Ufafanuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

ULINGANISHO WA MALENGO YA MAKUSANYO YA MADUHULI 2021/2022 NA 2022/2023

CHANZO	2021/2022	2022/2023	ONGEZKO/ UPUNGURU	ASILIMIA
UUZAJI NYARAKA ZA ZABUNI	15,000,000	6,000,000	-9,000,000	-60

Chanzo; Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

2.5.3 Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 99,105,506,000 katika **Fungu 44**. Kati ya Fedha hizo, Wizara inaomba kutengewa Shilingi 68,308,687,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 30,796,819,000 za Matumizi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Shilingi 8,728,788,000 za Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 59,579,899,000 za Mishahara. Fedha za Maendeleo zinajumuisha Shilingi 30,346,819,000 Fedha za ndani na Shilingi 450,000,000 Fedha za nje.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)


Kielelezo Na. 5 Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa Wizara ya uwekezaji, Viwanda na Biashara Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Maelezo	Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2022/2023 (TSHS)	
Matumizi ya Kawaida	Mishahara	59,579,899,000
	Matumizi Mengineyo	8,728,788,000
Jumla Ndogo (1)		68,308,687,000
Matumizi ya Maendeleo	Fedha za Ndani	30,346,819,000
	Fedha za Nje	450,000,000
Jumla Ndogo (2)		30,796,819,000
Jumla Kuu (1+2) 99,105,506,000		

Chanzo: Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023

ULINGANISHOBAJETI 2021/2022 NA 2022/2023					
FEDHA	CHANZO	2021/2022	2022/2023	ONGEZKO/UUNGURU	ASILIMA
MAENDELEO	NDANI	52,687,886,000	30,796,819,000	- 21,891,067,000	- 42
	NJE	400,000,000	450,000,000	50,000,000	13
	Jumla Ndogo	53,087,886,000	31,246,819,000	-21,841,067,000	- 41
MATUMIZI YA KAWAIDA	OC	9819,379,000	8,728,788,000	- 1,090,591,000	- 11
	MSAHARA	49,781,407,000	59,579,899,000	9,798,492,000	20
	Jumla Ndogo	59,600,786,000	68,308,687,000	8,707,901,000	15
JUMA		112,688,672,000	99,555,506,000	-13,133,166,000	- 12



Chanzo: Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati kuhusiana na mpango wa bajeti wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara umebaini mambo yafuatayo:-

- Kiasi hicho cha bajeti kinachoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa ajili ya **FUNGU 44** kimepungua kwa **asilimia 12** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Mwaka wa Fedha unaoishia yani 2021/2022;
- Bajeti ya Maendeleo NDANI imepungua kwa **asilimia 42**;
- Bajeti ya Maendeleo NJE imeongezeka kwa **asilimia 13** kutokana na kuongezeka kwa shughuli/kazi ambazo hazikuwepo katika mpango kazi kwa Mwaka 2021/22;
- Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 20**. Sababu za kuongezeka ni ajira pamoja na kupanda madaraja kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha juu ya upungufu huu wa bajeti sababu baadhi ya vifungu vilionekana kuongezeka Fedha na vingine kupungua, Kamati ilipata ufanuzi ufutao;

- a) Kwa Vifungu vilivyoongozeka ni kutokana na kuongezeka kwa majukumu ambayo yametokana na kuunganishwa kwa Wizara;
- b) Kwa Vifungu vilivyopungua ni kwa sababu ya Wizara kuzingatia vipaumbele vichache ambavyo vitatekelezwa kwa Mwaka 2022/2023; na
- c) Ukomo wa bajeti kwa bajeti kuu ya Serikali yaani *Ceiling* kwa Mwaka 2022/2023.

2.6 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali na kubaini kuwa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imeshuka kutoka **asilimia 0.30** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **asilimia 0.24** Mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Aidha, Kamati imebaini yafuatayo:-

- a) Fedha za Matumizi Mengineyo zimeshuka kutoka **asilimia 0.23** kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia **asilimia 0.19** kwa mwaka 2022/2023; na
- b) Fedha za ndani za miradi ya maendeleo zimeshuka kutoka **asilimia 0.49** kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia **asilimia 0.25** kwa mwaka 2022/2023.

Kielelezo Na. 7 Ulinganisho wa Bajeti ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara dhidi ya Bajeti ya Taifa

ULINGANISHO WA BAJETI TA WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022			
FEDHA	BAJETI TAIFA	BAJETI UVB	ASILIMIA
OC	4,189,190,000,000.00	9,819,379,000	0.23
MISHAHARA	8,155,090,000,000.00	49,781,407,000.00	0.61
MAENDELEO ND ANI	10,722,989,000,000	52,687,886,000	0.49
MAENDELEO NJE	4,254,626,000,000	400,000,000	0.01
DENI LA SERIKALI	10,663,278,000,000.00	0	-
JUMLA	37,985,173,000,000.00	112,688,672,000.00	0.30

ULINGANISHO WA BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023			
FEDHA	BAJETI TAIFA	BAJETI UVB	ASILIMIA
OC	4,493,500,000,000.00	8,728,788,000	0.19
MISHAHARA	9,740,800,000,000.00	59,579,899,000.00	0.61
MAENDELEO ND ANI	12,122,100,000,000	30,796,819,000	0.25
MAENDELEO NJE	3,399,200,000,000	450,000,000	0.01
DENI LA SERIKALI	11,308,400,000,000.00		-
JUMLA	41,064,000,000,000.00	99,555,506,000.00	0.24

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati inatoa Maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali:-

a) Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023

Pamoja na kuunganishwa kwa Mafungu matatu (Uwekezaji, Viwanda na Biashara) sasa Bajeti ya Fungu 44 imepungua kwa **asilimia 12** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ni mtazamo wa Kamati kua upungufu huu hautaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara ilihali ukizingatia majukumu ya Wizara yameongezeka. Aidha, kwa kiasi kilichotengwa, **Kamati inaishauri Serikali kuwa Bajeti ipelekwe kwa wakati kama ilivyotengwa ili isiathiri utekelezaji**

wa majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka huu
wa Fedha 2022/2023.

**b) Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati hususan mradi wa
Liganga na Mchuchuma;**

Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 (TDV 2025) inatarajiwa kukamilika Mwaka 2025 na moja ya vipaumbele vikuu ni kuhakikisha miradi yote ya kipaumbele iliyopo katika Mipango na Ilani ya Chama Tawala (CCM) inaanza utekelezaji; Lakini hadi sasa miradi ya kimkakati kuhusu sekta ya Viwanda iliyotajwa katika Ilani hajaanza kutekelezwa kama vile Liganga na Mchuchuma. Miradi hii ni kichocheo kwa baadhi ya Viwanda nchini hususani Viwanda vya Chuma kwa kuwa inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo zingetumiwa katika viwanda hivyo. Na pia miradi hii ni muhimu katika uzalishaji wa nishati ya umeme kutokana na makaa ya mawe;

Kamati inaishauri Serikali yafuatayo;

- i. Kuhakikisha majadiliano yanamalizika katika mradi wa Liganga na Mchuchuma, Aidha, itoe kipaumbele kwa miradi yote ya kimkakati ili utekelezaji wake uanze maramoja.
- ii. Kulipa fidia wananchi wote ambao ardhi zao zilitwaliwa bila kusubiri hatma ya mazungumzo katika utekelezaji wa miradi yote ya kimkakati.

c) Upatikanaji wa umeme Viwandani;

Kamati ilitembelea viwanda viwili na moja ya changamoto iliyoripotiwa ni upatikanaji wa umeme usio wa uhakika; Katika kiwanda kimoja ndani ya masaa manne umeme ulikatika zaidi ya mara kumi; **Ni Rai ya Kamati kwa Serikali, kuongeza kasi katika miradi ya uzalishaji wa umeme ili sasa umeme uweze kuwa wa kutosha kuhudumia maeneo mengi. Aidha, kwa maeneo ya viwandani, Serikali iweke msukumo katika kuhakikisha upatikanaji wa umeme ni wa uhakika, vilevile, kuwepo na laini ya umeme wa viwandani ambayo ni tofauti**

na laini ya majumbani ili sasa hata kama umeme unakatika kutokana na hitilafu ndogondogo basi zithiathiri upatikanaji wa umeme wa viwandani.

d) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE);

Tumeshuhudia Serikali ikiongeza nguvu kubwa katika kutenga Bajeti ya Wizara ya Kilimo, lakini Mamlaka ya maendeleo ya Biashara ambayo ndio inatafuta masoko imetengewa bajeti ya shilingi bilioni moja tu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Fedha kwa taasisi ya TANTRADE ili kupata nguvu ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo kuratibu shughuli za utafutaji wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

e) Uandaaji wa Kanzidata ya Viwanda

Pamoja na jitihada za Serikali kujenga kanzidata za viwanda Nchini, kazi ambayo pia inafanywa ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais. Na ikizingatiwa kuwa Kanzidata hiyo ni muhimu kwa kuwa itasaidia katika kufahamu na kupata taarifa sahihi, za uhakika na kwa wakati kuhusu viwanda (idadi ya viwanda, ujuzi na ajira, bidhaa zinazozalishwa nk). Kamati inasitisiza Kanzidata inayoandalowiwa iwe na hifadhi ya mkusanyiko wa taarifa na takwimu zilizochakatwa na kupangwa kwa namna inayorahisisha upatikanaji wa taarifa hizo (access), kuzitunza (preserve), kuzisimamia (manage) na kuzisasisha (updating).

f) Uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji;

Pamoja na mafanikio na jitihada za Serikali kufuta na kupunguza jumla ya ada na tozo 60 ambazo zilikuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea. Kamati inazidi kuweka msisitizo kwa Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na mfumo funganishi ili kuondoa kabisa adha kwa wawekezaji kupata huduma kwa haraka.

g) Utengaji wa Maeneo ya Kufanyia Biashara kwa Wafanyabiashara Wadogo (Machinga);

Serikali imefanikiwa kuchukua hatua za makusudi katika kuweka mazingira wezesi kwa wafanyabiashara wadogo (Machinga), kwa kutatua tatizo la maeneo ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo (Machinga).

Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha machinga nchi nzima wanapatiwa maeneo ya kufanyia biashara. Aidha, maeneo hayo yawe wezesi na rafiki kwa watu kufika ili wamachinga hawa waweze kupata soko la kuza bidhaa zao. Vilevile Viongozi wa mikoa na halmashauri wanapaswa kuwaongoza machinga vizuri katika kuwapanga, na kuhakikisha mazingira yao yanakua salama muda wote.

h) Mkataba wa kuijunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA);

Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuridhia Mkataba wa kuijunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), kwa Tanzania kuijunga na Mkataba huu inakuwa sehemu ya soko kubwa barani Afrika lenye takriban watu bilioni 1.3 na pato ghafi la jumla ya kiasi cha trilioni 3.4. kuititia mkataba huu Tanzania itanufaika kwa kuza bidhaa na huduma.

Katika eneo hili Kamati inaishauri Serikali yafuatayo;

i. kujipanga vyema katika eneo la uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa, Aidha, kuweka usimamizi mzuri katika kuratibu masoko yetu kimataifa.

ii. Kwakuwa Tanzania ilishawahi kuijunga na mikataba ya aina hii na ilikwama katika utekelezaji wake, basi ipo haja ya Serikali, kuangalia upya changamoto ambazo zilisababisha mkwamo huo ili zisiweze kujirudia tena katika awamu hii.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Mussa Azzan Zungu, Mb na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard);

- i) Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - **Mwenyekiti**
- ii) Mhe. Eric James Shigongo, Mb - **Makamu Mwenyekiti**
- iii) Mhe. Juma Hamad Usonge, Mb
- iv) Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
- v) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
- vi) Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
- vii) Mhe. Lucy John Sabu, Mb
- viii) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb
- ix) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb
- x) Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb
- xi) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb
- xii) Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb
- xiii) Mhe. Khatib Said Haji, Mb
- xiv) Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb
- xv) Mhe. Maryam Omar Said, Mb
- xvi) Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb
- xvii) Mhe. Zulfa Omary Mmaka, Mb
- xviii) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
- xix) Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb

- xx) Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb
- xxi) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
- xxii) Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
- xxiii) Mhe. Dkt. Alfred James Kimea, Mb
- xxiv) Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ashatu Kachambwa Kijaji, Mb. Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, na Naibu Waziri Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, Mb, Katibu Mkuu Prof. Godius Kahyarara, Manaibu makatibu wakuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022**, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023**.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athuman Hussein, *ndc*. Kaimu Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndg. Dickson Bisile, kwa usimamizi mzuri na kuratibu shughuli zote za Idara ya Kamati. Aidha, Nawashukuru sana makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Nyamwanja Chipanda Chilemeji pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika na kuwasilishwa kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara** kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023** kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile, Mb **MWENYEKITI WA KAMATI YA
KUDUMU YA BUNGE YA
VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

6 Mei, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante, ahsante kwa kusoma vizuri taarifa.

Waheshimiwa Wabunge tunaanza mjadala, Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate, jiandae Mheshimie *Engineer Ezra*, jiandae Mheshimiwa Bakar Ahmad Bakar, jiandae Mheshimiwa Aida Joseph.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika bajeti yake ya mwaka 2022/2023.

Kwanza napenda nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutengeneza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wa Tanzania na hatimaye kuongezeka kwa mapato ya Serikali kwa kutumia *TRA*. Hii ni juhudini binafsi ya kuitangaza nchi yetu, kuongeza watalii pamoja na kuwezesha wafanyabiashara kulipa kodi bila ya kuwa na kinyongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili niwashukuru sana Mawaziri wetu; Waziri pamoja na Naibu wake wamejitalidi kuweza kutatua changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wafanyabiashara ili kuhakikisha biashara inakwenda vizuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mchango wa leo mimi nitaongelea mambo matatu; la kwanza litakuwa ni Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na changamoto zake inazokutana nazo kutohana na bajeti finyu wanayopewa hawa wenzetu wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani upo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge hili kwa mazao yote ya kibiashara. Tunashukuru tulivyoanza mfumo tulikuja na changamoto nyingi, lakini tunaendea kadri tunavyokwenda kupunguza changamoto hizi na bahati nzuri kwenye mfumo wa korosho ndiyo ulioanza basi mfumo unaendelea vizuri ingawa kuna changamoto nyingi. Lakini

moja ya changamoto inatokana na bajeti; bajeti inayopewa Bodi ya Leseni za Maghala haikidhi haja ya kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi Ghalani nchini, kwa sababu fedha wanayopewa na eneo wanadolifanya kazi ni kubwa kuliko kiasi ambacho cha pesa wanachopewa sambamba na hilo watumishi ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Mfumo wa Stakabadhi Ghalani uweze kwenda lazima unahitaji fedha ili wafanyakazi wa Bodi ya Leseni za Maghala watembelee maeneo yote ambayo mfumo huu unatumika. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa bajeti ijayo waongeze fedha kwenye idara hii ili waweze kufanya kazi ya usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ipasavyo. Kwa sababu mwaka huu wametengewa shilingi 346,000,000 mfumo kwa sasa hivi unaendelezwa katika zao la korosho, kahawa, tumbaku, nadhani fedha hizi hazitoshi. Sambamba na hilo, mbele ya safari nadhani ni busara watumishi wasambazwe kila Wilaya kwenye Bodi hii ya Leseni za Maghala ili waweze kupata nafasi nzuri ya kusimamia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kutekelezwa katika maeneo tofauti unachangamoto zake ambazo Serikali inatakiwa izifanyie kazi. Moja ya changamoto ni kuchelewa kwa malipo kwa wakulima, hili jambo linakatisha tamaa sana wakulima na kuonekana mfumo huu hauna faida kwao. Mtu anakusanya mazao leo anakaa mwezi mzima hajapata fedha yake, hili jambo linatia doa pamoja na kuuza kwa bei nzuri, lakini kuna kuwa na hisia kwamba kuna mchezo unaochezwa kwa sababu fedha yao inacheleweshwa kwa ajili ya malipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua hizi changamoto, naiomba Serikali kuititia Bodi ya Leseni za Maghala basi watafute namna na kupata maghala kwenye vijiji vyetu ili kupunguza gharama za kusafirisha mazao, ili kupunguza gharama za kuwalipa Wajumbe wa Bodi wanaosindikiza

mazao kwenye maghala makuu. Jambo hili litafanya wakulima wapate faida zaidi kwa sababu gharama ya kusafirisha mazao itapungua, gharama ya watumishi wanaosindikiza mazao itapungua.

Ninaomba sana kwenye suala la maghala kwenye vijiji vyetu ni muhimu sana, ukitembelea huko vijiji maghala yanayotumika unaweza ukashangaa, wanatumia mpaka nyumba za watu binafsi, hazina *floor*, hazina umeme, kwa hiyo inasababisha ubora wa mazao ya wakulima unapungua na hatimaye na bei anayotoa mnunuzi inakuwa ni ndogo kwa sababu tumeshhindwa kuyatunza na upotevu wa mazao unakuwa ni mkubwa kitu ambacho kinasababisha unyaufu ambao unaosababisha mkulima akose fedha yake (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kwa kutumia wataalam wetu, tuandike maandiko, tupate maghala kwenye vijiji huko kwa sababu sheria inaruhusu kwamba ghala linaloweza kuhifadhi korosho au mazao yoyote kuanzia tani 200 linaweza kuingia kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Tunaomba kuanzia sasa *tu-focus* kwa namna ya kutatua tatizo la maghala kwenye vijiji vyetu ili kupunguza gharama za uendeshaji katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye gharama za uendeshaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani; nashukuru Serikali inatoa dira, tozo zote lakini matumizi ya tozo hizi hazielekezwi au hazielezwi kwa wananchi waliochangia hizi gharama. Kwa mfano, kwenye korosho kuna tozo 25 ya Bodi ya Korosho, kuna tozo ya Naliendele, inavyotumika wananchi kuititia vyama vyao vya msingi au mikutano yao hawaambiwi kwamba fedha hii imetumika kiasi fulani. Vilevile kwenye tozo za Halmashauri zetu wananchi hawaambiwi, kwa sababu tozo hizi zinatokana na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani wanapaswa waambiwe kwa mfano, kule Tunduru tuna timu yetu ya korosho, Tunduru Korosho inachangiwa na tozo za wakulima kutokana na wadau wa zao la korosho. Lakini tangu imanzishwa tozo ile Mfuko ule unachangiwa tu hakuna mahesabu, hakuna chochote, jambo ambalo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wananchi wanalamika kwamba fedha hii badala ya kuhudumia kama ilivyotakiwa inatumika tofauti. (*Makofii*)

Naomba sana hizi tozo ambazo tunaziweka kwenye Halmashauri zetu, zinawekwa na Serikali basi tozo zile zilete mrejesho wa makusanyo na matumizi kwa wananchi wa wanaohusika ili malalamiko yaweze kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili jambo liwe mfano kwa sababu zinakusanya kwa mujibu wa taratibu, kutumia vyama vyetu vya msingi, viongozi wetu wa vyama vikuu basi ni vizuri kuwa jambo hili walifanyie kazi kuhakikisha kwamba mapato na matumizi ya hizi tozo ambazo zinatumika kwenye Halmashauri zetu...

(Hapa kengele illilia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Ezra, jiandae Mheshiwa Bakar Hamad Bakar.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri na ushirikiano mzuri amba o amekuwa anautoa kwetu.

Mimi na *declare* kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; ndiyo maana nampongeza waziri kwa sababu tangu ameingia kwenye Wizara hii kwa kweli amejitaji kwa kiasi kikubwa kutoa ushirikiano kwa Kamati, lakini pia kuyapokea mawazo ya Wabunge na ushauri amba o tumekuwa tunautoa. Kwa hiyo, tumshukuru sana yeye na msaidizi wake na Katibu Mkuu na wengine wote amba o wanahusika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitajikita kwenye jambo moja tu, suala la mafuta ya kula ndiyo

nitakaloliongelea tu kwa leo, maana masuala ya Liganga na Mchuchuma nimeongea sana hapa mpaka nikafikia stage ya *kuchumba chima* (*kuchimba chuma*), kwa hiyo leo naomba niiache twende kwenye suala la mafuta ya kula. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumesimama hapa kwa jambo la dhalura tukijadili suala la mafuta ya *petrol, diesel* na mafuta ya taa. Lakini tukirudi huko mtaani suala la mafuta ya kula bado ni kero kubwa na ni mzigo mkubwa kwa Watanzania, bei zime-*shoot* sana *almost more than 100% increment* ukilinganisha na wakati uliopita.

Sasa nikirejea katika Ilani ya CCM, ilani yetu inasema ambayo tunaitekeleza kwamba tuhamasishe ujenzi wa viwanda lakini viwanda ambavyo vitaajiri watu wengi na watu wengi wakitoka katika killmo, mifugo na uvuvi. Lakini Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo unasema kwamba ni ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Sasa tukirejea huko kote nimekuwa nikipitia baadhi ya *papers*, nina *journal* hapa ambayo imeandikwa na Bwana Mgeni Nampenda wa *Department of Trade and Investment College of Economic and Business Study, Sokoine University*; inauliza *Can Sub-Saharan Africa become food safe sufficient? Analyzing the market demand for sunflower edible oil in Tanzania*. Lakini ikaja nyingine ninayo hapa ambayo nimekuwa nazipitia *investment analysis of sunflower farming and prospect of raising household income in Iramba District Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechukulia hizi *case study* mbili nikajaribu kupitia *demand* yetu ya mafuta, katika kupitia ni kwamba tumekuwa tuna *annual demand* ya *almost* tani 570,000 kwa mwaka. Uwezo wetu wa ndani wa kuzalisha ni tani 205,000 kwa *record* ambazo nimekuwa nazipata. Kwa hiyo, tumekuwa na *shortage* ya takriban tani 365 na *almost more than 90 something percent* tunaagiza haya mafuta kutoka Malaysia na *spending* yetu ilikuwa ni zaidi ya bilioni 443 tukiagiza haya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukijaribu kuangalia si kusema Watanzania hawataki kuweka viwanda vya kuzalisha mafuta haya ya alizeti, viwanda vipo lakini shida kubwa imekuwa ni upatikanaji wa alizeti yenyewe ambayo inabidi ikamuliwe ili iweze kutengeza mafuta. Sasa baada ya kupitia kwa muda mrefu nikijaribu kusoma huku na huku, nimejaribu kuangalia *demand*, ukijaribu kufuata Ripoti ya Shirika la Chakula Duniani - *FAO; average yield ya sunflower per hectare* ni kilo 979 ukilima hekta moja unaweza ukapata kilo 979.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kilo moja ya mafuta inayo ujazo wa lita 1.1 na kwa hekta moja tunaweza kuvuna lita zaidi ya 700. Sasa ukijaribu kuangalia ile *demand* yetu ya takribani tani 365,000 ambazo zimepungua, tunajikuta kwamba tunahitaji takribani lita 401,500,000 ili tuweze *ku-cover lile gap*. Sasa hizi lita 401,500,000 tukijaribu kuangalia uzito wa mbegu ya alizeti ambayo tunahitaji ili kuweza kuzikamua ni takribani tani 287,196. Tukirudi nyuma huku kwenye hii ambayo nimeisema kuhusu kuzalisha tunajikuta kwamba ili tuweze kupata mbegu hizi tani 289,196 tunahitaji tuwe na hekta 290,000 *average*. Sasa hekta 290,000 tukirudi hata kwenye maandiko ya dini nilikuwa najaribu *ku-refer* hapa mimi ni Mkristo, Mathayo 6:20-21 unasema: "Jiwekeeni hazina Mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuharibu wala wezi hawaingii maana pale ilipo hazina yako ndipo pia utakapokuwa moyo wako." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kuchangia, tunapopanga kufanya maendeleo ya viwanda ni lazima tuelewe, huwezi kumwambia mtu leo tumeshaongelea hapa tani zaidi ya 290,000 inabidi zilimwe alizeti. Unamwambia mtu aliyekaa Dar es Salaam abebe shilingi bilioni 50 akazifche Biharamulo au kwenye mapori kule ye ye kakaa kule, hazina iko kule moyo hautakuwepo. *Desire* ya mfanyabiashara yeyote yule ni apate *profit* anapowekeza sehemu kwa hiyo, kama hili jambo hatutalichukua kama Serikali hakuna anayeweza kuwekeza huku. Kwa sababu tunahitaji mbegu za alizeti ili tukamue mafuta. Sasa tunachoweza kukifanya hapa, baada ya kuangalia hizi

mbegu tani hizi zinaweza zikazalishwa kwa fedha kiasi gani ni *almost shilingi* bilioni 190. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukiweza kuibeba hii kitu kama Serikali tuka -*invest almost shillings 200 billion*, tunao vijana wengi sana ambao hawana ajira kwa sababu tani 190,000 ni kwamba hii nchi tutailima alizeti karibu kila sehemu. Sio tunazunguka hapa mapori yote yameshikiliwa na *TFS*, kila unapozunguka ni mapori, tunapozunguka ni mapori. Sasa ifikie hatua Serikali ibebe jukumu la kulima. Ikishabeba jukumu la kulima kwa kuwaweka vijana wakazunguka vijana wamemaliza *form four, imagine* lile darasa lenye wanafunzi 100 wanaofaulu ni nusu, nusu wanabaki tunawaapeleka wapi wale vijana? Tubebe JKT, tuwape maeneo, tuwape fedha, wabebe vijana wa Kitanzania, tukalime haya mapori tukishamaliza kulima, mavuno yatakayopatikana kama tunavyofanya kwenye *NFRA* wakati wa mahindi yakahifadhiwe pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mwenye kiwanda sasa anayeweza kuhamasishwa akajenge kiwanda cha shilingi milioni 200, shilingi milioni 300, shilingi milioni 400, shilingi milioni 500 hata sisi Wabunge tutaweza kufanya. Yule mtu ataondoka atakwenda atanunua mbegu kwenye ghala la Serikali, atasaga kwa muda wake kila mwezi anaweza kufanya. Kwa sababu kilimo cha alizeti ni zao la miezi minne tu sasa hata wenye viwanda wanapata shida. Maana mimi wakulima wamelima miezi minne hii, mimi natakiwa nifanye *production* mwaka mzima kinachonitokea ni nini, inabidi ninunue alizeti ya kusaga mwaka mzima ila benki wanani-*charge for something that I am just keeping it in my stock.*

Kwa hiyo, tungeweza kufanya hiki kitu kikafanywa na Serikali, Serikali ni sawa na inavyotuuzia mahindi ihifadhi alizeti wenye viwanda watakuwa wanakwenda wanununa, *in monthly consumption two months, three months or wherever, waweze kuzalisha mafuta.* Tutakapokuwa tumebeba hawa vijana tukawaweka *after four months* wanarudi mtaani wameshajifunza kilimo, lakini pia na wao wamepata fedha watakwenda hata wao wataanzisha kilimo. Kesho na kesho

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutwa tunakuwa kwenye *position* hata ya kuwalisha majirani zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana nimekuwa najiuliza *what if Malaysia* kesho watasema hawatuuzii sisi wanapeleka Marekani? Maana yake hapa hatutakuwa na mafuta. Huwezi kuendesha nchi kwa kutegemea mtu mwininge akuletee mafuta *more than 90 something percent.* (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuweze kuiona hii kama *focus* mpya Serikali iichukue sawa na tulivyo-*approve* shilingi bilioni 50 hapa mwaka jana tukapeleka kwenye mahindi, hebu tuone hii ili Waziri huyu anapohangaika na watu wenye viwanda kuja kuwekeza hapa mbegu za alizeti wazikute.

Mimi ninakuhakikishia kama tutalifanya hili kwa *study* ambazo nilmezifanya kama tutalifanya hili *in two or three years*, nakuhakikishia hatutakuwa na shida ya mafuta ya kula hapa tunaweza tukaanza kuwalisha na majirani zetu. Kwa sababu maeneo tunayo kinachohitajika ni nia tu, tukiweza kuweka nia chini tutatoka hapa tulipo tutasogea mbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu shida ya mafuta ya kula ni kubwa, wananchi mitaani wanalalamika yanazidi kupanda, sasa hatutegemei baada ya hapa yataelekea wapi. Kwa sababu *as long as anal-control* mtu mwininge hatuna ubavu nayo tutakwenda kununua ndio maana umeona *idea* inayokuja sasa hivi tunakuja na kuondoa *duty* tunataka *duty* irudi zero kwenye *importation* ya mafuta ya kula, maana yake ni nini, tunaleta tu mafuta ili tule tuishi Taifa halitapata faida yoyote kwa sababu mafuta yanazalishwa na Malaysia watatuletea hapa *with zero duty*, nchi haipati chochote kile ila tunachofanya tunaji-*sustain* ili tuweze kuendelea kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya mimi nimesema naongelea mafuta ya kula tu leo, ili kuwahi kengele na muda naomba niishie hapa, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, jiandae Mheshimiwa Aida.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na timu yake nzima ikiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote watatu. Tanzania ni mionganini mwa nchi chache ambazo zimebarikiwa na rasilimali nyingi mno, lakini rasilimali hizi tulizonazo bila ya kuweza kuzitangaza kwa nchi mbalimbali na zikajulikana duniani hatuvezi kufikia malengo na kuweza kuzitumia kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara ambazo anazifanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, pamoja na kujenga uhusiano mzuri, ziara hizi kati yetu na nchi hizo ambazo anazitembelea lakini pia zinalengo la kutangaza rasilimali zetu kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu kupata fursa za uwekezaji, lakini pia kwa kuangalia sana kwa watu wetu wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fursa nyingi zikiwemo bahari, maziwa lakini tunayo ardhi, tunavyo visiwa mbalimbali vingi sana bila vitu hivi kuvitangaza haviwezi kujulikana na haviwezi kuonekana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitazungumzia zaidi kwenye suala la uwekezaji; bado pamoja na mama kwenda na kufanya ziara hizi mbalimbali zenyenye lengo hili la kuzitangaza rasilimali zetu, tunazo changamoto za fursa au zenyenye kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji ili kuweza kupata fursa hizo kuja hapa. Tunayo changamoto ya urasimu kwa maana ya *bureaucracy*, bado jambo hili ni changamoto kubwa sana kwa nchi yetu. Endapo tutatatua changamoto

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii ninaamini ile kazi ambayo anaifanya mama basi inaweza ikawa rahisi sana kupata wawekezaji wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna changamoto ya rushwa, bado rushwa ni tatizo kwa nchi yetu endapo pia tutatatua changamoto hii, tutaweza kuweka mazingira rafiki sana kwa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyininge ambayo tulisema ni *political stability*, ili nchi yoyote iweze kuvutia watalii na kuweza kuvutia wawekezaji ni lazima kuwe na *stability ya political*. Tunashukuru sana kwa nchi yetu kwa sasa hivi amani na utulivu ambayo ipo ni jambo la kuweza kupongezwa na kuungwa mkono. (*Makofi*)

Niwaombe sana Watanzania niwaombe sana wanasiasa tuendelee kuidumisha amani tulyonayo, tukiidumisha amani hii ndio ambayo tutawahakikishia wawekezaji kuja nchini na kuweza kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto nyininge ambayo ni miundombinu ambayo bado miundombinu tulizonazo sio Rafiki, ukiangalia barabara zetu bado sio rafiki kwa wawekezaji, ukiangalia umeme, maji na miundombinu mingine. Tukiweza kurekebisha kwenye maeneo haya ya miundombinu ninaamini kwamba wawekezaji watakapokuja na watakapoona kwamba tumeweka sawa kwenye suala la miundombinu, ninaamini kwamba tutaongeza wawekezaji wengi sana wa nje na kuja kuwekeza katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwanza ni wakati sasa wa kuweza kuanzisha *system* (mifumo mbalimbali) itakayoondoa hivi vikwazo, hizi nenda rudi za wawekezaji, kuwarahisishia wao hizi njia za kuweza kupata vibali, lakini njia za kuweza kuona hizo fursa zinazopatikana katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sheria tulizonazo ni wakati wa kufanya marekebishi ya sheria ili sheria hizi ziwe

na fursa nzuri na ziwe na maslahi mapana kwa wananchi wetu, kwa nchi yetu lakini pia ziwe na maslahi mapana kwa wawekezaji ambao wanawekeza hapa nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *FDI inflow* ya *trend* ya *Africa* kwa sasa Tanzania ni kama vile haionekani. Unaona nchi kama Egypt, unaona nchi kama *South Africa*, unaona kama Nigeria, Congo, unaziona hizo kwenye suala hili la *Foreign Direct Investment (FDI)*, sisi bado tuko chini sana. Ni wakati wa kupiga hatua kuondoka hapa tulipo na kuelekea huko mbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kusema hayo niunge mkono hoja hii, ahsante sana nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii...

NAIBU SPIKA: Jiandae Mwambe.

MHE AIDA J. KHENANI: ... ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na *EFD machine*; *EFD machine* ni chombo ambacho kinasaidia Serikali kukusanya mapato. Pamoja na umuhimu wa chombo hiki bado utaratibu wake unavyotolewa mfanyabiashara mwenye mtaji wa shilingi 600,000 akanunue mashine yenye thamani ya shilingi 800,000; mfanyabiashara mwenye mtaji wa shilingi 800,000 na kuendelea mpaka shilingi milioni 10, shilingi milioni 20 mpaka shilingi milioni 200 ukiangalia utaratibu wa hii bei ya mashine haumsaidii mfanyabiashara mdogo. Kama mashine hii inasaidia Serikali kukusanya mapato, ni kwa nini Serikali, isitoe mashine hizi bure kwa wafanyabiashara ili zisaidie kukusanya mapato kwenye Taifa letu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa hii mashine unaonekana tu pale ambapo mfanyabiashara mkubwa ana uhakika wa kufanya biashara zake. Huyu mfanyabiashara mdogo leo hata anayetamani kuisaidia nchi hii kulipa kodi anaangalia mtaji wake wa ahilingi 600,000 halafu mashine ya ahilingi 800,000 nani anaweza kufanya hivyo biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, badala ya kuisaidia Taifa tunapoteza mapato kwa jambo ambalo linawezekana tu kukaa mezani, kuwe na utaratibu mzuri wa utolewaji wa hizi mashine na kulingana na umuhimu wake wa kukusanya mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kwenye hali ya mitaji ya wafanyabiashara wetu. Hali ya wafanyabiashara mitaji yao imezidi kushuka siku hadi siku, nini kinapelekeea mitaji yao inashuka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna utitiri wa tozo za ajabu na hali hii ikiendelea ina maana maduka yatakwendwa kufungwa. Maduka yakifungwa Serikali inakosa mapato, lakini pia tunapoteza ajira za vijana wetu ambao kwa sasa ni changamoto kwenye Taifa letu. Ni wakati wa Serikali kuchukua hatua kabla biashara hizi hazijafungwa, tusirudi huko tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza hapa badala ya sisi kuuza zaidi nje ya nchi, tunauza kwa asilimia 14 lakini tunaagiza kwa asilimia 87. Lazima tujue tunahitaji nini, sisi hitaji letu kama Taifa tunahitaji kuuza zaidi kuliko kununua kuleta kwenye Taifa letu. Kuna haja sasa aidha, kubadilisha mitizamo ya wataalam wetu kwenye Wizara hii, ianze kufikiri kwamba Wizara hii ni kiini cha kukuza uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waache kufikiri haya ambayo tunafikiri leo kwenye hii asilimia nane inayochangia kwenye Pato la Taifa. Tuanze kufikiri asilimia 26 ili tufike kwenye asilimia 26 ni lazima kubadilisha mtizamo waanze kufikiri nje ya box namna ya kulikombua Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hapa tunazungumza mfumuko wa bei, mfumuko wa bei hauwezi kudhibitiwa kwa mtutu wala polisi, unahitaji fikra makini na uzalendo wa nchi hii. Tunahitaji leo tunapozungumza hapa bidhaa zikipatikana kwa wingi huwezi kutumia nguvu kudhibiti mfumuko wa bei. Bidhaa zikipatikana kwa bei ambayo ni rafiki kwa wananchi huwezi kutumia nguvu, huwezi kutumia mtutu, kila kitu kinakuja automatically. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunazungumza mfumuko wa bei ukiangalia bei tu ya mafuta ya kula kwa nini Serikali isitumie taasisi zake. Leo tunapozungumza hapa Magereza wana maeneo makubwa kuliko yale ambayo wanayatumia. Kwa nini Serikali isiwekeze huko kwenye taasisi zake ikiwemo Magereza na JKT, ikapeleka mbegu nzuri, wakawapa vifaa nya kisasa, ni mwaka mmoja tutakuwa tunazungumza ni namna gani tunaweza kuuza nje ya nchi badala ya kufikiri leo kutoa nje kuleta ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu Gereza la Kitete, Wilaya ya Nkasi wale watu wanaweza kuzalisha alizeti, alizeti hiyo ukitoka hapo utakwenda kwenye Gereza lingine lipo Mpanda peke yao tu kwa maeneo ambayo yako nje hawazalishi na maeneo yapo na zile ni taasisi zenu tunahitaji Malaika Gabriel kwenye jambo hilo? (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji uthubutu tu wa viongozi mliopewa dhamana leo na mimi niwaambie hakuna majibu mepesi kwenye mambo magumu. Tunajua kuna vita inaendelea imetuathiri, lakini una popewa mamlaka hawamaanishi kwamba utapita kwenye kipindi kizuri tu na huu ndio muda wa kupimana uwezo wetu wa kuongoza Taifa kwenye mambo magumu kama haya. Hatutakuja tunasema unajua vita, ndio vita ipo, lakini onesha uwezo wako uliyepewa dhamana. Haya mafuta leo tutakwenda kwa wafanyabiashara kuwadhibiti, tukiwadhibiti wafanyabiashara, msifikiri ile athari ni ya wafanyabiashara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inakwenda kuathiri wananchi moja kwa moja mpaka wa kule chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali pamoja na hatua zenu ambazo mnazichukua, tunahitaji kuonesha uwezo wa kutosha wa kuwakomboa Watanzania wanaaoathirika leo. Kama ardhi tunazo mikopo tumeweza kufanya vizuri na mimi ninampongeza Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili na ninyi ambao mmepeewa dhamana mshaurini vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumechukua mikopo kwa ajili ya *Covid* tukajenga madarasa, nini kinapelekea leo tushindwe kudhibiti mfumuko wa bei huu ambao unaendelea pamoja na changamoto nyingine zinazoendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa mimi niwaombe Mawaziri ambao mmepeewa dhamana ya kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais, mumshauri vyema kwa kuangalia uhalisia namna ambavyo Watanzania wanateseka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili jambo naomba Wizara ya Kilimo na Wizara hii ninyi ni Wizara pacha, kwa hali ya kawaida kuna mambo ambayo yanawezekana kabisa, mkitanguliza uzalendo sio uzalendo wa kuvaai tai yenye nembo ya Serikali, tunataka uzalendo wa vitendo wa kusaidia Taifa hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yanaumiza sana, kwa hali ya kawaida mimi ninaamini mfumuko wa bei ambao leo unawaathiri Watanzania mtu ye yote aliyepo humu ndani na anayejua amechaguliwa na Watanzania, kuna haja sasa ya kuangalia ni namna gani pamoja na kwamba tutakuwa na udhibiti wa muda mfupi, lakini lazima tuwe na utaratibu mzuri kama Taifa. (*Makofi*)

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

TAARIFA

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tayari Serikali kuitia Waziri Mkuu wameshatoa maelekezo, kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya nchini kote kwenda kudhibiti na kuangalia mfumuko wa bei katika maeneo yetu huko. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida taarifa hiyo umeipokea?

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zake hizo ambazo amezitoa mimi szipokei.

NAIBU SPIKA: Endelea na mchango wako.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu tunazungumza mambo ambayo ni *serious*, ni vizuri tukajua haya mambo kwamba yanawaathiri wananchi walituleta hapa ndani ya Bunge hili. Hatuhitaji maagizo wala maelekezo, tunahitaji kudhibiti kwa mfumuko wa bei, kama maagizo yanakwenda kuondoa mfumuko wa bei sisi hatuna shida na maagizo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka ni mazingira yaliyopo sasa hivi, na mimi nawapongeza Watanzania kwa kuwa wavumilivu kwa mapito ambayo wanapitia. Ni kweli ni tatizo la sisi sote, lakini narudia tena ni wajibu wa Serikali iliyopo madarakani kuhakikisha jambo hili linadhibitiwa, halihitaji nguvu linahitaji uwezo mkubwa wa kufikiri kuwasaidia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninarudia tena hawa mnaowaona sijui *panya road*, sijui watu gani, ni mazingira haya ambayo yanatokana na hii hali iliyopo sasa hivi. Lazima tushirikiane kwa pamoja na tuieleze Serikali kwa ukweli. Lazima tuje na majibu ambayo tunategemea yataenda kuleta suluhisho kuondoa hali ambayo ipo sasa hivi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo unapozungumza suala la mafuta ya kula, halijatokea leo tu kwa sababu ya vita inayoendelea huko, tumeanza kuzungumza Bunge la mwaka jana hapa, lakini unakuwa unajiliza shida ni nini? Ni kwa sababu hatuna vipaumbele? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri, *slogan* ya Awamu ya Tano ilikuwa ni Serikali ya Viwanda. Serikali ni ileile ameondoka...

(Hapa kengele illilia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Antipas Mgungusi, jiandae Mheshimiwa Joseph Zacharius.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yetu na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo, ningependa kushauri Serikali baadhi ya mambo ili tuweze kuona namna ya kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo la kwanza kabisa, Mheshimiwa Mpakate hapa amechangia vizuri sana kwenye suala la stakabadhi za ghala, lakini yale yote aliyoyasema ili waweze kupata pesa ya kutosha kuna haja ya Sheria ya Stakabadhi za Maghala kuletwa ndani ya Bunge hili ili tuweze kuipitia waongezewe wigo mpana wa kufanya kazi, kwamba maghala yote yasimamiwe na Sheria ya Stakabadhi za Maghala kutoka kwenye bodi ya leseni za maghala. Kwa hiyo, ije sheria, tumuombe Mheshimiwa Waziri hapa ashirikiane na Waziri wa Kilimo na Waziri wa Viwanda na Biashara waone namna ya kuleta sheria sasa maghala yote Tanzania yasimamiwe na Bodi ya Stakabadhi za Ghala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo llingine liko kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 18; nilikuwa napitia hapa, Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri sana

anasema; mwenendo wa kupanda bei usipoendana na uhalisia wa soko ni kati ya changamoto zinazokabili sekta yetu ya biashara. Chini ametoa mfano wa bidhaa za kilimo, lakini pia ametoa mfano wa bidhaa za ujenzi; kwa upande wa vifaa vya ujenzi wastani wa bei ya nondo moja ya milimita 12 imepanda kutoka shilingi 20,393 kipindi cha mwezi Machi, 2021 na kufikia shilingi 26,875 mwezi Machi, 2022 maana yake kipindi cha mwaka mmoja kuna ongezeko zaidi ya shilingi 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ndio kinachoongelewa na Wabunge wengi humu ndani na hii ndio maana halisi ya mfumo wa bei na sisi tuko hapa kama Wabunge kuishauri Serikali yetu sikivu ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kutaka kuwasaidia wananchi wote kwamba, tusiambiane hapa kwamba hakuna mfumuko wa bei, mfumuko wa bei upo tena mkubwa na ni *real*. Lazima sasa sisi kama Wabunge tutafute *solution* tunatokaje hapa kwenda kudhibiti mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali, lakini lazima zifanyike hatua za dharura. Kama Waziri anakiri kuna mfumuko wa bei basi tuweze kujadili hili kwa kina na tutoke hapa na maazimio kwamba, ili kupunguza mfumuko wa bei, kwa sababu kuna upandishaji wa bei kiholela holela kwa wafanyabiashara huko chini pasipo kufuata uhalisia wa soko ama kwenye *importation documents* zao na hivi vitu vinafanyika makusudi kwa wafanyabiashara wenye tamaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utetezi wao mkubwa na Mheshimiwa Waziri hapa anasema kutokana na hili jambo ambalo linaendelea sasahivi, kuna hii vita ya huko Ukraine na maeneo mengine, lakini mambo haya ya kubadilisha-badilisha bei hayajaanza karibuni kwenye nchi yetu. Sasa mimi nataka nishauri kwenye mambo mawili matatu, niishauri Serikali na ione.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa leo kama mara ya nne au ya tano ninaongelea suala la *ETS* kwa sababu tunesema tunatafuta namna ya kuondoa mfumuko

wa bei. Ndugu zangu nataka nitoe mfano, *ETS* ni *stamps* za kielektroniki zinazotumika na kampuni nydingi, hasa hizi zinazozalisha vinywaji, lakini nimesikia kwamba inawezekana wakaingia mpaka kwenye sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *stamp* moja uchapishaji ambayo ni kampuni moja tu pekee sasahivi inaitwa *SISPA*, anachapisha *stamp* moja kwa shilingi nane mpaka shilingi kumi; na wale watu wenye viwanda vyao wanapokwenda kulipia zile *stamps* maana yake watalipa *stamps* kutokana na bidhaa walizozalisha. Na siku moja nilitoa mfano hata ndani ya Bunge, hata kwenye Kamati kwamba Serikali wanapata kiasi gani kutokana na hizi *stamps* zinazochapishwa na *SISPA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushangaza kabisa kwamba Serikali haijataka kujifunza zaidi kwenye hili Jambo. Sijaona hatua za waziwazi zilizochukuliwa ili kuweza kuwapunguzia wananchi mzigو wa uzalishaji kwa sababu gharama zote za uzalishaji zinazofanywa na kampuni, kwa mfano kampuni za vinywaji katika kila chupa moja inaweza ikaongezeka kati ya shilingi 10 mpaka shilingi 15 tuseme, lakini mwisho wa siku gharama hizi zinakwenda kwa mlaji wa chini kabisa. Hiyo ni moja ya vitu vinavyoongeza *inflation* kwenye uzalishaji. (*Makofii*)

Kwa hiyo, niiombe sana Serikali kabisa na ninafahamu kwamba mkataba mpya wameingia kati ya *SISPA* na *TRA*, mkataba ambao haukuwa wazi kwa wawekezaji wengine ambao wangeweza kuzalisha *stamps* hizi kwa gharama nafuu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaficha nini kwenye jambo hili? Kwa nini hatutaki kuwaondolea wananchi mzigو huu wa kulipia *stamps* za kielektroniki, jambo ambalo linaweza likafanywa kwa bei rahisi? Kuna wazalishaji wako tayari kuzalisha *stamps* hizi kwa shilingi mbili, sisi kama Serikali, sisi kama nchi tunang'ang'ania *stamp* za shilingi kumi kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika shilingi kumi hii Serikali inapata 18% tu pesa nyingine yote inayobakia inakwenda kwa yule mtu anayezalisha *stamps* na kuwauzia watu wenyewe viwanda. Tuliangalie hili kwa makini na niwaombe sana Wabunge wenzangu tulijadili hili jambo kwa umakini kwa sababu linawaumiza wananchi na sisi tuko hapa tunatafuta namna bora ya kupunguza *inflation* kwenye bidhaa mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za uzalishaji wa *stamps* ni kubwa, wenyewe viwanda wanalamika, kila siku wanakuja Bungeni mpaka sasa, mwisho wanatuona sisi Wabunge hatuwezi kuwasaidia kwa sababu, hatujatafuta *solution*, hatujakaa nao, hatujawasikiliza nab ado tunalazimisha mikataba hii izalishwe na wale watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine lipo kwenye vinasaba vyta mafuta. *TBS* sasahivi wanalipa karibu shilingi 16 kwa lita moja, wanalipa kwa *SISPA* haohao ambao wanazalisha na hizi *stamps* za kielektroniki. Tunasema tunataka kupunguza gharama, kwa nini tusiangularie tukatafuta vinasaba vyta gharama nafuu zaidi vinavyofanya kazi sawasawa na hivi vinavyoletwa na hizi kampuni, ili kupunguza gharama za uingizaji wa mafuta? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na malengo ya vinasaba ilikuwa ni kupunguza uchakachuaji. Sasa kama tunataka kupunguza uchakachuaji, tumefanikiwa kwa kiasi gani kwa wakati wote ulipita? Utafiti uko wapi unaoonesha kwamba, kuweka vinasaba kwenye mafuta kumepunguza huu uchakachuaji unaosemwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi kuletewa hapa Bungeni sisi tukafanya *review*. Sana sana tumewaongezea mzigo sasahivi *TBS*, *TBS* wanalamika kulipa kwa *SISPA*, *EWURA* nao wamalazimika kulipa kwa *SISPA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala la *Mtwara Corridor*, Bandari ya Mtwara pamoja na Mchuchuma na Liganga. Hivi ni lini Serikali itaamua kwa dhati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kabisa kufanya uzalishaji wa makaa ya mawe, lakini pia kufanya uzalishaji wa chuma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunahangaika hapa kwenye suala la bei ya mafuta. Kwa mfano gesi yetu, sasa hivi ni zaidi ya miaka 20 au miaka 30 tuseme tunaongea kuhusu Mchuchuma, tunaongea kuhusu Liganga, tunaongea kuhusu gesi ya Mtwara. Kama tungkuwa tumeanza kutumia gesi tusingehangaika leo na suala la bei ya mafuta, wako wapi watu wenye kufanya maamuzi? Kwa nini gesi ile ambayo tunajua kabisa iko pale na inatakiwa itumike na wananchi haitumiki? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwambe. Sasa namuita Mheshimiwa Antipas, jiandae Mheshimiwa Kamonga.

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara. Nina masuala kadhaa ya kuzungumza, lakini kubwa zaidi ni suala la ugonjwa wa malaria hapa Tanzania. Ni jambo la Wizara ya Afya, lakini suluhisho la malaria lipo katika Wizara hii ya Viwanda kwa maana tuna kiwanda cha kuzalisha viuwadudu kipo Kibaha (*Tanzania Biotech Limited*) ambacho kinapaswa kuzalisha dawa zinazoweza kuwa viuwadudu na kumaliza malaria hapa Tanzania. Hii ni ajenda ya Serikali tangu Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali ya Awamu ya Tano na sasa Serikali ya Awamu ya Sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mshabiki au nina *interest* kubwa kuona kwamba malaria inakuwa zero Tanzania. Tunajadili sana kwenye Kamati masuala haya, lakini ninachokiona kinachotakiwa ni nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha malaria inakuwa sifuri, lakini kwa sasa bado siaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri nafahamu kwamba Waziri ameingia mpya Mheshimiwa Dkt. Kijaji, ye ye ni mgeni. Nina imaninaye kubwa ninaamini anawenza kufanya

kitu, lakini pia Wizara ya Afya ina Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yuko pale Mheshimiwa Bashungwa, ninaimani nao kubwa sana wao pamoja na wasaidizi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kiwanda kilijengwa na kimeanza uzalishaji mwaka 2016 kwa ajili ya kuzalisha hiyo dawa iweze kumaliza malaria. Kiwanda uwezo wake wa kuzalisha ni lita milioni sita kwa mwaka, lakini uhitaji wetu ili kumaliza malaria tunahitaji lita milioni tano na laki saba kwa mwaka. Mpango ulikuwa ndani ya miaka mitano Tanzania iwe na *malaria free*. Kwa hiyo, ukiangalia hapa uzalishaji na uhitaji wa lita milioni tano na laki saba kwa mwaka, maana yake ndani ya miaka mitano tunahitaji lita milioni kama 28 na gharama yake ya jumla ni kama bilioni 330.

Kwa hiyo, kimsingi Tanzania haihitaji *story* nyingi, inahitaji bilioni 330 kufanya malaria sifuri, lakini jitihada ambayo sidhani kama imefanywa kwa ukubwa ambao unastahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hii kwa maana ya hiki kiwanda ambacho tunacho kilikuwa na mikataba miwili, kwa maana ya na taasisi mbili; ya kwanza na Kampuni ya *Labio Farm* ambao ndio wenye teknolojia ya uzalishaji wa hii dawa ya kule nchini Cuba. Tulikuwa na mikataba nao kama mitatu, wa kwanza watusaidie kujenga kiwanda, tuliweka fedha karibu shilingi bilioni 46 kiwanda kijengwe na kilijengwa pale Kibaha, lakini mkataba wa pili tulikubaliana nao watusaidie *ku-transfer technology* kwa maana ya kufanya *management* ya muda mfupi wa kile kiwanda kuwa-*train* Watanzania waweze kuzalisha dawa na baadaye tuwe *free* tuendelee kujitegemea. Mkataba wa tatu ulikuwa wa kutumia jina la *brand* yao, ile dawa ambayo inazalishwa kampuni yetu tutumie *brand* yao, tumesaini nao mkataba tumekubaliana nao ili tuweze kutumia zile dawa kwa maana kuweza kutumia lile jina kuweza kuuza nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto zipo kadhaa; kwenye mkataba wa kwanza kwa maana ya ujenzi

ulishakamilika, lakini kwenye *management*, mkataba wa pili ulikuwa kidogo una shida kwa maana wale mabwana wakawa wanafanya *management* yote ya kwao, wanazalisha dawa kwa ukubwa na udogo ambao walifanya, lakini uuzaaji wa dawa kwa asilimia nydingi ile kampuni kwa maana ya *Labio Farm* walikuwa wanauza wao. Wanauza dawa nje ya nchi na fedha nydingine mpaka leo Serikali tunawadai, kwa maana ya Tanzania inawadai hela wale mabwana wa Cuba, hizo fedha hawajatulipa mpaka leo ambazo wameuza dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala lingine ni suala la mkataba wa kutumia jina lao kwa zile dawa. Sioni kama hili jambo lina mantiki kwa sababu lengo letu la kwanza kufanya malaria iwe sifuri Tanzania. Tunashindwa kufanya hili jambo kuna sababu zilikuwa zikisemwa hapa kuna suala la ithibati, Umoja wa Mataifa kwa maana ya *WHO* hawajatoa ithibati kwa dawa ambazo tunazalisha pale Kibaha na hili jambo mchakato wake umechukua muda mrefu kidogo. Sasa nikawa nawaza unahitaji ithibati ya Umoja wa Mataifa kuuwa viuwadudu kule Nachingwea? Unahitaji *WHO* je itupe ithibati ili Malinyi kule malaria iishe? Katika hali ya kawaida haiingii akilini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, mimi jambo hili tumekuwa tumekuwa tukibishana nao muda mrefu na mpaka sasa suing mkono suala la mikataba hiyo ambayo ilikuwa imetokea. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ninachoishauri Serikali *management* ya sasa ya Watanzania ina uwezo mkubwa, wameshajifunza kutoka *Labio Farm* wanaweza kuzalisha dawa vijana wetu, wanaweza kufanya hivyo, hilo jambo lifanyike mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla ya kuzalisha dawa kwa maana ya kabla ya *operation* pale kuanza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maana ya *NDC* ilisaini mkataba na Wizara ya Afya, ilisaini mkataba na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tarehe 11 Machi, 2015 ili waweze kununua

dawa yote ambayo itazalishwa pale. Kwa hiyo, maana yake kiwanda kile hakina haja ya kuhangai ka kutafuta wateja, lakini kilisimama muda mrefu kwa kukosa wateja wa kuuza ile dawa ya kumaliza malaria. Wizara ya Afya ndio jukumu lake walisaini kukubaliana na NDC, lakini hawakununua dawa hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajaribu kuwaza, sitaki kutumia lile neno gumu ambalo huwa anatumia Mheshimiwa Halima, lakini nichukue tu la Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda, kweli hii ni busara? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha Serikali, fedha zilizojenga za Serikali, mteja anatakiwa awe Serikali Wizara ya Afya na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, halafu bado hainunui dawa zake yenye? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida inafikirisha na muda mwingine inatia hasira, lakini sijaona *seriousness* ya Serikali kwenye kumaliza malaria Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika,

(*Hapa kengele illilia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kengele ya pili. Ahsante kwa mchango mzuri mengine unaweza ukaandika. Mheshimiwa Kamonga, jiandae Mheshimiwa Nollo.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini vilevile niishukuru Serikali kwa kutusikiliza sisi Wabunge kwa sababu tunayoyasema ndio ambayo wananchi wetu wametutuma.

Ningependa nianze kwa kuchangia Wizara hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda amewasilisha bajeti nzuri sana. Nilikuwa naisoma hapa naifuatilia naona bajeti iko vizuri, ila nimuombe tu Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iongeze kasi katika kusimamia bei ya bidhaa, mfumuko

wa bei. Nimeona una mikakati mizuri, naomba sana uweze kusimamia ili wananchi waweze kupungukiwa na hizi changamoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano jana nilikuwa nazungumza na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbongo kilichopo Kata ya Manda, Wilaya ya Ludewa, alinipa bei ya vitu vichache sana na alisema atafurahi sana akiona nimekutajia. Alitaja bei ya sukari, mwaka jana ilikuwa shilingi 2,500 kwa kilo sasa ni shilingi 3,500; sabuni ilikuwa shilingi 2,000 leo ni shilingi 4,000 kwa mche mmoja; chumvi ilikuwa shilingi 500 sasa shilingi 700; mafuta ya kula yalikuwa shilingi 7,000 kwa lita sasa ni shilingi 16,000; petroli ilikuwa shilingi 2,500 sasa shilingi 4,000; nondo ilikuwa milimita kumi na mbili shilingi 22,000 leo shilingi 28,000 na mabati hizi ni bidhaa ambazo wananchi walikuwa wanantajia, pamoja na mbolea ambayo ilitoka shillingi 50,000 mpaka shillingi 150,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iongeze kasi ya kufuatilia hizi sababu ambazo Mheshimiwa Waziri ameziainisha kwenye bajeti yake. Sababu nyingi tunazozitoa zimekaa kitaalamu sana, zimekaa kisomi sana, wale wananchi kule Ligumbiro wanapata taabu sana kutuelewa. Unavyomueleza chumvi imepanda bei kwa sababu ya vita anashindwa kuelewa, unavyomueleza sabuni imepanda bei, wananchi hawatuelewi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisali misa ya Pasaka pale Ludewa wananchi walilalamika sana. Nimejaribu kujieleza mpaka nalia na machozi hawanielewi kabisa.

Kwa hiyo, naomba Wizara hii ijithidi sana kufanya kazi pamoja na mapendekezo ya Wabunge wengine ili wananchi waweze bkufurahia maisha kwenye nchi yao, lakini nina imani kubwa Mheshimiwa Waziri kwa wepesi wako, kwa umahiri wako hili linawezekana kwako, kwa hiyo, natarajia kuona mabadiliko na wananchi watafurahi. Na kwa kweli nikuhakikishie wananchi wa Ludewa hawana shida wakiona mambo yanakwenda vizuri wataendelea kuiunga mkono Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa nzungumzie huu Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Nimesoma kwenye ripoti mwaka jana ilikuwa kwamba majadiliano yanaendelea na sasahivi majadiliano yanaendelea. Pamoja na hii niipongeze Kamati ya Viwanda na Biashara ambayo iko chini ya Mheshimiwa Kihenzile, niliweza kushiriki kikao chao walivyojadili huu mradi, niliona kwa kweli Serikali ina mkakati mzuri, sasa naomba kwa kweli hili jambo limezungumzwa mno, kwa hiyo, hata wananchi tunavyowaeleza wanajua tunawapiga kamba tu, tunawadanganya. Kwa hiyo, naomba kwa kweli mambo yaanze kuonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano huu mradi ulipitishwa na Waraka wa Baraza la Mawaziri mwaka 1996 kwa Waraka Namba 06/96 kwamba mradi uanze. Ilivyofika mwaka mwaka 2011 mkataba ulsainiwa ubia kati ya *NDC* na Kampuni ya *Tanzania China International Mineral Resources Limited*. Kwa hiyo, toka mwaka 2011 uthamini ukaja kufanyika mwaka 2015 kwa nia ya kulipa fidia eneo la wananchi wale wa makaa ya mawe pale Nkomang'ombe, lakini na huku kwenye chuma cha Liganga huku Mundindi. Sasa toka mwaka 2015 mpaka sasa ni miaka saba/nane imepita, kwa kweli wananchi wamepoteza matumaini ila nimesoma kwenye bajeti yako kwamba umetenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila ningependa sana kuishauri Serikali lile wazo la kwenda kurudia kufanya uthamini, Serikali isilipe kipaumbele sana kwa sababu gani; mwananchi akishapewa ile fomu namba 69 kwamba sasa eneo lako tunalifanya uthamini, hupaswi kubadili chochote, hupaswi kuondoa chochote.

Kwa hiyo, wananchi w akule walitii Serikali, ukisema uende leo ukafanye uthamini upya ile itawaumiza sana wananchi, pale jambo la kwenda kuangalia ni thamani ya ardhi inaweza kuwa imeongezeka kidogo, lakini mambo mengine wananchi kule walitii sheria walivyoziwa kufanya chochote wale wananchi wa Nkomang'ombe na Mundindi hawakufanya chochote.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hatia hii sheria ambayo inasema kwamba maisha ya jedwali la uthamini ni miaka miwili ni Sheria ya Uthamini na Usajili wa Thamini Namba 7 ya mwaka 2016. Sasa hawa wananchi walitumia ile Sheria ya Ardhi ya Vijiji ndio iliyotumika kuwafanya uthamini ya mwaka 1999 sasa hii imekuwa baadaye na ni msingi wa haki na sheria duniani kote kwamba sheria inayotungwa leo haiwezi kunyang'anya haki zilizotolewa jana. Kwa hiyo, wale wananchi walielezwa kwamba watalipwa fidia pamoja na riba kwa kila muda unaochelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeshauri Serikali iweze kwenda kuwasikiliza wananchi wale na kuwalipa....

(Hapa kengele ililia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Nollo jiandae Mheshimiwa Kingu, jiandae Mheshimiwa Makamba.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nifanye rejea kwamba duniani kote na tukiangalia tangu kuanza kwa shughuli ya viwanda duniani katika historia imekuwa inahusishwa na sera ya mambo ya nje, wakati Japan kuitia Waziri wake wa Viwanda na Biashara, na wakati ule kipindi kile cha Marekani zaidi walikuwa wanaangalia Rais anayekuja ana mtizamo gani na katika siasa ya sasa ya mambo ya nje wanaangalia Rais anayekuja ana mtizamo gani na hiyo ina *reflect* biashara ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu katika vipindi mbalimbali tumekuwa na marais wetu katika Awamu ya Kwanza mpaka sasa Awamu ya Sita, sote tunajua sera ya Mwalimu Nyerere kuhusu *foreign policy* na suala la viwanda, tukija hivi karibuni katika Awamu ya Mheshimiwa Kikwete, Rais

Kikwete katika historia ya nchi yetu ndiye Rais aliyeenda zaidi katika kujunganisha na mataifa ya nje katika suala zima la biashara na wazungu wanasema kama alienda *ku-strike deal*, *ali-strike deal* nydingi lakini bahati mbaya utekelezaji wake haukuweza kwenda sawasawa na matamanio ya Rais Kikwete mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumempata Rais Magufuli yeye sera yake zaidi ilikuwa ni ya *protectionism*, si zaidi ya nje, lakini alitaka kukuza *base* ndani ya nchi. Tumempata Mheshimiwa Samia katika Awamu ya Sita yeye zaidi anaangalia *foreign policy* na anaangalia zaidi katika kutafuta mitaji ya nje katika kukuza biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, katika kipindi kifupi tumeona Mheshimiwa Samia ameenda katika nchi za Ulaya, ameenda Amerika, ameenda na Uarabuni. Safari ya Ulaya peke yake ina mikataba kiasi cha trilioni 11.7; lakini ile ni mikataba na katika mikataba kuna makubaliano, kinachosumbua katika nchi yetu ni namna gani sasa kufuatilia mikataba ile na kwa dhati mimi nataka nimpongeze sana Rais wa Awamu ya Sita anapokuwa nje mazungumzo yake mengi ni biashara na siyo misaada. Ukimnukuu na ukimfuatilia Rais wetu hayuko katika *syndrome* ya misaada anaangalia zaidi biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wasiwasi wangu ambao naupata kwamba tutapata mikataba mingi, lakini umadhubuti wa kutekeleza mikataba ndiyo changamoto tuliyonayo katika nchi yetu. Mikataba itakuja mingi na Rais atasafiri, lakini nani anafuatilia kutekeleza mikataba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo na Mheshimiwa Rais amekuwa anarudia kwamba kuna tatizo la *coordination* ndani ya Serikali na hili ni kweli ukiangalia katika Wizara hizi za biashara kwa maana ya Madini, Kilimo, Utalii na Uwekezaji, Viwanda na Biashara lakini nani anawaunganisha, hakuna chombo kinachowaunganisha.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na *Presidential Delivery Unit*, wenzetu wa Malaysia wanaendelea nayo na ile ndiyo unaweza ku-coordinate, watu wa Wizara wakishatoka nje na ziara na Mheshimiwa Rais wakifika *documents* zinawekwa inakuja ziara nyingine *documents* zinawekwa lakini ni nani anasema sasa mkataba ule wa Belgium mkataba ule wa Ufaransa ni nani anafanya sasa jambo lifanyike. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tutaenda sana nje, Rais wetu atafanya sana mahusiano ya mikataba, lakini utekelezaji ni changamoto. Kipindi cha Rais Kikwete tuliwahi kufanya makubaliano ya kwamba wale *IBM* ile *the brain behind* ya *computer* waje hapa Tanzania, lakini mikataba ile ilipotea, hatukuweza kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka tunaishauri Serikali kwanza iweke kitengo cha uwekezaji kwa mitaji ya nje na mitaji ya ndani, tunavutia wawekezaji waje ndani, lakini tuna Watanzania ambao wana uwezo mkubwa hatujaweza kuwaendeleza. Naishauri Serikali tuna makampuni makubwa wakina Azam, benki zetu kubwa kama CRDB sasa wako Burundi, je, tuna mpango gani wa kupanua zaidi kwamba na sisi watu wetu tuweze kuwatafutia maeneo na mitaji zaidi na masoko kwa ajili ya kwenda kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza tukataka kwamba tulete mitaji ndani, lakini mitaji tuliyonayo hatujaiendeleza, tunao Watanzania wenye mitaji kuanzia shilingi billioni 10 kwa nini Mheshimiwa Rais asikutane nao na tuweze kupanga namna gani tunaweza kuwasaidia ili waweze kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dangote tunayemuona leo ametengenezwa na Serikali ya Rais Obasanjo, Dangote alikuwa mchuuzi wa kawaida lakini akatengenezwa na Rais Obasanjo, sasa na sisi ni lazima tufanye hivyo tuwatengeneze matajiri wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa lipo suala la kupanda bei vitu, nataka niseme kwenye eneo moja tu na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anielewe. Nchi yetu kila inavyofika Disemba *cement* inapanda katika kipindi cha miaka mitatu minne iliyopita na tatizo lillopo ni kwamba muwekezaji mkubwa wa *cement* anazima kiwanda kila mwezi wa 11 afanye matengenezo. *Cement* ilikuwa shilingi 16,000 mwezi Novemba alipozima ikapanda ikaenda hadi shilingi 20,000 na inaendelea hivyo hivyo. Sasa na ninaamini na mwezi wa 11 mwaka huu tena atazima kiwanda na *cement* itapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini mchezo huu tuendelee kuwa nao ambao tunawaambia *Fair Competition* waangalie wadhibiti lakini hawawezi kufanya hivyo, ni kwamba kinachotokea ni kwamba ni mtu mmoja anazima kiwanda kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kingu, jiandae Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi leo nina maeneo matatu ya kuchangia kwa ajili ya kuishauri Serikali yangu katika masuala mazima ya biashara na uchumi wa nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma *research* iliyofanywa na *Price Waters Cooperkwa projection* ya uchumi na biashara ya dunia kwa miaka 27 inayokuja. Ripoti inaonesha *the imaging seven economies* ambazo zinajumuisha mataifa ya Indonesia, Uturuki, China, Brazil, Mexico na mataifa mengine. Utafiti huu unaonesha kwamba baada ya miaka 27 kufika mwaka 2050 mataifa kama Indonesia yanakwenda kuwa moja ya mataifa yanayokuza chumi zao sana kutokana na biashara na uwekezaji. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu sisi Tanzania *we cannot be jack of all trade*, kama nchi alikuwa anazungumza mdogo wangu Mheshimiwa Ezra na Mbunge mwenzangu hapo nimemsikia kwa makini sana. Sisi kama nchi lazima tuwe na vipaumbele vichache ambavyo vitawea kulifanya Taifa letu liweze kuwa na mambo ya msingi ya kujivunia katika biashara ya dunia. (*Makofi*)

Leo tunapozungumza habari ya nchi iko katika *shortage* ya mafuta, hivi ni kweli watanzania mnataka kuniambia sisi Tanzania tumeshindwa kabisa kuwa na uwezo wa kuwa na *sufficient* ya mafuta katika Taifa letu, mafuta ya kula? hili jambo mimi nimelizungumza Bunge lililopita nilizungumza alikuwa anazungumza Mheshimiwa Ezra. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mafuta kweli tumeshindwa kuwa na mikakati ya kuwa na mashamba na hili mimi nalizungumza Wizara ya Biashara najua mnafanyakazi nzuri na kuna *recommendation* zenu nitawapa. Wizara ya Kilimo iko na Waziri makini najua *it's doing the best*ila ninachotaka kusema ni kwamba hivi ni kweli Tanzania leo sisi ni wa kulia tuna *shortage* ya mafuta ya kula? *With all arable land* ambayo Mungu ametupatia kama nchi tunalia habari ya mafuta ya kula. *Can we give excuse* ya habari ya *war in Ukraine* for habari ya mafuta ya kula kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, shida moja tuliyonayo ni kwamba *we plan a lot*, hatuchukui maamuzi *serious* ya kufanya maamuzi ya kuleta mageuzi katika Taifa letu. Huu mfano alikuwa anauzungumza Mheshimiwa Ezra Serikali tukiamua kwa kupata wawekezaji tukawa na mashamba peke yake ya mashamba ya alizeti ya mfano maelfu ya heka, mimi ninawaambieni hili Taifa hatuhitaji kuagiza mafuta hapa haturuhusu tu kuwapa *deal wafanyabiashara* lakini *we are killing the economy of the country* na biashara kwenye nchi haiwezi kwenda. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi natoa ushauri Serikali Wizara ya Kilimo kaka yangu Bashe *you are very smart* Waziri wangu. Waziri wa Biashara mwalimu wangu umenifundisha *Mzumbe University* fanyeni *coordination* tuhakikishe na tuweke mipango ndani ya kipindi cha miaka kumi hili Taifa liondokane na habari ya utegemezi wa kuagiza mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linatu-*cost* pia sasa tunavyozungumza haya mambo mipango lakini hata ukiangalia Tume ya Mipango yenewe tumeiua. Tume ya Mipango tumeiua hatuna Tume ya Mipango, *all these great things* tunazozizungumza hatuna Tume ya Mipango. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa ndugu yangu Kingu kwamba Serikali imechukua hatua na kufuatia ushauri uliotolewa na Wabunge katika Bunge la bajeti lilllopita, Serikali imegawa mbegu katika mikoa mikuu mitatu ya alizeti ikiwemo Mkoa wa Singida na mwaka huu peke yake mkoani Singida tumegawa jumla ya tani 1,039 na Mkoa wa Singida baada ya *crop survey* itatuzalishia jumla ya tani 365,000 za ziada za alizeti zitakazotupatia lita 115,000 za mafuta katika uzalishaji wetu na mwaka ujao wa fedha tutagawa tani 5,000 kwa nchi nzima. (*Makofi*)

Kwa hiyo, siyo kwamba Serikali haijachukua hatua Serikali inachukua hatua na hii ni *budgetaryna* tumeshaanza kufanya kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kingu taarifa unaipokea?

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa taarifa ya Mheshimiwa Bashe, kwa kweli sina mashaka na utendaji wa Waziri Bashe, lakini tungependa kuona sasa kwenye *market* haya anayoyazungumza Mheshimiwa Bashe tuone uzalishaji unapatikana. Kwa sababu sasa hivi *scarcity* ya mafuta ninyi mnajua wote mnajua nchi iko kwenye *scarcity* kubwa ya mafuta, lakini kwa sababu ni hatua zinaendelea *it's well and good* ndiyo tunahitaji vitu vya namna hiyo vitokee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ambalo nilikuwa nataka kulizungumza tulikuwa tuna mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo mimi nimesoma ripoti ya utendaji kazi wa Bandari ya Salala iliyoko huko Mashariki ya Kati. Ujenzi wa mradi wa Bagamoyo sisi si tumezubaa sasa hivi tumekuwa tunazungumza, lakini nakwambia tukiacha kutekeleza ujenzi wa mradi wa Bagamoyo *in next ten years* mtaona wenzetu Mombasa ama Msumbiji wame-peak na sisi Tanzania tutabaki kuwa *observer*. Tukiweza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo sasa hivi tunazungumza habari za usafirishaji kwenye bahari zimekuwa kubwa, tukiweza kujenga mradi ule wa Bandari ya Bagamoyo, tutaweza kuleta meli kubwa za *fifth generation* ambazo zitaweza kuifanya Tanzania kuwa *hub* ya kuchukua mizigo na kuipeleka kwenye nchi za *interior* ambazo ziko *land locked* na hiyo itafungua biashara katika nchi.

Sasa shida kubwa ni kwamba tunapozungumza mambo kama haya tunayachukulia taratibu taratibu lakini lazima twende kwa *speed* ambayo dunia inatutaka kwenda kwa *speed* kwa lengo la kuwasaidia watanzania katika masuala mazima ya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza niipongeze sana Wizara, Wizara niwapongezeni sana...

(Hapa kengele illilia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kengele ya pili hiyo. Lakini sasa upate ulifanya nini? Hebu rudia ulifanya haya sekunde mbili. (*Kicheko*)

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niitumie nafasi hii kuipongeza sana Wizara na kwenye hili kwa kweli niwapongeze kwa mara ya kwanza nimeona mikataba iliyokuwa yamesainiwa Dubai, nimeona utekelezaji wa ujenzi wa viwanda 200 Kwala ukiendelea kwa macho yangu nimeenda kutembelea, nitoe pongezi sana kwa Katibu Mkuu wa Wizara na Waziri Mwalimu wangu Profesa Kahyarara ni mtu wa matokeo alipokuwa NSSF alisimamia ujenzi wa viwanda vya Bodi ya Nafaka vimetokea na sasa naona ujenzi wa viwanda 200 unaendelea hayo ndiyo mambo tunayoyataka kwa hili Serikali nawapongeza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante mengine andika.

Lakini Waheshimiwa Wabunge Serikali inafanya mambo mazuri na ni vyema Mheshimiwa Bashe na hii ndiyo roho ya Watanzania sasa hivi kilimo, haya mazuri unayoyafanya waambie Wabunge ili wajue na wao wakusaidie kusimamia huko katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Salome, jiandae Mheshimiwa Mgusu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii muhimu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba nchi nyngi ambazo zimeendelea waliwekeza, Serikali ilitenga bajeti kubwa ilielekeza fedha nyngi kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni Wizara ambayo ndiyo *engine* ndiyo ina uwezo wa kusimua uchumi kwenye Wizara zingine nyngi kwa sababu wao ndiyo *connection* kati ya uchumi kwa maana ya uwekezaji na maendeleo ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 Tanzania waliingia kwenye Mkataba wa Umoja wa Afrika Mkataba unaitwa *Africa Continental Free Trade Area*, mwaka 2021 sisi ndiyo tulisaini. Kwenye mkataba huu katika nchi 55 ambazo ni wanachama nchi 54 zimeshasaini na lengo la huo mkataba ni kufungua biashara na huduma katika nchi za Afrika ambazo ni wanachama kutufungua ili tuweze kusafirisha biashara na kuepuka ushuru na gharama mbalimbali ambazo zinaweza kuwa ni vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi kweli Tanzania tuko tayari kuanza kwenda kuuza kwenye hizo nchi zingine ambazo ni wanachama? Au ukiangalia kiuhalisia sisi ndiyo tutakuwa tunaletewa bidhaa kuliko kuuza huko nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwa mfano kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022; *SIDO* ambao ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo waliomba bajeti kwa ajili ya kuboresha mazingira ya uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo. Kwenye bajeti waliyoomba ya shilingi bilioni 21 ili waweze kuendeleza maeneo hayo wamepewa shilingi bilioni 1.7 na kwa sababu hiyo asilimia 70 ya maeneo ambayo ya kimkakati walidhani watakwenda kuendeleza kwa ajili ya kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo haikuendelezwa. Tafsiri yake ni kwamba Watanzania tumeshindwa kuwekeza kwenye viwanda hata kama Rais wa nchi akiwa na nia njema kiasi gani, akizunguka duniani kiasi gani kutafuta wawekezaji unufaikaji wa Watanzania kwenye eneo la viwanda na biashara ni ndoto. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 hapa Bungeni kwenye *Finance Bill* tulihamisha Shirika linalosimamia ubora wa chakula tulilihamisha tukalirudisha *TBS*. Sasa *TBS* inakagua ubora wa matairi, *TBS* inakagua ubora wa matofali, *TBS* inakagua ubora sijui wa magari. *TBS* hiyo hiyo ianze kuangalia ubora wa maparachichi, *TBS* hiyo hiyo ianze kuangalia ubora wa matikitiki maji, tutafika kweli Na hiyo *practice* dunia nzima ubora wa chakula una kitengo chake idara yake maalum ambayo inatakiwa isimamie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tukitangaza vipi Tanzania kwamba tunaweza kwenda kuwekeza na Waziri anasema sasa hivi tunaweza kwenda kuuza mazao yetu nje, huwezi kuuza mazao ambayo yamezalishwa chini ya kiwango. Waziri anaongelea habari ya uzalishaji wa parachichi, alizeti kama haijapimwa, haijasimamiwa ina afya *toxin* nyingi hayo mahindi ukitaka kwenda kuuza nje mwisho wa siku yatazuiwa mpakani yatarudishwa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho wa siku Tanzania rasilimali tuliyonayo wala hatuhitaji kuweka *incentive*, wala hatuhitaji kusema tunawavutia watu, Tanzania ina madini, mtu yejote anayetaka kufanya biashara atakuja kuchukua madini Tanzania bila kujali kwamba umempunguzia ushuru kiasi gani, mtu yejote anayefanya biashara atakuja kuchukua mazao Tanzania kwa sababu chakula ni hitaji muhimili kwa binadamu yejote, lakini mwisho wa siku ni lazima Wizara ya Viwanda na Biashara ikasimame kama muhimili ambao unasaidia kufungua Watanzania wawekezaji wadogo wadogo na Serikali na mataifa ya nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Viwanda na Biashara ni Wizara nyeti sana, ndio Wizara ambayo inatakiwa iwe na wachumi na watafiti wanaoweza kuishauri Serikali uwekezaji wa kimkakati ambao unaleta tija kwa Taifa na unaongeza pato la Taifa. Pale kwangu Shinyanga Mjini wamejenga inaitwa machinjo ya kisasa, *five billion* za Serikali zimewekezwa pale wanasema wakati wanaleta huo mpango kwa bashasha wanasema wanawekeza bilioni tano kujenga yale machinjo ya kisasa kwa maana gani, kwa siku tutaweza kuchinja ng'ombe na mbuzi wasiopungua 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa tatu/wa nne sasa hivi ng'ombe wanaochinjwa pale hawafiki 15; *five billion* imewekezwa hiyo ni kazi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuishauri Serikali uwekezaji wa kimkakati. Ukienda Kibaha kuna kiwanda pale Serikali imezika fedha *billions of money* kiwanda cha viuwadudu na kaka yangu ameeleza vizuri. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kiwanda pale Serikali imeweka fedha na viuwadudu hivyo vinavyotakiwa kuuwa malaria ni ugonjwa unaoongoza kuuwa Tanzania. Viuwadudu vinavyoweza kuuliwa na dawa ambazo zinazalishwa kwenye kiwanda kile ambacho tumeingia ubia na Cuba ni pamoja na wadudu wanaoleta malaria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekazana kununua neti, Serikali inatoa fedha nyingi kwenda kutibu watu na madawa tunajisifu kwamba tuna madawa na tumefungua hospitali kila kata, kila Kijiji, sijui kila nini, lakini kiuhalisia wale wadudu wangeweza kuteketezwa na hii ndio kazi ya Viwanda na Biashara, ndio maana hii Wizara imekuwa *unpopular* labda ni kwa sababu sijui haina fedha au haionekana kama ni Wizara ya muhimu, lakini sasa hivi ambapo Mheshimiwa Rais analeta uwekezaji ndani ya nchi Waheshimiwa Mawaziri mumsaidie kumshauri, ninyi ni *cross cutting*, ni Wizara mtambuka, mnauwezo wa kwenda kushauri kwenye kilimo, kwenye mifugo, kwenye afya, kwenye madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Biteko wakati anajibu hotuba yangu niliyoongea kuhusu madini anasema anakwenda kuwasaidia wafanyabiashara wa madini wale wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo na kuwaombea kwenye benki, lakini Wizara yako inatakiwa ije Je, hiyo mikopo wanayopewa wawekezaji wadogo ina tija, wale watu wanaenda kupewa mikopo *condition* namba moja anatakiwa apeleke hati, sasa yule mchimbaji mdogo mdogo anayekaa kule Mwakitalyo mchimbaji mdogo mdogo wa Mwazimba sijui kule..., anatoa wapi hati ya nyumba ili aweze kupata mkopo? Uwekezaji mdogo anaambiwa riba atalipa kwa mwezi na riba ya kibiashara kama mtu aliyefungua duka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ili niweze kupata madini lazima kwanza nianze kuchimba shimo, nifunge matimba, nivute maji nikimaliza kuvuta maji nianze kuchimba, nipeleke *plant*, niende nikachenjue, miezi tano, sita, saba, sasa miezi sita saba unamwambia huyu mfanyakibashara alipe riba kwa mwezi hiyo fedha anaitoa wapi? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kuangalia uwekezaji wenye tija na mimi nishauri Wizara hii itengeneze kamati maalum au timu maalum...

(Hapa kengele ililia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kengele ya pili hiyo ahsante kwa mchango mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mgusu, jiandae Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na nikuombe radhi sauti yangu sio nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili tukufu na kunipa nafasi kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana nikupongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu, Naibu Waziri na wasaidizi wako wote kwa kazi nzuri ambayo mmeendelea kuuifanya ambayo imeonekana kwenye hotuba uliyowasilisha katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na mjadala mkubwa hata kabla ya uwasilishaji wa bajeti ya Wizara hii hususani katika eneo zima la kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali na mimi naomba nichangie kwa bidhaa mbili ambazo zinawagusa wanawake wa Tanzania na hususani wanawake ambao ninawawakilisha wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mjadala huu lakini lazima tukubaliane sababu zinazotolewa za kupanda kwa bei ya bidhaa ikiwemo ugonjwa wa *Covid*, ikiwemo vita ya Ukraine na Urusi ni sababu za msingi, hata ukisoma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mitandao mbalimbali duniani sababu hizo zinatajwa. Kwa hiyo kwa sasa hatuwezi kubishania sababu, lakini sababu zipo na athari zake ndio hizi kupanda kwa bei za bidhaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nikubaliane na niipongeze Serikali kwamba imeonesha uongozi kwa namna mbalimbali, kwa mfano kwa bei ya mafuta kwa hatua ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo kuwa *champion* katika mazao yanayohusiana na bidhaa ya mafuta mfano, mawese, ufuta, karanga, soya na alizeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametoka kusema hapa namna ambavyo amegawa mbegu ya alizeti katika mikoa mbalimbali na mimi niseme kwa Mkoa wa Pwani tumefikiwa na mbegu za mawese na imewezesha kikundi kimojawapo cha Kata ya Ruwaruke, Kibiti kimepata biashara kubwa ya mafuta ya mawese kwa sababu Wilaya ya Kibiti mawese yanastawi. Lakini katika hili nishauri, niiombe Serikali kampeni hii iwe kaya kwa kaya kama ambavyo imetokea nyakati mbalimbali za wakati wa njaa kwa mfano Mkoa wa Mtwara kulikuwa na kampeni ya ondoa njaa Masasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika wakati huu wa kupambana kushusha bei ya mafuta niiombe Wizara ya Kilimo kwa kusaidiana na Wizara hii igawe mbegu kwa kaya zote katika maeneo yanayostawi alizeti, lakini Wizara ya Viwanda mtusaidie kuititia *SIDOKuzalisha vifaa vidogo vidogo* vya kuchakata haya mafuta yafike ngazi ya kaya ili kupunguza bei hiyo ya mafuta kwamba tutakuwa tunazalisha kwa wingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la mbolea pamoa na jitihada zinazoendelea uwepo wa kiwanda cha kuzalisha mbolea hapa Dodoma niiombe Serikali iifufue mazungumzo ya viwanda vya kuzalisha mbolea vya Kilwa na Mtwara ambako makampuni yalijitokeza na kilichobishaniwa pale ni bei ya gesi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kwakuwa hata Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais alilishughulikia hili mkamilishe na natambua uwezo huo upo kwa kuwa mmefanya kazi kubwa katika mradi wa kuchakata gesi asilia Lindi. Nina imani kwa bei ya gesi ili viwanda vile viwe vikianzisha vitapunguza bei ya mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye suala zima la ngano niiombe Serikali pia pamoja na kwamba tunaagiza kiwango cha ngano cha kutosha nje ya nchi ifufue mashamba ya ngano na kuwekeza zaidi ili tuweze kuzalisha kwa wingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima hili la bei najiuliza ni kweli bei zinapanda, lakini kama tungkuwa Serikali haitafakari kuongeza ajira, haitafuti wawekezaji nje ya nchi ili kuja kuanzisha viwanda hapa na katika hili nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na kuonesha uongozi, pamoja na changamoto inayoendelea lakini kwa hatua zake za kusafiri pamoja na sekta binafsi kufanya vikao, kuvutia uwekezaji, tutaendelea na kupanda kwa bei, lakini tuna uhakika sasa kwa mfano makubaliana ya Marekani ya zaidi ya trilioni 11 kuititia *Expo Dubai* trilioni 18; lakini wamesema hapa Jumuiya ya Ulaya wamekubaliana trilioni 11 tuna uhakika wa uwekezaji huo na hapa nishukuru Mkoa wetu wa Pwani wa kupata kongano eneo la Kwala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaokaa Mkoa wa Pwani tunaona namna ya safari za Mheshimiwa Rais na jitihada zake zinavyoleta matumaini, tunapokuwa na mfumuko wa bei unakuwa na vijana wengi wasiokuwa na ajira unakuwa na Watanzania wengi wasiokuwa na ajira, bei zimepanda hana kitu cha kununua bidhaa hizo haiwezekani, lakini unapokuwa na mfumuko wa bei unakuwa na nchi ambayo haizalishi kuna bidhaa hatuzalishi, lakini kuititia hatua hizi za kuvutia wawekezaji naamini tutavuka ingawa inaweza ikachukua muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niiombe Serikali, nikuombe Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu, sekta binafsi ni kama jimbo lako la pili ilee hii sekta binafsi...

(Hapa kengele ililia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri, ahsante sana kwa mchango. Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehma ambaye ametusaidia mpaka hivi sasa tumekuwa tukitimiza majukumu yetu. Lakini pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi kama nilivyowahi kufanya siku zote kwa kuweza kunisaidia kuniombea dua hivyo kuhakikisha kwamba matarajio yao tunayatimiza. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba Wizara hii ni Wizara muhimu sana katika nchi hii, lakini hata nchi yoyote ile duniani, kama haujajipanga vizuri kwenye Wizara hii ya muundo huu yenye viwanda basi wewe upange kwamba unakaribia kufeli. Nashukuru kwamba kwa namna moja ama nyingine kumekuwa na uthubutu mkubwa sana kutaka Wizara hii ifanye kazi kwa kadri tunavyotarajia, lakini bahati mbaya tumekuwa na mtazamo ambaio sio sahihi katika kuhakikisha kwamba Wizara hii inapewa uhalisia au inapewa hadhi inayostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu gani, ukiangalia bajeti ya Wizara hii ni bajeti finyu sana, lakini ukiangalia umuhimu wake utakuta kwamba hii Wizara ina umuhimu mkubwa kwa sababu biashara ipo kwenye Wizara hii, sekta ya uzalishaji mali nyingine kwa maana ya viwanda ipo katika Wizara hiyo, lakini sekta ya ujasiriamali pia inashughulikiwa kikamilifu katika Wizara hiyo na sekta ya uwekezaji pia. Sasa ukiangalia sekta ya biashara, uwekezaji, ujasiriamali, na viwanda ni kama vile ni Wizara nne tofauti ambazo zimebekwa katika Wizara moja kwa maana hii unaweza ukaona kwa jinsi gani Wizara hii ni muhimu sana

katika mhimili wa uchumi lakini uzalishaji na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivytangulia ukiangalia majukumu ambayo Wizara hii imepewa yameji-*limit* kwenye uratibu tu yaani Wizara hii hajajielekeza katika utekelezaji, kuna mambo mengi sana ambayo ni ya msingi sana katika kuhakikisha nchi inakwenda ambapo kama Wizara hii ingepewa jukumu hilo hayajapewa na hasa hasa tukiangalia kwa mtazamo huo inakuwa ni vigumu sana kwa Wizara hii kujidesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoomba kwa ujumla tunatakiwa wote sisi kwa maana ya Wabunge tukae pamoja na hii Wizara tuisaidie, itazame katika mtazamo sahihi, iwe ni Wizara sahihi ya uzalishaji lakini ni Wizara ya Kibashara lakini ni Wizara ya kiuwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali iliyopo sasa hivi imekuwa kama na Wizara inayojishughulisha na masuala ya uchuuzi tu, jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais kwa namna moja ama nyingine zinaonekana, lakini ninahofia kwamba hivi jitihada zinaweza zisifike popote kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya Wizara hii, lakini ufinyu wa utendaji kazi kwenye hii Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninawaomba sana ndugu zangu watu wa Wizara, lakini wadau wengine naomba tuishughulikie hii Wizara iwe na muonekano sahihi wa Wizara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia hapa linahusiana na vikwazo vyta Wizara hii kuna nyenzo muhimu sana ambayo Wizara hii kama kweli tunataka ifanye kazi nayo ni *blueprint*. *Blueprint* ni *assurance* kwa wafanyabiashara au wawekezaji kuja kuwekeza, hatuwezi kuwaambia tu kwa maneno kwamba mje muwekeze wakati hakuna sheria zinazo wa-*assure* kwamba wakija hapa mali zao zitakuwa *guided*, lakini pia uwekezaji wao utakuwa ni wenye tija.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna changamoto nyingi sana kwenye *blueprint* ukiangalia kwa mfano masuala ya kodi, kodi kwa mfano ya VAT ukiangalia unaona kwa jinsi gani inavyoathiri na kuwafanya wawekezaji washindwe kuweka fedha zao, tulipotembea kwenye shughuli za kikamati kwa mfano Dar es Salaam kwenye Kampuni ya ALAF na ile kampuni nyingine sikumbuki vizuri ambayo wanajishughulisha sana masuala ya uzalishaji wa mabati na *aluminum* kwa ujumla wanalamika kwamba wanaidai Serikali VATkwa takribani shilingi bilioni 20 ambazo zilitakiwa zirudishwe...

(Hapa kengele ililia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: ...kwa makampuni hayo mawili tu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mchungahela, ahsante sana.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahante naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mchangiaji wetu wa mwisho leo ni Ndugu Kavejuru Felix.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii, kwanza nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu nataka kuzungumzia juu ya upungufu wa mafuta ya kula. Kwanza nimpongeze Waziri Mkuu wa hamasa kubwa ambayo ameitoa katika Mkoa wa Kigoma hasa kwenye kilimo cha michikichi. Michikichi sasa hivi inalimwa katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu, Buhigwe, Kigoma na Uvinza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameitikia kilimo hiki kinaenda kuondoa uhaba wa mafuta ya kula nchini, kinachohitajika kwa Wizara hii ya Viwanda na Biashara ni kusaidia hawa wakulima kuhakikisha kwa haraka sana kwasababu wameitikia na wamelima mashamba makubwa sana kuhakikisha wanatengeneza mazingira mazuri ya kuleta viwanda vya kuchakata mawese Kigoma. Wakileta viwanda vikubwa ambavyo vitakamua mawese pamoja na bidhaa nyingine zinazotokana na michikichi uchumi wa Kigoma utabadilika na uchumi wa nchi nao utabadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze *S/DO* wanao mchango kwa wakulima wa michikichi, wanatoa mashine ndogo ndogo za kukamua mawese, wanatoa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na ukamuaji wa mawese, lakini shida ni moja tu riba ambayo wanaitoa kwa vikundi hivyo vya wajasiriamali ni kubwa. Mikopo hiyo ina riba ya zaidi ya asilimia 18 hadi 21; riba hiyo ni kubwa kwa wakulima, haiwezi kuleta tija kwenye makundi ya wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kwa dhati kabisa ili kuharakisha na kuondoa upungufu wa mafuta ya kula nchini cha kwanza Kigoma tuhakikishe vinaletwa viwanda vitakavyokamua michikichi ili tupate mafuta ya kula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Kigoma ina mazao mbalimbali, tuna zao lingine ambalo tumelishahau ni zao la mihogo ambayo inalimwa katika Wilaya zote za Kigoma, wakulima wa Kigoma wanavuna mihogo haina soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Kigoma wanaiomba Wizara ya Viwanda kuititia *TANTRADE* mtuhakikishie, mfanye jitihada za kututafutia soko la mihogo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, zao lingine ambalo tunahitaji msaada mkubwa sana kwa *TANTRADE* kututafutia soko ni tangawizi, takribani sasa Wilaya yote ya Buhigwe inalima tangawizi. Zao hili ni zao ambalo nalo ikiwezekana likawekwe kuwa zao la kimkakati. Tunaomba *TANTRADE* na Wizara ya Viwanda ihakikishe, itusaidie watu wa Kigoma kutuletea kiwanda cha kuchakata tangawizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nydingine naenda kuchangia ni kwenye biashara. Miaka ya nyuma Mkoa wa Kigoma ulikuwa ni mashuhuri sana kwenye biashara, lakini sasa hivi biashara zimedumaa. Hii imetokea ni baada ya meli ambazo tulikuwa tunazitegemea katika Ziwa Tanganyika ambazo zilikuwa zikisafirisha bidhaa na wafanyabiashara kwenda Congo, kwenda Burundi, kwenda Zambia, meli hizi ni Liemba na Mwongozo zilikwishaharibika ziko *grounded*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali meli hizi zitengenezwe ili kuwepo kwa biashara na majirani. Mkoa wetu wa Kigoma ndio mkoa ambao unapakana na nchi karibu tatu ambazo Mashariki yake kuna idadi kubwa ya watu lile ni soko, tunaomba Wizara ya Viwanda itengeneze mazingira na kuhakikisha inaleta wawekezaji waweke viwanda katika Mkoa wetu wa Kigoma ili uchumi wetu uinuke sambamba na wa nchi nzima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wamekwisha. Tuna wageni walioingia awamu ya pili, wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Khadija Taya ambao ni ndugu zake kutoka Zanzibar, Ndugu Mwanaisha Honda ambaye ni mama mdogo, karibu; Ndugu Warda Obathan – mdogo wake na *owner Arabic Chocolate*, Dar es Salaam na Dodoma, karibu; Ndugu Gloria Gosbert ni rafiki yake na *makeup artist*, karibu sana. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mgeni wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina Mbunge ambaye ni mtoto wake Ndugu Said Ravia Idarus, karibu. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Iddi Kassim ambaye ni Ndugu Musa Mwakitinya, Naibu Katibu Mkuu Vijana. (*Makofii*)

Wapo pia wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango, Dodoma. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Rais wa *Red Cross Tanzania*, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge anawaalika Wabunge wote kuhudhuria maadhisho ya miaka 60 ya *Red Cross Tanzania* yatakayofanyika kwa siku mbili tarehe 8 na 9 Mei. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na tarehe 8 Mei kuanzia saa moja asubuhi kupanda miti katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma - *General Hospital*. Mgeni rasmi atakuwa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo.

Pia kutakuwa na matembezi kuelekea ukumbi wa vijana kwa ajili ya mukutano mkuu, waalikwa kuelekea uwanja wa Jamhuri Dodoma kwa ajili ya michezo mbalimbali kati ya timu ya Bunge, *Red Cross* na nyinginezo, na tarehe 9 Mkutano Mkuu katika ukumbi wa vijana utaendelea na mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro pamoja na Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu. Waheshimiwa Wabunge wote na viongozi, wadau mbalimbali mnakaribishwa kuhudhuria sherehe hizi kwa siku zote hizi mbili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kwa michango mizuri. Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kazi nzuri unayoifanya, lakini mfumuko wa bei huu si tu Wizara hata ucheleweshaji wa meli kushusha bidhaa bandarini inasababisha, *congestion fees* zinawaumiza sana walaji nchini kwetu na hii vilevile ni hatari kubwa sana. Mfumuko wa bei utaongeza *inflation* na *inflation ina-diver currency* yetu. Kwa hiyo, hili nafikiri Serikali mpo mlitazame. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sasa jioni niombe Wabunge mtaendelea na Kamati zenu kuchambua bajeti na naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 9 Mei saa tatu asubuhi. (Makofii)

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatatu,
Tarehe 9 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*